

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 2 Juni, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Waheshimiwa tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Arobaini na Mbili. Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na;

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Pamoja na Maoni na ushauri wa Kamati Kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 351

**Mapambano Dhidi ya Madawa ya Kulevya Nchini**

**MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR** aliuliza:-

(a) Je, ni hatua gani zilizofikiwa kwenye mapambano dhidi ya madawa ya kulevya nchini?

(b) Je, ni watu wangapi wamekamatwa kuanzia mwaka 2019 – 2020 na wangapi wamehukumiwa kifungo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar, Mbunge wa Malindi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini, hadi sasa Serikali imechukua hatua zifuatazo;

Mheshimiwa Spika, kwanza imetungwa kwa sheria mpya ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu, Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Na.5 ya mwaka 2015. Sheria hiyo, ilianzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kama chombo maalum chenye nguvu ya kisheria ya kukamata, kupekua, kuzuia na kupeleleza makosa yote yanayohusiana na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, pili; kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kama vile Jeshi la Wananchi wa

Tanzania kitengo cha Wanamaji na Jeshi la Polisi, Serikali imeimarishaji operesheni za nchi kavu, anga na majini hasa katika viwanja vya ndege, maziwa na Bahari ya Hindi, ikiwa ni mkakati kwa kudhibiti njia na vipenyo vyote. Pamoja na kuendelea kutoa elimu ya athari za matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kupitia mamlaka imetambua mitandao mikubwa ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya nchini na kubaini njia mbalimbali za usafirishaji. Mkakati huo, umechangia kwa kiasi kikubwa kuziba mianya ya uingizaji wa dawa za kulevya na ukamataji wa dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu ya swali (b) kutokana na hatua hizi zilizochukuliwa na Serikali, katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2020, jumla ya dawa za viwandani (*Cocaine* na *Heroin*) zilizokamatwa ni kilo 426 na gramu 363. Jumla ya dawa za asili bangi na mirungi zilizokamatwa ni tani 28 na kilo 34. Aidha, katika kipindi cha Januari - Desemba 2020, na Januari - Mei 2021, jumla ya watuhumiwa 124 walikamatwa, kati yao 23 wametiwa hatiani na uskilizaji wa mashauri 40 unaohusisha watuhumiwa 83 unaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Omar, Mbunge wa Malindi.

**MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, ningeoomba tu niwe na swali moja tu la nyongeza kwa sababu majibu yake kwa kweli yamekamilika lakini ninalo swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nimepata malalamiko kutoka kwa wananchi wanapokwenda kutoa mashirikiano kwenye kitengo hiki cha madawa ya kulevya kwa kuwataja wanaohusika, baadhi ya maafisa hutoa taarifa zao za siri na kuwafikia wenyewe. Je, ni hatua gani mtakazozichukua endapo mtawabaini maafisa hawa ambao sio waaminifu ili

wananchi warejeshe imani ya kwenda kusaidia Serikali? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Muhagama tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, najua ni miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa mstari wa mbele kushughulikia tatizo hili la dawa za kulevyo nchini na hasa kwa pande zote mbili za muungano, nakushukuru na nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko ya uongozi wa Mamlaka na kama mlivyoshuhudia kilogramu takribani kama 895 kwa mara ya kwanza mzigo mkubwa umekamatwa mwaka huu kwenye Pwani ya Mkoa wa Mtwara ambayo ilikuwa inatoka Mashariki ya Mbali huko kwa hiyo ninawapongeza wote na Rais wetu tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tumekuwa na tatizo kubwa, baadhi ya watendaji na maafisa ndani ya Mamlaka lakini na vyombo vingine wamekuwa wakitoa siri, sio za watoa habari tu, hata siri ya mipango na mikakati ya kwenda kudhibiti na kuzuia matumizi na biashara hii na matumizi ya dawa za kulevyo. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mara zote tunapowabaini tumekuwa tukichukua hatua kali na wakati mwingine kuwafungulia mashtaka na kuwafikisha katika vyombo vya sheria ili waweze kuondoa kabisa tatizo hilo la ufichaji wa mianya ya biashara na matumizi ya dawa za kulevyo nchini.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kutoa onyo kwa watendaji wote wa Mamlaka na watendaji wengine wote kutokuthubutu kabisa kuwa ni sehemu ya biashara hiyo haramu ya dawa za kulevyo nchini kwa ustawi wa vijana wetu na Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

Na. 352

### **Kuanisha Mpaka Kati ya Wilaya ya Mkalama na Hanang**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je ni lini Serikali itaainisha mpaka kati ya Wilaya ya Mkalama na Hanang' eneo la Singa na Limbadau ili kuondoa taaruki kwa wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna mgogoro wa mipaka ya Vijiji kati ya Wilaya za Mkalama na Hanang ambao umekuwepo kwa muda mrefu licha ya jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ikwemo vikao vya ujirani mwema baina ya wahusika wa mgogoro, Serikali ilitekeleza uwekaji wa alama za mipaka iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 266 la tarehe 14 Desemba 1973 lililotangaza Wilaya ya Mbulu na Hanang'. Chanzo kikubwa cha mgogoro huo ni baaadhi ya wananchi kutokukubaliana na alama za mipaka zilizopo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 266 la uanzishwaji wa Wilaya ya Mbulu na Wilaya ya Hanang'.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri za Wilaya ya Hanang na Mkalama zimetenga jumla ya shilingi milioni 40 kwa ajili ya kupima Vijiji vya Singa

na Limbadau ambavyo ndio vipo kwenye eneo la mgogoro. Serikali inatarajia mgogoro huo utamalizika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge uliza swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba jina langu ni Francis Isack Mtinga, sio Mtenga, Mtenga ni Wachaga, Mtinga ni Wanyiramba.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri ya waziri ya kukiri mgogoro lakini nakiri sjaridhishwa kabisa na jibu walilolitoa. Na hivyo nitauliza swali moja tu la nyongeza ili nitoe na maelezo kidogo.

Mheshimiwa Spika, mpaka huu ni wa mkoa; mpaka kati ya Hanang' na Mbulu na Wilaya ya Mkalama ni mpaka wa Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Singida na amekiri kwamba tatizo hili ni la muda mrefu sana lakini majibu aliyoyatoa kwamba ni kupima, kupima hakutatui tatizo la mgogoro. Na tatizo hili limekuwa kubwa sasa kule Kijiji cha Eshkeshi, Wilaya ya Mbulu wameingia kilometa mbili katika Kijiji cha Ulamoto kule...

**SPIKA:** Uliza swali!

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aniambie kwamba lini tutakwenda naye akafanye mkutano na wataalam kwa vijiji hivi ili kutambua mipaka ili kuondoa mgogoro huu na wananchi wafanye kazi za utawala vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani la Wizara ya Ardhi zaidi hili jambo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Isaack.

Mheshimiwa Spika, suala la kutambua migogoro katika mpaka sio kufanya mikutano tu, kinachotakiwa pale

ni kwenda na GN zinazohusika na kufanya tafsiri ya GN kuangalia zile *coordinates* katika yale maeneo. Naomba nimuhidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tukimaliza tutampa wapima watakwenda wakiwa na zile GN zinazotaja mipaka ya Wilaya zote mbili ili waweze kutambua na kuweza kubainisha mipaka. (*Makofi*)

**SPIKA:** Na wataalam wakienda mkubali matokeo, mnaweza mkawa mnapiga kelele inakwenda ina-*chop* Tarafa nzima inahamia upande wa pili unanza kelele nyingine tena. (*Kicheko*)

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi.

Na. 353

### **Madai ya Miche ya Mikorosho**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi wanaodai miche ya mikorosho deni ambalo ni la muda mrefu tangu mwaka 2017?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela Mbunge wa jimbo la Lulindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2017/2018 Serikali kupitia Bodi ya Korosho iliingia mikataba na wazalisahji wa miche 678 ili kuzalisha miche 13,661,433 ya korosho yenye thamani ya shilingi 5,317,107,679. Aidha, jumla ya miche 12,298,000 sawa na asilimia 92 imesambazwa kwa wakulima katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani,

Tanga, Singida, Tabora, Dodoma, Kilimanjaro, Morogoro, Njombe, Mbeya, Iringa na Songwe.

Mheshimiwa Spika, malipo kwa wazalishaji hao yamechelewa kutokana na zoezi la uhakiki kuchukua muda ili kujiridhisha kabla ya kufanya malipo hayo. Kutokana na uhakiki uliofanywa katika awamu ya kwanza na timu ya wataalamu kutoka Serikalini jumla wazalishaji miche 382 waliozalisha miche milioni tano yenye thamani ya shilingi bilioni 2.3 wameshalipwa.

Aidha, kupitia uhakiki wa awamu ya pili uliofanyika mwezi Agosti hadi Oktoba 2020, ulibaini kuwa jumla ya miche milioni 5.8 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.660 ilihakikiwa na bado kulipwa. Aidha, Serikali inakamilisha utaratibu wa malipo kwa wazalishaji hao wa miche na watalipwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela!

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia suala hili kwa muda mrefu sana na majibu yamekuwa ni hivihivi. Naomba Serikali itoe *commitment* ni lini watalipa deni hili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kutokuwa na umakini hasa hasa katika ulipaji wa madeni ya ndani, Serikali haioni sasa ni muda wa kulipa riba katika madeni haya ya ndani pia kama vile wanavyolipa madeni ya nje na riba.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mchungahela maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la riba, mikataba ilikuwa haionyeshi kwamba kutakuwa na riba pale ambapo kunapokuwa kuna ucheleweshaji lakini siwezi kutoa *commitment* ya hilo jambo.



Mheshimiwa Spika, kuhusu lini watalipwa nataka nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na kweli amekuwa akifuatilia yeye na Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara na baadhi ya maeneo mengine ya nchi yetu kuhusu hawa waliogawa miche. Niwahakikishie kwamba mwaka ujao wa fedha watalipwa watu wote waliosambaza miche na sisi Wizara ya Kilimo tumeshamaliza zoezi hili na tumepeleka hazina.

Mheshimiwa Spika, vilevile waliokuwa watumishi wa umma kwa maana ya Wakurugenzi na Madiwani kwa kuwa kulikuwa na mikataba halali, haki zao zitalipwa na haziwezi kudhulumiwa kwa kuwa tu ni mtumishi wa umma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Cecil Mwambe, na baadaye Mheshimiwa Zungu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyo madeni kwa wakulima waliozalisha miche ambao hawajalipwa lakini Serikali inakiri kuwatambua. Pia kuna watu waliotoa huduma mbalimbali kwenye msimu ule wa korosho ambao Serikali ilinunua; watu walisambaza magunia, vifungashio na wengine *sulphur*. Tunataka pia Serikali itoe *commitment* kwa sababu watu hao walikopa kwenye mabenki, ni lini nao mtamalizana nao kwa kuwalipa pesa zao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kuhusiana na madeni mbalimbali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe. Ni kweli kwamba katika sekta ya korosho sio tu madeni yaliyotokana na msimu ambao Serikali ilinunua korosho a wakulima. Madeni yaliyotokana na Serikali/korosho zilizochukuliwa na wakulima, Serikali imelipa sehemu kubwa na imebaki kiwango kidogo kisichoziidi shilingi bilioni 2.8 ambazo zimahusisha madeni ya wasambazaji wa watoa huduma lakini sekta nzima ya korosho kuanzia vyama vya

msingi, Vyama Vikuu vya Ushirika, wakulima wenyewe wanadaiwa zaidi ya bilioni 66.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali hatua tuliyoichukua ya kwanza ni kukaa na wadai wote ikiwemo mabenki na watoa huduma na tukaweka utaratibu ambao tumeanza ku-*collect* fedha ambazo tutaanza kulipa kwa wale wanaohakikiwa na mchakato huo umekwishaanza na utaratibu unaendelea na kwa kuwa tutakuwa na kikao tarehe 6 Lindi ambacho kitaongozwa na Waziri Mkuu, naamini kwamba yote haya tutayajadili na tutatoka na majibu na wadai wote tumewaalika katika mkutano huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zungu, swali la nyongeza!

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Vietnam mwaka 1993 ilikuwa ni nchi maskini sana na walikuwa wanapewa msaada wa chakula. Leo Vietnam wanazalisha *surplus* ya mpunga tani milioni 20 na hii ilitokana na *geographical diversification policy* kwenye kilimo. Wame-*map* nchi yao na ile sera wakaiweka, haikuwa ni sera *blanket* moja ya nchi nzima, kila *mapping* ya eneo wakafanya *diversification* wa kujua eneo gani litumie sera ipi.

Mheshimiwa Spika, je, leo Serikali yetu ina mkakati gani wa kuhakikisha kuongeza tija ya kilimo na kuipitia upya sera ya kilimo nchini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali muhimu sana hilo, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Hussein Bashe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali alilouliza Mheshimiwa Zungu, Mbunge wa Ilala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa muda mrefu tumekuwa kama Taifa tukifanya makosa makubwa kufikiria kwamba kilimo kila zao linaweza likalimwa kila sehemu tuka-*think of extensive instead ya intensive agriculture*. Kwa hiyo, mkitazama hata bajeti ya mwelekeo wa Wizara ya Kilimo

tumeangalia zaidi kuhangaika namna gani tunaongeza tija. Mwelekeo wa bajeti yetu katika mwaka ujao wa fedha ume-*focus* katika tija badala ya kufikiria kuongeza kila zao kila sehemu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tunaomba ofisi za mamlaka ya juu, tutazindua timu mbili ambayo mojawapo ni suala la *financing* na nyingine ni suala la kupitia upya Sera na mtazamo wetu wa kilimo na tunaamini kwamba baada ya hapo tutakuwa na *roadmap* ambayo inaonyesha kila eneo litakuwa na *specialty* yake kutokana na *competitive age* yake na huko ndipo tutakapowekeza zaidi na teknolojia za kisasa katika hayo maeneo badala ya kufikiria kila zao linaweza kulimwa kila sehemu katika nchi. Kwa hiyo, huo ni mwelekeo wa Wizara na huko ndipo tunapotaka kwenda kama nchi.

**SPIKA:** Majibu mazuri, tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kweli ni vizuri mkaangalia maana yake yapo mazao kwa mfano mizeituni hii, hii ambayo inastawi vizuri sana *Middle East*. Mazingira yale ya *Middle East* na hapa Dodoma ni *almost the same* na tumeshajaribu mizaituni inastawi vizuri sana, lakini Wizara ya Kilimo haijaweza kuangalia *matrices* kama hizo, kwa hiyo, tunakushukuru. Bado tupo Wizara ya Kilimo hiyohiyo, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mwakilishi wa wanawake Tabora.

Na. 354

**Serikali Kujenga Miundombinu ya Kisasa ya Kukausha  
Mboga za Majani-Tabora**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango wa kuwajengea miundombinu ya kisasa akina mama wa Tabora itakayoweza kukausha mboga kama uyoga, mchicha na majani ya maboga kwa njia ya kisasa zaidi ili kuongeza kipato?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha masoko ya ndani na nje ya nchi ilia kina mama wa Tabora wanaokausha mboga waweze kuuza mboga hizo kwa faida?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri Hussein Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora kama ifuatavyo kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa kilimo wakiwemo *USAID*-kupitia mradi wa Lishe, Shirika la Mpango wa Chakula Dunia (*WFP*) na *JICA* kupitia mradi wa *TANSHEP* imekuwa ikijenga uwezo wa wadau kuhusu matumizi ya teknolojia mbalimbali ikiwemo usindikaji wa mazao ya bustani. Serikali pia inahamasisha matumizi ya teknolojia ya ukaushaji wa mboga kwa kutumia nishati ya jua kwa kuwa teknolojia hiyo ni nafuu na rahisi kutumika ikilinganishwa na teknolojia nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na *FAO* inatarajia kutekeleza Mradi wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7.3 utakaofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia ili kuwasaidia kina mama wa Mkoani Tabora na Katavi kuimarisha masoko na kusaidia katika teknolojia ya uhifadhi mazao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na *SIDO* na miradi na *TANSHEP* katika sekta *horticulture* kuunganisha wakulima na masoko ili kuboresha masoko ya ndani na nje ya nchi. Serikali kwa kupitia *SIDO* imekuwa ikiwapatia akinamama mafunzo ya ukaushaji wa mazao ili yawe na ubora unaotakiwa. Mafunzo yanalenga kufikia viwango vya bidhaa vinavyotambuliwa katika viwango vya *TBS*. Aidha, wasindikaji hao watakuwa wakipelekwa kwenye maonesho ya aina mbalimbali kama vilevile nanenane ili kutangaza

bidhaa zao. Serikali pamoja na Wizara ya Viwanda kupitia *SIDO*, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Umoja wa Wajasiriamali Mkoa wa Tabora wanaendelea kuwatafutia majengo wakinamama ambayo yatatumika katika kusindika na kama *display centres*. Aidha, *SIDO* imeandaa mkakati wa kuwaingiza wasindikaji watakaokidhi vigezo katika *portal* ya *SIDO*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanayowapa matumaini wafanyabiashara wa usindikaji wa mbogamboga hasa kwa Mkoa wa Tabora hususan kinamama.

Je, ni lini Serikali kushirikiana na *FAO* inaweza kuanza mradi huu wa kuwawezesha kina mama kuweza kufanya biashara ya Kitaifa na Kimataifa?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuwezesha mazao haya ya usindikaji wa mbogamboga ambayo wakinamama wengi wa Mkoa wa Tabora wamejikita katika biashara hiyo kuhakikisha kwamba yanakuwa yana masoko ndani ya nchi na ukizingatia unaweza ukaenda kwenye hoteli nyingi hatuna mboga za asili, tunatumia mboga ambazo ni *roast* na zilizoungwa unguwa zaidi. Naomba kupata jibu, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili wanataka mlenda uingie mpaka kwenye hoteli za kitalii. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naoba kumjibu Mheshimiwa Jacqueline maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lini tunaanza mradi wa *FAO*, tunaaza mwaka wa fedha unaokuja; ni mradi wa miaka mitano, tunaanzia majaribio katika Wilaya ya Kaliua ndipo tutakapoanzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwasaidia wakinamama wa Mkoa wa Tabora na Watanzania wote kuweza kuingia katika masoko. Sasa hivi tunapata *project* pamoja na wenzetu wa *SIDO* ili waweze kukidhi vigezo vya viwango vinavyoweza kuwasaidia kuingia katika masoko ndio maana mmesikia katika Mkoa wa Tabora tumesema kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Umoja wa Wanyabiashara sasa hivi pamoja na *SIDO* inatafutwa eneo moja ambalo litakuwa ni *center* ya kina mama kwa ajili ya kukaushia na hapo kuweza kufanya *packaging* waweze ku-*meet standard* za masoko. Kwa hiyo, ni hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi sio tu kuzalisha, je tunachokizalisha kinaweza kukidhi vigezo vinavyotakiwa vya sokoni, hiyo ndio kazi tunayoifanya katika sekta ya mbogamboga na matunda.

**SPIKA:** Jibu lilikuwa refu kwa hiyo tuendelee bila swali la nyongeza. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga.

Na. 355

### **Tatizo la Mawasiliano ya Simu Kijiji cha Matinje Ikombandulu**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano katika Kijiji cha Matinje Ikombandulu ambalo ni eneo la machimbo na lina idadi kubwa ya watu ili kurahisisha biashara katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, Eng!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA  
HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatekeleza miradi mitatu katika Jimbo la Manonga. Miradi hiyo inatekelezwa katika Kata za Igoweko; mnara huu unahudumia pia Kata ya Uswaya, Sungwizi pamoja na Ngulu. Utekelezaji wa miradi katika Kata hizi umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) itakifanyia tathmini Kijiji cha Matinje Ikombandulu na hatimaye kijiji hiki kitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika zabuni zitakazotangazwa katika mwaka wa fedha 2021/22, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali nimekuona.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya yetu ya Igunga hususan Jimbo la Manonga sisi ni wakulima wa pamba, mpunga, madini na mifugo kwa wingi. Katika vijiji kama hicho ambacho nimekitaja cha Ikombandulu, Mwakabuta, Ikungwi Ipina, Utuja na Shalamo ni katika maeneo yenye uzalishaji kwa wingi katika mazao niliyoyataja. Ipi mikakati ya Serikali kuhakikisha maeneo hayo yanapata mitandao ya simu kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Mwisi, Simbo, Choma, Ibologelo na Indembezi wanapata mawasiliano ya simu lakini mitandao hii ipo chini sana hasa kwenye *internet*. Je, Serikali kupitia wadau wanaotoa huduma katika maeneo hayo ipi mikakati yao na hasa ukitambua sasa hivi Tanzania tuna-*launch 5G*, nini mikakati ya Serikali kuhakikisha maeneo hayo niliyoyataja tunapata angalau *4G* kwa ajili ya kusaidia wataalam, watafiti na waandishi wa Habari...

**SPIKA:** Ahsante sana umeeleweka Mheshimiwa

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Hususan kwenye vijiji vilivyopo nchini Tanzania, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi kwamba Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tupo katika mkakati wa kufanyia tathmini Kijiji hicho sambamba na vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshavitaja ili kuhakikisha kwamba tujiridhishe ukubwa wa tatizo baada ya hapo vitaingizwa katika zabuni ya awamu zinazokuja katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu masuala ya *internet*. Tunafahamu kwamba kwa sasa hivi tunakoelekea katika uchumi wa kidigitali na tunaelewa kabisa kwamba *internet coverage* inahitajika ili Watanzania waweze kutumia vizuri katika shughuli zao za hapa na pale. Tumeshaelekeza watoa huduma wote wafanye tathmini katika minara ambayo bado inatumia teknolojia ya *2G* ili waweze ku-*upgrade* na kuweza kutumia teknolojia ya *3G*, *4G* na hatimaye baada ya kujiridhisha kwamba tutakuwa tunahitaji *5G* basi tutakuwa tumefikia huko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, nimekuona.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, maeneo mengi ya Mkoani Songwe ikiwepo Kata Maalum ya Mbangala ambayo ni Kata maalum kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya dhahabu yanakabiriwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano. Nataka kufahamu



nini mkakati wa Serikali katika kupeleka mawasiliano katika maeneo haya ya Wilaya nzima ya Songwe? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iko kwenye mchakato na katika hatua za awali kabisa katika kuhakikisha inafanyia tathmini Vijiji na Kata zote nchini ili kujiridhisha wapi tuna tatizo la mawasiliano ili tuhakikishe kwamba katika mwaka wa fedha ujao tuweze kuviingiza na kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata mawasiliano.

**SPIKA:** Haya twende Kagera sasa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, changamoto ya wananchi wa Manonga inafanana sana na wananchi wa Jimbo la Kyerwa. Nimekuwa nikiongelea changamoto ya Kijiji cha Kitega, Kata ya Songambebe ambacho kipo chini ya mlima na kipo karibu na Rwanda, hakuna mawasiliano ya Redio wala simu wala kitu chochote. Ni mpango gani wa Serikali na wa dharura kuhakikisha kile Kijiji tunakirudisha Tanzania kwa kukipa mawasiliano kwa sababu ni kama wapo gizani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali kupitia Wizara yetu na kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote tayari

tumeshafanya tathmini katika Vijiji na Kata zote zilizopo mipakani na katika maeneo ya mbuga na hifadhi. Tayari tunaenda kuvingiza katika mpango wa kuhakikisha kwamba mwaka huu tunaenda na utaratibu wa kuanza kwanza na maeneo ya mipakani.

Katika siku ambayo tunapitisha bajeti yetu tuliwaambia Waheshimiwa maeneo ya mipakani ndio ambayo tunaenda kuyapa kipaumbele yakiwepo maeneo ya Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoka Jimbo la Bariadi, Mbunge aliyepita alikuwa anaitwa Andrew Chenge na yeye sasa anaitwa Andrea Kundo; inaonesha kule Usukumani kila mtu ni Andrea. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mheshimiwa Rose.

Na. 356

### **Mkanganyiko wa Tafsiri ya Umri wa Miaka 18**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza: -

Kumekuwepo na mkanganyiko wa tafsiri ya umri wa miaka 18 katika Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mtoto na Sheria ya Kanuni za Adhabu na kupelekea kuvunja misingi ya Katiba.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzifanyia mapitio Sheria hizo hususan kifungu cha 131 (2) ya Sheria ya Kanuni za Adhabu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, mtu aliye na umri chini ya miaka 18 anatambulika kuwa ni mtoto. Pamoja na kwamba kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mtoto kinabainisha kuwa mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18, Kifungu cha 131(2) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu hakitoi tafsiri ya mtoto bali kinatoa adhabu kwa mtu mwenye miaka 18 au chini ya hapo anayekuwa na hatia ya kosa la kubaka na kupewa adhabu mbalimbali ikiwemo kuchapwa viboko kwa mkosaji wa mara ya kwanza, kufungwa jela kwa miezi 12 pamoja na viboko kwa mkosaji wa mara ya pili, au kifungu cha maisha kwa mkosaji kwa mkosaji anayejirudia kwa mara ya tatu. Kitaalamu hawa wanaitwa *young offenders'* au wakosefu wenye umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, Sheria zetu mbalimbali nje ya sheria ya Mtoto, zinaweka umri wa mtoto kulingana na muktadha na mazingira ya jambo mahsusi kama vile mikataba, jinai, kupiga kura, leseni za udereva na kadhalika. Kufuatia kutungwa Sheria ya Mtoto mwaka 2009, iliyotokana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto wa 1989 pamoja na masharti ya Ibara za Haki za ujumla za Binadamu kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, na kwa kuwa Kifungu cha 131(2) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kilifanyiwa marekebisho mwaka 2009 na baada ya kutungwa kwa Sheria ya Mtoto, ni dhahiri kuwa hakivunji misingi ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Serikali sasa inapoendelea kuzipitia sheria mbalimbali, itakipitia pia kifungu hicho cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu ili kufanya marekebisho kutokana na uhitaji uliopo kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Serikali imeona umuhimu na imekubali ombi langu la kupitia na kufanya marekebisho ya kifungu hicho cha sheria, nishukuru pia sitakuwa na swali la nyongeza nitasubiri utekelezaji wa mabadiliko ya sheria hiyo, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea na Fedha na Mipango, swali litaulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

Na. 357

### **Mfumuko wa Bei Nchini**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mfumuko mkubwa wa bei za bidhaa ulioanza tangu Desemba, 2020 ambao umefanya gharama za maisha kupanda?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei ulipanda kutoka asimilia 3.2 mwezi Desemba 2020 hadi asilimia 3.5 mwezi Januari 2021. Hii ilitokana na upungufu wa baadhi ya bidhaa sokoni ambao hutokea mara kadhaa katika vipindi vya mwanzo wa mwaka kama hivyo.

Aidha, mfumuko wa bei ulishuka na kufikia asilimia 3.3 mwezi Februari 2021 ikiashiria kuwa bidhaa na huduma zilianza kupatikana kwa bei nafuu kulinganisha na mwezi Januari mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unaendelea kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0. Lengo hili linaweza kufikiwa kutokana na mikakati mbalimbali ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuimarisha usambazaji wa chakula kutoka maeneo ya uzalishaji hadi katika maeneo ya walaji, kuimarisha usimamizi wa Sera ya Fedha na bajeti na kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka mashambani hadi katika masoko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba bado bei ya bidhaa sokoni ni kubwa na haijashuka hasa kwenye vifaa vya ujenzi. Je, Serikali inasema nini juu ya suala hili?

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka kama mitano au kumi hatujawahi kupata utulivu wa uhakika wa bei ya mafuta ya kula, sukari na unga wa ngano ambayo ni mahitaji muhimu kwa wananchi kila siku. Serikali inasema nini juu ya suala hili? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Cecilia ni mfuatiliaji sana wa masuala haya ya mfumuko wa bei, nakumbuka hata kwenye michango yake ya hotuba mbalimbali nimewahi kujibu swali linalohusiana na mfumuko.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei (*inflation*) sio bei kama ambavyo amesema bei za bidhaa fulani bado zipo juu. Mfumuko wa bei ni ile kasi ya bei kubadilika, tofauti na bei zenyewe kama bidhaa ipo katika bei hii hauwezi ukai-

*judge* hapa Bungeni kama ipo juu au chini kwa sababu itategemeana tu na bidhaa zenyewe zimepatikana kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachoongelea na tunachoshughulika nacho ni ile kasi ya bei zenyewe kubadlika na katika Tanzania utakumbuka kwa takribani karibu miaka zaidi ya 10 tumefanikiwa kushusha mfumuko wa bei na tumefanikiwa kuuweka ucheze kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 ambacho ni viwango vya Afrika Mashariki. Na hilo ndio lengo kubwa la kuweza kuhakikisha kwamba bei zetu hazibadilikibadiliki kwa kiwango ambacho kinasababisha vitu visitabirike katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ambalo ametaja bidhaa mahususi, kuna mikakati ambayo ni mahususi kwenye mazao hayo aliyoyataja ikiwemo mafuta ya kula pamoja na masuala kama ya sukari. Utakumbuka hotuba ya Waziri wa Viwanda ilielezea vizuri jinsi Serikali ambavyo imejikita kwenye kuongeza uzalishaji wa sukari ambapo kutakuwepo na upanuzi wa mashamba pamoja na uzalishaji wa sukari ambao sasa utaenda kutoa jibu la uhakika na la kudumu kuhusu hizo bei zinazokuwa zinapandapanda na kubadilikabadilika kwenye masuala ya sukari.

Mheshimiwa Spika, na hii ilikuwa inatokea kwa sababu, kwenye masuala ya sukari kuna vipindi ambavyo viwanda vinakuwa havizalishi. Tulikuwa tunalazimika kutafuta sukari kutoka maeneo mengine kuziba pengo la aina hiyo, lakini kwa mkakati ambao umewekwa wa kuziba pengo hilo la sukari kwa uzalishaji wa ndani, utaenda kutoa jibu la kudumu la mabadiliko ya harakaharaka ya bei za sukari.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mafuta ya chakula utaona jinsi ambavyo Waziri Mkuu kila wakati utamuona yuko katika maeneo mahususi ambayo yanashughulika na masuala ya uzalishaji, kuhamasisha uzalishaji wa mazao haya ambayo yatatupatia mafuta ya chakula, ili kupata jawabu la kudumu la upungufu wa mafuta ya chakula ambao ndio unasababisha kupanda kwa bei.

Umeona jinsi anavyofanya kazi Kigoma, anavyofanya kazi Singida pamoja na maeneo mengine ambayo anashughulikia masuala ya aina hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. tunaendelea na Wizara ya Maji. swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha Mjini, Mheshimiwa Silvestry Koka.

Na. 358

### **Kusuasua kwa Mradi wa Maji – Kibaha**

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Jimbo la Kibaha Mjini bado lina changamoto kubwa ya maji katika maeneo ya Kata za Mbwawa na Pangani; na Mradi wa Ujenzi wa matanki ya maji unakwenda kwa kusuasua. Je, ni lini Mradi huo utakamilika ili Wananchi wa Kibaha Mjini waondokane na adha ya maji?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji ambao ulihusisha ulazaji wa bomba kuu pamoja na mabomba kwa ajili ya kutawanya maji kwa wananchi yenye urefu wa kilomita 27. Wananchi wapatao 6,500 wa Kata ya Mbwawa wananufaika na huduma ya maji tangu mwezi Aprili, 2021. Kwa upande wa Kata ya Pangani usanifu kwa ajili ya ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lita milioni 6 umekamilika.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2021/2022, jitihada za kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya

Kibaha Mjini zinaendelea na kazi ya ujenzi wa tenki kubwa utanza na ulazaji wa bomba kuu urefu wa kilomita tano utanza katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022. Mradi huu utanufaisha wananchi wa Kata ya Pangani, pamoja na eneo la Viwanda la Kibaha Mjini (*TAMCO*).

**SPIKA:** Mheshimiwa Koka nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, asante. naipongeza Serikali kupitia *DAWASA* kwa kazi nzuri iliyofanyika kule Mbwawa wananchi sasa wamepata maji kwa mradi kukamilika kwa asilimia 90. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa matenki mawili ya maji katika Kata ya Pangani, kwa maana ya Mtaa wa Vikawe na Mtaa wa Pangani, unaodhaminiwa na Benki ya Dunia unajengwa kwa kusuasua. Tenki la Vikawe limefikia asilimia 50, lakini tenki la Pangani kwa ajili ya kuhakikisha sasa wananchi wa Kata ya Pangani wote wanapata maji bado halijaanza kujengwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhimiza sasa, ili hili tenki la pili liweze kuanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, wananchi wa Kata ya Misugusugu na Visiga na hususan maeneo ya Zogoale, Jonuga pamoja na Saeni, kupitia Zegereni Viwandani, wana shida kubwa ya maji na wanahangaika kutumia maji ya visima na haya ni maeneo muhimu ya uchumi katika Jimbo letu la Kibaha Mjini. Ninafahamu kuna mradi wa takribani bilioni 3.3 unaotakiwa kujengwa.

Je, ni lini Serikali sasa inaanza kujenga mradi huu, ili kuwaondolea wananchi kero na kustawisha uchumi katika Mji wetu wa Kibaha?

**SPIKA:** Ahsante sana kwa maswali hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, *Engineer* Maryprisca Wilfred Mahundi, majibu tafadhali.



**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kibaha ni moja ya miji ambayo Serikali imeelekeza fedha nyingi kwa kuona kwamba, maji sasa yanakwenda kupatikana. Katika eneo la Pangani ni mradi mkubwa ambao tayari Serikali mpango ni kuelekeza zaidi ya bilioni tano na kazi zinatarajiwa kuanza mapema robo ya kwanza ya mwaka wa fedha ujao, kwa maana ya kuanzia mwezi wa tisa tunatarajia kazi itaenda kuanza katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika maeneo ya viwandani, kama mwenyewe Mheshimiwa Mbunge alivyoongea, na nipende tu kumshukuru kwa kuweza kutoa pongezi zake kwa Serikali. Ni kweli Wizara bado imelekeza fedha za kutosha zaidi ya bilioni tatu na katika mwaka ujao wa fedha tunatarajia mradi huu uweze kutekelezwa na kasi ya mradi huu itategemea upatikanaji wa fedha katika Wizara, lakini lengo letu kubwa tunaelekea kwenye mageuzi makubwa. Miradi kama hii yote mikubwa tutahakikisha tunaisimamia kwa wakati.

**SPIKA:** Bado tuko Wizara hii. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Singida Kaskazini, Mheshimiwa Ramadhani Ighondo.

Na. 359

### **Upatikanaji wa Maji Safi na Salama – Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itavipatia huduma ya maji safi na salama Vijiji vya Kinyamwenda, Igauri, Matumbo, Itamka na Msimihi katika Jimbo la Singida Kaskazini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali. Mhandisi Maryprisca.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 imekamilisha miradi ya maji katika vijiji 7 ambavyo ni Mughamo, Mgori, Ngimu, Sefunga, Ghalunyangu, Kijota na Malolo hivyo, huduma ya upatikanaji wa maji kufikia asilimia 66.4 katika Wilaya ya Singida Vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 utafanyika utafiti wa kina kwa ajili ya kuainisha maeneo yenye maji ya kutosha chini ya ardhi. Hivyo vijiji vya Kinyamwenda, Igauri, Itamka na Msimihi vitapata maji baada ya kukamilisha uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji.

Aidha, kijiji cha Matumbo kitapata huduma ya maji ya uhakika baada ya ukarabati wa mradi wa maji kukamilika mwezi Julai, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kukamilisha miradi ya maji, hasa vile visima virefu, huanzisha kamati za watumiamaji, lakini kamati hizi zimekuwa zikishindwa kujiendesha na hivyo kufikia mahali kushindwa kabisa kutoa huduma au kufa. Na ningependa kushauri pengine Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wale watumishi wanaotakiwa kuajiriwa na watumiamaji, na hizi kamati, waajiriwe moja kwa moja na Wizara badala ya hizi kamati halafu zile fedha kidogo zinazopatikana zielekezwe kwenye ukarabati na ununuzi wa vifaa?

Mheshimiwa Spika, lakini swali lingine la pili. Serikali ilichimba visima virefu katika Kijiji cha Misinko na Kijiji cha Kitongoji cha Gairo katika Kijiji cha Sagara, lakini baada ya kukamilisha kuchimba visima vile maji yale yalionekana yana chumvi nyingi sana na hivyo hayafai kwa matumizi ya binadamu. Serikali iliahidi kuchukua *sample* ya yale maji na kuyapima ili yaweze kutumiwa na binadamu, jambo ambalo hadi sasa halijafanyika.

**SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa.

**MHE. ABID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuhakikisha kuja na mkakati mbadala wa kuwapatia maji safi na salama wananchi wa vijiji vile? Na hapa ningepomba Mheshimiwa Naibu Waziri angeambatana na mimi twende tukaonje yale maji yalivyo na chumvi na hayafai kabisa kwa matumizi ya binadamu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abeid Ramadhan, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Kamati za Watumiamaji, hili Mheshimiwa Waziri ameshakuwa akiongea mara nyingi na ameshawaagiza mameneja wote wa maeneo yote ya Mamlaka za Maji pamoja na *RUWASA* kuona kwamba, wanaajiri vijana wetu wanaotokana na chuo chetu cha maji pale Dar-Es-Salaam, hasa kwenye eneo la uhasibu. Hii ni kwa sababu, kumekuwa na ubadhirifu mkubwa sana katika hizi jumuiya.

Mheshimiwa Spika, na mfano mzuri uko pale kwenye Jimbo lake Pangani. Palikuwa hakuna mhasibu, waliweza kukusanya labda laki saba tu kwa mwezi, lakini baada ya kumuajiri binti ambaye ni mhasibu, msomi, mwenye *profession* hiyo sasa hivi wanaweza kukusanya takribani milioni nne na nusu. Hivyo, tunaendelea kutoa wito katika majimbo yote

tuweze kushirikiana kuona kwamba, kamati zile tunaruhusu hawa vijana wanaajiriwa.

Mheshimiwa Spika, na kuhusiana na mishahara yao itoke Serikalini; kwa sasa hivi inakuwa ni ngumu, lakini kwa sababu wao wenyewe wanakusanya fedha za kutosha wana uwezo wa kujisimamia na kuweza kulipana hiyo mishahara. Pamoja na hilo, tayari Mheshimiwa Waziri ametupia jicho la ziada kuona nyakati zile za kiangazi namna gani ya kuweza kuzisaidia jumuiya hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala la maji chumvi kuweza kupatikana baada ya kisima kuchimbwa:-

Mheshimiwa Spika, tayari pia wataalamu wetu wameelekezwa kwenda kusimamia na kuona namna bora ya kuona chumvi hii inaweza ikatibika. Na endapo itashindikana basi, chanzo mbadala cha maji kitaweza kufikiwa na kutumika katika utoaji maji kwenye jamii.

**SPIKA:** Nilikuona Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Naibu Waziri ya kuvipatia huduma ya maji Vijiji vya Nkonekoli, Nkure, Njani, ambayo aliitoa wakati alipozuru jimboni kwetu mwezi Disemba kuelekea sikukuu za Christmas? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, ahadi kwa wananchi ambayo ilikuwa ni zawadi ya Christmas, ya maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ni deni, kwa sababu tumeahidi lazima tuje tutekeleze. Mara baada ya utaratibu mzima wa upatikanaji wa fedha kwenye eneo lako, lazima wataalamu waje na ni lazima maji yapatikane kwenye Jimbo lako la Arumeru, ahsante.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi. Mheshimiwa Zeno.

Na. 360

### **Ufinyu wa Eneo la Kilimo – Malinyi**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Sehemu kubwa ya maeneo ya Kilimo cha Mpunga Malinyi imemegwa na Mamlaka ya Wanyamapori (*TAWA*) kwa Mipaka mipya iliyowekwa Mwaka 2017 bila maridhiano na Wananchi wa sehemu ya bonde la Kilombero. Je, Serikali haioni kuwa ni vema kufanya upya mapitio shirikishi kwenye mipaka ya eneo la Hifadhi?

**SPIKA:** Majibu ya uhakika ya Serikali kuhusu swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mary Masanja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Bonde la Kilombero ni sehemu ya ardhioevu yenye umuhimu kitaifa na kimataifa kutokana na kuhifadhi bioanuai mbalimbali na zilizo adimu duniani kama vile mnyama aina ya sheshe. Aidha, Bonde hilo huchangia takriban asilimia 62.5 ya maji yote ya Mto Rufiji na hivyo kuwa chanzo muhimu cha maji kwa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, uwekaji wa mipaka wa Bonde la Kilombero ulizingatia mfumo halisi wa kiikolojia wa Bonde hilo, ili uweze kukidhi matarajio ya uhifadhi wa ardhioevu. Hivyo basi, Pori Tengefu Kilombero lilianzishwa mwaka 1952 kwa *GN. Na. 107/1952* na halijawahi kubadilishwa mipaka yake. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zeno Mgungusi, swali la nyongeza, nimekuona.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri hatma ya mgogoro wa bonde hilo na mipaka hiyo kutoka kwa Kamati ya Mawaziri Wanane maisha yaliendelea na wananchi wa kule tulinima na sasa mpunga uko tayari kwa ajili ya kuvunwa. Je, Wizara haioni haja ya kutoa ushirikiano na wananchi tuweze kuvuna mpunga huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli bonde hili kuna baadhi ya wananchi walikuwa wamevamia kwa ajili ya kilimo na sasa hivi ni kipindi cha mavuno. Kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaweza ikawaruhusu na sisi kwa sababu, yale ni mazao na ili kuepuka njaa kwa wananchi wetu. Na kwa kuwa Serikali hii inawathamini wananchi, tutatoa vibali maalum ambavyo vitawasaidia kwenda kwenye maeneo hayo wavune kwa utaratibu ambao utasimamiwa na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Naibu wake, walipokuja jimboni kwetu walichukua hatua kuhusu askari wa *TAWA*, baadhi ambao walikuwa

wakiwaonea wananchi wetu. Na kuwa Mheshimiwa Waziri aliahidi pale katika mkutano ule kwamba atatujengea soko la samaki, Ifakara, Kilombero. Naomba kuiuliza Serikali ni lini ahadi ile nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii itaanza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Ni lini ahadi itaanza, Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Asenga kwa kuuliza swali hilo na kujali wananchi wake:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kujenga soko katika Daraja la Mto Kilombero upo katika bajeti ya Wizara katika mwaka huu 2021/2022. Kwa hiyo, mara baada ya bajeto hiyo kupitishwa mkakatin huo utaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga jiandae kupitisha bajeti hiyo keshokutwa. Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, nilikuona.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale inazungukwa na Pori la *Selous*, lakini sasahivi mkakati wa Serikali ni kuimarisha utalii wa picha badala ya utalii wa uwindaji na sisi kwenye Kanda ya Kusini kuanzia ukanda wa Kilwa mpaka Tunduru hakuna lango la utalii wa picha.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutuwekea sisi lango la utalii wa picha na sisi tuweze kunufaika na uwepo wa *Selous*?

**SPIKA:** Mheshimiwa kule Liwale unadhani lango lingeweza kukaa wapi kwa mfano?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, palepale Liwale Mjini ndio panafaa kwa sababu, Kambi ya Selou iko palepale Liwale.

**SPIKA:** Lango lazima liwe kwenye mpaka wa hifadhi. Kama kule Kimambi, Ndapata, Mtawatawa, Barikiwa, eeh. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, tafadhali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kuchauka kwa maswali yake mazuri, lakini pia kwa kutambua wananchi wanaoishi Liwale. nimuahidi tu kwamba, mageti yanayohusiana na hii hifadhi yatafunguliwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mageti mengine yote.

Mheshimiwa Spika, hili naliongea kwa kujiamini kwa sababu, wiki iliyopita tu nilikuwa katika Mkoa wa Kilimanjaro, Same pamoja na Mwanga, pia kuna maombi hayo ya kufungua mageti mbalimbali kwenye Hifadhi ya Mkomazi. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yale ambayo yanahitaji kufunguliwa mageti ya ziada, ili kurahisisha watalii mbalimbali waweze kuingia na kurahisisha namna ya kuingia kwenye hifadhi, tutayafungua na bajeti hii itakayoanza keshokutwa imezingatia kufunguliwa kwa mageti hayo. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa sababu ya muda kama mnavyoona tumeshafika Saa Nne, kipindi cha maswali kinapaswa kikamilike ili tuendelee na mambo mengine.

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo ya wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani. Waziri wa Nishati ambao ni viongozi wa Wizara Taasisi za Wizara na Mashirika ya Maendeleo wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, Mhandisi Masanja, Katibu Mkuu ahsante sana karibu sana wewe na timu yako yote. *(Makofi)*

wageni wengine 15 wa Mheshimiwa Kalemani ni familia yake wakiongozwa na Mke wake Vaileth Kalemani,



ahsante sana Vaileth, tunakushukuru kumtunza huyu mtani wangu huyu. *(Makofi)*

Pia wapo wenyeviti sita wa Bodi, Bodi ya *TANESCO* Mwenyekiti Alexander Kyaruzi karibu sana, *REA* Mwenyekiti Julius Kalolo ahsante, *PURA* Mwenyekiti Prof. Gaspar Muhinzi ahsante, *TBPA* Dkt. Lutengano Mwakahesya ahsante sana *EWURA* Ahmed Kilima ahsante sana. Wageni wengine 12 wa Mheshimiwa Kalemani ni Kamati ya Siasa nadhani kutoka kule Chato nadhani wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wilaya ndugu Raphael Masambo, Kamati ya Siasa ya Wilaya karibuni sana, karibuni sana wageni wetu kutoka Chato karibuni Dodoma msimange mange mkiwa hapa! *(Makofi)*

Wageni wengine 31 wa Mheshimiwa Kalemani ni Madiwani wakiongozwa na Diwani wa Chato Mheshimiwa Mange Luhomya, Madiwani wa Chato, karibuni sana sana karibuni sana ndugu zetu wa Chato. Wageni wengine 24 ni wenezi wa kata wakiongozwa na Mwenezi Kata ya Buziku ndugu Deogratius Didi Mwenezi hawa ndio majembe yenyewe haya, Waheshimiwa Wabunge mnaleta Makatibu, Wenyeviti mnasahau wenezi, wenezi ndio wenyewe, karibuni sana wenezi wa Kata za Jimbo la Chato, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni 102 ambao ni wajasiliamali wakiongozwa na Ndugu Suzana Isdory wale wageni walioongozana na Suzana Isdory simameni wote, karibuni sana sana sana karibuni mno. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Stephen Byabato Naibu Waziri wa Nishati ni kaka yake ndugu Fredy Mwesigwa, Fredy karibu sana yule kule ahsante. Wageni watatu wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi Naibu Waziri wa Maji ambaye ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam ndugu Moureen Balbina Salla na ndugu Careen Kapulima na ndugu Doreen Bahati karibuni sana wako pale. Lakini pia ninao kipekee wageni sita kutoka Benki ya *NMB* wakiongozwa na Meneja wa Kanda ya Kati ndugu yetu kijana wetu Nsolo Mlozi karibu sana, karibu sana Nsolo kijana maarufu mnamfahamu

ndio Meneja kanda ya Kati *NMB* na huwa anaandaa mashindano ya *Marathon* hapa Jijini Dodoma. (*Makofi*)

Lakini amefuatana na mwandamizi wateja wakubwa Hamisi Njapuka ahsante yupo na Mahusiano wateja wakubwa Joseph Edward ahsante yupo, Meneja Mahusiano wateja wakubwa Mathew Mandara ahsante, yupo na Meneja Mahusiano Makao Makuu Denis Vegulla bila kumsahau Meneja wetu Grace, ahsante sana Grace kwa kazi nzuri wakubwa wake msinune kwa sababu amepigiwa makofi mengi huyo ndio Meneja wetu sisi Waheshimiwa, ahsante Grace kwa kazi nzuri. (*Vicheko/Makofi*)

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Munde Tambwe na Jacqueline Kainja ambao ni wenyeviti na Makatibu wa *UWT* wa Wilaya pamoja na Makatibu wa *UWT* wa Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Katibu wa *UWT* Mkoa ndugu Hawa Siri, amakweli Wanyamwezi mmependeza karibuni sana sijui mmejipanga siku ngapi kuja hapa, halafu wamenijia na magauni ya kunikomesha mpaka kidole hakionekana marefu kweli kweli. Wananchokoza wananiambia haya Mheshimiwa Ndugai sema sasa leo hapa sina la kusema Wanyamwezi wangu. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Wilbard Kapori *UDOM* karibuni sana. Wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Kamonga ambao ni wapiga kura wake wanaoishi jijini Dodoma kutoka Rudewa Mkoani Njombe wakiongozwa na ndugu Stanley Gowele karibuni sana wale wa kutoka kule Rudewa. Wageni 20 wa Mheshimiwa Samwel Hhayuma ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* wanatoka Wilaya ya Hanang Mkoani Manyara wakiongozwa na ndugu Petro Yoke wale wa Hanang karibuni sana. Ama kweli yaani mtu anayesema nchi hii eti elimu sijui imefanyaje kila siku ninazidi kumshangaa. Yaani hawa wote Hanang tu, wamang'ati lakini wasomi wengi hongereni sana au *Wabarbaigi* naweza nikawa nimekosea kuwaita wamang'ati mnisamehe. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Asia Halamga ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Mipango kutoka jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Magdalena Boniface karibuni sana wale pale karibuni sana, mgeni wa Mheshimiwa Amsabi Mrimi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa *TCCIA*-Serengeti ndugu Bisare Ngocho yule pale karibu sana. Wageni wawili wa Mheshimiwa Assa Mekanika ambao ni wachungaji wa kanisa la *FAPCT* kutoka Mkoani Kigoma Mchungaji Yoram Masunzu na Mchungaji Damiani Yobegwa wale pale karibuni sana.

Basi baada ya matangazo hayo tuendeleo. Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**SPIKA:** Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani ili aweze kutuwasilishia hoja mbele yetu ya kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati mwaka 2021/2022. Mheshimiwa Waziri karibu sana tafadhali una nusu saa. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha hoja yangu ninaomba kumbukumbu zote za taarifa na hoja hii pamoja na viambatisho vyake viingie katika kumbukumbu za Bunge lako Tufuku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kutoa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi kupitia Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniamani kuendelea kuisimamia Sekta ya Nishati, nampa pole sana yeye na Watanzania wote kwa kuondokewa na Shujaa wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Awamu wa Tano tulimpenda sana lakini Mungu kampenda zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Awamu ya Nane wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge kwa kuendelea kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati Mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu kwa utendaji kazi wenu mahiri. Kipekee namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali Mbunge Wajumbe wote wa Kamati hiyo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri na maelekezo mnayonipatia katika kutekeleza kazi za Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Stephen Byabato Mbunge, Naibu Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kwa

karibu kutekeleza majukumu yangu. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Robert Masanja na Naibu Katibu Mkuu bwana Kheri Abdul Mahimbali kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli za Wizara yangu. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti, Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wanaonipatika katika kutekeleza malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo. Wazazi wangu na wananchi wote wa Jimbo la Chato naomba mtembee kifua mbele, kijana wenu niko imara katika kuwawakilisha, na kuwaahidi kuwa sitawaangusha nitaisimamia Wizara katika kutekeleza majukumu ya Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mke wangu kipenzi Mama Kalemani pamoja na watoto wangu wapendwa kwa kuendelea kuniombea, kunipa faraja na kunipatia ushirikiano katika kutekeleza malengo ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2020/21 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021. Bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/2021 ni jumla ya shilingi trilioni 2.197 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa shilingi trilioni 2.168 sawa na asilimia 98.7 ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa shilingi bilioni 28.4 sawa na asilimia 1.3 ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia mwezi Mei, 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trilioni 1.35 fedha hiyo ni sawa na asilimia 61.5 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa Maduhuli. Wizara ya Nishati katika mwaka 2020/2021 ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 160.62. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya shilingi bilioni 160.6 zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na shilingi milioni 20.4 kupitia shughuli za utawala. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2021, Wizara kupitia shughuli za TPDC ilikusanya shilingi bilioni 100.4 kutokana na shughuli za utafiti wa mafuta mauzo ya gesi asilia pamoja na shughuli za miamba, makusanyo hayo ni sawa na asilimia 63 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2020/2021 yalikuwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo Mradi wa Julius Nyerere *megawatt* 2,115 mradi wa Rusumo *megawatt* 80, Kinyerezi I *megawatt* 185 Ruhudji *megawatt* 358, Rumakali *megawatt* 222, Malagarasi *megawatt* 49.5, mradi wa umeme wa Jua *megawatt* 150, Umeme wa Upepo *megawatt* 200 na Makaa ya Mawe *megawatt* 600. Miradi mingine ni ujenzi wa njia mbalimbali za kusafirisha umeme.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Awamu ya Tatu wa mradi kabambe wa kupeleka umeme vijini pamoja na ujenzi wa Bomba la mafuta ghafi kusafirisha kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga Chongoreani mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati kutokana na utekelezaji wa maeneo hayo ni kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, fanikio la kwanza ni kuendelea na Ujenzi wa Mradi kimkakati na wa kielelezo wa Julius Nyerere wa *megawatt* 2,115 ambao hadi sasa napenda kutoka taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu umefikia asilimia 52 ya utekelezaji wake. Mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Juni mwakani 2022 na umeme wake kuunganishwa kwa Watanzania na kuanza kuutumia mara moja. Gharama ya mradi huu ni shilingi Trilioni 6.5 zilizotolea na Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Mkandarasi amelipwa shilingi trilioni 2.46 sawa na asilimia 100 kulingana na mpango kazi wake. Mafanikio ya pili ni kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa njia ya kuendesha treni ya kisasa ya mwendokasi kwa kutumia umeme al-maarufu *standard gauge*. Awamu ya kwanza ya urefu wa kilometa 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira Morogoro imekamilika kwa asilimia 100 toka mwezi Septemba mwaka jana. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 76.26. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa fedha za ndani kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huu kutaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kuendesha treni ya kisasa ya mwendokasi inayotumia umeme katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo na mafanikio ya tatu kuendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini na kuongeza vijiji vyenye umeme kutoka vijiji 2,018 sawa na asilimia 16 ya vijiji vilivyokuwa na umeme mwaka 2016 na kufikia vijiji 10,312 mwezi Mei, 2021 sawa na asilimia 86 ya vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, usambazaji huu wa umeme vijijini umeifanya Tanzania kushika nafasi ya kwanza Barani Afrika kufikisha umeme kwa kiwango hicho. Shirika la Umeme nchini kuanza kupata faida ya wastani wa shilingi milioni 53 kati ya mwaka 2018 na 2020 lakini pia kuanza kulipa gawio Serikalini kwa shilingi milioni 100.5 mwaka jana 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya tano ni kuondoa gharama kubwa wanazotozwa wananchi wa kawaida kuuziwa umeme kwa maana ya Ankara za umeme kutoka kwa wazalishaji wadogo wa umeme kutoka shilingi 3,500 au zaidi kwa *unit* moja hadi shilingi 100 kwa *unit* kama inavyofanywa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, elekezo hili lilitolewa mwaka jana na ninaomba nisisistize kwa mara nyingine ni marufuku wazalishaji wadogo wanaozalisha umeme na kuwauzia

wananchi zaidi ya shilingi 100 kwa *Unit* yapo maeneo ya Nyanyantakara yapo Visiwani, yapo Kyara Uvinza yapo Njombe na maeneo mengine, niwaagize wakandarasi na wanaozalisha umeme tabia hiyo wakome mara moja na wananchi wauziwe umeme kwa bei ya shilingi 100 kwa *unit*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* na *REA* kuendelea kuunganisha umeme wa wateja wa shilingi 27,000 katika maeneo yote vijijini na katika mitaa yote inayofanana na vijiji badala ya shilingi 177,000 ama zaidi. Serikali inaendelea kusisitiza kuwa imeondoa gharama ya kuuziwa nguzo kwa wateja wote nchini. Na hapa ninaomba nisisitize tena niwaagize wakandarasi na *TANESCO* ni marufuku kuwauzia nguzo wananchi wateja wa aina zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya saba ni kukamilika kwa majadiliano ya mkataba hodhi kati ya Serikali ya uwekezaji na kuanza taratibu za ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania. Mafanikio ya nane ni kuendelea na kukamilisha utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere unaonesha uwepo wa mafuta katika visima vitatu katika maeneo ya Luono, Iramba Singida, Kining'inila Igunga Tabora na Nyalanja Meatu Simiyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kupungua kwa matumizi ya mafuta ya taa kutoka wastani wa lita milioni moja kwa mwezi mwaka 2016/2017 hadi lita 450,000 mwaka 2021 kutokana na uwepo wa umeme vijijini. Mafanikio ya 10 ni kuongeza matumizi ya nguzo za zege katika njia za kusafirisha na kusambaza umeme kutoka takriban nguzo 3000 mwaka 2019/2020 kufikia zaidi ya nguzo 15,000 mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya 11 ni kuendelea na majadiliano yaliyosimama kwa muda mrefu ya ujenzi wa mradi wa kusindika gesi asilia na kuwa na kimiminika almaarufu LNG katika eneo la Likong'o Lindi kati ya Serikali yna wawekezaji. Majadiliano yanatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba mwaka huu 2021.



Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango 2021/2022 katika mwaka 2021/2022 Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza kipaumbele mbalimbali vikiwemo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini kufikia *megawatt* 5000 katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi mkubwa wa kimkakati na wa kielelezo wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 maeneo mengine ya kipaumbele yatakozizingatiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme, mradi wa *LNG* katika maeneo ya Likong'o Mkoani Lindi na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu wa mzunguko wa pili wa mradi wa kupeleka umeme vijijini almaarufu *REA III round I*. Mpango mahsusi katika mradi huu ni kuhakikisha kuwa vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara vinafikiwa na umeme ifikapo Desemba 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nirudie hili, mpango mahsusi wa REA inayoendelea kwa sasa ni kuhakikisha kuwa vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara vinafikiwa na umeme ifikapo Desemba, 2022 yaani mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere MW 2,115 katika kipindi cha mwaka 2021/2022 Serikali imetenga jumla ya shilingi trilioni 1.4 fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Juni 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022. Kukamilika kwa mradi huu pamoja na miradi mingine kutafanya nchi yetu kuwa na jumla ya takriban MW 5,000 kufikia mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho mahitaji yetu ya juu ya umeme yanatarajiwa kufikia takriban MW 2,677 hivyo kuwa na ziada ya umeme takriban MW 2,323 na kuweza kuuza umeme nje ya nchi na kuongeza mapato ya shirika. Aidha, Serikali itaweza kutekeleza azma yake ya kupunguza umeme na gharama za umeme kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Ruhuji – MW 358 katika mwaka 2021/2022 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kupatikana kwa mkandarasi wa ujenzi wa mradi lakini pia ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza Julai mwaka huu na kukamilika mwezi Juni 2024. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 407.4 sawa na takriban shilingi bilioni 958.25. Utekelezaji wa mradi huu utaenda Pamoja na mradi wa Rumakali utakaozalisha MW 222 kati ya mkoa wa Njombe Makete na Mbeya Busokelo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Malagarasi – MW 49.5 katika mwaka 2021/2022 kazi zitakazofanyika ni Pamoja na kumpata mkandarasi na kuanza ujenzi wa mradi Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya shilingi milioni 231.41 kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba mwaka huu 2021 na kukamilika ifikapo mwezi Septemba 2024. Gharama za utekelezaji wa Mradi ni Dola za Marekani milioni 138.1 sawa na takriban shilingi milioni 324.83.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300, Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 421.1 sawa na takriban shilingi bilioni 990.47. Mradi huu unaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 253 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu. Ujenzi wa mradi huu utaanza mwezi Agosti, 2022 na kukamilika mwezi Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa KV 132 kutoka Urambo Mkoani Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma. Mradi huu utahusisha ujenzi wa vituo vitatu vya kupoza umeme msongo wa kV 132 vya Urambo, Nguruka, Pamoja na Kidahwe pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Tabora. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 69.7 Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100. Mradi unatekelezwa na TANESCO kwa kutumia wataalamu wake wa ndani. Ujenzi wa mradi ulianza

mwezi Oktoba mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022.

Mheshimiwa Spika, mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kv 132 kutoka Tabora kupitia Katavi Ipole hadi Inyonga. Gharama za mradi huu ni shilingi milioni 64.5, mradi unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100. Aidha, ujenzi wa mradi utafanywa na TANESCO kwa Kutumia wataalam wake wa ndani. Gharama za mradi ya mradi ni bilioni 35.6. Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Oktoba 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Ibadakuli Shinyanga hadi Imalilo Mkoani Simiyu. Katika mwaka 2021/2022 Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.49 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2022. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 75 fedha za ndani kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme vya Handeni na Kilindi Mkoani Tanga utanza Julai mwaka 2021 yaani mwaka huu. Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini TANESCO katika kipindi cha mwaka 2021/2022 imetenga jumla ya shilingi bilioni 4.5. kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivyo vya kupoza umeme na Njia ya Kusafirisha Umeme. Ujenzi wa miradi hii utakamilika mwezi Juni 2023. Gharama ya miradi ni shilingi bilioni 19.71.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini, hadi kufikia mwezi Mei 2021 vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme ni 1956 sawa na asilimia 14 ya vijiji vyote vya Tanzania Bara. Vijiji hivyo vilivyobaki vitapelekewa umeme kupitia mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini Awamu ya Tatu mzunguko wa pili. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi mwaka huu wa 2021 na gharama ya mradi ni trilioni 1.24. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2022.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huu kutafanya vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara kufikiwa na nishati ya umeme. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba tumetoa namba za wakandarasi wote ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatafuta na kuwapata tutaweka kwenye *pigeon hall* lakini tutaendelea pia kuweka mwenye mitandao yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ujazilizi Katika Vitongoji Mzunguko wa Pili (*Densification* IIA na IIB). Miradi hii inalenga kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Miradi hii itahusisha kupeleka umeme katika vitongoji Zaidi ya 3,000 na kuunganisha jumla ya wateja wa awali wapatao 17,000.

Mheshimiwa Spika, gharama ya miradi ni shilingi bilioni 366.32, gharama ya miradi hii katika awamu hii ya *Densification* IIA Pamoja na IIB itakamilika katika mwaka 2020 mwezi Septemba tarehe 24. Miradi inayokwenda kutekelezwa katika awamu hii ni pamoja na *Densification* IIB mikoa iliyobaki 11 ambayo utekelezaji wake utanza mwezi Julai 2021 na kukamilika mwezi Juni 2022.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kusambaza Umeme katika Maeneo yaliyo Pembezoni mwa Miji (Vijiji Miji) almaarufu *Peri Urban*.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Peri - Urban* unalenga kusambaza umeme katika maeneo, vitongoji na mitaa iliyopo pembezoni mwa majiji, manispaa, halmashauri za miji, mikoa na yenye uhitaji mkubwa wa umeme ambayo maeneo hayo yanashabihiana sana na tabia ya kivijijini. Gharama ya kuunganisha umeme katika maeneo hayo ni shilingi 27,000. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 160 na mradi unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa kikanda na Kimataifa kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo wote, Jumuiya na nchi wahisani

ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kupitia bajeti ya mwaka 2021/2022 Wizara ya Nishati itahakikisha inazalisha umeme wa kutosha wa uhakika unaotabirika na wenye gharama nafuu. Katika mwaka 2021/2022 Wizara ya Nishati inakadiria kutumia jumla ya shilingi trilioni 2.386 ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.197 iliyotengwa mwaka 2020/2021. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 8. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liridhie bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 2,358,980,809,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo ni kama ifuatavyo; shilingi trilioni 2,358,756,128,000 sawa na asilimia 98.9 ya bajeti yote ya Wizara kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha hizo shilingi trilioni 2,178,756,128,000 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 180 ni fedha za nje. Pili shilingi bilioni 27,224,681,000 sawa na asilimia 1.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kati ya fedha hizo shilingi bilioni 15,025,821,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 12,198,860,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa sana naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**HOTUBA YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI MHE. DKT.  
MEDARD MATOGOLO CHANJA KALEMANI AKIWASILISHA  
MAKADIPIO NA MAPATO YA MATUMIZI YA WIZARA YA  
NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2021/2022 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. *Mheshimiwa Spika***, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/21 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2021/22.

**2. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kutoa taarifa ya utekelezaji wa Serikali kupitia Sekta ya Nishati. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali.

**3. Mheshimiwa Spika**, tarehe 17 Machi, 2021 Taifa lilimpoteza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naungana na Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kutoa pole kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Mke wa Hayati Mama Janeth Magufuli, Watoto, ndugu, jamaa, marafiki na watazania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Shujaa wetu, tulimpa lakini Mungu alimpa zaidi. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Hayati mahali pema peponi, Amina.

**4. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa maelekezo yake thabiti ambayo yameendelea kuniwezesha kuisimamia vema Sekta ya Nishati. Ni dhahiri kuwa Rais wetu amekuwa chachu katika kuendelea kutekeleza mipango mikubwa na yenye tija katika Sekta ya Nishati hapa nchini.

**5. Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali

Mwinyi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Awamu ya Nane wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, nampongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa kuendelea kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Sita.

**6. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kusimamia Sekta ya Nishati. Nikiri kuwa maelekezo na miongozo ya viongozi hawa ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati.

**7. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kuiongoza Wizara ya Nishati. Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri walioteuliwa na walioaminiwa kuendelea na nafasi zao. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

**8. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati Mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu kwa utendaji kazi wenu mahiri. Napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Makamu Mwenyekiti Mhe. Seif Khamis Gulamali (Mb.), na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na maelekezo wanayoendelea kutupatia katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

**9. Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kuendelea kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Leonard Robert Masanja na Naibu Katibu Mkuu Bw. Kheri Abdul

Mahimbali kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku za Wizara. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha malengo ya Wizara.

**10. Mheshimiwa Spika**, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo. Wazazi wangu na wananchi wote wa Jimbo la Chato naomba mtembee kifua mbele, kijana wenu niko imara katika kuwawakilisha, na ninaahidi kuwa sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nanyi katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu la Chato. Naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mke wangu Mama Kalemani pamoja na watoto wangu kwa kuendelea kuniombea, kunipa faraja na ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa.

**11. Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2020/21 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/22.

## **B. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/21**

### ***Bajeti na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/21***

**12. Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/21 ni jumla ya **Shilingi Trilioni 2.197** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa **Shilingi Trilioni 2.168** sawa na **asilimia 98.7** ya bajeti yote ya Wizara na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa **Shilingi bilioni 28.4** sawa na **asilimia 1.3** ya bajeti yote ya Wizara.

**13. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei, 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 1,350.43** Kiasi hicho



kilichopokelewa na Wizara ni sawa na **asilimia 61.5** ya bajeti yote ya Wizara.

***Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali***

**14. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Nishati katika mwaka 2020/21 ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 160.62**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi bilioni 160.6** zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na **Shilingi milioni 20.4** kupitia shughuli za utawala. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2021, Wizara kupitia shughuli za TPDC za utafiti wa mafuta na mauzo ya gesi asilia imekusanya **Shilingi bilioni 100.4**. Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 63** ya lengo.

**C. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21**

**15. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/21, maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati yalikuwa ni pamoja na: kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo: Julius Nyerere (**MW 2,115**), Rusumo (**MW 80**), Kinyerezi I – *Extension* (**MW 185**), Ruhudji (**MW 358**), Rumakali (**MW 222**), Malagarasi (**MW 49.5**), Umeme wa Jua (**MW 150**), Umeme wa Upepo (**MW 200**), JotoArdhi (**MW 200**), Makaa ya Mawe (**MW 600**); ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ikiwemo Singida – Arusha – Namanga **kV 400**, *North – West Grid Extension* (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi) **kV 400**, Rufiji – Chalinze – Dodoma **kV 400**, Chalinze – Kinyerezi **kV 400**, Geita – Nyakanazi **kV 220**, Rusumo - Nyakanazi **kV 220**, Bulyanhulu – Geita **kV 220**, Tabora – Kigoma **kV 132**, Tabora – Katavi **kV 132**, Ibadakuli – Imalilo **kV 220**; na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini.

**16. Mheshimiwa Spika**, maeneo mengine ya kipaumbele yalikuwa ni pamoja na: Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania; kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG); kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia; kuvutia

uwekezaji katika Sekta ya Nishati; na kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi chini ya Wizara ili kuongeza ufanisi katika Sekta ya Nishati.

#### D. MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

**17. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati kutokana na utekelezaji wa maeneo hayo ya kipaumbele ni pamoja na:

(i) Kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHP) **MW 2,115** ambao hadi kufikia mwezi Mei, 2021 utekelezaji wake kwa ujumla umefikia **asilimia 52**;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo **MW 80** ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 80** na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Ruhudji (**MW 358**) na Rumakali (**MW 222**);

(iii) Kukamilika kwa Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme msongo wa **kV 220** kutoka Bulyanhulu hadi Geita yenye urefu wa kilomita 55 ambao ulikamilika mwezi Septemba, 2020 na kuunganisha umeme vijiji takriban 10 katika Wilaya ya Geita vinavyopitiwa na mradi huo;

(iv) Kukamilika kwa ujenzi wa Mradi wa Njia ya Kuendesha Treni ya Kisasa ya Mwendokasi ya kutumia umeme (*Standard Gauge Railway – SGR*). Awamu ya Kwanza yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro ilikamilika mwezi Septemba, 2020 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 76.26** kwa fedha za ndani kwa **asilimia 100**. Kukamilika kwa mradi huu kutaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kuanza kuendesha treni ya kisasa ya mwendokasi ya kutumia umeme katika nchi za Afrika Mashariki;

(v) Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji **10,312** vimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na vijiji **2,018** vilivyokuwa vimeunganishwa umeme mwaka 2015 sawa na ongezeko la vijiji **8,294** sawa na **asilimia 86** ya vijiji vya Tanzania Bara vimepata umeme;

(vi) Kuendelea kuhamasisha na kusisitiza uzalishaji wa vifaa vya kujenga miradi ya umeme nchini na kuzuia uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, mashineumba (transfoma), nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo na kuokoa takriban **Shilingi bilioni 162.23**. Uzalishaji huo pia umechangia ongezeko la ajira nchini ambapo takriban Watanzania wapatao 22,820 wameajiriwa katika viwanda hivyo kati ya mwaka 2017 hadi sasa;

(vii) Kuendelea kuunganisha umeme wateja wapya nchini kwa kasi ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya Watanzania wanaonufaika na huduma ya umeme wamefikia takriban **milioni 47** sawa na **asilimia 78** ya Watanzania wapatao **milioni 60**;

(viii) Kuondoa hasara za Shirika la TANESCO zilizokuwepo za **Shilingi bilioni 349** katika kipindi cha miaka 2015-2017. Hasara hizi, pamoja na mambo mengine zilizotokana na kutumia mafuta mazito na kuagiza vifaa kutoka nje ya nchi;

(ix) Kuondoa gharama kubwa wanazotozwa wananchi wa kawaida za kuuziwa umeme na wazalishaji wadogo kutoka **Shilingi 3,500** au zaidi kwa uniti moja ya umeme hadi **Shilingi 100** kwa uniti kama inavyotozwa na TANESCO. Utekelezaji wa agizo hili ulianza mwaka 2019/20;

(x) Kuongezeka kwa mapato ya Shirika la TANESCO kutoka wastani wa **Shilingi bilioni 72** kwa mwezi mwaka 2016 kufikia wastani wa **Shilingi bilioni 160** kwa mwezi mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la takriban **asilimia 102**. Ongezeko hili pia limetokana na kutumia mfumo wa LUKU wa kulipa ankara za umeme kwa wateja wote nchini;

(xi) Kuongeza kasi ya kufuatilia madeni sugu ya wateja wa TANESCO na kupungua kwa madeni haya kutoka **Shilingi bilioni 272** mwaka 2017 kufikia **Shilingi bilioni 48.9** mwaka 2020;

(xii) Shirika la TANESCO kuendelea kujitegemea na kuendesha shughuli zake bila kupata ruzuku ya takriban **Shilingi bilioni 143** kwa mwaka kutoka Serikalini;

(xiii) Serikali kupitia TANESCO na REA kuendelea kuunganisha umeme kwa **Shilingi 27,000** katika maeneo yote ya vijijini ikiwa ni pamoja na Mitaa katika Majiji na Manispaa (Vijiji Miji) kulingana na Mpango wa Kupeleka Umeme Vijijini; tofauti na ilivyokuwa huko nyuma ambapo wateja wa aina hii walikuwa wanaunganishwa kwa **Shilingi 177,000** au zaidi;

(xiv) Kuongeza matumizi ya nguzo za zege katika kujenga njia za kusafirisha umeme katika baadhi ya maeneo yenye mahitaji hayo. Aidha, viwanda vya ndani vya kuzalisha nguzo za zege vimeongezeka kutoka kimoja (1) mwaka 2018 na kufikia vitano (5) vinavyozalisha zaidi ya nguzo **15,000** kwa mwaka;

(xv) Kukamilika kwa majadiliano na kusainiwa kwa Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (*Host Government Agreement – HGA*), Mkataba wa Ubia (*Shareholding Agreement – SHA*) na kuanza taratibu za ujenzi wa mradi wa EACOP;

(xvi) Kuimarika kwa shughuli za kaguzi za gharama za uwekezaji na mapato yatokanayo na uzalishaji wa gesi asilia (*PSA Audit*) na kuokoa **Shilingi bilioni 26.45** kwa kaguzi zilizofanyika mwaka 2019 na 2020 ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 10.14** zilizookolewa kwa kaguzi zilizofanyika kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2018;

(xvii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi asilia hadi kufikia **Futi za Ujazo bilioni 56.13** kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2020 hadi mwezi Mei, 2021 ikilinganishwa na **Futi za Ujazo bilioni 53.10** kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la **asilimia 6**;

(xviii) Kuendelea na utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambao umeonesha viashiria vya uwepo wa mafuta au gesi asilia katika visima vifupi vitatu (3)

vilivyochorongwa katika maeneo ya Luono – Iramba (Singida), Kining'inila – Igunga (Tabora) na Nyalanja – Meatu (Simiyu);

(xix) Kukamilika kwa mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia yenye urefu wa kilomita 27.1 na uwezo wa kuunganisha nyumba zaidi ya 10,000 na viwanda vipya zaidi ya 20 katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara hivyo kufanya usambazaji wa gesi viwandani kufikia viwanda 50. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 mtandao wa usambazaji wa gesi asilia umeongezeka hadi kufikia kilomita **129.6** ilikinganishwa na kilomita **102.5** za mwezi Juni, 2020 sawa na ongezeko la **asilimia 26.4**;

(xx) Kuendelea na uunganishaji wa wateja wa gesi asilia kufikia nyumba **1,191** mwezi Juni, 2021 ikilinganishwa na nyumba **500** zilizofikiwa mwezi Juni, 2020 sawa na ongezeko la **asilimia 138.2**. Zaidi ya magari **700** yamefungwa mfumo wa matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na magari **400** yaliyofungwa mfumo huo kufikia mwezi Juni, 2020 sawa na ongezeko la takriban **asilimia 75**;

(xxi) Kuongezeka kwa uhakika wa upatikanaji wa mafuta ya ziada nchini kutoka lita **milioni 160** zinazotosheleza kwa siku 15 hadi kufikia lita **milioni 420** zinazotosheleza kwa siku zaidi ya 32;

(xxii) Kupungua kwa siku za meli kusubiri (*demurrage*) kushusha mafuta kutoka wastani wa siku 75 kwa mwaka 2015 hadi wastani wa siku tano (5) kwa sasa na hivyo kupunguza gharama za *demurrage* kutoka wastani wa **Dola za Marekani 45** kwa tani hadi wastani wa **Dola za Marekani 3.6** kwa tani. Hivyo, kuokoa wastani wa takriban **Shilingi bilioni 320** kila mwaka;

(xxiii) Kupungua kwa matumizi ya mafuta ya taa, hususan vijijini kutoka lita **milioni 1** kwa mwezi mwaka 2016/17 hadi lita **laki 4.5** mwaka 2020/21 kutokana na kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme vijijini; na

(xxiv) Kuongezeka kwa matumizi ya gesi ya mitungi (*Liquefied Petroleum Gas - LPG*) nchini kutoka **tani 106,301** mwaka 2019 hadi kufikia **tani 171,828** mwaka 2020 sawa na ongezeko la **asilimia 61.64**.

#### **E. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA 2020/21 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22**

**18. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/22, Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza vipaumbele mbalimbali vikiwemo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini kufikia **MW 5,000** katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati na ya kielelezo ya Julius Nyerere (**MW 2,115**), Ruhudji (**MW 358**) na Rumakali (**MW 222**) pamoja na miradi mingine ya Kinyerezi I - *Extension* (**MW 185**), Rusumo (**MW 80**), Malagarasi (**MW 49**), Mtwara (**MW 300**) na Somanga Fungu (**MW 330**).

**19. Mheshimiwa Spika**, pamoja na miradi hiyo ya uzalishaji umeme, Serikali pia itaendelea kutekeleza miradi ya kuimarisha mifumo ya usafirishaji umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa kusafirisha umeme wa: *North - West Grid Extension* **kV 400**; Singida – Arusha – Namanga **kV 400**; Rufiji - Chalinze – Dodoma **kV 400**; Chalinze – Kinyerezi **kV 400**; Rusumo – Nyakanazi **kV 220**, Geita – Nyakanazi **kV 220**; Ibadakuli (Shinyanga) – Imalilo (Simiyu) **kV 220**; Tabora – Kigoma **kV 132**; na Tabora – Katavi **kV 132**; pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Handeni na Kilindi mkoani Tanga.

**20. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/22 maeneo mengine ya kipaumbele yatakayozingatiwa na Wizara ni: kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa pili wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini; kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania; Mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG); Utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu

vya kimkakati vikiwemo Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi Wembere; kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia; kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati; na kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara (TANESCO, TGDC, REA, TPDC, PURA na PBPA) ili kuongeza ufanisi katika Sekta ya Nishati.

**21. Mheshimiwa Spika**, pamoja na maeneo hayo ya kisekta, Wizara pia itazingatia maeneo mengine yanayolenga kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na: kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta; kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi ili kutoa huduma bora; na kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya nishati.

## **SEKTA NDOGO YA UMEME HALI YA UPATIKANAJI UMEME NCHINI**

**22. Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa imefikia **MW 1,573.65** kati ya hizo **MW 573.70** zinatokana na vyanzo vya maji, **MW 901.32** gesi asilia na **MW 10.50** tungamotaka (*Biomass*). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia **asilimia 86.57** na mitambo ya wazalishaji binafsi (*IPP/SPPs*) ambayo huchangia **asilimia 13.43**. TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa yenye uwezo wa kuzalisha **MW 32.21** na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia **MW 1,605.86**.

**23. Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya juu ya umeme yameendelea kuongezeka na kufikia **MW 1,183.28** sawa na ongezeko la **asilimia 2.75** ikilinganishwa na **MW 1,151.66** ya mwaka 2019/20. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya urefu wa njia za kusafirisha umeme umefikia kilomita **6,111.27** sawa na ongezeko la **asilima 25.94** ikilinganishwa na kilomita **4,852.7** za mwaka 2015/16. Kati ya hizo, njia za msongo wa **kV 400** ni kilomita **670**; **kV 220** ni kilomita **3,225.7**; **kV 132** ni kilomita

**1,672.57**; na **kV 66** ni kilomita **543**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 miundombinu ya usambazaji umeme imeendelea kuongezeka na kufikia jumla ya kilomita **147,156.80** sawa na ongezeko la **asilimia 139.77** ikilinganishwa na kilomita **61,373.76** zilizokuwa zimefikwa mwezi Juni, 2015. Kati ya hizo, njia za msongo wa **kV 33** ni kilomita **47,106.07**, msongo wa **kV 11** ni kilomita **12,457.21** na msongo wa **kV 0.4** ni kilomita **87,593.52**.

## MIRADI YA KUZALISHA UMEME

### *Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115*

**24. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kimkakati na wa kielelezo wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere *Hydro Power Project (JNHPP)* utakaozalisha **MW 2,115** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Gharama za mradi huu ni **Shilingi trilioni 6.55** zinazotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**.

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha uchimbaji na ujenzi wa handaki la kuchepusha maji ya Mto Rufiji (*diversion tunnel*), kuendelea na ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*), ujenzi wa kituo cha kuzalishia umeme (*Power House*) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (*Switch yard*). Hadi kufikia mwezi Mei, 2021, jumla ya **Shilingi trilioni 2.495** zimelipwa kwa mkandarasi sawa na **asilimia 100** ya fedha iliyotakiwa kulipwa kulingana na hatua ya utekelezaji wa mradi iliyofikiwa.

**26. Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla utekelezaji wa mradi katika maeneo muhimu matano (*critical path*) hadi kufikia mwezi Mei, 2021 umefikia wastani wa **asilimia 52**. Hadi sasa jumla ya wafanyakazi **7,243** wameajiriwa. Kati ya wafanyakazi hao; **6,452** ni Watanzania sawa na **asilimia 89.1** na kutoka nje ya nchi ni **791** sawa na **asilimia 10.9**.

**27. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi ambapo kazi



zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea na kukamilisha: ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*); ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*); ujenzi wa kituo cha kuzalishia umeme (*Power House*); na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (*Switch yard*). Jumla ya **Shilingi trilioni 1.4** fedha za ndani zimetengwa katika mwaka 2021/22 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Juni, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.

**28. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi huu pamoja na miradi mingine kutafanya nchi yetu kuwa na jumla ya takriban **MW 5,000** kufikia mwaka 2025. Katika kipindi hicho mahitaji yetu ya juu ya umeme yanatarajiwa kufikia **MW 2,677** hivyo kuwa na ziada ya takriban **MW 2,323** na kuweza kuuza umeme nje ya nchi na kuongeza mapato ya Shirika. Aidha, Serikali itaweza kutekeleza azma yake ya kupunguza bei za umeme kwa wananchi.

#### ***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Ruhudji – MW 358***

**29. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 358** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji mkoani Njombe hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 407.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 958.25** na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** unaokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 53.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 125.13**. Katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kuhuisha Upembuzi Yakinifu (*Update of Feasibility Study*) wa mradi na kuandaa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kujenga mradi.

**30. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kusaini mkataba wa ujenzi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 65.60** zimetengwa katika mwaka 2021/22 ili kutekeleza kazi hizo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 45.00** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 20.60** ni fedha za nje. Ujenzi wa mradi

unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2021 na kukamilika mwezi Julai, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rumakali – MW 222***

31. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 222** kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 150 kutoka katika mitambo hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Gharama za mradi huu kwa pamoja zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 388.22** sawa na takriban **Shilingi bilioni 913.14**. Katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kuhisha Upembuzi Yakinifu wa mradi na kuandaa makabrasha ya kumpata mkandarasi wa kujenga mradi.

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kusaini mkataba wa ujenzi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 30.03** zimetengwa katika mwaka 2021/22 ili kutekeleza kazi hizo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 10.00** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 20.03** ni fedha za nje. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo – MW 80***

33. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 80** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera. Mradi huu unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda. Kwa upande wa Tanzania mradi unahusu pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa **kV 220** kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za mradi wa kuzalisha umeme kwa upande wa Tanzania ni **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 265.9** kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

34. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa: uchimbaji wa eneo la kusimika

mitambo (*power house*); milango ya kuingiza na kuchepusha maji (*spillway and intake gates*); na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi. Aidha, kazi zinazoendelea ni pamoja na: uchimbaji wa handaki la kupitishia maji; ufungaji wa mitambo; na ujenzi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (*switch yard*). Hadi sasa utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 80**.

**35. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2021/22 ni kukamilisha: uchimbaji wa handaki la kupitishia maji; ufungaji wa mitambo; ujenzi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (*switch yard*); na utekelezaji wa miradi ya kijamii kwa upande wa Tanzania. Fedha za nje **Shilingi bilioni 3.85** zimetengwa katika mwaka 2021/22 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185***

**36. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I – **MW 150** kwa kujenga mitambo itakayozalisha **MW 185** na hivyo kufanya kituo kuzalisha jumla ya **MW 335**. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 435.48**. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi hadi sasa umefikia **asilimia 84**.

**37. Mheshimiwa Spika**, hata hivyo; kutokana na Mkandarasi (M/s Jacobsen Elektro AS ya Norway) aliyepewa kazi hiyo kushindwa kutekeleza mradi ipasavyo taratibu za kumpata Mkandarasi mpya wa kumalizia kazi zipo katika hatua za mwisho. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 88.58** zimetengwa katika mwaka 2021/22 kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi huu. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Mei, 2022.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Malagarasi – MW 49.5***

**38. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 49.5** kwa kutumia maji ya Mto

Malagarasi Mkoani Kigoma. Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 53.8 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe mkoani Kigoma. Gharama za utekelezaji wa Mradi ni **Dola za Marekani milioni 138.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 324.83**. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: upatikanaji wa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi; ulipaji wa fidia kwa wananchi; kukamilika kwa usanifu wa awali wa mradi (*basic design*); na kukamilisha Maboresho ya Andiko la Mazingira.

**39. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kumpata Mtaalam Mshauri na Mkandarasi wa ujenzi wa mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi milioni 231.41** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2021 na kukamilika mwezi Septemba, 2024.

#### ***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kakono – MW 87***

**40. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 87** kwa kutumia maji ya Mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** kutoka Kakono hadi Kyaka yenye urefu wa kilomita 38.5 pamoja na ukarabati wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka. Gharama za ujenzi wa mradi ni **Dola za Marekani milioni 287.6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 676.47** zitakazotolewa na Serikali, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).

**41. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, kazi zilizokamilika ni pamoja na: usanifu wa awali (*basic design*) wa mradi; na uandaaji wa makabrasha kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi. Kazi zinazoendelea ni pamoja na: kukamilisha taratibu za fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuhuisha taarifa za kimazingira.

**42. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha taratibu za ufadhili; kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi milioni 150** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kikonge – MW 300***

**43. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuhu mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 53 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Jumla ya gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 750** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.76**.

**44. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizofanyika hadi sasa ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu ikiwa ni pamoja na: kukamilisha Tathmini ya Mazingira na Jamii (*Strategic Environmental & Social Assessment – SESA*). Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kumpata Mtaalam Mshauri wa kusimamia mradi na Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.04** fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2022 na kukamilika mwezi Desemba, 2025.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300***

**45. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia gesi asilia katika Mkoa wa Mtwara. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 421.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 990.47**. Mradi huu unaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 253 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu.

**46. Mheshimiwa Spika**, hadi sasa kazi zilizokamilika ni pamoja na: kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme; na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika miundombinu wezeshi. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni: kuanza kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kukamilisha taratibu za ufadhili wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi milioni 50** kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2022 na kukamilika mwezi Agosti, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Somanga Fungu – MW 330***

**47. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 330** kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Somanga Fungu Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 423** sawa na takriban **Shilingi bilioni 994.94**. Mradi huu unaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 253 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi. Kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Mazingira na Jamii. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2021/22 ni pamoja na: kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kukamilisha taratibu za ufadhili. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2023 na kukamilika mwezi Desemba, 2025.

***Miradi ya Kuzalisha Umeme ya Nishati Jadidifu (Umeme Jua – MW 150, Upepo – MW 200 na Makaa ya Mawe – MW 600)***

**48. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na taratibu za kuwapata Wawekezaji Binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme wa jumla ya **MW 950** kwa kutumia jua, upepo na makaa ya mawe. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni: kukamilisha tathmini ya zabuni kwa kampuni 11 zilizorudisha zabuni kati ya 38 zilizopita mchujo wa kwanza na kupata kampuni sita (6) zilizokidhi vigezo baada ya mchujo wa mwisho; na kuwasilisha maombi ya ridhaa (*No Objection*)

toka Serikalini kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuanza majadiliano na wawekezaji hao.

**49. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/22 kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kuanza majadiliano ya: mikataba ya mauziano ya umeme (*Power Purchase Agreements – PPAs*); mikataba ya utekelezaji wa mradi (*Implementation Agreements – IAs*); na kufanya tathmini ya uwezo (*Due Diligence*) wa wawekezaji waliofuzu kutekeleza miradi hii. Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2021 na kukamilika mwezi Julai, 2023.

#### **MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME**

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji, Chalinze hadi Dodoma***

**50. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni mahususi kwa ajili ya kusafirisha umeme utakaozalishwa katika mradi wa kielelezo wa JNHPP (**MW 2,115**). Mradi unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 505 kutoka Rufiji kupitia Chalinze Mkoani Pwani hadi Dodoma. Aidha, mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Dodoma. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa ni **Dola za Marekani milioni 192.67** sawa na takriban **Shilingi bilioni 453.18**.

**51. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha Tathmini ya Athari ya Mazingira na Jamii na kupata hati ya mazingira; kuandaa na kutangaza zabuni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze; kuanza kazi ya kusafisha mkuza wa njia ya kusafirisha umeme; na kukamilisha uthamini wa fidia ya mali za wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 8.2** zimetolewa kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi wa mradi huu.

**52. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi

watakaopisha mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 180** fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2022.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Kinyerezi hadi Chalinze***

**53. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 93 kutoka Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Chalinze, Pwani pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 66.34** sawa na **Shilingi bilioni 156.04**.

Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuandaa zabuni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi hadi Chalinze; kukamilisha uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi; na kuanza kulipa fidia ambapo **Shilingi bilioni 29.4** zimetolewa kwa ajili ya kazi hiyo.

**54. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na: kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi hadi Chalinze; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi. Jumla ya **Shilingi bilioni 40** fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2022.

***Mradi wa Njia ya Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita***

**55. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulihusu: ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita na kituo cha kupoza umeme cha Geita; upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Bulyanhulu; ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme msongo wa **kV 33** katika Vijiji 10 vinavyopitiwa na mradi; na kuunganisha wateja wapya zaidi ya 1,500 katika Mkoa wa



Geita. Mradi huu umegharimu **Dola za Marekani milioni 23** sawa na takriban **Shilingi bilioni 54.1**. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Januari, 2019 na umekamilika kwa **asilimia 100** na umeme kuwashwa mwezi Septemba, 2020.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 ya Geita – Nyakanazi***

**56. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu: ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi; na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi maeneo ya Geita hadi Bwanga, Nyakanazi hadi Kakonko. Gharama ya mradi huu ni **EURO milioni 45** sawa na takriban **Shilingi bilioni 127**.

**57. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na: ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambao umefikia **asilimia 64**; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita ambao umefikia **asilimia 65.7**; na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia zaidi ya **asilimia 51.6**.

**58. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2021/22 ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita kupitia Bwanga, Chato hadi Nyakanazi; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; na kuendelea na kazi ya kusambaza umeme katika vijiji 32 vitakavyopitiwa na mradi. Fedha za nje **Shilingi bilioni 20.33** zimetengwa kwa ajili ya shughuli za mradi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Agosti, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2021.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga***

**59. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa

kilomita 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha. Mradi unahusisha ujenzi wa kituo kipyua cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo Mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Singida na usambazaji wa umeme katika vijiji 19 vilivyo jirani na mkuza wa njia ya umeme kwenye mkoa ya Singida, Manyara na Arusha. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na takriban **Shilingi bilioni 608.77**.

**60. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na: kukamilisha zoezi la ulipaji wa fidia katika vijiji vyote 82 vilivyopitiwa na mradi; kuendelea na shughuli za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme mjini Arusha na Singida; na kuendelea na usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 91.6**.

**61. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zilizopangwa kufanyika ni kukamilisha shughuli za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 10.21** fedha za nje zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2021.

### ***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 Rusumo – Nyakanazi***

**62. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 94 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 35** sawa na takriban **Shilingi bilioni 82.32**. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**63. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi; kukamilisha upimaji wa kina (*Detail Survey*); usanifu wa mradi; na ujenzi wa misingi na usimikaji wa nguzo. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 46**. Katika mwaka 2021/22 kazi itakayofanyika ni kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Mradi huu ulianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2021.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma***

**64. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme vijijini. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 187** sawa na takriban **Shilingi bilioni 439.84** na zinatolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Exim ya Korea Kusini (EDCF) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**65. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ulipaji wa fidia katika eneo la Kidahwe; kukamilisha kazi ya upimaji na kufanya tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambapo **Shilingi bilioni 2.6** zimetolewa kwa ajili ya malipo kwa wananchi 3,220 watakaopisha mradi; kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi Mjenzi na Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kuandaa zabuni ya vituo vya kupoza umeme; na kuanza ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme.

**66. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kuendelea kulipa fidia wananchi watakaopisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme; kuanza ujenzi wa mradi; na kuanza usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni**

**14.06** fedha za nje zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2023.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga***

**67. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 624. Mradi huu utahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga. Mradi huu unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za kusini mwa Afrika kupitia *Southern African Power Pool (SAPP)*. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 595** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.4** ambazo zitatolewa na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**68. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kupitia na kuhuisha taarifa zilizoandaliwa awali kuhusu mazingira; kukamilisha mpango wa kuhamisha wananchi wanaopisha mradi (*Resettlement Action Plan – RAP*) katika maeneo ya Iringa hadi Mbeya; na kuandaa zabuni kwa ajili ya kuwapata Mtaalam Mshauri na Mkandarasi Mjenzi wa mradi.

**69. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na: ulipaji wa fidia wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha tathmini ya athari kwa mazingira; kukamilisha mpango wa kuhamisha wananchi wanaopisha mradi (*Resettlement Action Plan – RAP*) katika maeneo ya Mbeya hadi Sumbawanga; kuwapata Mtaalam Mshauri wa kusimamia ujenzi wa mradi na Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2022 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga – Mpanda – Kigoma***

**70. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilomita 480. Mradi huu unatarajiwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 200** sawa na takriban **Shilingi bilioni 470.42**. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni kuendelea na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayehuisa Upembuzi Yakinifu na kuandaa taarifa ya mazingira. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu na kukamilisha taratibu za ufadhili wa mradi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2022 na kukamilika mwezi Oktoba, 2024.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma kupitia Urambo na Nguruka***

**71. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 395 kutoka Tabora hadi Kigoma na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme msongo wa **kV 132/33** vya Urambo, Nguruka, Kidahwe pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Tabora. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 69.7** na unagharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100**. Vilevile, mradi huu unatekelezwa na TANESCO kwa kutumia wataalamu wake wa ndani.

**72. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi kwa maeneo kati ya Tabora na Urambo; kukamilisha ujenzi wa majengo ya vituo vya kupoza umeme vya Urambo na Nguruka kwa **asilimia 100**; kuanza zoezi la uthamini kutoka Urambo hadi Kigoma (Kidahwe); na kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme.

**73. Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2021/22 ni: kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; kulipa

fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwenda Kigoma kutokea Tabora. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 12.6** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Mradi ulianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga***

**74. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** kutoka Tabora hadi Katavi yenye urefu wa kilomita 381 pamoja na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme msongo wa **kV 132/33** vya Ipole, Inyonga na Mpanda. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 64.5**. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100**. Aidha, ujenzi wa mradi utafanywa na TANESCO kwa kutumia wataalamu wake wa ndani.

**75. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha zoezi la Upembuzi Yakunifu wa awali; uwekaji wa alama katika njia ya kusafirisha umeme (*Route survey and demarcation*); tathmini ya athari za mazingira (*Environment Impact Assessment – EIA*); na kukamilisha majengo ya vituo vya Ipole, Inyonga na Mpanda kwa **asilimia 100**; na kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme. Kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2021/22 ni: kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwenda Katavi kutokea Tabora. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 35.6** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Mradi ulianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023.

***Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme cha Imalilo katika Mkoa wa Simiyu***

**76. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita

109 kutoka Ibadakuli Mkoani Shinyanga hadi Imalilo Mkoani Simiyu pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Imalilo na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ibadakuli. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 75** utakaogharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100**. Mradi huu unajengwa na TANESCO kwa kutumia wataalamu wake wa ndani.

**77. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha usanifu wa awali wa kituo cha kupoza umeme cha Imalilo na upimaji wa njia kutoka Shinyanga hadi Simiyu kwa **asilimia 100**; kuanza taratibu za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme; na kuanza Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii. Katika mwaka 2021/22, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 1.49** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2022.

### ***Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme vya Handeni na Kilindi Mkoani Tanga***

**78. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenye uwezo wa **MVA 20, kV 132/33** katika Wilaya ya Handeni na kitahusisha pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 46.8 kutoka Mkata hadi Handeni. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 8.38** sawa na takriban **Shilingi bilioni 19.71**. Wilaya ya Kilindi inatarajiwa kupata umeme wa Gridi kupitia kituo cha kupokelea umeme (*switching station*) itakayojengwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kijungu kinachotarajiwa kujengwa mpakani mwa mikoa ya Tanga na Manyara. Gharama ya ujenzi wa kituo cha kupokelea umeme zinatarajiwa kuwa **Shilingi bilioni 4.5**. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Februari, 2023.

***Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadi Kyaka***

**79. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Benaco hadi Kyaka Mkoani Kagera. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 80.99** na unagharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100**. Kazi inayoendelea sasa ni kufanya Upembuzi Yakunifu kwa kutumia wataalam wa ndani wa TANESCO. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakunifu; kuandaa zabuni (*tender documents*); usanifu wa mradi (*conceptual design*); kufanya Tathmini ya Mazingira na Jamii; na kuanza ujenzi wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza kujengwa mwezi Julai, 2022 na kukamilika mwezi Desemba, 2023.

***Mradi wa Backbone Transmission Investment Project – Awamu ya Pili (BTIP – Phase II)***

**80. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni wa awamu ya pili ambao unalenga kuongeza uwezo (*upgrade*) wa vituo vinne (4) vya kupoza umeme vya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma kutoka **kV 220** mpaka **kV 400**. Awamu ya kwanza ya mradi ilihusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida wenye urefu wa kilomita 670. Mradi huu ulikamilika mwezi Desemba, 2016 kwa **asilimia 100** na kwa sasa unaendeshwa kwa msongo wa **kV 220**. Gharama ya mradi huu wa BTIP awamu ya pili ni **Dola za Marekani milioni 120** sawa na takriban **Shilingi bilioni 282.25**.

**81. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuendelea na ujenzi wa vituo vya Singida na Dodoma ambapo utekelezaji wake kwa ujumla umefikia **asilimia 95**; kukamilisha ununuzi wa vifaa; na kupata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Iringa na Shinyanga. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni: kukamilisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida; na kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza



umeme vya Iringa na Shinyanga. Jumla ya **Shilingi bilioni 12.59** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Julai, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi***

**82. Mheshimiwa Spika**, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 198 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi mkoani Dar es Salaam. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 150** sawa na takriban **Shilingi bilioni 352.82**. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na: kudurusu Taarifa ya Upembuzi Yakinifu ili kujumuisha njia ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha JNHPP kupitia Kibiti; na kuendelea na malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni: kuendelea na taratibu za kupata ufadhili wa mradi; na kukamilisha malipo ya fidia. Jumla ya **Shilingi bilioni 8.53** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2021 na kukamilika mwezi Mei, 2023.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendokasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Kwanza***

**83. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulihusu ujenzi wa njia ya kuunganisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro kwa ajili ya kuendesha Treni ya Mwendokasi (*Standard Gauge Railway – SGR*) awamu ya kwanza. Aidha, mradi huu ulihusisha upanuzi wa kituo cha kupoza umeme msongo wa **kV 220** cha Kinyerezi. Gharama ya mradi huu ni **Shilingi bilioni 76.23** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** kutoka Kinyerezi hadi Kingolwira; kuunganisha njia ya umeme katika vituo vinne

vya Reli (TPS 4); na kukamilisha upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kinyerezi na Morogoro. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Januari, 2019 na ulikamilika kwa **asilimia 100** mwezi Januari, 2021.

***Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendokasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Pili***

**84. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kuunganisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 410 kutoka Msamvu, Morogoro hadi Kintinku, Singida kwa ajili ya kuendesha Treni ya Mwendokasi (*Standard Gauge Railway – SGR*) awamu ya pili. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 138.2** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika kwa usanifu wa mradi; kuanza ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kukamilisha ununuzi wa vifaa na ujenzi wa mradi. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Novemba, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2021.

**MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI**

**85. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu ulilenga kufikisha umeme katika vijiji **7,873**. Aidha, hadi kufikia Desemba 2015, jumla ya vijiji **2,018** vilikuwa vimefikwa na huduma ya umeme. Idadi hiyo imeongezeka na kufikia vijiji **10,312** mwezi Mei, 2021 sawa na ongezeko la vijiji **8,294**.

**86. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme ni **1,956** sawa na **asilimia 14** ya vijiji vyote **12,268** vya Tanzania Bara na vitapelekwa umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (*Turnkey Phase III – Round II*) ambao unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022. Kukamilika kwa mradi huo kutafanya vijiji vyote **12,268** vya Tanzania Bara kufikiwa na umeme.

**87. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizofanyika katika mwaka 2020/21 ni pamoja na: kukamilisha Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza; kuendelea kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (*Peri Urban*) katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; kukamilisha usambazaji umeme katika vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati kupitia Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Kwanza (*Densification I*) katika mikoa nane (8); kuanza usambazaji umeme katika vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati kupitia Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili (*Densification II*) katika mikoa 25; na kuendelea kuunganisha wananchi kwa kutumia mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyopo mbali na Gridi zikiwemo Taasisi za Umma katika visiwa vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Delta ya Rufiji.

**88. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili, 2020 hadi kufikia mwezi Aprili, 2021, jumla ya Taasisi **18,844** zimeunganishiwa umeme na hivyo kufanya jumla ya Taasisi zilizounganishiwa umeme kufikia **28,044** sawa na ongezeko la **asilimia 84.5**.

***Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu – Mzunguko wa Kwanza (REA III – Round I)***

**89. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulilenga kupeleka umeme katika vijiji **3,559** na kuunganisha wateja wa awali **180,768**. Utekelezaji wa mradi huu pia ulihusisha kupeleka umeme katika vitongoji **419** ambavyo vina Taasisi zinazotoa huduma kwa jamii zikiwemo Taasisi za Afya na Elimu ndani ya vijiji vilivyofikiwa na umeme, na hivyo kupelekea wateja wa awali kuongezeka hadi kufikia **227,561**. Gharama ya mradi ni **Shilingi trilioni 1.157**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji **3,378** kati ya **3,559** sawa na **asilimia 94.9** na vitongoji **317** kati ya **419** sawa na **asilimia 75.7** vilipelekewa umeme na kuunganisha jumla ya wateja **162,198** kati ya **227,561** sawa na **asilimia 71.3**. Mradi ulianza mwezi Julai, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

***Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu – Mzunguko wa Pili (REA III – Round II)***

**90. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vijiji **1,956** ambavyo havijafikiwa na umeme na hivyo kukamilisha kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vyote **12,268** vya Tanzania Bara. Vilevile, mradi unahusisha kupeleka umeme katika vitongoji **1,492**. Gharama za mradi ni **Shilingi trilioni 1.24** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Mradi huu ulizinduliwa rasmi kitaifa tarehe **15 Machi, 2021**. Katika mwaka 2021/22 **Shilingi bilioni 181.99** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

***Miradi ya Ujazilizi Katika Vitongoji Mzunguko wa Pili (Densification II)***

***(i) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili A (Densification IIA)***

**91. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika mikoa tisa (9) ambayo ni Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Mbeya, Pwani na Tanga. Mradi huu utahusisha kupeleka umeme katika vitongoji **1,103** na kuunganisha jumla ya wateja wa awali **69,079**. Gharama ya mradi ni **Shilingi bilioni 117.02**. Mradi huu ulizinduliwa rasmi kitaifa tarehe **24 Septemba, 2020**. Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Agosti, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021.

***(ii) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B (Densification IIB)***

**92. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vitongoji **1,686** na kuunganisha jumla ya wateja wa awali **95,334** katika mikoa kumi (10) ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 249.3** na unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa. Mradi huu upo katika hatua za kuwapata Wakandarasi na unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2021 na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 12.

***Miradi ya Kusambaza Umeme katika Maeneo Yaliyo Pembezoni mwa Miji (Vijiji Miji) – Peri Urban***

**93. Mheshimiwa Spika**, mradi wa Peri - Urban unalenga kusambaza umeme katika maeneo, vitongoji na mitaa iliyopo pembezoni mwa miji (vijiji miji) yenye uhitaji mkubwa wa umeme na maeneo hayo yanashabihiana na maeneo ya vijijini.

***(i) Mradi wa Peri Urban katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni***

**94. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (vijiji miji) katika Wilaya zote za Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni mkoa wa Dar es Salaam ambapo maeneo **216** yalipangwa kupatiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali **37,713**. Gharama ya mradi huu ni **Shilingi bilioni 80.5** na unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021, jumla ya maeneo **214** kati ya **216** yamefikishiwa umeme sawa na **asilimia 99.1** na kuunganisha wateja wa awali **28,875** kati ya **37,713** sawa na **asilimia 76.6**. Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Novemba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2021.

***(ii) Mradi wa Peri Urban katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Mwanza***

**95. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umelenga kusambaza umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji kwa mikoa ya Dodoma, Mwanza na Arusha ambapo maeneo **160** yamepangwa kupatiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali **16,328**. Gharama ya mradi ni **shilingi billioni 31.34**. **Mradi huu umeanza mwezi Mei, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2022.**

***Miradi wa Kusambaza Umeme Unaotokana na Nishati Jadidifu katika Maeneo Yaliyo Nje ya Gridi ya Taifa (Off – Grid Projects)***

**96. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kupeleka umeme katika vijiji vilivyopo

katika maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa ambapo vijiji **119** vitanufaika kupitia mradi huu. Vijiji hivyo vinahusisha pia Visiwa vyote ambavyo havijafikiwa na huduma za umeme. Mradi unatekelezwa kupitia utaratibu wa Ufadhili wa Malipo kwa Matokeo (*Results Based Financing - RBF*) na unalenga kukuza Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi ya nishati jadidifu kwa maeneo yaliyo nje ya gridi ya Taifa. Gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na takriban **Shilingi bilioni 42.34** na unafadhiliwa na nchi za Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo (Sida) na Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo (DFID).

**97. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021, Serikali kupitia REA ilifadhili miradi **13** yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa jumla ya **MW 9.635** kwa kutoa ruzuku ya **Dola za Marekani milioni 10.07** sawa na takriban **Shilingi bilioni 23.69** ambapo jumla ya vijiji **108** kati ya **119** sawa na **asilimia 90.7** vilipatiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali **18,023** kati ya **20,020** sawa na **asilimia 90**. Mradi huu ulianza mwezi Julai, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022.

## MIRADI YA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI UMEME

### *Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma*

**98. Mheshimiwa Spika**, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** kutoka Zuzu kwenda Msalato na kutoka Zuzu kwenda Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili (2) vipya vya kupoza na kusambaza umeme katika maeneo ya Msalato na lhumwa Jijini Dodoma. Gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 167.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 394.45**. Kazi iliyofanyika kwa mwaka 2020/21 ni kudurusu Upembuzi Yakinifu. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: kupata fedha za ujenzi wa mradi; na kuwapata wakandarasi wa mradi. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2022 na kukamilika mwezi Septemba, 2023.

***Mradi wa Kujenga Kituo Kipya cha Kupoza Umeme Luguruni chenye Msongo wa kV 220/33***

**99. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Luguruni kitakachohusisha ufungaji wa transfoma mbili zenye uwezo wa **MVA 90** kila moja. Mradi huu utakuwa na matoleo (*outgoing feeders*) sita (6) ya msongo wa **kV 33** ambayo yataboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Gharama ya mradi ni **Shilingi bilioni 15.2**. ujenzi wa mradi utafanywa kwa kutumia fedha za ndani za TANESCO.

**100. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha: usanifu wa mradi (*detailed design*); ununuzi wa vifaa vya ujenzi; na kuendelea na kazi za ujenzi wa misingi ya kufunga transfoma na vifaa vya kudhibiti mfumo wa umeme. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 70**. Kazi zitakazofanyika katika mwaka 2021/22 ni kuendelea na kukamilisha ujenzi wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi milioni 916.48** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Mradi huu ulianza mwezi Aprili, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2021.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Dege Beach***

**101. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 14 kutoka Kibada hadi Dege Beach mkoani Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Dege Beach chenye uwezo wa **MVA 60, kV 132/33**. Gharama ya mradi ni **Shilingi bilioni 26.2** na umetekelezwa kwa fedha za ndani na wataalamu wa TANESCO. **102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mradi ambapo umeme umewashwa tarehe 29 Aprili, 2021.

## SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

### *Uwekezaji Katika Miradi Midogo ya Nishati Jadidifu*

**103. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miradi midogo ya nishati jadidifu nchini kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu, kuongeza mchango wa nishati hiyo katika uzalishaji umeme na kutunza mazingira. Katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia EWURA ilidurusu Kanuni za kusimamia uendelezaji wa miradi midogo ya umeme chini ya **MW 10** “*The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2020*” na kutangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Julai, 2020 kupitia GN Na. 491.

**104. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa kanuni hizi kumewezesha TANESCO kuingia makubaliano na Kampuni saba (7) za Wawekezaji binafsi wa Miradi Midogo ya Umeme kwa kusaini mikataba ya kuuziana umeme (*Standardized Small Power Projects Agreements – SPPA*). Kampuni zilizosaini SPPA na TANESCO ni: *NextGen Solawazi Ltd* (Umeme Jua **MW 5** – Kigoma), *SSI Energy Tanzania Ltd* (Umeme Jua **MW 10** – Kahama), *Lung’ali Natural Resources Company Ltd* (Maji **MW 1.28** – Kilolo), *Luponde Hydro Ltd* (Maji **MW 1** – Njombe), *Nishati Lutheran (DKK) Investment Ltd* (Maji **kW 360** – Makete), *Madope Hydro Company Ltd* (Maji **MW 1.7** – Ludewa) na *Turiani Hydropower Company Ltd* (Maji **MW 5** – Mvomero). EWURA imetoa leseni moja (1) ya kuzalisha umeme wa **MW 2.4** kwa kutumia nishati jadidifu ya upepo kwa kampuni ya Mwenga Hydro Ltd. Mradi huu wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ni wa kwanza nchini na umeme unaozalishwa unasambazwa katika maeneo yanayohudumiwa na kampuni hiyo katika Wilaya ya Mufindi. Mradi huu umeanza uzalishaji umeme mwezi Novemba, 2020.

### *Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency)*

**105. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati unalenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya matumizi sahihi ya nishati katika sekta za uzalishaji na matumizi



bora ya nishati majumbani. Katika mwaka 2020/21, Wizara imeendelea kushiriki katika maandalizi ya mradi wa kikanda wa *Energy Efficient Lighting and Appliances (EELA)*; na kubainisha mahitaji ya vifaa na huduma (*service*) katika Taasisi zitakazohusika katika utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya Nishati. Katika mwaka 2021/22 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kuhuisha Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*National Energy Efficiency Strategy*) katika Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati; na kuanzisha miradi ya Mfano ili kuhamasisha matumizi bora ya nishati nchini.

### ***Programu ya Nishati Endelevu kwa Wote (Sustainable Energy for All – SE4ALL)***

**106. Mheshimiwa Spika**, programu hii inalenga kuongeza upatikanaji wa nishati kwa wote, kuongeza mchango wa nishati jadidifu na kukuza matumizi bora ya nishati. Programu hii inafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa – UNDP. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakinifu katika eneo la Mkwese, wilayani Manyoni; na kuhamasisha Halmashauri ya Wilaya ya Same na vijiji vinavyozunguka eneo la Kandoto kufanya Upembuzi Yakinifu wa awali, ambapo kuna uwezekano wa kuzalisha **MW 50** za umeme jua. Katika mwaka 2021/22 kazi zilizopangwa ni kufanya Upembuzi Yanikifu wa awali katika eneo la Kandoto na kuendelea kuhamasisha wadau katika kufadhili kazi za programu hiyo.

### ***Kuridhia na Kutekeleza Mikataba ya Kimataifa Kuhusu Nishati Jadidifu***

**107. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha na kuhamasisha uendelezaji wa teknolojia za nishati jadidifu nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea na utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (*International Solar Alliance – ISA*) ili iweze kunufaika na uwekezaji katika miradi ya umeme jua. Serikali pia imeendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Taasisi ya Nishati

Jadidifu (*International Renewable Energy Agency – IRENA*) ili nchi iweze kunufaika na uendelezaji wa aina zote za nishati jadidifu. Vilevile, Serikali imeshiriki katika maboresho ya rasimu ya Itifaki Mpya ya Nishati ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ambayo inatarajiwa kupitishwa na nchi wanachama na kuanza kutumika.

### ***Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (Geothermal)***

**108. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi nchini (*Tanzania Geothermal Development Company – TGDC*) ambayo ni Kampuni tanzu ya TANESCO, katika mwaka 2020/21 imeendelea na utekelezaji wa miradi mitano (5) ya kimkakati ya kuzalisha umeme kwa kutumia Jotoardhi nchini ili kufikia lengo la **MW 200** ifikapo mwaka 2025. Miradi inayotekelezwa ni: Ngozi (**MW 70**) na Kiejo-Mbaka (**MW 60**) mkoani Mbeya; Songwe (**MW 5**) mkoani Songwe; Luhoi (**MW 5**) mkoani Pwani; na Natron (**MW 60**) mkoani Arusha. Ili kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ikiwemo kuandaa Sheria kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza jotoardhi ambapo Rasimu ya Pili na Andiko la Sheria hiyo vimewasilishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya maamuzi. Kujenga uwezo wa ndani wa wataalam na vifaa kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zikiwemo vyuo vya elimu ya juu (UDSM, UDOM na MUST). Aidha, kwa mwaka 2020/21 Serikali kupitia TGDC iliendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

#### ***(i) Mradi wa Jotoardhi wa Ngozi (Mbeya) – MW 70***

**109. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uzalishaji wa umeme wa **MW 70** katika chanzo cha mlima wa volkano wa Ngozi Mkoani Mbeya ambapo utekelezaji wa mradi utaanza kwa kuzalisha **MW 30** ifikapo mwaka 2023. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na: taratibu za ununuzi wa mtambo wa kuchoronga (*drilling rig*); na kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kukamilisha: ununuzi wa mtambo; kumpata Mkandarasi

Mjenzi. Jumla ya **Shilingi milioni 616.82** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2023.

**(ii) Mradi wa Jotoardhi wa Songwe (Songwe) – MW 5**

110. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uzalishaji wa umeme wa **MW 5** na matumizi mengine (*direct heat uses*) katika eneo la Majimoto Songwe, Mkoani Songwe. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha majaribio ya teknolojia ya matumizi mengine (*direct heat uses*) ikiwa ni pamoja na teknolojia ya uanguaji wa vifaranga vya kuku kwa kutumia maji moto (*Geoincubator*); na kufanya majaribio ya teknolojia ya kukusanya taarifa za kijiolojia (*hotspring logger*) kwa ajili ya kupunguza gharama za utafiti. Katika mwaka wa fedha wa 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na uchorongaji wa visima vifupi (*shallow wells*) kwa ajili ya kuboresha taarifa za utafiti zilizopo kabla ya uchorongaji wa visima virefu vya majaribio. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.7** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi unatarajiwa kukamilika mwaka 2023.

**(iii) Mradi wa Jotoardhi wa Kiejo-Mbaka (Mbeya) – MW 60**

111. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uzalishaji wa umeme wa **MW 60** na matumizi mengine (*direct heat uses*) katika Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya ambapo utekelezaji wa mradi huu utaanza na uzalishaji wa **MW 10** za awali. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuanza uchorongaji wa visima vifupi (*shallow wells*) vitatu (3) kwa kuingia mkataba na Mkandarasi (*M/s STAMICO*) ambapo kazi hii inasimamiwa na wataalamu wa ndani wa TGDC. Katika mwaka 2021/22 kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kusimamia kazi za uchorongaji wa visima virefu; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.13** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Kati ya hizo **Shilingi bilioni 3.77** ni fedha za nje na **Shilingi milioni 360.79** fedha za ndani.

**(iv) Mradi wa Jotoardhi Natron (Arusha) – MW 60**

112. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uzalishaji wa umeme **MW 60** na matumizi mengine (*direct heat uses*) na unatekelezwa na TGDC katika Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuanza na kukamilisha utafiti wa kina wa kisayansi (*detailed surface explorations*); na kupata fedha za ujenzi wa mradi kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jotoardhi Afrika Mashariki (*Geothermal Risk Mitigation Facility – GRMF*). Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kufanya utafiti wa kina wa kisayansi juu ya ardhi (*detailed surface study*) katika eneo la mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo ambapo **Shilingi bilioni 1.02** ni fedha za nje na **Shilingi milioni 478.16** ni fedha za ndani.

**(v) Mradi wa Jotoardhi Luhoi (Pwani) – MW 5**

113. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uzalishaji wa umeme **MW 5** na matumizi mengine (*direct heat uses*) mkoani Pwani. Kwa sasa, mradi huu upo katika hatua za uchorongaji wa visima. Katika mwaka 2021/22 kazi zitakazotekelezwa ni: kufanya maandalizi ya uchorongaji wa visima vya uhakiki. Jumla ya **Shilingi milioni 562.59** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

**SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA**

***Shughuli za Utafutaji, Uendelezaji, Uzalishaji na Usambazaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini***

114. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia PURA imeendelea na udhibiti wa shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Kupitia mikataba 11 ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Production Sharing Agreement - PSAs*), hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni takriban **Futi za Ujazo Trilioni 57.54**. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2020 hadi Mei, 2021, uzalishaji wa gesi asilia umeongezeka hadi kufikia **Futi za Ujazo**

**Bilioni 56.13** ikilinganishwa na **Futi za Ujazo Bilioni 53.10** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la **asilimia 6**. Ongezeko hili la uzalishaji wa gesi asilia limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme hapa nchini, matumizi viwandani, katika magari na majumbani.

#### **UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI UNAOTEKELEZWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)**

**115. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika eneo la utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa vitalu vya Mnazi Bay Kaskazini na EyasiWembere. Utekelezaji wa miradi hiyo umefikia hatua zifuatazo:

##### ***(i) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini***

**116. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kilichopo Bahari ya kina kifupi kusini mashariki mwa Tanzania. Serikali kupitia TPDC imepanga kuchoronga visima viwili (2) vya utafutaji na uendelezaji katika kitalu hiki kwa gharama ya **Shilingi bilioni 204.32**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2021, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kupatikana kwa Mtaalam Mshauri wa uchorongaji wa visima vya utafutaji na uendelezaji (*Drilling Management Consultant*).

**117. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kutafsiri taarifa za kijiolojia; kusanifu na kuandaa mpango wa kina wa uchorongaji wa kisima cha utafutaji na kisima cha uhakiki; na uchorongaji wa visima hivyo. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 95.89** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

##### ***(ii) Utafutaji wa Mafuta Kitalu cha Eyasi- Wembere***

**118. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu utafutaji wa mafuta katika kitalu cha EyasiWembere, Kaskazini Mashariki

mwa Tanzania kwenye Bonde la Ufa (*Great East African Rift System*). Tafiti za awali za kijiolojia na kijiifizikia zilionesha uwepo wa miamba yenye uwezo wa kuzalisha na kuhifadhi mafuta au gesi asilia (*source rock*). Hadi kufikia mwezi Mei, 2021, Serikali kupitia TPDC imekamilisha uchorongaji wa visima vifupi vitatu (3) vya utafutaji vilivyopo maeneo ya Luono – Iramba (Singida), Kining'inila - Igunga (Tabora) na Nyalanja - Meatu (Simiyu). Tathmini ya kijiolojia ya sampuli za visima vilivyochorongwa imeonesha viashiria vya uwepo wa mafuta au gesi asilia.

**119. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukusanya, kuchakata na kutafsiri taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D umbali wa kilomita 260; kuandaa moduli ya mfumo wa 3D kwa kutumia taarifa za kijiifizikia; na kukusanya taarifa na kufanya tathmini ya kijiokemia juu ya uwepo wa viashiria vya miamba inayozalisha mafuta (*hydrocarbon seep detection*). Katika mwaka 2021/22 Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 14.41** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2015/16 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2022/23

#### **MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI GESI ASILIA**

**120. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia ni kazi endelevu ambapo kwa kuanzia, mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam imeshafikiwa na miundombinu hiyo. Serikali itaendelea kuongeza wigo wa mtandao wa usambazaji gesi asilia na kufikia mikoa mingine kulingana na upatikanaji wa fedha. Utekelezaji wa miradi na mipango ya usambazaji gesi kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya usambazaji ni kama ifuatavyo:

##### **(i) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani**

**121. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar

es Salaam na Pwani kwa njia ya mabomba pamoja na vituo vya kushindilia gesi asilia (*Compressed Natural Gas (CNG) Mother & Daughter Stations*). Mradi wa CNG utasaidia kuongeza matumizi ya gesi asilia kwa kusambaza gesi katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao wa mabomba ya gesi. Mradi wa CNG pia utachochea ongezeko la matumizi ya gesi asilia katika magari. Vituo vya CNG vitajengwa katika kituo cha mabasi ya DART kilichopo Ubungo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pembezoni mwa barabara ya Sam Nujoma. Vituo vidogo vya kupokelea na kusambaza gesi asilia (*Daughter Stations*) vitajengwa katika maeneo ya Soko la Samaki Feri, Hospitali ya Taifa Muhimbili na katika kiwanda cha Kairuki *Pharmaceutical Company* kilichopo Zegeleni-Kibaha.

**122. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa kilomita 12 katika Mkoa wa Dar es Salaam itakayounganisha zaidi ya nyumba 6,000 kwa maeneo ya Sinza, Kijitonyama, Chang'ombe, Kurasini na Keko; kutangaza zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa vituo vitano (5) vya CNG; kuendelea na Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii kwa mradi wa ujenzi wa Bomba la gesi kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach; kuendelea kuunganisha gesi asilia katika nyumba zaidi ya 1,000 katika maeneo ya Sinza na Kurasini; kukamilisha ujenzi wa miundombinu yenye urefu wa kilomita 7.1 katika Mkoa wa Pwani itakayounganisha viwanda zaidi ya 20; kuendelea na kazi ya kuunganisha viwanda viwili vya awali (*Balochistan na LN Future*) eneo la Mkuranga; na kukamilisha Tathmini ya Mazingira na kuanza hatua za awali za ujenzi wa Bomba la gesi asilia kutoka Tegeta hadi Bagamoyo.

**123. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2021/22 ni pamoja na: kuanza ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach; na kuanza ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Tegeta hadi Bagamoyo. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 51.53** kwa ajili ya usambazaji wa gesi asilia mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

**(ii) Usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Lindi na Mtwara**

**124. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo viwandani, taasisi na majumbani katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendelea na Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Kampuni ya Dangote imekamilisha ujenzi wa kituo cha kujazia gesi asilia (CNG) katika magari ambapo jumla ya magari **250** ya awali yamewekewa mfumo wa matumizi ya gesi asilia na hivyo kufikia magari zaidi ya **700** yanayotumia nishati hiyo nchini; kukamilisha ujenzi wa miundombinu (*trunk line*) yenye urefu wa kilomita 8 na kuendelea kuunganisha wateja wa majumbani 300 ambapo kwa sasa kazi hii imefikia **asilimia 83**; kukamilika kwa usanifu wa kihandisi wa ujenzi wa bomba la gesi asilia (*trunk line*) kutoka bomba kuu hadi Mnazi Mmoja na miundombinu ya usambazaji gesi majumbani katika Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo; na kuendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi Mjenzi (*EPC Contractor*) wa bomba hilo (*trunk line*).

**125. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mkoa wa Mtwara ni pamoja na: kuunganisha gesi asilia katika nyumba zaidi ya 500; Kwa Mkoa wa Lindi, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa kilomita 10 kutoka BVS-3 hadi Mnazi Mmoja pamoja na kujenga miundombinu hiyo; Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia majumbani yenye urefu wa kilomita 16.2 itakayounganisha zaidi ya nyumba 200 za awali eneo la Mnazi Mmoja. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 10.74** kwa ajili ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

**(iii) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda**

**126. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kujenga Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda. Hadi



sasa, timu ya pamoja ya Wataalamu wa Tanzania na Uganda (*Joint Technical Committee – JTC*) imeandaa Hadidu za Rejea pamoja na miongozo mbalimbali ya kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakiniifu wa mradi na kuandaa rasimu ya Makubaliano ya Pamoja (*Bilateral Agreement*) kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda. Katika mwaka 2021/22, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni: kukamilisha majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uganda kuhusu namna bora ya kutekeleza mradi huu; kuandaa kanuni za pamoja za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakiniifu; na kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi milioni 489** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### **MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA KUWA KIMIMINIKA (*LIQUEFIED NATURAL GAS – LNG*)**

**127. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu kusindika gesi asilia na kuwa kimiminika katika gesi ya Vitalu Na. 1, 2 na 4 na kuuzwa katika masoko ya nje. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani bilioni 30** sawa na takriban **Shilingi trilioni 70.563**. Kazi zilizotekelezwa hadi kufikia mwezi Machi, 2021 ni pamoja na: Kukamilisha malipo ya **Shilingi bilioni 5.71** kwa ajili ya fidia na riba kwa mujibu wa Sheria kwa Wananchi 642 waliopisha Mradi; na kuweka mpaka eneo la mradi (Likong’o, Mto Mkavu na Masasi ya Leo).

**128. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha majadiliano ya kimkataba (*Host Government Agreement negotiations*) na wawekezaji wa mradi; kukamilisha mapitio ya mikataba ya ugawanaji mapato (*Production Sharing Agreements – PSAs*). Jumla ya **Shilingi bilioni 3** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ujenzi wa Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2023 na kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2028.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA MATUMIZI YA GESI ASILIA (*NATURAL GAS UTILIZATION MASTER PLAN – NGUMP*)

**129. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP). Mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015. Katika Mpango huo, jumla ya **Futi za Ujazo Trilioni 19.7** za gesi asilia zinataraajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani katika uzalishaji wa umeme, viwandani, majumbani, taasisi na magari.

**130. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza mpango huu, Serikali imeendelea kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia JICA kuandaa Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (*Domestic Natural Gas Promotion Plan – DNGPP*). Mpango huu unalenga zaidi usafirishaji wa gesi asilia kwenda maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuainisha matumizi ya teknolojia nafuu katika usambazaji wa gesi asilia.

**131. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (*Draft Domestic Natural Gas Promotion Plan – DNGPP*); na kukusanya taarifa na kupitia stadi mbalimbali kwa ajili ya uhakiki wa mahitaji ya gesi asilia nchini.

**132. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuhuisha Mpango na kukamilisha DNGPP; kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa teknolojia kwa mujibu wa Mpango wa DNGPP; kuhakiki mahitaji ya gesi asilia nchini; na kuanza hatua za awali za utekelezaji Mradi wa mfano katika Jiji la Dodoma.

## MIRADI YA KUHIFADHI NA KUSAFIRISHA MAFUTA

*(i) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline – EACOP)*

**133. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi (*crude oil*) kutoka Hoima nchini

Uganda hadi Tanga nchini Tanzania. Lengo la mradi huu ni kusafirisha mafuta hayo kwenda katika Soko la Kimataifa. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani bilioni 3.558** sawa na takriban **Shilingi trilioni 8.369**. Kazi zilizotekelezwa hadi mwezi Mei, 2021 ni pamoja na kukamilisha majadiliano na kusainiwa kwa mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (*Host Government Agreement – HGA*) na Mkataba wa Ubia (*Shareholding Agreement - SHA*) kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji. Aidha, majadiliano yamekamiliwa na kuridhiwa kusainiwa (*intialed*) kwa mikataba ya uendeshaji wa Bandari ya Chongoleani na mikataba ya ukodishaji wa ardhi kwa ajili ya mkuza na maeneo ya kipaumbele ya mradi; na kukamilisha taratibu za kuanza kulipa fidia kwa Wananchi wa maeneo hayo.

**134. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo; na kusimamia ujenzi wa mradi pamoja na wawekezaji wengine. Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 2.6** kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa mradi umeanza mwezi Mei, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

**(ii) Uhifadhi na Biashara ya Mafuta**

**135. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imeendelea na utekelezaji wa kuanzisha na kusimamia Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura (*Strategic Petroleum Reserve – SPR*). TPDC inamiliki maeneo yanayotazamiwa kujengwa maghala ya kuhifadhia mafuta (*Tank Farms*) katika mikoa ya Shinyanga (Isaka), Katavi (Mpanda), Njombe (Makambako), Uyole (Mbeya) na Kigoma. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, TPDC imekamiliwa utwaaji wa ardhi katika mikoa ya Dodoma (Zuzu), Tanga (Chongoleani) na imeendelea na taratibu za utwaaji ardhi Mkoa wa Dar es Salaam (Kigamboni). TPDC itajenga maghala ya kuhifadhia mafuta ya ujazo tofauti kulingana na ukubwa wa eneo kuanzia tani **45,000** hadi **100,000**. TPDC imeanza kufanya biashara ya uagizaji na uuzaji wa mafuta ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2021 shehena nane (8) za mafuta zenye jumla ya ujazo wa takriban tani 8,253 zimepokelewa katika Bandari ya Dar es Salaam.

**136. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia TPDC itaendelea na biashara ya uagizaji na uuzaji wa mafuta kwa ujazo usiopungua tani 2,000 kwa mwezi na kiwango hiki kitaendelea kuongezeka. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 47.95** kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa mafuta (*oil cargo stock*).

**(iii) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (Refined Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)**

**137. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia lenye urefu wa takribani kilomita 1,710 likiwa na matoleo ya mafuta (*take-off points*) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Bomba hili litajengwa katika mkuza wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la TAZAMA na litamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zambia. Kukamilisha hadidu za rejea za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa Mradi zimeandaliwa na Kamati ya Pamoja ya Wataalamu wa nchi zote mbili (*JTC*).

**138. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi pamoja na kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani zimetengwa kugharamia kazi zilizopangwa.

## **UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA**

**139. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia PURA imekamilisha uhakiki na ukaguzi wa gharama za uwekezaji na mapato yatokanayo na uzalishaji wa gesi asilia kwa mwaka 2019 na 2020 na kuokoa jumla ya **Shilingi bilioni 26.45** na hivyo kuongeza pato la Serikali katika mgao wake wa uuzaji gesi asilia.

**140. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2021/22 Serikali kupitia PURA itasimamia uchorongaji wa kisima kimoja cha utafutaji (Chikumbi-1) katika kitalu cha Ruvuma; kisima kimoja (1) cha utafutaji (Mruka-1) na kisima kimoja (1) cha uendelezaji (Mambakofi-2) katika kitalu cha Ruvu; na kisima kimoja (1) cha utafutaji (Tausi-1) katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini. PURA itaendelea na ukaguzi katika maeneo yote ya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini. Katika mwaka 2021/22, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.69** fedha za ndani ili kuwezesha shughuli za udhibiti za mkondo wa juu wa Petrol.

### **HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa mafuta nchini imeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka 2020/21, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini ni **lita bilioni 3.14** ikilinganishwa na **lita bilioni 3.11** zilizoingizwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la **asilimia 1.14**. Kiasi cha mafuta kilichoingia hapa nchini kwa ajili ya nchi jirani (*Transit products*) mwaka 2020/21, hadi kufikia mwezi Aprili 2021 ni **lita bilioni 2.23** ikilinganishwa na **lita bilioni 2.06** zilizoingizwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la **asilimia 8.3**.

**141. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti katika upokeaji wa mafuta kutoka katika meli kwa kufunga *flowmeter* za teknolojia ya kisasa inayotumika kupima bidhaa za mafuta ya petroli yanayoshushwa ili kupata kodi na tozo stahiki. *Flowmeter* hizo zimefungwa katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Serikali kupitia EWURA imeelekeza kampuni zinazomiliki maghala ya mafuta kufunga *flowmeter* katika mabomba yote yanayoingia kwenye maghala yao ili kuhakikisha mafuta yanapokelewa sehemu iliyokusidiwa. Serikali kupitia Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) inaendelea na utaratibu wa upatikanaji wa teknolojia (SCADA) itakayosoma *flowmeter* zote wakati wote ili kutambua matatizo yatakayojitokeza mapema iwezekanavyo.

142. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia PBPA imeendelea kusimamia mpangilio wa meli zinazoleta mafuta nchini ili kupunguza siku za meli kusubiri (*demurrage*) kushusha mafuta kutoka katika meli ambapo wastani wa siku za kusubiri kwa sasa ni siku tano (5) ikilinganishwa na wastani wa siku 75 kwa mwaka 2015. Gharama za *demurrage* zimepungua kutoka wastani wa **Dola za Marekani 45** kwa tani hadi wastani wa **Dola za Marekani 3.6** kwa tani kutokana na siku za meli kusubiri kushusha mafuta kupungua. Kwa tathmini hii, mfumo huu unaokoa takribani **Shilingi bilioni 320** kwa mwaka zilizokuwa zinatumika kulipia *demurrage*.

143. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia PBPA imeendelea kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ambapo gharama za uletaji mafuta zimeendelea kuwa na wastani wa **Dola za Marekani 36** kwa tani ikilinganishwa na **Dola za Marekani 83** kwa tani mwaka 2015 kabla ya mfumo huu kuanza na kuokoa wastani wa **Shilingi bilioni 360** kila mwaka.

144. *Mheshimiwa Spika*, kiasi cha gesi ya mitungi (*Liquefied Petroleum Gas - LPG*) kinachoingizwa nchini kimeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2020, kiasi kilichoingizwa kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini na nchi jirani ni **tani 194,597** ikilinganishwa na **tani 166,436** zilizolingizwa mwaka 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 16.92**. Matumizi ya ndani yameongezeka hadi kufikia **tani 121,834** mwaka 2020 ikilinganishwa na **tani 106,301** mwaka 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 14.61**. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi mbalimbali za Serikali kwa kushirikiana na Kampuni zinazouza LPG katika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutumia LPG katika kutunza mazingira na kupunguza madhara ya kiasia yanayotokana na matumizi ya kuni na mkaa.

## MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA

145. *Mheshimiwa Spika*, kwa miezi kumi na moja ya mwaka 2020/21, wastani wa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia ilikuwa **Dola za Marekani 52.96** kwa pipa ikiwa ni sawa na pungufu ya **asilimia 0.5** ikilinganishwa na wastani wa **Dola za**

**Marekani 53.22** kwa pipa kwa kipindi kama hicho katika mwaka 2019/20. Bei ya mafuta ghafi katika soko la Dunia ilishuka mwaka 2020/21 kwa sababu matumizi ya mafuta duniani yalipungua kutokana na kupungua au kisimamishwa kwa shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali duniani ikiwa ni hatua zilizochukuliwa na nchi hizo kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

**146. Mheshimiwa Spika**, kushuka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la Dunia kwa mwaka 2020/21 kulipelekea kushuka kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa ambapo kwa mwaka huo, wastani wa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilikuwa **Dola za Marekani 413, 382 na 369** kwa tani kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia, ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 574, 542 na 552** kwa tani kwa kipindi kama hicho katika mwaka 2019/20. Hii ni sawa na pungufu ya **asilimia 28, 30 na 33** kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia.

**147. Mheshimiwa Spika**, kama ilivyokuwa kwa bei ya mafuta ghafi na yale yaliyosafishwa, bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyopokelewa kupitia bandari ya Dar es Salaam nazo zilipungua kwa miezi kumi na moja ya mwaka 2020/21. Wastani wa bei za mafuta kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa mwaka 2020/21 kwa lita moja ilikuwa kama ifuatavyo: petroli **Shilingi 1,910**, dizeli **Shilingi 1,815** na mafuta ya taa **Shilingi 1,723** wakati wastani wa bei za mafuta hayo kwa mwaka 2019/20 ilikuwa **Shilingi 2,158** kwa mafuta ya petroli, **Shilingi 2,107** kwa mafuta ya dizeli na **Shilingi 2,039** kwa mafuta ya taa ambazo ni sawa na punguzo la **asilimia 11, 14 na 16** mtawalia.

## UWEKEZAJI NA UDHIBITI WA UBORA WA MIUNDOMBINU NA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI

148. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kuhakikisha miundombinu ya mafuta inajengwa na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango stahiki. EWURA pia imeendelea kutoa leseni kwa miundombinu ambayo inakidhi viwango ambapo kwa mwaka 2020, imetoa jumla ya leseni 514 za aina mbalimbali na vibali 248 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta. Hii ni ongezeko la **asilimia 11.3 ikilinganishwa na leseni 462 zilizotolewa mwaka 2019. Hali hii inaonesha uwekezaji unazidi kuimarika katika sekta ndogo ya mafuta hususan kwa ujenzi wa vituo vya mafuta.**

149. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeelekeza EWURA kuendelea kusimamia upatikanaji wa mafuta vijijini na kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo kutokana na uhaba wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo ya vijijini. Serikali inaangalia utaratibu wa kupunguza gharama za tozo mbalimbali za taasisi za Serikali ili kupunguza gharama za uwekezaji kwa vituo vya mafuta vijijini. Katika mwaka 2020, jumla ya vituo vya mafuta 68 vya vijijini vilikidhi vigezo na kupewa leseni na EWURA. Hadi kufikia tarehe 30 Desemba, 2020 kulikuwa na vituo vya mafuta 197 vijijini kutoka vituo 129 mwaka 2019.

150. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli zinazosambazwa na kuuzwa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2020, EWURA ilipima sampuli 558 ambapo kati hizo, sampuli 68 sawa na **asilimia 12.2** hazikukidhi viwango na hatua stahiki za kisheria zilichukuliwa dhidi ya wafanyabiashara waliokutwa na mafuta ambayo hayakidhi viwango. Aidha, juhudi zinaendelea kuwekwa kwa kufanya ukaguzi zaidi na kusimamia ubora wa miundombinu ili kuhakikisha mafuta yanakuwa na ubora wa viwango stahiki.

151. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22 Serikali itaendelea kusimamia sekta ya mafuta nchini ili kuhakikisha uwepo wa mafuta yakutosha, yenye ubora stahiki, miundombinu ya mafuta yenye kukidhi ubora, usalama na



utunzaji wa mazingira pamoja na ushindani ulio sawa wakati wote.

## **UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA KATI NA WA CHINI WA GESI ASILIA**

**152. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia EWURA imeendelea kudhibiti sekta ndogo ya gesi asilia kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara katika miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Kupitia kaguzi hizo, miundombinu ya gesi asilia hapa nchini ipo katika hali nzuri inayokidhi viwango vya ubora na usalama.

**153. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kampuni za wazawa zinashiriki kikamilifu katika shughuli za uendelezaji wa sekta ndogo ya gesi asilia hapa nchini Serikali kupitia EWURA, iliendelea kuhuisha Kanzidata ya Watoa Huduma wa Ndani (*Local Suppliers and Service Providers Database – LSSP*). Kwa mujibu wa Kanuni ya ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ndogo ya gesi asilia (*The Petroleum (Local Content) Regulations, 2017*) kampuni za nje haziruhusiwi kutoa huduma katika tasnia ya mafuta na gesi asilia ikiwa huduma hizo zinaweza kutolewa na kampuni za wazawa. Hivyo, Kanuni inaelekeza kutambua kampuni za wazawa kwa njia ya kujisajili kwenye Kanzidata ili ziweze kupewa kipaumbele dhidi ya kampuni za nje wakati kandarasi zinapotangazwa. Aidha, kufikia mwezi Machi, 2021 EWURA ilikuwa imesajili kampuni za wazawa 570 kwenye Kanzidata.

## **MIRADI YA KUJENGA UWEZO KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA**

### ***Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Rasilimali za Asili Tanzania***

**154. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Juni, 2017 kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania. Lengo la mradi ni kujijengea uwezo na kusaidia taasisi za Serikali ili kusimamia

rasilimali za nchi. Taasisi zinazolengwa na mradi huu ni pamoja na Wizara ya Nishati, TRA, EWURA, PURA, TPDC na NEEC. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 29.54** ambapo Mfuko wa Maendeleo wa Afrika unachangia **Dola za Marekani milioni 26.59** sawa na **Shilingi bilioni 62.54** na Serikali ya Tanzania inachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na **Shilingi bilioni 6.94**. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021.

#### **UIMARISHAJI WA MAWASILIANO KATI YA WIZARA NA JAMII**

**155. Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu mengine, Wizara imeendelea na kazi ya utoaji wa taarifa kwa wadau kupitia Televisheni, Magazeti na Redio. Aidha, utoaji wa taarifa unajumuisha kupitia Tovuti ya Wizara, mitandao ya kijamii ya Wizara ambayo ni *facebook*, *Twitter*, *Instagram* na *YouTube* pamoja na Jarida la Wizara ya Nishati linalotolewa kwa kila mwezi.

**156. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2020/21 Wizara iliendelea kutoa taarifa mbalimbali za miradi mikubwa inayotekelezwa chini yake ikiwemo miradi ya uzalishaji na usafirishaji umeme, miradi ya mafuta na usambazaji wa gesi asilia na miradi ya usambazaji umeme vijijini. Katika mwaka 2021/22 Wizara itaendelea kutoa taarifa mbalimbali katika maeneo muhimu ya miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya Wizara.

#### **AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALIWATU**

**157. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia Miundo ya maendeleo ya Watumishi wake pamoja na kutekeleza vema Muundo wake ulioidhishwa mwaka 2018 kwa kusimamia kanuni na sheria zinazosimamia utumishi wa umma.

**158. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Wizara iliwajengea uwezo watumishi wawili (2) katika mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 260 katika mafunzo ya muda mfupi. Kwa mwaka 2021/22, Wizara inatarajia kupeleka mafunzo ya muda mrefu Watumishi 7 na mafunzo ya muda mfupi kwa Watumishi 52.

**159. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo Watumishi 70 kuwathibitisha kazini Watumishi 14 na kumbadilisha kada Mtumishi mmoja (1). Jumla ya watumishi 1,925 wanatarajiwa kuajiriwa katika Taasisi zilizo chini ya Wizara zikiwemo: TANESCO (1,856), TPDC (34), REA (15) na PURA (20).

#### **USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA**

**160. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Jumuiya na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), United Bank for Africa (UBA); Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea), Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa), DFID (Uingereza), Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani).

**161. Mheshimiwa Spika**, pia natoa shukrani kwa Serikali za Burundi, Canada, China, Iceland, Japan, Kenya, Norway, Korea ya Kusini, Malawi, Misri, Msumbiji, Sweden, Norway, Denmark, Marekani, Uingereza, Ujerumani, Rwanda, DRCCongo, Afrika Kusini, Namibia, Algeria, India, Ufaransa, Uganda, Zambia na nchi nyingine kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Naishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta hii.

#### **HITIMISHO**

**162. Mheshimiwa Spika**, kupitia Bajeti ya Mwaka 2021/22 Wizara inalenga kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa inazalisha umeme wa kutosha, wa uhakika, unaotabirika na wenye gharama nafuu. Bajeti imelenga kuimarisha shughuli za utafutaji na biashara ya mafuta na

gesi asilia pamoja na kuwezesha wananchi kunufaika na rasilimali hizo.

**163. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2021/22, Wizara ya Nishati inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 2.386** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 2.197** iliyotengwa kwa Mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la **asilimia 8**.

**164. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya **Shilingi 2,385,980,809,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 2,358,756,128,000** sawa na **asilimia 98.9** ya bajeti yote ya Wizara kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,178,756,128,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 180,000,000,000** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi 27,224,681,000** sawa na **asilimia 1.1** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 12,198,860,000** kwa ajili ya mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**165. Mheshimiwa Spika**, kwa unyenyekevu mkubwa sana naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz). Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

**166. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt Medard

Kalemani kwa kuwasilisha hoja yako vizuri sana na tumeisikiliza kwa umakini mkubwa ahsante sana.

Sasa bila kupoteza muda nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini Kamati ya Kudumu ili aje atupitishie maoni ya kamati kuhusu Wizara hii ya Nishati anakuja Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti karibu sana na una nusu saa pia. (*Makofi*)

**MHE. DUNSTAN L KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba Taarifa yote ya Kamati iliyowasilishwa Mezani iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametupa kibali cha kuiona siku ya leo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(9) na Sehemu ya 7(a), (c) na (d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Julai, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati Fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatatazo: Kwanza ilitembelea na Kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, lakini vile vile ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kamati ilitekeleza matakwa ya *Kanuni ya 117(2)* kwa kufanya Ukaguzi wa Miradi, miradi wa kwanza ikiwa mradi wa uzalishaji wa umeme wa maji wa Julius Nyerere uliopo Rufiji, Pwani; lakini vile vile ilitembelea Miradi ya *REA III* iliyopo Sengerema, Mkoani Mwanza. Maelezo kuhusu mradi wa Julius Nyerere yanapatikana katika ukurasa

wa 4 hadi 8 wa taarifa zetu. Aidha, changamoto zilizobainika katika ukaguzi wa miradi hii ni pamoja na ubovu wa barabara kwenda kwenye eneo la mradi ambao umekuwa kikwazo katika kutoa huduma mbalimbali zinazohitajika katika mradi hususan kipindi cha mvua. Pili kuna tatizo la Utoaji wa fursa sawa za ajira kwa jinsia zote.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*) maelezo ya eneo hilo yanapatikana ukurasa wa 9 hadi 18 wa Taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kutokana na ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao: Kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji na upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo iliyoitembelea chini ya Wizara ya Nishati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji Madhubuti wa Miradi hii; vile vile Kwa kuwa maeneo mengi ya Vijiji na Vitongoji yanarukwa katika kusambaziwa huduma ya umeme; na kwa kuwa bado TANESCO wana kasi ndogo sana ya kuunganisha Wateja, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo (*scope*) kwa Wakandarasi wanaopewa kazi za kupeleka umeme ili kukidhi mahitaji ya Wananchi waliopo vijijini. Aidha, Pindi inapobainika kuwa Mkandarasi aliyepewa kazi anasuasua katika kutekeleza majukumu yake ya kimkatiba, *REA* ihakikishe inachukua hatua za haraka kusitisha Mikataba hiyo kwa mujibu wa sheria ili kuepuka ucheleweshaji wa wananchi kufikiwa na huduma za umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni sekta ndogo ya gesi asilia maelezo kuhusu Sekta ndogo ya gesi asilia yanapatikana Ukurasa wa 21 wa taarifa yetu. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ya Utekelezaji wa Mikataba hii ili kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika na Sekta hii ya Gesi Asilia na kuhakikisha kwamba Watanzania walio wengi wanaendelea kupata

fursa za ajira na biashara zinazojitokeza katika uwekezaji unaofanywa katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, miradi ya utafutaji wa gesi asilia na mafuta taarifa yetu Ukurasa wa 24 hadi 25 unalizingumzia jambo hili kwa kina.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanaji umeme nchini maelezo ya kamati kuhusiana na hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini yapo katika Ukurasa wa 27 hadi 30 wa Taarifa yetu. Kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na Wizara kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ili kuuboresha zaidi mfumo wetu ni Rai ya kamati kuwa ipo haja ya kufanya mapitio ya mfumo wetu kwa lengo la kuuboresha ili uweze kuvutia ushiriki wa Makampuni mengi zaidi kwenye minada ya uagizaji wa mafuta na hivyo kuwezesha nchi na hivyo nchi kuweza kunufaika na ushindani wa soko na kupata mafuta kwa uhakika kwa bei nzuri kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini maelezo kuhusu hali ya upatikanaji wa Umeme nchini yanapatikana Ukurasa wa 32 hadi 33 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kulitokea tatizo kubwa la Upatikanaji wa Huduma ya Luku kutokana na sababu zinazohusiana na matatizo ya kimfumo. Athari za tatizo hili ni kubwa katika Uchumi na ustawi wa wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Tatizo hili halijirudii na jitihada za dhati zichukuliwe ili kuwa na mifumo ya ndani inayotumika katika utoaji wa huduma za Luku nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini *(REA III)* Mzunguko wa Tatu maelezo kuhusu tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini Mzunguko wa Tatu Yanapatikana Ukurasa wa 34 hadi 36 wa Taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kamati inaona ipo haja ya Wakandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa Miradi hii. Aidha, Serikali inapaswa kuendelea kuweka nguvu ya kiusimamizi na ufuatiliaji wa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi hii kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na matakwa ya Mikataba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na uzingatiaji wa maoni ya kamati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha. Katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Nishati ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 602.05. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya shilingi bilioni 602.04 zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na Gesi Asilia na shilingi bilioni 12 kupitia shughuli za Utawala. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo; Shughuli za TPDC za utafiti wa mafuta; Mauzo ya Gesi Asilia; na Mauzo ya Nyaraka za Zabuni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Februari 2021 jumla ya shilingi bilioni 377.15 zilikusanywa kutokana na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia zilizoratibiwa na TPDC. Kamati ilibaini kuwa kiasi hicho ni sawa na asilimia 89.5 ya lengo la makusanyo ya shilingi bilioni 421.36 kwa kipindi hicho. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Wizara kuendelea na jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo vya Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, katika mwaka wa Fedha 2020/202. Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi tirioni 2.19 kwa Wizara ya Nishati. Kati ya Fedha hizo, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ni shilingi tirioni 2.1 sawa na asilimia 98.7 ya bajeti yote ya Wizara. Aidha, kati ya fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi tirioni 1.9 sawa na asilimia 90.7 ya Bajeti



yote ya Maendeleo ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 200.7 sawa na asilimia 9.3 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 ni shilingi bilioni 28.3 sawa na asilimia 1.3 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi 15.02 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 13.3 kwa ajili ya kulipa Mishahara. Ni rai ya Kamati kuwa mara baada ya madai husika ya wakandarasi wanaofanya kazi katika miradi iliyoko chini ya Wizara hii kufikishwa uhakiki wa madai hayo ufanyike kwa haraka ili fedha za Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati taarifa yetu ukurasa wa 41 na 42 unaonyesha nini kilichotokea ni rai ya Kamati kuwa iendelee kufanya kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kamati vile vile ilifanya uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kawa mwaka wa fedha 2021/2022 na uchambuzi huo unaonekana kwenye ukurasa wa 43.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio na mapato na matumizi katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Nishati fungu 58 inakadiria kutumia jumla ya Shilingi tirioni 2.35 ikilinganishwa na shilingi tirioni 2.1 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na hii ni sawa na ongezeko la asilimia 8. Kati ya fedha hizo shilingi tirioni 2.3 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi bilioni 27.2 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 ni shilingi bilioni 27.1 sawa na asilimia 1.1 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 15 zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 12.1 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makadirio ya Bajeti ya Maendeleo, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa Fedha 2021/2022 unakadiriwa kutumia jumla ya shilingi tirioni 2.3 ambazo ni sawa na asilimia 98.9 ya bajeti yote ya Wizara. Katika hizo Bajeti ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi tirioni 2.1 sawa na asilimia 92.4 ya Bajeti yote ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kamati ilibaini kuwa kiasi kikubwa cha fedha za ndani za Maendeleo kimeelekezwa katika Miradi ya kielelezo na Kimkakati ambayo ni Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere; Mradi wa kuzalisha Umeme Vijijini Awamu ya Tatu; Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi *Extension I*; na Miradi ya Ruhudji, Rumakali, Singida - Arusha - Namanga, Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Kigoma na lakini vile vile mradi *LNG*, ambapo mazungumzo yataanza pamoja na mradi wa *EACOP*. Aidha, Bajeti ya fedha za Nje inayopendekezwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni 180 sawa na asilimia 7.6 ya Bajeti yote ya Maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka huu wa Fedha unaokuja yanapatikana ukurasa wa 46 wa Taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya Maduhuli, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 20.3 kutokana na Shughuli za Utawala. Makadirio ya ukusanyaji Maduhuli katika mwaka wa fedha 2021/2022 yamepungua kwa asilimia takribani 100 ikilinganisha na mwaka wa fedha uliopita ambapo Makadirio ya Maduhuli yalikuwa shilingi bilioni 602. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba wakati ambapo ukusanyaji wa Maduhuli uliokua ukifanywa na Wizara ukishuka, ukusanyaji Maduhuli kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha ujao umeongezeka kwa takribani Asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili limetokana na Mabadiliko ya Sera ya Ukusanyaji Maduhuli katika Sekta hii

ambayo kwa sasa inataka *TPDC* ndiyo ikusanye Mapato yanayotokana na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kuziweka hizo fedha katika Mfuko wa Fedha zitokanazo na Shughuli za Utafutaji wa Gesi Asilia jambo ambalo halikufanyika katika mwaka wa fedha 2020/2021. (*Makofi*)

Mheshimwa Spika, ufuatao ni uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kulinganisha na mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa mwaka ujao. Ulinganisho huo ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati katika mwaka ujao wa fedha.

Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika; Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni shilingi trilioni 2.3 ni sawa na asilimia. 6.5 ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni shilingi trilioni 36.3.

Mheshimiwa Spika, aidha, mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 4 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; wakati Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 8 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021. Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.76 katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 36.68 ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022; wakati bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Nishati ambayo ni sawa na asilimia 6.5 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Nishati dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 umeonyeshwa katika Jedwali Na.02: ukurasa wa 49 wa Taarifa ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ina Maoni na Ushauri ufuatao kwa Serikali:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere;

Kwa kuwa, Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji katika Bonde la Mto Rufiji una umuhimu wa Kimkakati kwa uchumi wa Taifa letu;

Na kwa kuwa, katika mwaka wa fedha 2020/2021 utekelezaji wake ulijielekeza katika ujenzi wa Miundombinu wezeshi kama vile ujenzi wa bwawa, ujenzi wa njia Kuu za kupitisha maji), ujenzi wa Kituo cha kuzalishia umeme na ujenzi wa Kituo cha kusafirishia umeme

Hivyo basi, katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza usimamizi, na kuhakikisha fedha za uendelezaji wa mradi zinapatikana kwa wakati kama zilivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge ili kufikia lengo la kuanza kupokea Maji kwa bwawa hili ifikapo Mwezi Novemba 2021 na kuanza uzalishaji ifikapo mwezi Juni, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia Hivyo basi katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza usimamizi, na kuhakikisha fedha za uendelezaji wa Mradi zinapatikana kwa wakati kama zilivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge ili kufikia lengo la kuanza kupokea Maji kwa bwawa hili ifikapo Mwezi Novemba 2021 na kuanza uzalishaji ifikapo mwezi Juni, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwalipa wakandarasi wa Miradi hii kwa Wakati Kwa kuwa, Miradi ya

Kimkakati inayotekelezwa na Wizara ni muhimu sana katika kuchangia pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi kwa ujumla;

Na Kwa kuwa, Miradi hii inatumia Wakandarasi mbalimbali na Watoa huduma kutoka Ndani na nje ya nchi;

Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kulipa kwa Wakati Madeni na Fedha zote zinazotakiwa kulipwa kwa Wakandarasi hao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa wakati kwa ajili ya kuikamilisha Miradi hii ndani ya lengo lililowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Nishati, kamati inaishauri Serikali kuendelea kutengeneza Mazingira rafiki zaidi kwa Wawekezaji ili wapate motisha ya kuwekeza katika Sekta ya Nishati kwa kutumia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali iliyopo. Aidha, Miongozo ya kutangaza miradi inayotekelezwa kwa kutumia vyanzo vya Makaa ya Mawe, Jua, na Upepo kwa njia ya ushindani iendeleo kutumika na Zabuni husika kutangazwa kwa uwazi ili Miradi mipya inapokuja Michakato ya kupata Wakandarasi ifanyike kwa ufanisi na uwazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa matumizi ya Gesi Asilia ni rai ya Kamati ili tuweze kunusuru nchi yetu na janga la uharibufu wa mazingira hatuna budi kuwekeza zaidi na kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika miradi ya usambazaji na uunganishaji wa gesi majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo usimamizi wa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya *REA*; kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi wa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya *REA* ili Miradi hiyo ikamilike kwa wakati kama ilivyo katika matakwa ya Mikataba yao. Aidha,

ipo haja Serikali kuongeza wigo wa utekelezaji wa Miradi hii ili kuweza kuwafikia watu wengi zaidi katika awamu hii.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni masuala ya jumla ya kisekta eneo hili tunajielekeza katika uwekaji wa vina saba kwenye mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwekaji wa Vinasaba kwenye Mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa hapa nchini ulianzishwa kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuzuia uuzwaji wa mafuta yasiyolipiwa kodi katika soko la ndani yanayokwenda nchi jirani mafuta yenye msamaha wa kodi yanayotumika kwenye miradi maalum na mafuta yanayoweza kuingia nchini kwa kupita njia za panya halikadhalika kudhibiti uchakachujaji wa mafuta unaosababisha kuaribika kwa ubora wa mafuta na Na kwa kuwa katika siku za karibuni umekuwepo mjadala ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba Mzabuni aliyekuwa akifanya kazi ya uwekaji Vinasaba amekuwa akifanya kazi hiyo kwa kutoza gharama kubwa; na kwamba serikali ije na mfumo utakaopunguza gharama hizo ili fedha zitakazookolewa ziweze kuelekezwa kwenye miradi ya Maji na Barabara za Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa kuzingatia ushauri huo Serikali ilifanya Maamuzi ya kulipatia Shirika la Viwango Taifa TBS jukumu la kutoa huduma ya Uwekaji wa Vinasaba kwenye Mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa hapa nchini, kamati inatoa Ushauri ufuatao kuhusu suala hili; Serikali makini na kuchukua taadhari zote muhimu katika kuishughulikia suala hili ili nchi isipate hasara; Serikali ijiridhishe kama kwa sasa TBS inayouwezo wa kutekeleza jukumu hilo bila kuleta athari. Hivyo Sheria inayounda TBS ifanyiwe marekebisho na dhamana na uwezo TBS kutoa huduma hii uwekwe katika sheria na utekelezwe na kanuni madhubuti zinazotengenezwa na sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue jitihada za dhati za haraka katika kujengea uwezo TBS ili iweze kutoa huduma

hii kwa ufanisi msisitizo uwekwe hasa katika eneo la rasilimali watu na teknolojia iliyo sahihi katika utoaji wa huduma hii; Serikali itenge bajeti ya kutosha ili TBS iweze kutekeleza majikumu yake kwa ufanisi na kwa ubora unaotakiwa; grama za huduma ya uwekaji vinasaba inayotolewa na TBS ziwe za chini ikilinganishwa na gharama zilizokuwa zikitozwa na mzabuni wa awali kwa kufanya hivyo mbali ya kuleta unafuu wa mtumiaji wa mafuta ambaye ni mwananchi wa kawaida. Vile vile kutawezesha kufikia kwa lengo la kuokoa fedha na hivyo kuelekeza fedha zilitakazookolewa kwenye miradi ya maji na barabara vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi hiki cha mpito ambacho *TBS* ndio imeanza kutekeleza jukumu hili Serikali ihakikishe taratibu zote za manunuzi zinafuata kikamilifu kwa mujibu wa Sheria za nchi na kwamba lisiwepo ombwe la kiutendaji linaloweza kuleta madhara kwa nchi; *TBS* iipatie kwa haraka *EWURA* vitendea kazi muhimu vinavyohitajika kwamujibu wa makubaliano yaliyopo ili *EWURA* Ukaguzi katika vituo vyote vya mafuta na kuhakikisha kwamba huduma ya vina saba inaendelea kutolewa kwa usahihi ili kuzuia upotevu wa mapato kwa nchi na kuondoa uwezekana wa uchakachujaji wa mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *TBS* ihakikishe katika kipindi kifupi iwezekanavyo inajenga uwezo wa kuzalisha yenyewe vina saba hapa nchi hili kuokoa fedha zinazotumika kununua vina saba hivyo toka kwa wazabuni ambao hutoza fedha nyingi. Serikali ifanye mapitio ya haraka ya sheria iliyoanzisha *EWURA* na kanuni zake ili kuondoa vifungu vinavyochangia kuweko kwa hali ya kutoaminiana kwa kiwango cha hali ya juu miongoni mwa taasisi zinazoshiriki kwenye mfumo wa uwekaji wa vina saba, kwani ipo hofu miongoni mwa washiriki kuwa ipo mianya ya kuwa *victimize* katika suala zima la uwekaji wa vina saba.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo kutawezesha kupatikana kwa suluhu ya njia bora inayoweza kutumika katika uwekaji wa vina saba hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hitimisho nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri mnayoifanya kuliongoza Bunge letu Tukufu mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya wajumbe wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani Mbunge, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato Naibu Waziri wa Nishati pamoja na watendaji wote wa wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Eng. Leonard Masanja na Naibu Katibu Mkuu ndugu Kheri Mahimbali kwa kusimamia vyema shughuli za wizara na kwa ushirikiano wao mkubwa kwa kamati yetu kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru wajumbe wote wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa weledi na umakini waliouonyesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuchukuwa nafasi hii kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano aliotoa kwa kamati wakati wote wa utumishi wake katika Bunge la Tanzania, kwa dhati kabisa namtakia utumishi na mafanikio katika majukumu yake mapya kama Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipee nampongeza sana Katibu wa Bunge mpya ndugu Nenelewa Joyce Mwiambi *ndc* kwa kuteuliwa katika nafasi hii na hasa kwa kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Katibu wa Bunge katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake, nawashukuru sekretarieti ya kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za



Bunge ndugu Athumani Husseni, Mkurugenzi Msaidizi ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati ndugu Felister Mgonja, ndugu Angelina Sanga na ndugu Dunford Mpelumbe kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi Fungu 58 Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama yalivyowasilisha na mtoa hoja ambayo ni Shilingi tirion 2.38.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA  
MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA  
NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021  
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za  
Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba Taarifa yote ya Kamati iliyowasilishwa Mezani iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (9) na Sehemu ya 7(a, c na d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatatazo:-

(a) Kutembelea na Kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 [*Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020*]; na

(b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 [*Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020*].

### 1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Nishati (Fungu 58). Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Pwani na Mwanza. Lengo la ziara ilikuwa ni kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Nishati iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Maji wa Julius Nyerere uliopo Rufiji, Pwani; na

(ii) Miradi ya umeme Vijijini REA III iliyopo Sengerema, Mwanza.

**Mheshimiwa Spika**, ziara ya Kamati kuelekea katika Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Rusumo Mkoani Kagera ulisitishwa Tarehe 18 Machi, 2021 kutokana na Msiba wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ni Rai ya Kamati kwamba kutokana na ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kusitishwa, Ofisi ya Bunge

iangalie uwezekano wa kukamilisha ukaguzi huu katika Mwaka wa Fedha ujao kwa Kadri Mazingira yatakavyoruhusu.

## 1.2 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya Miradi pamoja na changamoto ambazo Kamati ilizibaini kwa kila mradi wakati wa ukaguzi wake:-

### a) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere Rufiji (2,115 MW)

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu Mradi huu yanapatikana ukurasa wa **4 hadi 8** wa taaarifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zilizobainika wakati wa ukaguzi wa Mradi huu ni pamoja na:-

(i) Ubovu wa barabara ya kwenda eneo la Mradi ambao umekua kikwazo katika kutoa huduma mbalimbali zinazohitajika katika Mradi, hususani kipindi cha mvua.

(ii) Utoaji fursa wa kazi mbalimbali katika mradi haujazingatia masuala ya Jinsia hivyo *kusababisha* kuwa na Idadi ndogo ya Wanawake walioajiriwa kwenye Mradi takriban Wanawake **263** tu kati ya jumla ya Wafanyakazi **7132** walioajiriwa ambayo ni asilimia **4** tu ya Wafanyakazi wote.

### b). Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) Mkoa wa Mwanza

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu Miradi ya Wakala wa Umeme Vijini yanapatikana **ukurasa wa 9 hadi 18** wa Taarifa ya Kamati.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

(i) Elimu iendelee kutolewa kwa Wananchi juu ya gharama za uunganishwaji wa huduma ya umeme;

(ii) TANESCO iongeze kasi ya usambazaji wa umeme katika Vijiji vilivyobaki; na

(iii) TANESCO iwe makini na kuharakisha kuwafikia Wananchi pale kunapotokea hitilafu ya umeme kama kuanguka kwa nguzo n.k.

### **1.3 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji na upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo iliyoitembelea chini ya Wizara ya Nishati. Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji Madhubuti wa Miradi hii;

(ii) Kamati inashauri kwamba ajira katika Miradi yote iliyokaguliwa itoe kipaumbele kwa Watanzania na izingatie fursa sawa za Kijinsia ili kujenga uwezo na ustawi wa makundi maalumu katika Jamii hasa Wanawake na Watu wenye ulemavu kwa kadri itakavyowezekana;

(iii) Kwa kuwa maeneo mengi ya Vijiji na Vitongoji yanarukwa katika kusambaziwa huduma ya umeme; na kwa kuwa bado TANESCO wana kasi ndogo sana ya uunganishaji wa huduma ya umeme kwa Wateja, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo (scope) kwa Wakandarasi ili kuweza kukidhi mahitaji ya Wananchi kufikiwa na nishati ya umeme katika maeneo mbalimbali;

(iv) Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi juu ya gharama za uunganishwaji wa huduma ya umeme ili Wananchi wapate uelewa wa namna ya kuunganishwa na huduma ya umeme kwa kuhusisha gharama zinazohusika wakati wa kuunganishiwa na huduma ya umeme.

(v) Pindi inapobainika kuwa Mkandarasi anasuasua kutekeleza majukumu yake ya kimkataba, REA ihakikishe inachukua hatua za haraka kusitisha Mkataba huo kwa kufuata taratibu za kimkataba. Kufanya hivi kutasaidia kuepuka ucheleweshaji wa upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

#### 1.4 Sekta Ndogo ya Gesi Asilia

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu Sekta ndogo ya Gesi Asilia yanapatikana **Ukurasa wa 21 wa** taarifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kutengeneza Mazingira yenye unafuu kwa Sekta Binafsi na hasa Makampuni yanayojishughulisha na Shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi kutokana na Mdororo wa bei ya Mafuta na Gesi duniani.

#### 1.5 Umuhimu wa Kufanya Marejeo ya Mikataba Shirikishi ya Uzalishaji (PSAs)

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu umuhimu wa Kufanya Marejeo ya Mikataba Shirikishi ya Uzalishaji (PSAs) yanapatikana **Ukurasa wa 22 hadi 23 wa** Taarifa ya Kamati.

**Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ya Utekelezaji wa Mikataba hii ili kuhakikisha kwamba Taifa linafaidika na Sekta hii ya Gesi Asilia na kuhakikisha kwamba Watanzania wengi Zaidi wanaendelea kupata fursa za ajira na biashara zinazojitokeza katika uwekezaji unaofanywa katika Sekta hii.**

#### 1.6 Miradi ya Utafutaji wa Gesi Asilia na Mafuta

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu Miradi hii yanapatikana **Ukurasa wa 24 hadi 25 wa** Taarifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, faida Mahsusi zitokanazo na Miradi ya Uendelezaji, Uzalishaji na Usafirishaji wa Mafuta na Gesi Asilia ni kama ifuatavyo:-

(i) Itapunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa Mazingira na Kuni kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya Gesi Asilia nyumbani na Viwandani ambayo inapatikana kwa gharama nafuu;

(ii) Itaimarisha uchumi kwa kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa mafuta na nishati nyingine mbadala;

(iii) Itaongeze uwekezaji wa Kigeni nchini (Foreign Direct Investments); na

(iv) Itatoa fursa kwa Watanzania kujifunza Teknolojia mpya za ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa Mitambo ya kuchakata Gesi Asilia.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima-Kabaale nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga Tanzania unakadiriwa kutumia Dola za Marekani **Bilioni 3.55**. Bomba hili lina urefu wa **Kilomita 1,443**, **Kilomita 366** zikiwa nchini Uganda na **Kilomita 1,137** zikiwa nchini Tanzania. Kwa upande wa Tanzania Bomba litapita katika Mikoa 8 na Wilaya 24.

Baadhi ya faida za Mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Utaimarisha Matumizi ya Bandari ya Tanga na hivyo kuongeza Mapato yatokanayo na shughuli za Bandari;

(ii) Utaongeze Uwekezaji wa Kigeni nchini "Foreign Direct Investments";

(iii) Utatoa fursa kwa Watanzania kujifunza Teknolojia mpya za ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa Mabomba ya Mafuta; na

(iv) Utaongeze fursa za biashara kwa Watanzania wakati wa Ujenzi na baada ya Ujenzi kukamilika.

### 1.7 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini yanapatikana Ukurasa wa **27 hadi 30** wa Taarifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na Wizara kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine. Ili kuuboresha zaidi mfumo wetu ni Rai ya kamati kuwa ipo haja ya kufanya mapitio ya mfumo wetu kwa lengo la kuuboresha ili uweze kuvutia ushiriki wa Makampuni mengi zaidi kwenye minada ya uagizaji wa mafuta na hivyo kuwezesha nchi kunufaika na ushindani wa soko katika kupata mafuta kwa uhakika na kwabei nzuri kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, tayari Ulimwengu umeanza kushuhudia Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii kusimama, biashara na uzalishaji Viwandani kushuka na hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta. Kufuatia kushuka kwa matumizi ya mafuta ulimwenguni tumeshuhudia vilevile katika siku za hivi karibuni bei ya mafuta kwenye soko la kimataifa kushuka kwa kiwango kikubwa ambacho hakijawahi kushuhudiwa. **Hivyo basi kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa soko la mafuta ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka Mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote. Aidha, Serikali itumie mwanya huu wa mdororo wa bei ya mafuta ulimwenguni kuzungumza na nchi rafiki zinazozalisha mafuta ili kama nchi tuweze kupata mafuta kwa masharti nafuu sasa, na kupitia TPDC tuweze kuanzisha hifadhi ya mafuta ya Kimkakati kwa ajili ya kuhami uchumi wetu kwa siku zijazo.**

### 1.8 Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu hali ya upatikanaji wa Umeme nchini yanapatikana **Ukurasa wa 32 hadi 33** wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kulitokea tatizo kubwa la Upatikanaji wa Huduma ya Luku kutokana na sababu zinazohusiana na matatizo ya kimfumo. Athari za tatizo kama hili ni kubwa katika Uchumi na ustawi wa wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Tatizo hili halijirudii na jitihada za dhati zichukuliwe ili kuwa na mifumo ya ndani inayotumika katika utoaji wa huduma ya Luku nchini.

#### 1.9 Tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini (REA III) Mzunguko wa Tatu

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu tathmin ya Miradi ya Umeme Vijijini (REA III) Mzunguko wa Tatu YANAPATIKANA Ukurusa wa 34 hadi 36 wa Taarifa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ipo haja ya Wakandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa Miradi hii, hata hivyo, Serikali inapaswa kuendelea kuweka nguvu ya kiusimamizi na ufuatiliaji wa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi hii kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na matakwa ya Mikataba. Aidha, iko haja ya Serikali kupanua wigo (scope) wa utekelezaji wa Miradi hii ili kuwafikia Watanzania wengi kwa wakati mfupi.

### SEHEMU YA PILI

#### 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo Makuu matatu ambayo ni:- Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2020/2021; Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; na Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.



## 2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Nishati ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 602.05**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi Bilioni 602.04** zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na Gesi Asilia na **Shilingi 12,000,000.00** kupitia shughuli za Utawala. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo; Shughuli za TPDC za utafiti wa mafuta; Mauzo ya Gesi Asilia; na Mauzo ya Nyaraka za Zabuni.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Februari 2021 jumla ya **Shilingi Bilioni 377.15** zilikusanywa kutokana na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia zilizoratibiwa na TPDC. Kamati ilibaini kuwa kiasi hicho ni sawa na **asilimia 89.5** ya lengo la makusanyo ya **Shilingi Bilioni 421.36** kwa kipindi hicho. Aidha, **Kamati inatoa rai kwa Wizara kuendelea na jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo vya Mafuta na Gesi Asilia.**

### (a) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Bunge lako Tukufu liliidhinisha Bajeti ya Jumla ya **Shilingi 2,196,836,774,000** kwa Wizara ya Nishati. Kati ya Fedha hizo, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 2,168,437,184,000** sawa na **asilimia 98.7** ya bajeti yote ya Wizara. Aidha, kati ya fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, **Shilingi 1,957,689,292,000** sawa na **asilimia 90.7** ya Bajeti yote ya Maendeleo ni fedha za ndani, na **Shilingi 200,747,892,000** sawa na **asilimia 9.3** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 ni **Shilingi 28,339,590,000** sawa na **asilimia 1.3** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 13,373,769,000** kwa ajili

ya kulipa Mishahara (P.E) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Februari 2021 Fedha zilizopokelewa kwa bajeti ya Wizara ya Nishati ni **Shilingi Bilioni 801, 028,895,524** sawa na **asilimia 69.5** ya lengo la miezi minane (8). Kati ya Fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi Bilioni 11,109,213,999** ni fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) ambayo ni sawa na **asilimia 100** ya lengo na **Shilingi bilioni 7,031,719,470.00** ni Mishahara sawa na **asilimia 78.9** ya lengo.

Aidha, **Shilingi 782,887,962,055** ni za Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 69.11** ya lengo la fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni 595,257,575,145** sawa na **asilimia 60.16** ya lengo na **Shilingi 151,348,519,972** sawa na **asilimia 105.6** ya lengo la fedha za nje. Kamati ilibaini kuwa utolewaji wa Fedha hizo umezingatia malipo kwa kazi ambazo tayari zimekamilika na hati za madai (*certificates and invoices*) kuwasilishwa na kuhakikiwa. Aidha, Kamati ilibani vilevile kuwa ipo baadhi ya Miradi ambayo hupokea fedha za nje moja kwa moja, hivyo Taarifa zake huingizwa katika Hesabu za Wizara mwisho wa mwaka husika wa fecha.

Kwa kazi ambazo zinaendelea, Kamati ilielezwa kuwa madai yake hayajawasilishwa kwa ajili ya malipo, na kwamba pindi kazi husika zikikamilika na hati za madai husika kuwasilishwa na kuhakikiwa; madai hayo yatalipwa.

**Ni Rai ya Kamati kuwa mara baada ya madai husika kuwasilishwa, uhakiki wa madai hayo ufanyike kwa haraka ili Fedha za Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa wakati.**

**Mheshimiwa Spika**, muhtasari wa fedha zilizopokelewa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi february 2021 unapatikana Ukurasa wa 40 wa taarifa ya Kamati.

(b) **Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na

Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Juni, 2020. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi unaendelea kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Maoni ambayo kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi yameainishwa **Ukurasa wa 41 hadi 42** wa Taarifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika, Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kufanyia kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati.**

## **2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 (Fungu 58).**

### **2.1.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Nishati inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wake. Kulingana na Mpango Mkakati huo Wizara ina malengo makuu sita (6) kama yanavyoonekana katika taarifa ya Kamati **Ukurasa wa 43** wa Taarifa ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo hayo Wizara inapaswa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta ya Nishati ikiwemo kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.

## **2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi**

### **2.2.1 Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 2,385,980,809,000** ikilinganishwa na **Shilingi 2,196,836,774,000** zilizotengwa kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 sawa na ongezeko la **asilimia 8**. Kati ya fedha hizo

**Shilingi 2,358,756,128,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi 27,224,681,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 ni **Shilingi 27,224,681,000** sawa na **asilimia 1.1** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 12,198,860,000** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

### 2.2.2 Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa Fedha 2021/2022 unakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,358,756,128,000** ambazo ni sawa na **asilimia 98.9** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 2,178,756,128,000** sawa na **asilimia 92.4** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa kiasi kikubwa cha fedha za ndani za Maendeleo kimeelekezwa katika Miradi ya kielelezo na Kimkakati ambayo ni:-

- (i) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere, **MW 2,115**;
- (ii) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu;
- (iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I Extension **MW 185**; na
- (iv) Miradi ya Ruhudji, Rumakali, Singida - Arusha - Namanga, Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Kigoma na LNG, EACOP.

Aidha, Bajeti ya Fedha za Nje inayopendekezwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 180,000,000,000** sawa na **asilimia 7.6** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 yanapatikana ukurasa wa 46 wa Taarifa ya Kamati.

### 2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 20,393,000** kutokana na Shughuli za Utawala. Makadirio ya ukusanyaji Maduhuli katika Mwaka wa fedha 2021/2022 yamepungua kwa asilimia takribani 100 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo Makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli yalikuwa **Shilingi 602,000,000/=**.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba wakati ambapo ukusanyaji wa Maduhuli uliokua ukifanywa na Wizara ukishuka, ukusanyaji Maduhuli kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 umeongezeka kwa takribani **Asilimia 100**. Ongezeko hili limetokana na Mabadiliko ya Sera ya Ukusanyaji Maduhuli katika Sekta hii ambayo kwa sasa inataka TPDC ndiyo ikusanye Mapato yanayotokana na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kuziweka hizo fedha katika Mfuko wa Fedha zitokanazo na Shughuli za Utafutaji wa Gesi Asilia (Natural Gas Reserves Fund), jambo ambalo halikufanyika katika mwaka wa fedha 2020/2021.

### 2.2.4 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ulinganisho huo ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati katika mwaka ujao wa fedha. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

(i) Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni **Shilingi Trilioni 2,358,756,128,000** ni sawa na asilimia **6.5** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni **Shilingi Trilioni 36.3 /=**.

(ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa **asilimia 4** ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; wakati Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa **asilimia 8** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021; na

(iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la **asilimia 2.76** katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na **asilimia 36.68** ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022; wakati bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Nishati ambayo ni sawa na **asilimia 6.5** ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa **asilimia 8.6** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Nishati dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 umeonyeshwa katika **Jedwali Na.02:** ukurasa wa 49 wa Taarifa ya Kamati.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ina Maoni na Ushauri ufuatao kwa Serikali:-

#### 3.1 Utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere - MW 2,115

**Kwa kuwa** Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji katika Bonde la Mto Rufiji (Julius Nyerere - MW 2,115) una umuhimu wa Kimkakati kwa uchumi wa Taifa letu;

**Na kwa kuwa** katika mwaka wa Fedha 2020/2021 utekelezaji wake ulijielekeza katika ujenzi wa Miundombinu wezeshi kama vile ujenzi wa bwawa (Main dam and Spill ways, ujenzi wa njia Kuu za kupitisha maji (Tunnels), ujenzi wa Kituo cha kuzalishia umeme (Power House) na ujenzi wa Kituo cha kusafirishia umeme (Switch Yard);

**Hivyo basi** katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza usimamizi, na kuhakikisha Fedha za uendelezaji wa Mradi zinapatikana kwa wakati kama zilivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge ili kufikia lengo la kuanza kupokea Maji kwa bwawa hili ifikapo Mwezi Novemba 2021 na kuanza Uzalishaji ifikapo mwezi Juni, 2022.

### 3.2 Utekelezaji wa Ufanisi wa Miradi yote ya Maendeleo

**Kwa kuwa** Wizara ya Nishati ni Wizara ya Kimkakati na iliyo na mchango Mkubwa sana katika pato na uchumi wa Taifa;

**Na kwa kuwa** Wizara hii ni Wizara pekee ambayo asilimia **98.9** ya Bajeti yake yote ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

**Hivyo basi** Kamati inatoa Rai kwa Serikali kutoa Fedha kwa Wakati ili kutekeleza kwa Ufanisi Miradi yote ya Maendeleo na ya Kimkakati iliyo chini ya Wizara (National Flagship and Strategic Projects).

### 3.3 Umuhimu wa Kuwalipa Wakandarasi wa Miradi hii kwa Wakati

**Kwa kuwa** Miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na Wizara ni muhimu sana katika kuchangia pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi kwa ujumla;

**Na Kwa kuwa** Miradi hii inatumia Wakandarasi mbalimbali na Watoa huduma kutoka Ndani na nje ya nchi;

**Hivyo basi** Kamati inashauri Serikali kulipa kwa Wakati Madeni na Fedha zote zinazotakiwa kulipwa kwa Wakandarasi hao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa wakati kwa ajili ya kuikamilisha Miradi hii ndani ya lengo lililowekwa.

### **3.4 Bei ya Umeme unaozalishwa na Wazalishaji Wadogo (SPPs/Minigrids)**

**Kwa kuwa** Serikali ilifanya uamuzi mahsusi wa kuwashirikisha wazalishaji wadogo wa umeme (Small Power Projects – SPP) kuwekeza nchini ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa uhakika kutoka katika vyanzo mchanganyiko;

**Na kwa kuwa** Wazalishaji Wadogo waliitikia wito wa Serikali kuwekeza na sasa uzalishaji wao wa umeme umefikia asilimia 13.43, ili kulinda uwekezaji ambao tayari umefanywa na Wazalishaji Wadogo ambao wanahudumia zaidi ya wateja 100,000 hapa nchini;

**Na kwa kuwa** ili kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji kuwa mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanatabirika;

**Hivyo basi, Kamati inaona ipo haja** kwa Serikali kuharakisha kuweka mfumo unaoendelea kuvutia uwekezaji katika miradi ya wawekezaji binafsi ya kuzalisha umeme na yenye nafuu ya bei kwa wateja wa umeme.

### **3.5 Kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Nishati**

**Kwa kuwa** Sekta ya Nishati ni Muhimu katika kuchangia Pato la Nchi na Ukuaji wa Uchumi;

**Na kwa kuwa** Mazingira ya Uwekezaji Tanzania ni mazuri na yanaruhusu Wawekezaji kutoka nje;

**Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutengeneza Mazingira rafiki zaidi kwa Wawekezaji ili wapate motisha ya kuwekeza katika Sekta ya Nishati kwa kutumia Sera, Sheria,



Kanuni na Miongozo mbalimbali iliyopo. Aidha, Miongozo ya kutangaza Miradi inayotekelezwa kwa kutumia vyanzo vya Makaa ya Mawe, Jua, na Upepo kwa njia ya ushindani iendelee kutumika na Zabuni husika kutangazwa kwa uwazi ili Miradi mipya inapokuja Michakato ya kupata Wakandarasi ifanyike kwa ufanisi na uwazi.

### 3.6 Matumizi ya Gesi Asilia Majumbani

**Kwa kuwa** Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petrol (TPDC) imeanza kutekeleza Miradi ya usambazaji wa Gesi Asilia katika maeneo ambayo tayari kuna Miundombinu wezeshi;

**Na kwa kuwa** mpaka sasa tayari Miundombinu yenye urefu wa **Kilomita 10.8** imejengwa ikiwa na uwezo wa kuunganisha zaidi ya nyumba 10,000; **kwa mtazamo wa Kamati** kasi ya uunganishwaji gesi asilia majumbani hailingani na uhitaji uliopo, wala kasi ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi makubwa ya nishati ya mkaa nchini;

**Hivyo basi** ili tuweze kunusuru nchi yetu na janga hili la uharibifu wa mazingira hatuna budi kuwekeza zaidi na kuruhusu Sekta Binafsi kushiriki katika Miradi ya usambazaji na uunganishaji wa gesi majumbani.

### 3.7 Tahadhari ya Athari za COVID -19, Kuhusiana na Upatikanaji na Matumizi ya Mafuta Nchini

**Kwa kuwa**, katika mwaka wa Fedha 2020/21 Dunia imekabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu (COVID -19);

**Na kwa kuwa** changamoto hii imesababisha kuwepo na mdororo wa uchumi duniani ambao uliathiri Sekta ya usafiri wa Anga, Utalii, Biashara, Uzalishaji Viwandani na kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi na biashara ya Mafuta na hivyo kuathiri bei ya mafuta katika soko la Kimataifa;

**Na kwa kuwa** licha ya kuendelea kuwepo kwa tishio la ugonjwa wa Homa ya Mapafu Duniani , kwa siku za hivi karibuni mwenendo wa bei za mafuta katika soko la Dunia umebadilika na hivyo kuathiri mwenendo wa bei nchini;

**Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Mfumo wetu wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ili kuweka Mikakati Madhubuti ya kuongeza ushindani na kuvutia ushiriki wa Makampuni mengi zaidi ya Mafuta kushiriki katika minada ya kuingiza mafuta nchini ili ushindani huo ulisaidie taifa kupata mafuta kwa uhakika, kwa wakati, na kwa bei ya chini.

### **3.8 Ulipaji wa Haraka wa Fidia kwa Wananchi katika Miradi inayotekelezwa na Serikali;**

**Kwa kuwa** Serikali inaendelea kutekeleza Miradi mbalimbali ya Kimkakati katika mwaka ujao wa fedha;

**Na kwa kuwa** utekelezaji wa Miradi hii unaathiri haki mbalimbali za Wananchi wa maeneo husika;

**Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kulipa fidia stahiki kwa Wananchi wote wanaoguswa na utekelezaji huu ili kuwapa nafasi na uwezo wa kuhamia maeneo mengine na kuweka mazingira sahihi ya kuendelea na shughuli mbalimbali za kiuchumi na uzalishaji mali.

### **3.9 Utaratibu wa uagizaji wa Liquefied Petroleum Gas (LPG)**

**Kwa kuwa** matumizi ya Gesi ya LPG hapa nchini yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku;

**Na kwa kuwa** gharama ya upatikanaji wake ni kubwa, hali inayosababisha bei kwa mtumiaji wa mwisho kuwa juu;

**Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi zake husika, hususani EWURA, WMA, TPA, TRA pamoja na Wafanyabiashara wa LPG kuendelea kukaa pamoja kuja na mapendekezo yatakayowezesha Gesi ya LPG kupatikana nchini kwa Mfumo wenye tija kwa watumiaji na Taifa kwa ujumla.

### **3.10 Usimamizi wa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya REA;**

**Kwa kuwa** bado zipo changamoto kadhaa katika Miradi ya REA;

**Na kwa kuwa** mzunguko wa Pili wa Awamu ya Tatu ya REA umeshaanza;

**Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi wa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya REA ili Miradi hiyo ikamilike kwa wakati kama ilivyo katika matakwa ya Mikataba yao. Aidha, ipo haja Serikali kuongeza wigo (scope) wa utekelezaji wa Miradi hii ili kuweza kuwafikia watu wengi zaidi katika awamu hii.

### **3.11 Udhhibiti wa upotevu wa Mafuta katika Miundombinu ya kupokelea mafuta**

Ili kuendelea kudhibiti upotevu wa Mafuta katika Miundombinu ya upokeaji wa Mafuta, Kamati inashauri Kampuni zote za Mafuta zinazomiliki Hifadhi za Mafuta kufunga *flowmeters* kwa kila njia ya kupokelea Mafuta. Aidha, Serikali kupitia wakala zake wasimamie zoezi hili ili kuhakikisha linatekelezwa kikamilifu na kwa wakati.

### **3.12 Wigo wa kutoa huduma kwa Wananchi wa Mijini na Vijijini**

Serikali ielekeze TANESCO kubuni njia bora zaidi ya kusogeza huduma zake karibu na Wananchi bila kutumia gharama kubwa kwani wateja wengi hususan wa sehemu za Vijijini wanakosa huduma kwa kuwa maeneo yao hayajafikiwa na Ofisi za TANESCO.

## **MASUALA YA JUMLA YA KISEKTA**

### **3.13 Huduma ya Uwekaji Vinasaba Kwenye Mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa Nchini Tanzania**

**Kwa kuwa** uwekaji wa Vinasaba kwenye Mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa hapa nchini ulianzishwa kwa lengo

la kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuzuia uuzwaji wa mafuta yasiyolipiwa kodi katika soko la ndani (Mafuta yanayokwenda nchi jirani, mafuta yenye msamaha wa kodi yatumikayo kwenye miradi maalum, na mafuta yanayoweza kuingia kwa kupitia njia za panya), na halikadhalika kudhibiti uchakachujaji wa mafuta unaosababisha kuharibika kwa ubora wa mafuta;

**Na kwakuwa** katika siku za karibuni umekuwepo mjadala ndani ya Bunge kuwa Mzabuni aliyekuwa akifanya kazi ya uwekaji Vinasaba amekuwa akifanya kazi hiyo kwa kutoza gharama kubwa; na kwamba serikali ije na mfumo utakaopunguza gharama hizo ili fedha zitakazookolewa ziweze kuelekezwa kwenye miradi ya Maji na Barabara za Vijijini

**Na kwa kuzingatia** ushauri huo Serikali ilifanya Maamuzi ya kulipatia Shirika la Viwango Tanzania (Tanzania Bureau of Standards) jukumu la kutoa huduma ya Uwekaji wa Vinasaba kwenye Mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa hapa nchini, kamati inatoa Ushauri ufuatao kuhusu suala hili;

i) Sheria inayounda TBS ifanyiwe Marekebisho na dhamana na uwezo wa TBS kutoa huduma hii uwekwe katika Sheria na Utekelezwe na Kanuni Maalumu zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii;

ii) Serikali ichukue jitihada za dhati na za haraka katika kujengea uwezo TBS ili iweze kutoa huduma hii kwa ufanisi. Msisitizo uwekwe hasa katika eneo la Rasilimali watu na matumizi ya Teknolojia iliyo sahihi katika utoaji wa huduma hii;

iii) Serikali itenge bajeti ya kutosha ili TBS iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa ubora unaotakiwa;

iv) Gharama za huduma ya uwekaji Vinasaba inayotolewa na TBS ziwe za chini ikilinganishwa na gharama zilizokuwa zikitizwa na mzabuni wa awali; kwa kufanya hivi mbali na kuleta unafuu kwa mtumiaji wa mafuta ambaye ni

mwananchi wa kawaida, vilevile kutawezesha kufikiwa kwa lengo la kuokoa fedha; na hivyo kuelekeza fedha zitakazookolewa kwenye miradi ya Maji na Barabara za Vijijini;

v) TBS iendelee kutoa Mafunzo kwa watumishi wake ili kujenga uwezo kwa watumishi wake katika kada mbalimbali ili kutoa huduma hii kwa ubora na utaalamu sahihi;

vi) Katika kipindi hiki cha mpito ambacho TBS ndio imeanza kutekeleza jukumu hili Serikali ihakikishe taratibu zote za manunuzi zinafuata kikamilifu Sheria za nchi zilizopo; na kwamba lisiwepo ombwe la kiutendaji linaloweza kuleta madhara kwa nchi.

vii) TBS iipatie kwa haraka EWURA vitendea kazi muhimu vinavyohitajika kwamujibu wa makubaliano yaliyopo ili iendelee kufanya Ukaguzi katika vituo vyote vya Mafuta na kuhakikisha kwamba huduma ya Vinasaba inaendelea kutolewa kwa usahihi ili kuzuia upotevu wa mapato kwa nchi na kuondoa uwezekano wa uchakachujaji wa Mafuta (Adulteration);

viii) TBS ihakikishe katika kipindi kifupi iwezekanavyo inajenga uwezo kuzalisha yenyewe Vinasaba hapa nchini ili kuokoa fedha zinazotumika kununua vinasaba hivyo toka kwa wazabuni ambao hutoza fedha nyingi (kwasasa TBS inanunua vinasaba toka kwa kampuni ya **SISPA SA** ambayo ni mbia wa mzabuni wa awali kampuni ya GFI);

ix) Serikali ifanye mapitio ya haraka ya Sheria iliyoanzisha EWURA na Kanuni zake ili kuondoa vifungu vinavyochangia kuwepo kwa hali ya kutoaminiana kwa kiwango cha hali ya juu miongoni mwa taasisi zinazoshiriki kwenye mfumo wa uwekaji Vinasaba, kwani ipo hofu miongoni mwa washiriki kuwa ipo mianya ya kuwa victimised. Kufanya hivi kutawezesha kupatikana kwa suluhu ya njia bora inayoweza kutumika katika uwekaji na ukaguzi wa Vinasaba.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kulliongoza Bunge hili Tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi.

Aidha, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemuni (Mb), Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato (Mb) - Naibu Waziri wa Nishati, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Eng. Leonard Masanja na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Kheri A. Mahimbali kwa kusimamia vema shughuli za Wizara na kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge:-

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru aliyekua Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano aliotoa kwa Kamati wakati wote wa Utumishi wake katika Bunge la Tanzania. Kwa dhati kabisa namtakia utumishi wa mafanikio katika majukumu yake mapya kama Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Kipekee nampongeza sana Katibu wa Bunge Mpya Ndg. Nenelewa J. Mwihambi, kwa kuteuliwa katika nafasi hii na hasa kwa kuwa Mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Katibu wa Bunge katika historia ya Nchi hii. Tunamtakia utekelezaji mwema wa Majukumu yake. Nawashukuru Sekretariati ya Kamati hii ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Ndg. Felister Mgonja, Angelina

Sanga na Ndg. Dunford Mpelumbe kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja ambayo ni **Shilingi 2,385,980,809,000**.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Dunstan Luka Kitandula, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

2 Juni, 2021.

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Kitandura kwa kutupitisha katika maoni ya Kamati na naipongeza sana Kamati kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya ya kuchambua kwa umakini mkubwa masuala yanayohusiana na Wizara hii ya Nishati. Tunawashukuruni sana kwa niaba yetu. (*Makofi*)

Sasa tunaingia katika uwanja wa uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Shanif Mansoor na atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage na Mheshimiwa Anton Mavunde ajiandae.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kipekee ya upendeleo niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukuwe nafasi hii pia ku-*declare interest* mimi ni mdau kwenye biashara ya mafuta na mdau mkubwa kwa Wizara ya Nishati. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana

ambayo ameitoa leo hapa pia naomba nichukuwe nafasi hii kuunga mkono hotuba yake mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mie nitachangia maeneo machache la kwanza ningeomba kuchangia kwenye sehemu ya *REA* III. Mpango wa kuusambaza umeme vijijini, kwenye Jimbo la Kwimba umeanza miaka mingi 2013 *REA round* III, ilianza kuna vijiji tulikuwa tumekubaliana tulipewa orodha kwamba vitapata umeme kwenye miaka miwili ya 2019 na 2020.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *REA* III kwenye Jimbo la Kwimba unasuasua sana kuna maeneo mkandarasi anasuasua sana wameweka nguzo lakini waya bado hajasambaza umeme kwa kweli unaenda kwa suasua sana kwa wananchi, pia kuwaunganisha wananchi pia imekuwa ni changamoto kwa sababu ukienda kwenye *REA* unaambiwa elfu 27 wananchi wakienda kwenye Ofisi ya *TANESCO* waambiwa 177,000 kwa kweli ni mkanganyiko mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri aliweke wazi kwamba Jimbo la Kwimba ni jimbo ambali lina vijiji 59 ina mitaa 14 lakini ni sehemu ambayo kama kijiji kwa hiyo inatakiwa iwe ni bei ya 27,000 lakini kuna maeneo wananchi wanatozwa 177,000 wanashindwa kulipa na pia kuunganisha wananchi wengi sana wameshalipia lakini kuunganisha umeme pia ni shida sana.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri pia kwamba *TANESCO* kila mradi ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amewapa *TANESCO* watafanya, lakini *TANESCO* naona kama uwezo wao utakuwa umekuwa ni mdogo sana kwa sababu kila mradi *TANESCO* unatekeleza. Ningeshauri pia maeneo mengine tuweke wakandarasi waweze kusaidiana na *TANESCO* tukiwapa *TANESCO* kazi zote hizi za kuunganisha wananchi nyumbani kwao itakuwa ni shida sana ningeshauri pia wakandarasi wengine waweze kuunganisha wananchi wapate umeme kwa haraka.



Mheshimiwa Spika, *TANESCO* nafikiri *out-stress* hawana watumishi wa kutosha wapo lakini hawatoshi kwa sababu kazi ni kubwa tunataka tufike vijiji vyote vipate umeme awamu hii sasa maana yake lazima tufanye kazi ya ziada.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la *REA* ningeomba hilo walifanyie kazi lakini pia maeneo mengi wanaweka nguzo za miti lakini kwetu kwenye Jimbo la Kwimba kuna maeneo wakati mvua ikinyesha maji yanapita nguzo zinaanguka wanarudia kazi ya marudio imekuwa nyingi sana. Ningeshauri kwamba kuna maeneo wanaona ni korofi waweke nguzo za zege kwa nini wanarudia kwa hiyo watu wanapenda kufanya kazi ya marudio maana yake labda inalipa posho kwa hiyo watu wacha turudie lakini wananchi pia wanapata shida. Umeme unakatika mara kwa mara kwa sababu ya nguzo zimeanguka mimi ningeshauri maeneo korofi mengine waweke nguzo za zege angalau kazi isiwe ya kurudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ningependa kuisemea ni sehemu ya *EWURA* nimeshasema kwamba ni mdau kwenye sheria ya *EWURA* ningeomba kama ungeweza kukubali ungeagiza Serikali waletе sheria *EWURA* ifunguliwe upya hapa Bungeni tuanze kuiangalia upya kwa sababu sheria *EWURA* tuliunga miaka 20 iliyopita. Sasa hivi sheria *EWURA* imekuwa ni sheria kandamizi kwa vituo vya mafuta, imekuwa kandamizi kwenye kuendeleza sekta ya mafuta kwa sababu faini zao zimekuwa ni kubwa sana kwenye vituo ambavyo kwa kweli vituo vinashindwa kulipa vinakula mtaji. Tunataka vituo viende mpaka vijijini lakini masharti na kanuni za *EWURA* hazitafanya mtu apeleke kituo kwenye Kijiji kwa sababu gharama zao ni kubwa sana kwanza kupata kibali ni gharama mazingira ukienda vibali ni vingi sana ningeomba suala hili la *EWURA* tuliangalie kwa upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza *EWURA* wamekamata maji, nishati, mafuta nao wamezidiwa, ningeshauri hii sheria iangaliwe upya labda tuwe na taasisi inasimamia maji peke yake, kuna taasisi inasimamia nishati peke yake, kuna taasisi inasimamia mafuta peke yake. Kwa hiyo, sasa hivi ukiangalia

Bodi wa *EWURA* pia inateuliwa na Waziri wa Maji lakini huku Waziri wa Nishati nae anatakiwa afanye kazi na wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inakuwa ni ngumu sana ningeshauri *EWURA* tungeweza kuifumua upya tena sheria yake tukawa na taasisi tofauti tofauti. Mfano nilikwambia juzi *EWURA* wametangaza kwamba gari ya abiria ikiingia kwenye kituo utatozwa faini milioni 7 kwenye kituo, sasa mwenye kituo una makosa gani kama basi imeingia na abiria anataka mafuta unatozwa wewe milioni 7. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, milioni saba ni pesa nyingi sana kwenye kituo, labda uuze lita laki moja ndio upate milioni 7 hiyo, maana yake hizi faini wanazitoa wapi sijui ningeomba tuliangalie hili kwa undani sana kwamba hizi faini zimekuwa ni kubwa sana mfano ukikutwa na kosa na *EWURA* unatozwa faini ya milioni tano kosa la pili milioni 10 kosa la tatu milioni 20 kosa ya nne unafungiwa sasa hizo pesa ni nyingi sana ningeomba suala hili la *EWURA* tuliangalie upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uliagize waambie wakuletee faini wanazozitoa *EWURA* utashanga kituo huwezi kuendesha hii sekta ya mafuta kutoa huduma vijijini inataka iwe tuboreshe huduma ya mafuta ipatikane mpaka vijijini haitafika huko kwa sababu masharti haya hatutafikisha huko tuisaidie Serikali tuangalie utaratibu mpya wa kupata vibali vya kujenga pia vibali vya kujenga vijijini pia vina masharti kibao unawaambia milioni 2 ulipie mazingira pia umpe usafiri wa kufika kwenye eneo husika kweli vibali ni vingi sana hatupata maendeleo kwenye sekta hii, ningeshauri hilo kwamba *EWURA* tuliangalie upya ili tuweze kufanikisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ningependa kuchangia ni sehemu ya vina saba nawashukuru sana Serikali wamefanya maamuzi mazuri kwamba *TBS* wasimamie vina saba waweke *TBS*, lakini sheria ya *TBS* ni kusimamia ubora wa mafuta kwenye sheria yao hawana sheria ya kusema pia vina saba ni sehemu ya kazi yao. Kwa hiyo, muhimu sana tuangalie hiyo sheria ya *TBS* kama inawaruhusu kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, pia suala lingine pia tumelisema sana kwamba *GFI* alikuwa ni mkandarasi wa nje alipata gharama kubwa lakini lazima tujuwe *GFI* alikuwa ni mwekezaji ni kampuni ya kitanzania, *GFI* ni Tanzania *Limited* ni kampuni ambayo inalipa kodi ndani ya nchi yetu. Lazima tulijue hili kwa sababu hawa ni wawekezaji sisi tunataka Mheshimiwa Rais amesema anataka wawekezaji waje ndani ya nchi basi tuwe na utaratibu wa kuwatoa kwenye mikataba kwa sababu tunataka wawekezaji waje watulipe kodi *GFI* atalipa kodi kila mwezi analipa *VAT* analipa kodi ya mapato, *TBS* hizo atalipa.

Mheshimiwa Spika, tumeamua tunaenda huko lakini ninachosema tuwe na *process* ya kuachana na mtu kwa utaratibu hilo ndio nimeona niliseme mimi kuhusu vina saba napongeza Serikali kwa maamuzi kwamba *TBS* wafanye lakini pia utaratibu mwingine ni kwamba *TBS* sasa hivi wananunua vina saba, kwa walewale wazungu wako na ubia na *GFI*. Kwa hiyo, lazima wajibadilishe pia. Watafute tenda watangaze wanunue kwa utaratibu wa Serikali sasa hivi inanunuliwa bila kufuata utaratibu kwa hivi ni muhimu ningeshauri Serikali wafanye utaratibu *TBS* wanunue kwa utaratibu wa *PPRA* wafuate sheria zote za nchi ili tupate unafuu, unafuu wa vina saba tunapoelekea kwamba tu-save pesa kwenye gharama za vina saba ili tupate pesa kwenye *TARURA* basi tufike pale kwenye lengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mansoor Shanif. Sasa nilimtaja Mheshimiwa Charles John Mwijage kwamba ndiye atakayefuata, Mheshimiwa Anthony Mavunde ajiandae na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Nishati na kabla sijaanza kuchangia nipende kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri kwamba nimepata simu kutoka kwa *Engineer* Maro na *Engineer* Said wa *TANESCO*

na *Engineer* Fumbuka nashukuru sana wamefika kwetu wanasema Wilaya ya Muleba watashughulikia vijiji 22 lakini nikasema mzee wa Mbongoshi mbona niliomba 28?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru kwa 22 na endelea kuomba kwa vile vinane lakini katika vile vijiji vilivyobaki kuna Kijiji kimoja kina utata, Kijiji cha Bugasha, kilichopo kando kando ya jeshi la Kaboya ambacho kinapiganiwa na watumiaji wetu mzee angaliaangalia uwape kipaumbele vijana wale wana kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia, ni mdau wa mafuta ni mtoto wa sekta hii na leo nitachangia nishati upande wa mafuta tu. Najua unajua, niliingia kwenye sekta hii mwaka 1984 nikiwa kijana navaa kaki na malapulapu na *radio call* nikifungua *valve* la kupima matenki mapenzi ya Mungu nikapanda mpaka nikawa Naibu Waziri Nishati. yaani kutoka kufungua *valve* mpaka kuwa Naibu Waziri unaweza kuona mambo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafuta ni jambo muhimu na katika ukusanyaji wa mapato sekta ya mafuta inasaidia Serikali kukusanya mapato kwa kutumia jasho kidogo. Yaani *TRA* wanakuta pesa zinakuja mezani kwa kutumia sekta ya mafuta, tunatumia lita karibu bilioni 3.14 kwa mwaka, na kwa *petrol* Serikali inakusanya shilingi 792, *diesel* shilingi 668 kwa kila lita na mafuta ya taa shilingi 615. Mafanikio ya umeme tumepata mafanikio mazuri makubwa sana katika kusambaza umeme yametokana na sekta ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka ukiwa umekaa kiti hicho ukiwa Naibu Spika na mimi nikiwa mjumbe wa kamati nikiwa pale nimeshika *microphone* tuliweza kutenga pesa zilizoweza kusababisha *REA* isambaze umeme kiasi hiki. Lakini hata kasi hii tunayoiyona ya *RUWASA* kusambaza maji kama anavyosema Waziri wa Maji kwamba unapomuona Kobe juu ya mti ujue amepandishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji imepandishwa na sekta ya mafuta kwa sababu ile pesa *ring fenced* ya mafuta

ndio inasababisha kasi hii tunayoiona. Hata sekta nyingine iwe reli, iwe nini wana pesa wanapata kutokana na mafuta. Mheshimiwa imebidi niyaseme hayo ninapokumbuka miaka 37 ya utumishi katika sekta ya mafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie bomba la mafuta niwapongeze marais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Jeneral Kaguta Museveni wa Uganda kwa kufanikisha mchakato wa bomba la mafuta kufika hapa.

Mheshimiwa Spika, kwangu katika bomba la mafuta la zaidi la mno ni kwamba kuwa na mkuza wa bomba la mafuta unasaidia kuamasisha utafutaji wa mafuta kitaalam sisi tunayo mafuta katika bonde la kutoka Albert kushuka mpaka Tanganyika na Rukwa Eyasi Wembele kuja mpaka kwetu huku. Lakini zile wanaziita *stranded reserve* lakini zile wanaziita *stranded reserve* yani ni *reserve* ziko uwezi kuzifikia kwa sababu hakuna miundo kuwepo kwa bomba ili kutatusaidia, ndio faida kubwa ninayoiona ninachoomba kazi kubwa iendelee.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa wakati napongeza hiyo nipende kuiomba Serikali na hii naiomba Serikali kwa ujumla wake sio Waziri Tanzania tumekuwa na mapungufu katika kutafuta mafuta kumbukumbu zangu haziko sawa sikumbuki kama kutoka mwaka 2011 kuna leseni ilitolewa ya kutafuta mafuta.

Mheshimiwa Spika, huwezi kupata mafuta bila kutafuta lazima kutafuta na kutafuta kuna gharama nimesoma taarifa ya Kamati nimesoma hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri atujafanya lolote hizi pesa zilizotengwa katika kutafuta Eyasi, Emelele sijui Mnazibay si chochote si lolote kucholonga kisima unahitaji bilioni 100 hizi pesa zilizotengwa si lolote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kazi ya *TPDC* kubwa ilikuwa kuhamashisha *promotion*, u-*promote* kusudi wadau waje wachimbe ukitaka uchimbe wewe kama Taifa utamaliza

miaka minne miaka 100 sisi tunataka kuishi leo tuchimbe mafuta leo tuweze kuyapata.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha hatujatafuta mafuta kwa zaidi ya miaka 10 hukuna kilichofanyika, hata hii mafanikio ya Embele nimesoma kwenye taarifa Embele hakuna kitu kimefanyika. Tuamue kama Taifa na ninajua utata ulipo nani atachimba atapata nini ni kanuni ya dunia uwezi kuibadilisha ama uende *PSA* au uwe na pesa umtafute mkandarasi au utumie *concession* kama unadhani utaliwa wewe tafuta pesa zako utumie *contract* uchimbe yakikosa inakula kwako.

Mheshimiwa Spika, kisima kimoja bilioni 100 vichimbe 10 vikose tirioni 1 utawaaambia nini watu hapa kwa hiyo ama utumie *PSA* kama anavyosema mzee mmoja ukitaka kula na wewe uliwe kidogo *PSA* mgawane mwende mbele. Au uende kwenye *concession* kusudi mwende ule mlaba haina ujanja lakini *bottom* tunataka mafuta leo tuchimbe na huwezi kupata bila kuchimba. Nimeangalia Uganda kutoka mwaka 2002 mpaka sasa wamechimba visima 100 hivi vya Eliyasi, Embele vitatu tena vifupi hatutafika popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bomba la kwenda Uganda litapeleka gesi ya kupikia au *natural gas* Uganda. Na kuna agenda ya kupeleka gesi Kenya, ni muhafidhina katika hilo, na niliwahi kuwa katika kiti cha maamuzi nikiwa *Gasco*; nilikuwa nakataa gesi kwenda Kenya. Tutapeleka gesi Kenya atatengeneza mbolea tatuuzia mbolea. Yanakuwa yale yale ya parachichi, yanakuwa yaleyale ya mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchimbe gesi Mtwara, kina kifupi; tuchimbe Lindi; tuchimbe nyumbani Mkuranga, kuna gesi, tutengeneze kiwanda cha mbolea. Kiwanda cha mbolea kina makandokando; haiwezekani tukatafuta makandokando kuyaondoa kwa miaka yote. Tukubaliane leo kiwanda cha mbolea kianze kwa sababu tunahitaji mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie usalama wa mafuta, na amelizungumza mwenzangu, Mheshimiwa Mansoor, na wewe ulilizungumza wakati tunahitimisha ile bajeti ya Mazingira. Tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Spika, tunayo sekta ya bodaboda, na wale wanahitaji mafuta kwa sababu mafuta ni upatikanaji wake, waipoyapata watayatafuta vyovyote. Namna ya kufanya – na kweli *EWURA* mjiangalie – zamani tulikuwa na vituo vya aina tatu; *fuel service station, fuel station* na *cab site*. Wale wakongwe wenye faida ya umri kama mimi, ulikuwa ukienda kununua mafuta utayaona yanapanda kwenye chupa wanasonga hivi halafu yanakwisha.

Mheshimiwa Spika, tuanzishe vituo hivyo vidogo ambavyo vinaweza kuwa vijijini, vijana wanatunza lita 100, 200, 300 salama. Yataangalia ubora wa mafuta, usalama wa mafuta na uwezo wa kupatikana kwa karibu walipo watu. Hatuwezi kuepuka biashara ya bodaboda, tunazihita pikipiki leo kuliko siku nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *EWURA* – na mnaweza kuja, nitawaelekeza bure – lazima muende kwenye *cab site* muweze kupunguza gharama ndiyo tutaweza kusambaza vituo mpaka vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie uagizaji wa mafuta. Nimesoma taarifa; yako maendeleo yameonekana. Lakini katika mafuta ninachotafuta ni nafasi ya mafuta kuchangamsha uchumi wa nchi hii. Sisi *location advantage* ya Tanzania ambayo nasema *location advantage* siyo faida, faida ni kutumia hiyo *location advantage*.

Mheshimiwa Spika, sisi tuko kwenye nafasi nzuri ya kuweza kuwauzia wenzetu. Pamoja na taarifa ya Waziri kwamba tumepunguza *premium* kwenda wastani wa 36 lakini tujipime na Kenya; Tanzania tunaposema *premium* ya 22, 25, 58, Kenya wanasema 4, 5, 6. Kwa nini *premium* Kenya zinakuwa nafuu *premium* Tanzania zinakuja juu?

Mheshimiwa Spika, lakini jiulize; kwa nini unapowaita watu walete *bid* ku-*supply* mafuta wanakuja wawili kila siku? Ukimuita ni yuleyule, Magesa na Mwijage, kila siku haohao; kwa nini hawaji kumi? Lazima tujipime tuangalie katika mfumo mzima, kuna nini hapa? Ndiyo maana tunapata mafuta yenye gharama kubwa kiasi kwamba hatuwezi kupata *competitive advantage*. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage. Mheshimiwa Anthony Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nianze kwanza kwa kuipongeza Wizara, hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo mmeendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo amejitoa sana kwenye sekta hii. Na kazi nzuri aliyoifanya tunaona hivi sasa; vijiji takribani 10,312 vimeshafikiwa. Na ninaamini kabisa azma ile ya kufikia vijiji vyote itafikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, hapa Mkoa wa Dodoma ametuletea watendaji wazuri kwa *TANESCO*. Alikuwepo meneja wetu hapa Frank Chambua, amefanya kazi nzuri, umem-*promote* amekuwa Meneja wa Kanda. Lakini hivi sasa ametuletea Boimanda, na yeye anafanya kazi nzuri sana; tunamshukuru sana kwa kuona umuhimu wa kuwaleta watendaji hawa katika Mkoa wetu wa Dodoma. (Makofi)



Mheshimiwa Spika, nataka nianze kuzungumzia masuala ya utekelezaji wa miradi ya nishati ya umeme katika Jimbo la Dodoma Mjini, na hasa katika miradi hii mikubwa miwili ya *densification* na *peri urban*. Mheshimiwa Waziri, nataka nikushukuru sana na niishukuru sana Serikali kwa kutenga zaidi ya shilingi bilioni 100 ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii tafsiri yake ni kwamba itakwenda kuiwasha Dodoma nzima, na hapo sasa tutakuwa tumefikia malengo ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya kweli ya Nchi ambayo umeme utawaka maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kwenye mradi *densification* tunashukuru kwamba mkandarasi aliyepo anafanya kazi yake vizuri sana, ameyafikia maeneo mengi yale ambayo yalikuwa hayajafikiwa na umeme. Na nimpongeze sana kwa kweli Mkandarasi *Derm Electrics* kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, na hivi sasa karibia maeneo yote ambayo yalirukwa kwenye umeme wa *REA* Awamu ya Kwanza na ya Pili, yanatekelezewa mradi huu wa *densification*. Kwa imani yangu ni kwamba yatakamilika yote na Dodoma yote itaendelea kuwaka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, jana nimepigwiwa simu na nimekutana na mkandarasi wa *CILEX* ambaye ndiyo atakwenda kutekeleza mradi wa *peri urban* ambao kwa mara ya kwanza utakwenda kuwasha umeme kwenye Kata za Chihanga na Mbalawala ambazo hazijawahi kuona nguzo hata moja tangu kuumbwa kwa ulimwengu huu. Lakini pia utafika mpaka maeneo ya Mkoyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ombi langu; hivi sasa Jiji la Dodoma linakua kwa kasi sana, maeneo ni mengi sana ambayo yanaendelezwa. Niwaombe watendaji wako waongeze kasi na hasa katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, tuna maeneo yametengwa kwa ajili ya viwanda; eneo la Nala na eneo la Mpunguzi. Wawekezaji wengi wanashindwa kuja kuanza kuwekeza kwa sababu hakuna miundombinu ya nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, ulitoa msisitizo mkubwa sana kwa mkuu wa mkoa na mkuu wa mkoa amelibeba suala la kiwanda cha mbolea pale Nala. Walishindwa kuanza kwa sababu hakukuwa na miundombinu ya umeme. Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Anthony Mtaka, ameshinda pale Nala siku mbili na watu wa *TANESCO* na Jumamosi umeme unawaka na mwekezaji ataanza kujenga kiwanda kile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara, Dodoma maeneo haya mawili yanafahamika, ya Mpunguzi na Nala; nikuombe Mheshimiwa Waziri, twendeni tukawekeze kule tuweke miundombinu ili wawekezaji wengi zaidi waje. Kwa sababu hivi sasa tunamtegemea mwekezaji mkubwa wa *SBL* na *TBL* lakini wao wakifika itakuwa pia kichocheo kwa wawekezaji wengi kuja kuwekeza Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, nikuombe katika mipango yako angalia sana maeneo ya *industrial park* ili tukaweke umeme kuwavutia wawekezaji wengi zaidi. Akija *TBL* hapa Dodoma, akija *SBL*, atawavutia wawekezaji wengine na viwanda vingi vitajengwa. Hivyo nikuombe Mheshimiwa Waziri uliangalie hili kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, suala la mradi wa bomba la mafuta (*EACOP*); kwanza kabisa nataka nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameharakisha na ameshiriki katika mchakato wa kusaini mikataba hii muhimu sana kwa ajili ya bomba hili.

Mheshimiwa Spika, bomba hili lina urefu wa kilometa 1,443. Bomba hili ni refu sana na eneo kubwa liko eneo la

Tanzania. Inapotoka kule Kabahale, Hoima, mpaka Chongoleani, maana yake ni kwamba katikati kote hapa bomba hili litaacha athari chanya.

Mheshimiwa Spika, sasa mchango wangu ni kuomba Serikali kwamba pamoja na uwepo wa bomba hili, lakini bomba hili lazima lilete manufaa kwa wananchi wetu wa Tanzania na hasa jumuiya ya wafanyabiashara na wajasiriamali katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba kwenye bomba hili ajira takribani 15,000 zitatengenezwa. Lakini nawaomba Wizara kupitia *EWURA* najua mmewasajili wale watoa huduma takribani 570, lakini twende mbele zaidi. Uganda kwenye bomba hili hili Mheshimiwa Waziri, wame-*ring fence* baadhi ya *categories* ambazo lazima zifanywe na wazawa. Mheshimiwa Waziri, na hapa Tanzania mme-*ring fence categories* nyingi sana ambazo zitafanywa na wazawa isipokuwa hamjazitangaza. Mheshimiwa Waziri, tunaomba msiwa-*take by surprise business community*; mtangaze tujue maeneo gani Watanzania watafanya. Mkiwa-*take by surprise* watahindwa kujiandaa vizuri, watakuja wageni watazichukua hizi nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kama tayari tunafahamu maeneo gani ambako huduma zitatolewa na bidhaa zitahitajika, naomba mtangaze mapema ili watu wajiandae. Kwa hivi sasa hamjatoa tangazo lolote Mheshimiwa Waziri, watu wanajua tu kwamba kuna fursa lakini hawajui fursa gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba *EWURA*, kama mmeshawasajili hawa watoa huduma toeni matangazo kila mtu ajue ili kama kuna masuala ya mafundi wa kuchomelea watu wajue, kama kuna masuala ya kuleta *crane* watu wajue; hayo yote lazima yaainishwe na Watanzania wajiandae katika hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, lakini kwenye Watanzania kujiandaa katika hili, naomba pia msiwasahau

wajasiriamali wadogowadogo. Nimeona Wizara mmejelekeza sana kwa wafanyabiashara wakubwa wenye makampuni, lakini tunawasahau wale wajasiriamali wadogowadogo ambako bomba hili linapita.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba upitie kufanya vikao pamoja na mikoa yote ambako bomba hili linapita ili tuwaandae akinamama, vijana na watu wenye ulemavu pia kushiriki kwenye mradi huu mkubwa. Najua mama lishe watahitajika, najua vijana nguvukazi itahitajika, lakini tuwaandae mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika hili niombe Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Nishati na Madini mkae pamoja muwasaidie wafanyabiashara ambao wamekuwa *listed* pale *EWURA* ili waweze kufanya kazi hii vizuri. Kwa sababu najua moja kati ya changamoto kubwa ni changamoto ya mitaji.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hawa ambao watashiriki kwenye bomba la mafuta wakienda kwa aina ya mikopo ya asilimia 21 katika *commercial rate*, hakuna mtu ataweza kufanya. Lakini Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la Taifa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Fedha, naomba mkae na taasisi za benki, taasisi za kifedha, mkubaliane kwamba kwa sababu bomba hili mahitaji yake yanafahamika, wale wote ambao wamekuwa *listed*, yale makampuni 570, wakienda kuomba mkopo basi riba yao iwe tofauti na riba iliyoko hivi sasa katika soko la biashara ya kibenki kwa sababu asilimia 21 hawataweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Wachina wanafanikiwa sana kwa sababu Serikali yao inaingia katikati na mikopo yao ni asilimia tatu mpaka nne. Asilimia 21 hakuna Mtanzania ataweza kufanya kazi hiyo, lakini mnao uwezo wa kukaa pamoja na benki.

Mheshimiwa Spika, hoja ya benki ni kwamba wakitoa mikopo mingi *risk* yake ni kubwa kwenye *repayment*. Lakini

mkikaa nao kwa pamoja uko mfumo unaitwa *contract cash flow discounting*; unachukua mkataba aliyopewa huyu mtoa huduma unaupeleka benki, benki anafungua akaunti ya huyu mtoa huduma, mtoa huduma huyu akilipwa malipo yapitie katika benki iliyomkopesha, benki wakate hela yake iwe sehemu ya malipo ya deni halafui naye abaki na kile cha ziada. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa *trend* ambayo tunakwenda nayo hivi sasa, asilimia kubwa ya Watanzania hawataweza, watahindiwa kwa sababu mikopo yetu iko juu sana.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara ya Fedha; mnaweza mkaenda mpaka ikafikia asilimia nane katika riba. Hili linawezekana sana kwa sababu benki atakuwa na uhakika wa *repayment* ya mkopo wake. Lakini vinginevyo wazawa, wafanyabiashara wa Kitanzania wataishia kuuona mradi huu kwa mbali, watakuja Wachina na Wazungu hapa watachukua shughuli zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tutafurahi tukiona Watanzania wananeemeka na huu mradi, lakini Serikali lazima muweke mkono wenu. Muwawezeshe kama ambavyo mataifa mengine yanafanya. Mkiwaacha waende wenyewe *blindly* tu, naona hatari kwamba mwisho wa siku Watanzania wengi hawatanufaika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, niwaombe Wizara ya Fedha, mnao uwezo wa kukaa pamoja na hizi taasisi za kifedha mkaweka huu utaratibu mzuri. Riba ishuke kutoka asilimia 21 iende asilimia nane mpaka kwenda chini huko ili Watanzania wengi zaidi waweze kushiriki kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anthony Mavunde. Bahati nzuri maafisa wa Benki ya *NMB* bado wapo, wanasikia jinsi ambavyo masuala ya riba ni muhimu sana katika

uwekezaji wa bomba hili la mafuta Uganda kuwawezesha Watanzania kuweza kushiriki lakini pia benki kupata faida katika shughuli nyingi zitakazoendana na bomba hili la mafuta. Tukizubaa wenzetu watachukua nafasi, wakichukua nafasi tusilalamike.

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ajjandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii maalum sana, Wizara ya nguvu, Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na hoja tatu tu za kusema leo; hoja mbili naomba nizungumze hoja za Kitaifa, na hoja moja kubwa nizungumze Jimbo langu la Same Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tunaishi na Serikali humu ndani. Wakati Serikali inafanya jambo zuri, ni vyema Wabunge tujifunze kuisifu Serikali. Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na mama Samia Suluhu Hassan, mpaka sasa tuliposimama hapa, inakwenda vizuri sana upande wa Mradi wa Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu Mradi wa Rufiji Serikali ilipoanza kulikuwa na maneno mengi sana. ukweli naomba niipongeze Serikali kwa kuthubutu. Serikali imefanya kitu ambacho wengi tulikuwa hatukijui vizuri, lakini mpaka sasa hivi Serikali imefanya mradi ambao ni mkubwa kweli katika Afrika Mashariki. Na Mradi huu wa Umeme wa Rufiji katika Afrika Mashariki ni wa kwanza wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, ukija katika Afrika nzima, mradi wenye hadhi hii nikiri wa kwanza uko Ethiopia, tukubali; wa pili uko Nigeria; wa tatu uko angola; wa nne uko Tanzania. Tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, na ninakumbuka nilikuwepo humuhumu ndani, kulikuwa na migongano mingi nje ya nchi, huko ulimwenguni walisema maneno mengi. Nimpongeze Rais wa Awamu ya Tano, alisimama imara sana, tena alitumia nguvu nyingi sana; Mungu amuweke mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Megawatt* 2,113 siyo ndogo. Tanzania na Watanzania wote kwa ujumla tutaona mafanikio makubwa mradi huu utakapokwisha. Mradi huu umefikia asilimia 52. Nimpongeze na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Nishati mwaka 2017 ndio alianza hii Wizara hapa, zilikuwa zipo mbili; Nishati na Madini. Zikatenganishwa 2017, huyu kijana akachukua hii Wizara.

Mheshimiwa Spika, nikiri kabisa na niseme ukweli Mheshimiwa Waziri, ukitembea mtu hasikii hata hatua zako zinavyokwenda, lakini unakwenda mbio sana, unajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na niseme; sina kawaida ya kusifu Mawaziri, lakini huyu kijana nimeona leo nimwambie ukweli, jitahidi sana, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kikubwa; huu mradi tunaujenga kwa pesa zetu wenyewe Watanzania jamani. Huu mradi ni mradi wa trilioni 6.5; hatukukopa mahali, hatukupewa msaada, zote ni pesa za Watanzania. Hivi kwa nini tusijivune? Trilioni 6.5 siyo pesa ndogo, ni hela zinazotaka uthubutu mkubwa. Nawapongeza sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, na ninaomba niwaambie ukweli; leo nimeamka vizuri sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa mama Kilango; ni kwamba kitu kinachofurahisha mkandarasi hadai hata senti tano kwa kazi alizofanya. Kwa hiyo, Serikali imefanya vizuri na Mheshimiwa mama Samia, Rais wetu, anaendeleza gurudumu lilelile. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilango, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, tena naipokea kwa unyenyekevu. Mheshimiwa mama Manyanya, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme ukweli; tusipoisemea Serikali yetu vizuri, nani ataisemea? Ni sisi tumeweka madarakani. Tumepambana tukashinda; Chama Cha Mapinduzi, Serikali inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nimempenda sana; huu mradi wa kupeleka umeme vijijini. Nilikuwepo tangu mwaka 2000 humu ndani, niliona umeme ulivyokuwa unasuasua, niliona. Nilikata tamaa. Lakini katika vijiji 12,268 vya nchi yetu sisi, leo hii kuna vijiji 10,312 vimepelekewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kama umeme umefika kijijini haujaenda vitongojini, lakini ni mwanzo mzuri kwamba umefika vijijini *next* utakwenda kwenye vitongoji vyetu. Serikali mmenifurahisha sana katika hilo pia, haswa sisi mnaotuona tulio simama hapa wengi wetu tunatoka vijijini, tumezaliwa vijijini, tumekulia vijijini bado tupo vijijini huku tumekuja kutembea sisi ni watu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 86 ya vijiji vyetu tayari wameona umeme, tuishukuru Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na ile mikakati Wabunge mlloiweka hapa kwamba chukueni pesa hapa kwenye mafuta pelekeni huku mkakati



ule ulikuwa mzuri sana. Ulikuwa mkakati mzuri sana, lakini niseme ukweli mnakumbuka mwaka 2015 ambao mpo sawa tulikuwa namba 39 katika nchi 54 za Afrika tulikuwa namba 39, nikisema hivyo sijui mnanielewa, kwamba katika nchi 54 za Afrika tulikuwa namba 39 kwa kupeleka umeme vijijini. Leo tukizungumza hapa katika Afrika sisi ni namba moja katika kupeleka umeme vijijini, hivi hapa mtasema Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inacheza? Inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Naomba niipongeze Serikali sana, sasa naomba niachane na Serikali naomba tugombane kidogo na Serikali. Naomba nigombane na nyie kidogo ili mfanye kazi. Nimezungumza kitaifa sasa naenda kwa walionichagua jamani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba uniangalie vizuri, nimeingia Jimbo la Same Mashariki mwaka 2005 nikawa nasema humu ndani nagombana na Ngeleja, nagombana na Muhongo kuhusu umeme wa Tarafa ya Mambavunda, wananchi wangu wanaishi mlimani sana na wanapoishi kule wanaishi na migomba, na miti, mitangawizi kuna giza sana, nilisema kwa miaka tisa, 2014/2015 Serikali ndiyo ilipoona ikanipa pesa za kupeleka umeme katika Tarafa ya Mambavunda, nikashukuru, nikafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha kwanza nilichokiona kinaitwa Mwala kilipata umeme mwaka 2015 nikafurahi nikaona umeme. Mradi ule Serikali ilisema utakwenda 2015, 2018 utakwisha, wananchi wakafurahi, wakashangilia, leo ni 2021 mradi ule 2015 ulikwenda kidogo ulisimama, 2015 ukasimama, 2016, 2017, 2018, 2019 waziri juzi ndiyo umeanza kidogo.

Mheshimiwa Spika, nasimama vizuri kukwambia waziri huu mradi wale wananchi walitegemea sana nao waingie kwenye taa, waingie kwenye mwanga, mliwaacha tangu 2015 mkaenda vijiji viwili, vitatu tu mradi huu mpaka leo nimeanza kwa kuwasifu Serikali narudi kuwaomba tafadhalini huu mradi umalizeni, hawa watu mliwapelekea taa kidogo vijiji viwili, vitatu mradi huu ni wa tarafa nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mradi ulikuwa uende Vunta, uende Papa, uende Miombo, Uende Mwala, uende Kidandini, uende Mwatani, Njagu, Kirangare, Makasa, Mshewa, Pangani, Vugwamakati, Hedaru, Mweteni, Tambwe, Tintin na cha Nguruwe. Mlikwenda sehemu kama tatu tu, sasa mimi ni Mbunge Same Mashariki kama mlilala hapo katikati sababu sijui, leo nakwambia Mheshimiwa Waziri utoe majibu kwa wale wananchi kwanini ulisimama tangu 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umerudi kuanzia 2020 hapa mwishoni niliiona nimekwenda mwenyewe naona una wakandarasi kule, lakini wananchi wangu wana wasiwasi kwamba huenda utasimama tena, naomba Mheshimiwa Waziri sitakamata shilingi, lakini uniambie kwanini ulisimama, na utamaliza lini huu mradi.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja kwanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Anne Kilango Malechela, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nitajikita katika kusesitiza umakini, usimamizi kwenye mikataba yetu kwa maslahi ya Taifa letu, hatuhitaji kujikwaa tena, lakini viporo tulivyoviacha lazima tuvifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unajua mwaka 1997 Kampuni ya *SONGAS* ilianzishwa kama kampuni binafsi ambapo Serikali tulikuwa tuna hisa ya asilimia 40 na kampuni hii ilikuwa inafua umeme kutoka katika visima vya *gas* vya Songosongo. Sasa tunajua kwa nini Serikali iliamua kuingia ubia ni kutokana na tatizo kubwa la umeme ambalo iliikumba Taifa letu miaka ya 1990 mpaka 2000.

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na kusuasua na sintofahamu kutokea kutokana na uhalali wa hisa na mali za Serikali katika uwekezaji huu. Bunge lako Tukufu kupitia kamati inayohusiana na masuala ya nishati mwaka 2008 ilitoa taarifa kwamba mradi huu hauinufainishi Taifa letu, Serikali yetu inapunjwa na ikapelekea CAG kufanya uchunguzi. Moja ya mambo yaliyobainika ni kwamba mbali ya uwekezaji wa Serikali ya Tanzania wa asilimia 40 TANESCO ilihamisha mali na madeni kwenda kwenye kampuni ya SONGAS. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mali ambazo zinazohamishika zilikuwa na thamani ya dola za Kimarekani milioni moja, lakini pia mali zingine ni sehemu ya Ubungo Complex, mali zingine ni sehemu ya ardhi iliyokuwa inajengwa bomba la gas kupeleka kwenye Kiwanda cha Saruji Wazo. Lakini vilevile makubaliano yalikuwa yanasema SONGAS ilipe deni la mkopo lenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 45.88 hadi tunapozungumza leo SONGAS hawakuamisha lile deni, zile pesa, lile deni linalipwa na TANESCO kupitia capacity charge kwenye ankara ya kila mwezi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na hii CAG amesema kwa sababu TANESCO inaendelea kulipa lile deni wenyewe Serikali yetu ingeongeza thamani kwenye mradi na tungekuwa tuna hisa, lakini mpaka tunavyozungumza hili halijafanyika, mbali na kamati yako, Kamati ya Bunge inaisimamia Serikali kutoa maoni mbali na CAG tunapata kigugumizi wapi kulinda mali ya nchi yetu na mkataba unaturuhusu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na kipindi hicho hicho tuliingia mkataba na makampuni 936 katika kuhakikisha tunazalisha umeme wa dharura na makampuni yale uchunguzi ulivyofanyika ukaonyesha kabisa yalikuwa na gharama kubwa mpaka tunavyozungumza, mpaka 2018 kutokana na mikataba ile ya makampuni yale 936 TANESCO imekuwa na deni la bilioni 938. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza kati ya makampuni 936 yaliyofanyiwa uhakiki ni makampuni 23 ambayo yenye thamani ya deni ya bilioni 643 hivi

tunavyozungumza *IPTL* yenyewe imeshindwa kuthibitisha deni la bilioni 1.2 hivi tunavyozungumza makampuni 913 yameshindwa kuthibitisha deni ya bilioni 291, tujiulize kama Taifa tuna wanasheria, tujiulize kama Taifa hata kama tunapata *crisis* lazima tuwe makini katika kuingia mikataba, tuwe makini katika kuhakikisha mbali na kutatua tatizo tusingie gharama kubwa hizi pesa zingeenda kumaliza miradi ya umeme vijijini, hizi pesa inawezekana tungepeleka katika miradi ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kaka yangu Dkt. Kalemari nenda kamalize haya madudu yanatia aibu na inafanya *TANESCO* lishindwe kujiendesha, lakini tukija kwenye madeni bado sijazungumzia deni la *TPDC* la bilioni 246, Mheshimiwa Dkt. Kalemari unajua, hili deni tena la *TPDC* hili deni *CAG* amesema shirika letu linaweza likaporwa mali na Benki ya *Exim* ya China kwa kushindwa kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wakati hii *TPDC* ni shirika la Serikali, Serikali wenyewe mnadaiwa, mnadaiwa na *TANESCO* bilioni 258, ili kulikomboa shirika letu mngeweza tu kwenye lile deni mnalodaiwa mngewalipia hawa *TPDC* hiyo bilioni 240 na, bilioni 9 inayobaki mngewapa *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye uzembe wa kusimamia mikataba hata kama inatulinda. Mwaka 2004 Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya *PANGEA* kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya umeme kwenye mgodi wa Buzwagi. Kwenye makubaliano ya ule mkataba ilikuwa kwanza wafungue benki ya pamoja kwa sababu kwenye makubaliano *TANGEA* walikuwa wanakata dola 5000 mpaka 3500 katika kila nusu saa ya ankara ya mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninavyozungumza mpaka sasa hivi na yale makubaliano ili zile pesa ziende *TANESCO*, hivi tunavyozungumza na lengo lake lilikuwa kufanya miundombinu ikitokea hitilafu hivi tunavyozungumza takribani miaka kumi benki ya pamoja hajifunguliwa zile pesa zilikuwa zinaingia kwenye akaunti ya *PANGEA* na *TANESCO* ilikuwa inafanya ukarabati kupitia pesa zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza bilioni kumi *TANESCO* haijalipwa aibu na hii tabia ya kutosimamia makubaliano ya pesa zetu wenyewe mikataba tunayoingia tunapata kigugumizi gani tunawaogopa wawekezaji wakati mikataba inatu- *favor* haya hata mikataba yetu wenyewe Mheshimiwa Waziri unajua *TANESCO* haijaingia makubaliano ikaenda kufanya ukarabati wa Mkongo wa Taifa na mpaka sasa hivi inaidai Wizara ya Mawasiliano bilioni nane hakuna mkataba na mpaka juni 2020 *CAG* anasisitiza ingieni mikataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri lazima tufanye uchunguzi kwenye mitambo yetu ya kuzalisha umeme. Mtambo wa Kinyerezi I na Kinyerezi II ilijiwekea malengo ya kuzalisha *Megawatt* 398, lakini hivi tunavyozungumza malengo hayajatimia wamezalisha *Megawatt* 290, nenda kule Mwanza - Nyakato najua una mradi kule ilikuwa izalishe *Megawatt* 63, lakini wamezalisha *Megawatt* 36 hiyo ni miradi miwili ukijumlisha hapo ni *Megawatt* 155 zimepotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na hii yote wanasema ni tatizo la mitambo, huu wa Nyakato wanakwambia ni tatizo la, kulikuwa na matatizo kwenye mashine nne sasa hii ukienda haya matatizo ya kiufundi, matatizo ya kiufundi kwenye miradi mingi hivi ni *Megawatt* ngapi ambazo tunapoteza. Sasa Mheshimiwa Waziri haya ni mambo ya msingi ya kwenda kuyaangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kuzungumzia Mheshimiwa Waziri tatizo la mita kwenye mita kuu ambazo linasoma ni namna gani umeme wetu unavyozalishwa ni kiwango gani unapotea. Najua mlinunua mita 666, lakini mita zinazosoma ni mita 336 hii inachangia kutojua umeme unaozalishwa ni kiasi gani unapotea, lakini vile vile hili tatizo linatuletea hasara na inaongeza gharama ya uendeshaji.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ester Bulaya tunakushukuru sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia bajeti ya wizara hii muhimu sana ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni mara ya kwanza kusimama kungea katika Bunge hili lako Tukufu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu aliyenipa neema na kibali cha kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kikiongozwa na Mwenyekiti wetu wa Chama mama yetu mama Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni rahisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuiteua kuweza kupeperusha Bendera ya Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mhambwe ambao wamenipa ridhaa kwa kunipatia kura za kutosha ili niweze kuwatumikia, ninawaahidi wananchi wa Mhambwe kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru familia yangu kipekee mume wangu mpenzi Sadoki Mgendi, Watoto wangu Naomi, George, Georgette na Noah kwa uvumilivu, lakini na ushirikiano wao walionipa kipindi chote cha harakati hizi, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Wabunge wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi, wakiongozwa na Wabunge wa Mkoa wa Kigoma kwa mchango wao wa hali na mali ulioniwezesha kuweza kufanikisha safari hii. Napenda

niwashukuru ndugu jamaa na marafiki wote ambao walikuwa na mimi katika safari hii nzima, Mungu awabariki sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu waliokwisha kuongea kuendelea kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri Stephen Byabato, lakini na Katibu Mkuu Mheshimiwa Leonard Masanja na viongozi wote wa Wizara hii, lakini na viongozi na wafanyakazi wote wa TANESCO kwa kazi kubwa, lakini kwa ripoti nzuri ambayo kwa ukweli imetujibu mambo mengi ambayo tulikuwa tukiyafikiria, mmetoa ripoti nzuri, mmefanya vizuri hongereni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa sana inayofanya ya kutuunganisha umeme wananchi wake, umeme wa uhakika, lakini umeme wa bei rahisi, hii inajidhirisha kwa miradi mbalimbali ambayo Waziri wetu wamewakilisha, lakini pia kwa miradi ile inayoendelea ule ukanda wangu wa Jimbo la Muhambwe ikiwemo ujenzi wa kituo cha kufua umeme katika maporomoko ya Rusumo *megawatt* 80.

Mheshimiwa Spika, lakini na ujenzi wa kituo cha kufua umeme katika Mto Malagarasi *Megawatt* 49.5. Hii ni dhahiri kwamba baada ya miradi hii kukamilika basi itatupunguzia mzigo wa kuendesha umeme kutumia *generator* ambayo ni gharama kubwa kutumia mafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile itatusaidia tuweze kupata umeme wa uhakika, naipongeza sana Serikali kwa jitihada hizo tunaomba miradi hii isimamiwe vizuri ili iweze kuisha katika kipindi kilichopangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo bado pana changamoto hasa katika usambazaji wa umeme vijijini. Jimbo langu la Muhambwe lina vijiji 50, katika vijiji hivyo 50 umeme umeunganishwa katika vijiji 8 tu na uunganishaji huo ni ile tunaita katikati ya Kijiji tu. Haujafika kwenye nyumba nyingi za wananchi, lakini haujafika kwenye taasisi kama vile,

shule, makanisa, misikiti na kadhalika, hospitalini na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ilitokana na ucheleweshaji wa vifaa vya mkandarasi bandarini, ambavyo vifaa vile vilikaa zaidi ya miezi 12 vikidaiwa kodi. Nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ambayo iliingilia kati na kutusaidia kuvitoa vile vifaa, vifaa hivyo vimetoka wiki iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa basi, nimuombe Waziri wa Nishati kutokana na ucheleweshaji huu, naomba sasa Jimbo langu la Muhambwe lipewe kipaumbele. Maana vijiji ambavyo havijapata umeme ni vingi, ikiwemo Kigaga, Kichananga, Rukaya, Magalama, Kumkuyu, Kibuye, Kukinama, Nyakilenda, Malolegwa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kasi iongezeke, ili tuweze kusambaziwa umeme katika vijiji vyetu. Sambamba na hili, tunayo Kata ya Bitale, hii Kata iko takribani kilometa 2 kutoka Mji wa Kibondo kwa maana ni karibu sana. Lakini Kata hii bado imepata umeme katikati tu ya hiyo Kata, lakini vijiji vyake kama vile Kumuhama na Rubanga bado haijafikishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Kata hii ipewe kipaumbele, maana iko karibu mno kukosa umeme ni aibu kwa Jimbo langu la Muhambwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali, kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa vifaa kufika eneo la utekelezaji kwa madai ya ucheleweshaji wa kodi au kwa ucheleweshaji wa kibali cha kusafirisha vifaa ambavyo vina uzito. Lakini naamini taasisi zote hizi ni za Serikali kwa maana kwamba, bandari, *TANROADS* zote ni mali ya Serikali na *TANESCO* ni Shirika la Serikali. Na *TANESCO* hii inatekeleza miradi ambayo ni mali ya Serikali, basi kuwepo na mazungumzo ndani ya taasisi hizi. Taasisi hizi ziweze kuongea kwa maana kwamba, ucheleweshaji huu usilete madhara kwa wananchi, wananchi wanahitaji kuona matokeo chanya. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, hivyo ikibidi basi kibali kitolewe cha kuruhusu vifaa hivi viweze kufika eneo la tukio huku kodi zikiendelea kulipwa. Hii itaharakisha mradi kutekelezeka, lakini pia, itatupunguzia gharama za kutekeleza mradi. Lakini pia, itatusaidia kwamba mradi uishe kwa wakati uliopangwa, ili Serikali iweze kulipa gharama ambazo ni sahihi kwa mlaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge makofi hayo hayatoshi, ahsanteni sana kwa Mbunge ambaye ni mara ya kwanza kuongea Bungeni, kwa kweli amejitahidi sana. Naamini watu wa Muhambwe wamepata chombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca David Kishoa na Mheshimiwa Abdallah Jaffari Chaurembo na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, wajandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na mimi tena kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Lakini wakati naanza kuchangia, nikumbushe kidogo historia yangu labda na historia ya Wilaya yetu ya Masasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafanya hivyo kwa sababu, tuna tatizo kidogo kwa hiyo, nataka niishauri Serikali, niipongeze kwa kazi nzuri walizozifanya. Lakini pia sasa, tukubaliane kimsingi tunakwenda kufanya nini, ili kuhakikisha Wilaya ya Masasi inapata umeme wa uhakika na vijiji vyake vyote pamoja na Majimbo yote na hasa zaidi Mkoa wa Mtwara wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Bunge lililopita, nikiwa natokea huko huko Wilaya ya Masasi na ninapoitaja Wilaya ya Masasi Waheshimiwa Wabunge naomba mkumbuke kwamba, ni kati ya wilaya kongwe sana zilizoko nchini

Tanzania ilianzishwa kati ya mwaka 1920 na mwaka 1928. Na Wabunge wengi wamepita pale mbalimbali ndiko alikotokea hata Mheshimiwa Rais wa nchi hii wa Awamu zilizopita, Mheshimiwa Rais Mkapa na mimi nilikuwa kwa mara ya kwanza Mbunge nikitokea kwenye Chama cha upinzani, lakini wananchi wa Masasi walinichagua wa Wilaya ya Masasi na Jimbo la Ndanda hasa ambalo lilikuwa jipya kabisa ili niweze kuwawakilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wao walitambua kabisa kwamba, wamenichagua ili nishirikiane nao kuja kuisemea Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ndani ya Bunge lako Tukufu na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi toka wakati huo na kipindi chote, inatambua kwamba na imeahidi kila kijiji kitapata umeme na kila sehemu kwenye zile huduma kubwa za kijamii kama kanisa, misikiti na maeneo mengine yatapata umeme. Sasa, wakati naingia kuliwakilisha Jimbo la Ndanda mwaka 2015 tulikuwa na vijiji 42 ambavyo havina umeme kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka sasa hivi Wizara hii imefanya kazi nzuri na vijiji vilivyobakia bila kuwa na umeme ni 19 tu. Lakini kwa ahadi hapa ya Mheshimiwa Waziri anatuambia kwa sababu, mambo hayo yapo ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kazi hiyo itakwenda kufanyika ndani ya muda mfupi ujao. Lakini, nataka niwakumbushe na kuwapongeza sana Wizara kwa kazi yao, nipongeze pia uongozi wa Wilaya ya Masasi kwa maana ya *Management* nzima ya *TANESCO* Wilaya ya Masasi kwa kazi nzuri wanayoifanya, Mkoa Eng. Fadhili pamoja na Kanda Mzee wetu pale Mzee Makota kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia *TANESCO* kwamba, tulikuwa tunatamani sana sisi tuliotokea Wilaya ya Masasi kwa sababu miradi ya *REA* kipindi kilichopita, ilikuwa imekwama sana kutokana na aina ya mkandarasi ambaye walimleta wakati huo. Tumepata mkandarasi bora kabisa ninaamini katika wakandarasi wengi walioko pale ambaye ni Namis *Cooperate*, amefanya kazi nzuri sana ya umeme

vijijini kwenye maeneo mengi na ninaamini sasa amekuja kuwa suluhu ya tatizo la umeme, kwenye Wilaya yetu ya Masasi na Mkoa wa Mtwara, Majimbo ya Ndanda, Masasi pamoja na Lulindi na ninaamini kazi hii ataifanya kwa uhakika mkubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikutana na Waziri siku chache na nikamuambia mapendekezo yangu, kuna Kata mbili ambazo hazina umeme kabisa, Kata ya Msikisi na vijiji vyake vyote, vijiji vya Namalembo, Liwale pamoja na Msikisi yenyewe. Kata ya Mpanyani na vijiji vyake vyote, ikiwemo Namalembo, Mpanyani, Muungano pamoja na vijiji vingine vilivyobakia havina umeme kabisa. Kwa hiyo, ninaomba kabisa mkandarasi huyu atakapokuwa anakwenda kufanya shughuli yake ya umeme kule, ambaye tunaambiwa sasa hivi yuko *site*. Kabla hawajaenda eneo lingine lolote kwenda kufanya kazi ya umeme, waanzie na maeneo haya kwa sababu, watu hawa hawana umeme kabisa bora hata Kata zingine na vijiji vingine wanao umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna tatizo kubwa la usambazaji kwa maana ya kwamba, miradi iliyokuwa imekwenda kwenye maeneo hayo ikianza maeneo ya Nanganga, maeneo ya Mumbulu ukija maeneo ya Mkwera, ukienda maeneo ya Ndanda Kijiji cha Ndolo, ukienda maeneo ya Mwena Kijiji cha Ndunda, ukija Chikundi Kijiji cha Mkalapa, lakini pamoja na maeneo ya kanisani, ukija Chigugu maeneo ya Mbemba pamoja na Mbaju umeme haujajitoshleza. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri huduma ile ya ujazilizi sasa wakati *TANESCO* wanafanya shughuli zao zingine na umeme unasambazwa kule basi wahakikishe kwa namna ya pekee wanakwenda kufanya ujazilizi kwenye maeneo haya, ili wananchi wa Kata hizi wote kwa pamoja wapate umeme sawa sawa, kwa mujibu wa Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwa sababu, ndio iliyosimama na ndio inayotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mashaka kidogo na namna ambavyo Wizara hii imejipanga kuhusu kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na hapa nataka niongelee suala la

gesi. Mpaka sasa hivi gesi iliyoko Mtwara inatumika kwa wastani wa asilimia 10 tu. Lakini nataka niwakumbushe Wizara kwamba, Serikali ilikopa fedha nyingi sana kuona lile bomba linatolewa kutokea Mtwara na linapelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya matumizi hii ni kwa ajili ya kukuza uchumi wa Mtwara na watu wake.

Mheshimiwa Spika, lakini mkumbuke pia kwamba, sehemu kubwa ya uchumi sisi tunategemea kwenye gesi kwa sasa, tunaomba sasa basi miradi hii itekelezwe mapema sana. Kwa sababu, sehemu pekee iliyobakia tunafanya tu kazi za korosho, ndio maana inapofika wakati wa korosho maana wote tunalazimika kusema kwa sababu, ni sehemu ambayo tunategemea kupata fedha kidogo. Lakini miradi ya gesi ikianza hata uzalishaji wa korosho nao utaongezeka na sisi tutakuwa tuna amani kwa sababu, na bandari yetu ya Mtwara pamoja na Mtwara *Corridor* kwa ujumla, kwa maana ya hii *Southern* Reli pamoja na bandari ya Mtwara, ambayo Serikali imeweka fedha nyingi na yenyewe itaweza kufanya kazi zake vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe kabisa Mheshimiwa Waziri atakapokuja *ku-windup*, atueleze mkakati madhubuti wa kurudi tena kwenye matumizi ya gesi kujenga kile kiwanda kwa ajili ya kuchenjua hii gesi asilia maeneo ya Lindi, kwa maana ya mradi wa *NLG* na matumizi makubwa ya gesi. Kwa sababu, inashangaza kuona wilaya kama wenzetu Wilaya ya Madaba, ambako anatokea rafiki yangu hapa, Mheshimiwa Muhagama kwamba ni wilaya iliyoanzia mwaka 2015, unailinganisha na Wilaya ya Masasi yenye miaka zaidi ya 50, kwa sababu imeanza miaka 28 kabla ya uhuru wa nchi yetu kwamba, Madaba wao wamejitosheleza kwa umeme na vijiji vyake vyote vimepata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sisi bado tunaongelea umeme uliobora kwa maana ya kutokukatika katika lakini pia, umeme unaotosha kwenye vijiji vyote. Sasa mtutendee haki wilaya hii ni ya siku nyingi na kama vigezo vya mgawanyo wa mikoa, ilikuwa ni kutokana na umri wa wilaya, Wilaya yetu ya Masasi ingekuwa imeshakuwa mkoa siku nyingi kabisa

kabla hata ya wilaya nyingi za Tanzania hii hazijazaliwa. Hata mikoa mingine imekuta Wilaya ya Masasi ikiendelea *ku-exist*. Kwa hiyo, niombe sana kazi hii muifanye kwa uhakika kwa sababu, sisi tunatoka kwenye wilaya kongwe kabisa, lakini miundombinu yetu sio mizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri Serikali kwamba, iangalie uwezekano wa kuwa na *line* maalum kabisa inayokwenda Masasi kwa sababu, itapita Ndanda kutokana na ukuaji wa eneo hili kwasababu, sasa hivi ni kama *business hub*. Ni Mji mkubwa kibiashara unaotegemewa sana na Mkoa wa Mtwara, ukiacha Mkoa wa Mtwara wenyewe mjini kwa sababu, sehemu kubwa ya uchumi wao walikuwa wanategemea uchumi wa gesi. Lakini Wilaya ya Masasi sehemu kubwa ya uchumi wao sasa hivi ni masuala ya mazao ya korosho.

Mheshimiwa Spika, lakini pale ndipo kuliko na *junction* ya barabara inayokwenda Songea, inayokwenda Nachingwea, inayokwenda Newala na inayorudi Mtwara Mjini. Kwa hiyo, ni eneo kubwa la kibiashara lakini uchumi wake unazorota kutokana na matatizo ya kukatikatika umeme mara kwa mara. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri hakikisha sasa ile *line* ambayo iko kilometa 120 kutokea Masasi kwenda Mahumbika, mnatupa *line* pekee ambayo haitakuwa *interrupted* hapa njiani. Itoke Mahumbika moja kwa moja iende Masasi moja kwa moja kiasi kwamba, likitokea tatizo lolote la umeme njiani ni rahisi kuirekebisha na bajeti yake nadhani imeletwa kwenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wataalam wa pale wanatuambia, nilikuwa naongea na *Engineer* Fadhili hapa karibuni kwamba, mkiamua kutumia nguzo za *cement* itatumika kama bilioni 10, lakini mkiamua kutumia nguzo za miti ni kama bilioni 6 ambayo sio njia ya kudumu sana. sasa hicho ndio kiasi pekee tunachokiomba, hatutamani miradi mikubwa kama ile iliyofanyika kule Namtumbo hapo karibuni. Kama miradi iliyofanyika Madaba, kama ambavyo walisema pale mwanzoni, tunataka mradi ambao utatuhakikishia umeme

wa uhakika Masasi ili tuweze kupata umeme ambao utakuwa haukatikikatiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaposema Masasi ni Wilaya yenye Majimbo matatu matatizo yetu sisi yanafanana, tunatambua hapa Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Geofrey kila mara huwa mnakutana. Kwa hiyo, ona namna na wewe ya kumshauri Waziri mnakuwa wote kwenye *cabinet* tuweze kupata Masasi umeme wa uhakika. Tuweze kupata Lulindi umeme wa uhakika, tuweze kupata Ndanda umeme wa uhakika kwa sababu Mji huu unakua na ili wawekezaji waweze kuja eneo letu, ni pamoja na kupata uhakika wa umeme pamoja na miundombinu mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niendeleo kumkumbusha Waziri kwamba, ili kufanikisha vizuri kwenye hii Mtwara *Corridor* na matumizi ya bandari ya Mtwara basi ihakikishe sasa miradi ile ya gesi inafufuliwa. Kulikuwa kuna ahadi ya Serikali kutengeneza kituo cha uzalishaji wa umeme wa gesi Mtwara, nakumbuka ilikuwa kama KVA 380 hivi au kitu kama hicho, lakini hatuoni chochote kinachoendelea. Sasa ni muda mrefu na tuone kwamba, tutumie *advantage* iliyopo sasa kufufua miradi yetu ya gesi kwa sababu, si vizuri sana kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na mgogoro ulioko Mozambique bado watu wanatamani kuwekeza Tanzania kwa sababu, ya amani iliyopo, mazingira yetu ni rafiki kabisa kwenye masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nikuombe, kama ambavyo nimesisitiza toka mwanzo mkandarasi ameshafika Masasi ambaye ni Kampuni nzuri sana ya Namis Cooperate, akaanze kazi kwenye Jimbo la Ndanda, kwenye Kata ya Msikisi na Kata ya Mpanyali tu. Akimaliza hapo huko kulikobakia kwingine sisi wenyewe tutakaa tutaongea na kujua nini tunataka tukifanye, lakini naomba kazi hiyo ikafanyike hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nisisitize tu kuhusu usambazaji umeme vijijini, kwenye vijiji nilivyovitaja kwasababu, maeneo haya yanapitiwa na umeme mkubwa unaokwenda Masasi.

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. Naomba haya niliyoshauri Serikali basi ikayafanyie kazi kwa mujibu wa Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecil David Mwambe, nilishakutaja Mheshimiwa Jesca David Kishoa na utafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana, Wizara ya kimkakati, Wizara ambayo ina mchango mkubwa sana kwenye pato la uchumi wa nchi yetu. Mimi nitajikita kwenye maeneo matatu na eneo langu la kwanza, linakwenda kujikita kwenye eneo la bomba la mafuta ghafi la *EACOP*. Naomba nichukue fursa hii kwa moyo wa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha *Host Government Agreement* na kwa namna ambavyo anakuwa *proactive* katika kufanikisha masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimefurahishwa na *shareholding structure* iliyopo kwenye mradi huu. Ukiachana na masuala mazima ya namna ambavyo mgawanyo ulivyo, lakini pia mradi huu unakwenda kutunufaisha sana ukiangalia kwamba, unakwenda kupita kwenye mikoa 8, lakini wilaya ziko 24, kata 134, vijiji 257 na vitongoji 527. Ni kwa uhakika kwamba, watu wa maeneo haya ambao bomba hili linapita wanakwenda kunufaika, lakini mradi huu unakwenda kutengeneza ajira zaidi ya 10,000. Nilikuwa ninatazama taarifa mbalimbali za Wizara, ninaona vitabu vya Wizara viko *silent* kueleza suala la wafanyakazi ambao watakuwa *skilled* na *unskilled*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ipo changamoto nyingine kubwa sana pamoja na yote ambayo nimeyazungumza juu. Kuna changamoto kubwa ambayo nitaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hapa, utoe ufafanuzi kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu, utata huu kwa kweli unazidi kuwapa watu sintofahamu. Nina swali la kuuliza, mradi huu wa *EACOP* ni nani anakwenda *ku-finance* mradi huu? Ninajua kwamba Serikali inatenga bilioni 2.6 kwa ajili ya kulipa fidia lakini mradi huu wenye thamani ya *USD* bilioni 2.5, ni nani anakwenda kuilipa? Kwa sababu, mtu ambaye mlikuwa mnamtegemea ambaye ni Kampuni ya *TOTAL*, ambaye ni *majority share* kwenye mkataba huu, hana uwezo wa kulipa fedha hizo mpaka hivi ninavyozungumza sasa nitatoa sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mezani kwangu nina jarida la *UK* ambalo ni *very prominent magazine* la *energy voice*. Mapema sana mwezi wa 5 hata kabla ya mkataba huu kuingiwa, mabenki ya *UK*, mabenki ya Ufaransa ambayo yalikuwa yametoa ahadi kutoa fedha kwa Kampuni ya *TOTAL*, kwa ajili ya *ku-facilitate* mradi, ujenzi huu wa bomba la mafuta, mabenki yametangaza kwamba, hayatatoa fedha hata senti tano tena. Sababu ya mabenki haya kutoa tangazo hili, mabenki yamegoma kwa sababu, wamesema wanakwenda kuunga mkono kampeni ya *ku-burn emission* masuala ya *carbon dioxide*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na naomba nirejee kwa ufupi sana eneo ambalo la *magazine* hii imeripoti wanasema hivi: "*French banks have committed not to provide projects financing for the TOTAL East African Crude Oil Pipe Line – EACOP*". Ukiangalia kwamba kwenye makubaliano yetu, tumekubaliana kwamba mradi huu ujengwe mpaka kufikia 2024 uwe umekwisha kamilika. Lakini kampeni ambayo mabenki haya yanasema *yanai-support*, kampeni hii inakwenda mpaka kufika mwaka 2050. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kutuambia, kama hafahamu basi ninamuomba awatafute watu wa *TOTAL* wamuambie fedha hii au mradi huu nani anakwenda *kuu-finance*? Kwa sababu wao fedha waliyokuwa wanategemea kutoka



kwenye mabenki ya Ufaransa, mabenki yamesema hayatoi fedha tena.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa, nakukubalia tuendeleo.

### T A A R I F A

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji, inawezekana kweli anachokizungumza anakijua, lakini sisi hatufungi mkataba na mabenki ya Ufaransa. Tunafunga mkataba na mkandarasi ambaye ni TOTAL, ambaye tayari kwenye mkataba alikuwepo anaweka. Yeye ana uhakika gani kwamba, mkandarasi ana fedha kiasi gani za kuweka hapo? Kwa sababu sisi hatufungi mkataba na yale mabenki, kama ameona hiyo *document* ni ya kwake na yeye, sisi tunakubaliana na mkataba unaoendelea sasa hivi. Mpaka siku mkandarasi atakapoamua kwamba, hana uwezo wa namna hiyo ndio tutaelewa jambo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa unapokea taarifa hiyo.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, siwezi kuipokea taarifa hii, labda nimuelimishe kidogo Mheshimiwa Mbunge. Mkandarasi na TOTAL ni watu wawili tofauti. Mkandarasi anayehusika kwenye ujenzi wa mradi wa EACOP sio huyo TOTAL unayemsema wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niipe *challenge Economic Intelligence System* ya Taifa letu. Haya ndio mambo ambayo ni *very sensitive* katika Taifa hili ambayo tunategemea hawa watu watusaidie. Kwa maana taarifa kama hizi kama zimetokea toka Mwezi Mei mwanzoni kabla ya mkataba huu kuingia hizi nchi mbili ilikuwa ni vyema wizara

wakakaa chini na *TOTAL* wakakubaliana kwamba hizi fedha zinakwenda kutolewa wapi kwa sababu kimsingi toka mwanzo *TOTAL* walikwishaeleza kwamba fedha wanapata kutoka kwenye Mabenki ya Ufaransa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendeleo, suala jingine ambalo ninaomba leo kauli ya mwisho kutoka Serikalini. Hivi hii itakuwa mara yangu nne ndani ya Bunge lako Tukufu kuzungumzia suala hili kwasababu nimelishazungumza Bunge lililopita na sasa nalizungumza kwa mara ya kwanza katika Bunge la Awamu hii. Suala la Mkataba wa *SONGAS*, nimelizungumza suala hili mara nyingi sana na nakumbuka hata Mheshimiwa *AG* amekuwa akisimama humu ndani akitoa ahadi kwamba wanafanyia *review* mikataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumebakiza miaka miwili tu ili mkataba wa *SONGAS* uweze kuendelezwa na nina taarifa, nina taarifa watu wa *SONGAS* wameshaanza kufanya *robbing* hata kwa wabunge kutaka mkataba wao uendeleo kuwepo. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na Bunge lako Tukufu tuungane kwa pamoja tupinge mkataba huo kuendelea kama mkataba huu haujafanyiwa *review*. Kwa sababu kama Taifa hatunufaiki kwa namna yoyote na masuala haya yameanza kuzungumzwa toka mwaka 2009 na *CAG*; mwaka 2018 na *CAG*, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge mwaka 2005 wakati huo alikuwa Mheshimiwa Shelukindo amezungumza suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapoteza kila mwezi zaidi ya Dola milioni 5 kwa sababu ya mkataba huu mbovu. Ninaelewa, ninaelewa huenda wakati huo walikuwa wanataka ku-*rescue* nchi, kuitoa nchi kwenye giza lakini tunapokwenda sasa mwaka 2024 wakati mkataba huu unakwenda kuendelezwa, kukubaliwa kuendelezwa. Namuomba Mheshimiwa Rais, nakuomba na wewe kupitia Bunge lako Tukufu, tupinge mkataba huu kuendelea kama haujafanyiwa *review* ya aina yoyote ili wananchi wetu waweze kunufaika kwa kiwango kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kama sisi tuliwekeza kwa sehemu kubwa kwasababu sisi tuliwekeza 73% kwenye *Capital Structure* halafu SONGAS waka-*invest* kwa 27% kwenye *investment structure* lakini kwenye *shareholding structure* SONGAS wao ndio *majority* kwa kumiliki 54% haiwezekani. Ninaomba suala hili litazamwe upya na tuangalie na tulitazame kwa namna ya kipekee.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa jambo dogo sana kwa ufupi najua dakika zangu zimekwisha, suala la umeme wa upepo. Leo tunazungumzia suala la *energy mixing*. Unazungumzia suala la *energy mixing*, tunajua kuna vyanzo mbalimbali; lakini ni kwa nini upepo umesahaulika?

Mheshimiwa Spika, natoka Mkoa wa Singida; Mkoa wa Singida ni miongoni mwa maeneo ambayo yanaongoza kwa upepo mkali *East Africa* nzima na inauwezo wa kuzalisha *Megawatts* za kutosha kutokana na umeme wa upepo. Lakini suala hili limekuwa likipigwa danadana miaka nenda miaka rudi na ninakumbuka mwaka 2017 nilisimama humu Bungeni nikamuomba Mheshimiwa Waziri na ninashukuru huyu huyu ambaye aliyepo sasa, nikamuhoji kuhusiana na suala hili na akasema ndani ya miaka miwili umeme wa upepo Singida mradi utanzaanza kutekelezeka. Lakini mpaka ninavyozungumza hapa hata nguzo hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba suala hili mkumbuke basi na chanzo hiki muhimu sana cha upepo ili kuweza kutusaidia wananchi wa Singida lakini pia na Taifa kwa ujumla kwa kuzalisha *Megawatts* za kutosha. Baada ya kusema hayo, nashukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki Wabunge wote Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jesca Kishoa kwa mchango wako. Nishakutaja Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo na Jacqueline Kainja Andrea ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara hii ya Nishati na Madini.

Kwanza kabisa niipongeze sana Serikali yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya katika miradi mikubwa, miradi ya kitaifa, ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameizungumza. Kwa kweli na mimi niendeleo kuuunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na viongozi wote wa wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha suala hili la Nishati na Madini linakwenda vizuri katika Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Februari, 2018 Serikali yetu ilitujengea *sub-station* kubwa pale Mbagala ambayo imekuwa na uwezo wa kuzalisha *Megawatts* 42 za umeme ambazo zimekwenda sana kunufaisha katika Jimbo la Mbagala. Katika kipindi hiki ambacho tumeanza kutumia *sub-station* hiyo kwa kweli wananchi wa Jimbo langu la Mbagala walikuwa hawana tatizo lolote la umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kufika mwaka 2020 mahitaji ya Jimbo letu la Mbagala ni *Megawatts* 32; 2020 ilipofika kwa kuwa Ndugu zetu wa Mkuranga Mkoani Pwani wao hawana *sub-station* ya umeme, umeme ule ambao unatoka kwenye *sub-station* ya Mbagala umepelekwa Mkuranga pamoja Lindi. Kitu kilichosababisha Jimbo la Mbagala libaki na *Megawatts* 8 tu, kitu ambacho kimesababisha sasa tatizo kubwa la umeme katika Jimbo la Mbagala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika hivi sasa tumekuwa tukipewa umeme kutoka Ilala, Kinyerezi na umeme mwingine ukitoka pale Kurasini. Kwa kuwa umeme huu umekuwa ukitoka sehemu tofauti tofauti; umekuwa na shida kubwa sana ya ukatikaji wa mara kwa mara. Kwa wastani siku moja nilimuonesha Naibu Waziri, kwa siku umeme umekatika zaidi ya mara 45. Sasa tunajuliza sisi wananchi wa Mbagala tuna tatizo gani? Kama *sub-station* Serikali yetu imetujengea yenye uwezo wa kuzalisha *megawatts* 42 uwezo

wetu wa kutumia ni *Megawatts* 32; kwa nini umeme ambao unatokana na *sub-station* ya Mbagala unapelekwa Mkuranga? Huku ukituacha watu Mbagala tukiwa na masikitiko na malalamiko makubwa ya ukatikaji wa umeme mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali la msingi hapa katika Bunge lako hili Tukufu, Mheshimiwa Waziri alinjibu kwamba *sub-station* ile inakwenda kufungwa *transformer* ya *MVA* 50; lakini nimepitia bajeti ya wizara sijaona mahali ambapo imetengwa fedha kwa ajili ya mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Jimbo la Mbagala ndio jimbo lenye watu wengi katika Nchi hii, na ndio jimbo lilitoa kura nyingi kwa Chama Cha Mapinduzi, sasa niwaombe sana, niwaombe sana, tafuteni utaratibu mwingine wa kuwapa umeme watu wa Mkuranga. Watu wa Jimbo la Mbagala tuendeleo kunufaika na *sub-station* ambayo imejengwa katika Jimbo letu la Mbagala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni mzalendo wa Nchi kwa ujumla, naamini kwamba Mkuranga nao wanahitaji sana suala zima la umeme. Hebu tuangalie namna ya kujenga *sub-station* Mkuranga ili waweze kujitegemea na sisi Mbagala tuendeleo ku-*enjoy* na matunda ya *sub-station* ile ambayo imejengwa Mbagala.

Mheshimiwa Spika, wateja wa umeme walioko katika Jimbo la Mbagala ni wateja 75,563. Naamini idadi hii ni kubwa kulinganisha na mkoa mingine ya ki-*TanESCO* katika Nchi yetu. Idadi ya maunganisho mapya kwa mwezi tuna wastani wa maunganisho 400 kwa kila mwezi. Sasa sielewi kwa nini *TanESCO* na wizara hii tunashindwa kufanya Mbagala ikawa mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa Mbagala kuwa mkoa, tunakwenda kuondokana na matatizo mengi ukiangalia mita, nguzo na vifaa vingine lazima twende tukapate *main store* ambayo iko mkoani. Na kulingana na ukubwa wa Mbagala na maunganisho haya mapya ya kila mwezi

yanapelekea kunakuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kupata huduma hiyo. Wakati nauliza swali Mheshimiwa Waziri alinjibu tuandike maombi; sidhani kama ipo haja ya kuandika maombi. Ninyi wenyewe *TanESCO* mnaona, ninyi wenyewe wizara mnaona umuhimu wa eneo, hebu niwaombe sana muangalie Wilaya hii ya Mbagala iweze kupata hadhi ya kuwa mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mbalimbali inaendelea katika jimbo langu la Mbagala. Upo ule mradi wa Malela kule Tuangoma, Yamoto Band kule Mbande, Machimbo pale *Azam*, Mponda, Yatima n.k. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii imekuwa na changamoto kubwa baadhi ya maeneo zinaletwa nguzo kulingana na idadi ya mradi lakini ukifika pale baadhi ya wananchi kwa kutaka umeme walikuwa wameshajiungia umeme kwa kulipa *TANESCO* na wakaletewa nguzo. Zile nguzo zinazobaki kwenye mradi zinarudi kwanini zirudi wakati bado upo uhitaji wa umeme katika maeneo yale? Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kama wananchi wamejitahidi kuvuta umeme na mradi umekuja katika eneo lile; basi nguzo zinazobaki ziendele kufanya extension katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nimekuwa nikipata changamoto sana katika maeneo ya Kata ya Chamazi, Charambe, Mianzini, Kirungule, Kiburugwa, Mbagala, Mbagala Kuu, Tuangoma, Kijichi, pamoja na kata ya Kibondemaji. Niwaombe sana wizara, niwaombe sana, nguzo zile zinazobaki ziendele kuhudumia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo la zile zilizokuwa mita za zamani, wananchi wetu wengi wa Mbagala mnafaham vipato vyao ni vya chini, wengine wameuza majumba yao Kariakoo wamekuja kuhamia Mbagala, nyumba walioyoikuta wameikuta ina mita ya zamani ina deni mpaka milioni 8; leo hii unamtaka mwananchi akinunua umeme wa shilingi 1,000 akatwe nusu ya fedha ile illipe deni la nyuma. Kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki wakazi

wetu wa Mbagala. Niiombe sana wizara, iangalie namna bora ya kuweza kumaliza haya madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie, Mbagala bado wanakaa watu wa vipato vya chini Mheshimiwa Waziri; hebu tuangalie namna ambayo watu wa Mbagala si kupata huduma ya umeme wa *REA* bali wafanye maunganisho kama wanavyounganishwa katika watu wanaopata huduma ya *REA*. Kwa sababu miundombinu ipo, isipokuwa uwezo wao ni mdogo wa kulipia. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, nafahamu sana utendaji wako wa kazi na kwa sababu lengo letu ni kuongeza mapato katika Shirika letu hili la Umeme la *TANESCO* basi tutoe namna wananchi wale wanapoweza kuunganishwa umeme kwa kutumia gharama za *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nikushukuru sana na niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah J. Chaurembo kwa mchango wako. Mheshimiwa Jacqueline K. Andrea akifuatiwa na Mheshimiwa Francis I. Mtinga.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Nipende kumpongeza Waziri na Naibu wake Waziri kwa kazi nzuri. Nimpongeze Waziri kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa, lakini vile vile nipongeze kwa kazi nzuri wanazozifanya hususan katika umeme wa *REA* vijijini. Pamoja na kazi nzuri wanazozifanya bado tuna changamoto nyingi hususan katika Mkoa wetu wa Tabora. Umeme umekuwa ni wa shida, umeme una katikatika katika wilaya zote zinazopatikana Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mkubwa unaotarajiwa kutengeneza *sub-station* katika Wilaya ya Urambo pamoja na Sikonge. Urambo kwenda Kaliua mpaka Kigoma na Sikonge kwenda Katavi. Lakini umekuwa mradi ambao ulikuwa na malengo yake yalianza toka mwaka 2016 mpaka hivi sasa ni miaka mitano bado hatujaweza kufikia malengo.

Na tatizo kubwa linalokuja hapa mkandarasi ameshapatikana lakini shida ni *due diligence* ambayo inayochelewesha sana kufikia ukamilishaji wa kupata *transformer* kuweza kupeleka kwenye huu mradi ulipangwa Urambo na Sikonge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini mradi huu toka umeanza kitu ambacho kimeweza kufanyika ni kujenga majengo ya kupokelea umeme na pamoja kuweza ku-*identify* njia za kupitishia umeme. Lakini changamoto za kupeleka *transformer* bado ni shida kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri mwezi wa tatu alikuwa Wilaya ya Igunga pamoja na Uyui kuzindua umeme wa *REA* ambapo Wilaya ya Igunga waliweza kumueleza wanahitaji kutengenezewa vituo vya kupozea umeme pamoja na Uyui alizindua umeme katika Kijiji cha Ivumba na akaahidi utawaka kuanzia Aprili. Lakini mpaka leo wanakijiji wale wa Izumba wanasubiri sana umeme huo uweze kuwashwa lakini bado haujawashwa zaidi tu ya usumbufu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile nilikuwa naiomba wizara iweze kuharakisha huu mpango na mchakato wa kuweza kuhakikisha *transformer* zinafika kwa wakati katika kujenga vituo vya kupozea umeme katika Wilaya ya Urambo. Tunachangamoto nyingi sana katika Mkoa wetu wa Tabora hususan ni hizi wilaya ambazo nimezitaja umeme unakatika, hatuwezi tukasema Tanzania ya viwanda kama bado hatujawa na umeme unaoweza kujitosheleza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kusema watu wajajiri kama bado tunawakwamisha katika kuhakikisha wanajitafutia kipato na kukuza uchumi wao. Inafikiwa wakati kuna kina mama ambao wengi wamejikiti kwenye kufanya biashara za saluni, vijana na wenyewe saluni za kiume lakini mtu ana mteja umeme unakatika; hakuna utaratibu kwamba leo tutakuwa tumewashiwa kwa siku tatu au nne lakini leo umekaa tu unamuweke mteja *rollers* umeme umekatika. (Makofi)



Mheshimiwa Spika, lakini kwa Mkoa wa Tabora wananchi wengi wamejikita katika uwekezaji wa mashine za kukoboa na kusaga. Mashine hizo zinatakiwa zitumie umeme, sasa kama umeme hauna nguvu ndio mtu ameweka tu mpunga kwenye mashine yake umeme katika haujulikani utawaka lini tunategemea huyu mtu mapato yake aweze kupata kwa wakati gani. Wakati huo huo TRA bado inamuhitaji kupeleka mapato ambayo yametokana na biashara anayofanya; biashara yenyewe inategemea umeme, umeme unakatika bila ya mpangilio tuweze kuangalia katika huu Mkoa wa Tabora ambao kidogo kila kitu naona kama kinakuwa kipo nyuma nyuma.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wizara mturahisishie upatikanaji wa umeme wenye tija, wenye nguvu, ili wanawake hawa wa Mkoa wa Tabora wanaojikita katika shughuli zao za saluni wafanye kazi zao vizuri na shughuli zote zinazotumia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew. Sasa ni Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi kuchangia katika Wizara hii ambayo ni kichocheo kikubwa na muhimu sana cha maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na wananchi wangu. Wilaya yangu ya Mkalama ina vijiji 70 na katika vijiji hivyo 20 bado havijapata umeme na katika vijiji hivi ambavyo havijapata umeme Mheshimiwa Waziri iko kata nzima ya Mwanga ambayo haijawahi kuona umeme kata hii. Mheshimiwa Waziri, tarehe 17 Aprili, 2020 ulikuja Mwanga na Serikali ikakosa pale kwamba kesho yake tu tarehe 18 nguzo za umeme zitamwagika kama maji pale, wananchi walishangilia sana. Lakini, mpaka leo Kata hii wananchi wa

vijiji hivi vya Kata ya Mwanga ambavyo ni Msisai, Kidarafa, Mwanga, Kidigida, Msiu na Marera bado wanaota tu kwamba nguzo zitamwagika alisema Waziri. Nashukuru kwamba umeendelea kuwa Waziri katika Wizara hii na hivyo naamini sasa hutaiangusha kauli hii ya Serikali ambayo ilionesha kwamba nguzo zingemwagika kama mvua lakini mpaka leo kata hii haijapata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wziri nikuombe katika Awamu hii ya *REA III* kata hii iwe kata ya kwanza kupata umeme katika vijiji hivi 20 vilivyobaki. Mbaya zaidi Mheshimiwa Waziri, katika wakandarasi uliowaagiza kwenye Mkoa wa Singida ulimuagiza *Ms Central Electrical International Limited* kwenda kufunga umeme Singida. Lakini tulipomfuata akasema hana *scope* ya Mkalama. *Scope* yake ni Ikungi na Singida *Rural*. Kwa hiyo, mpaka hivi ninavyoongea *REA* Awamu ya III sisi hatuna mkandarasi, tuna kiini macho. Labda ningepomba katika majibu utakayokuja nayo utuambie mkandarasi wetu nani ili tumfuate tuweze kuona umeme unapatikana Mkalama.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Waziri kweli bei tumeshusha shilingi 27,000 kuingiza umeme na ametangaza leo hakuna kuuziwa nguzo lakini umeme unapofika huko vijijini wananchi wanakuwa wengi sna wanasubiri kuwekewa umeme. Waliolipia 27,000 na ambao hawajalipia 27,000. Hawa wanaoweka umeme wanasema sababu za vifaa vingine ambavyo vinasababisha uweze kuwekewa umeme. Nguzo zenyewe za *LV* kwa mfano kwenye Jimbo langu nguzo zinatakiwa 1400, hakuna. Kuna waya za *ABC* milimeta 50, kilometa 74 zinatakiwa, hakuna! Hiyo ni *reference* najua na majimbo mengine itakuwa hakuna. *Suspension clamp* karibu 990 hamna! *Tension clamp* 60 hamna, *staycompletewith* 140 hamna.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri tunapopeleka tuwapelee na hivi vifaa ili ile foleni ya kuwekewa umeme sasa kwa 27,000 iweze kufanikiwa. Kwa sababu, tunasema 27,000 lakini wananchi wako wengi wameshafanya *wiring* wengine wanasubiri lakini ukiwagusa

TANESCO hivi vifaa hawana na ukifuatilia kweli, hawana! Nakushukuru Mheshimiwa Waziri umekuwa mwepesi sana wa kuchukua hatua kw watendaji wazembe, hilo nikupongeze. Lakini nikuombe wapelekee na hivi vifaa ili unapowachukulia hatua wasiwe na sababu ya kulalamika hukuwapelekea vifaa halafu umewachukulia hatua kwamba ni wazembe ili hili zoezi la 27 na umeme kufika kule vijijini wananchi walipate kwa kuhakikisha basi vifaa hivi vinakwenda. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa kuna taarifa endelea.

### T A A R I F A

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe Taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa kwamba wako baadhi ya watu wenye uwezo wao ambao kutokana sasa na vifaa vile kutokuwepo wanakuwa tayari kwa hiari yao kulipa nguzo pamoja na zile gharama kwa hiari yao. Kwa hiyo, wale watu walioko kule nao wanashindwa kufanya hivyo hata kama wangeweza kufanya hivyo kutokana na kwamba bei imewekwa elekezi 27,000 wale wenye uwezo walio wachache.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea lakini sifurahishwi sana na hii. Wenye uwezo wanaweza wakasababisha TANESCO wakalalia huko kwenye uwezo na wananchi wetu wenye vipato vidogo ikashindikana. Kwa hivyo, ningeomba tu vifaa viende halafu wananchi wote wapate umeme kwa hiyo 27,000 ambayo Serikali yetu imeiweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niusemee na Mkoa wangu, Mheshimiwa Waziri wakati unafungua matumizi ya gesi majumbani kule Lindi ulisema kwenye hotuba yako kwamba mikoa itakayofuata baada ya Dar es Salaam ni Mikoa ya

Morogoro, Dodoma na Singida uliitaja. Tulishangilia sana jambo hili kwamba sasa na sisi tutapata umeme wa gesi kupitia bomba ili kwenye nyumba zetu tuweze kusambaziwa gesi. Lakini katika hotuba yako nilikuwa nasikiliza kwa makini sana ili niweze kuona ule msukumo wa hotuba yako ukiendana na bajeti, sikulisikia hili.

Mheshimiwa Spika, nikuombe, jambo hili ni la muhimu sana, kupata gesi ya majumbani ambayo tumeweka bomba kwa gharama kubwa sana limefika Dar es Salaam na tunatumia kidogo mno kwa kiasi cha gesi inayofika pale.

Sasa huu mpango uliusema kwenye hotuba ambayo nilikuwa najua ni hotuba ya ukombozi hujalisema kwenye bajeti. Labda pengine utakapokuja kwenye kujumuisha useme huu mpango wa kutoa bomba lile la gesi kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro kuja Dodoma na hatimaye kufika Singida kwenye mkoa wangu kama upo au au haupo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini niwaombe tu Serikali hivi vitu vingine kama bajeti inakuwa ngumu na miradi hii ni mikubwa, tuisahau *private sector*. Najua shirika la *TPDC* limepewa mamlaka ya kisheria kama hodhi kufanya hili jambo peke yake. Mzigo huu unakuwa mzito, *private sector* ipo na watu wana fedha. Mimi ningeshauri Wizara muwe mnaangalia na vitu vingine kama hivi vizuri mnaruhusu *private sector* isaidie basi huduma hizi zinaweza kufika haraka sana katika nyumba zetu.

Mheshimiwa Spika, hii gesi itasaidia sana kulinda mazingira, ni faida mtambuka, kwanza maisha ya wananchi yatashuka kwa maana gharama zitashuka kwa sababu wataacha kununua mkaa kwa bei kubwa lakini vile vile mazingira ya nchi katika mikoa yetu hii yataboreka kwa sababu watumiaji wakubwa sana wa mkaa wako mjini. Sasa kama mabomba ya gesi yakifika ina maana soko la mkaa litakufa na mazingira yetu yatapona na fedha nyingi zinazokwenda Wizara ya Mazingira kwa ajili ya kuokoa miti zitakuwa zimepona. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu ni mradi ambao utakuwa ni wa kimkakati kabisa. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, jambo hili ullisema wewe kama Serikali. Usiliweke kando. Ni jambo la muhimu sana, najua gesi ikifika Singida mwisho itakwenda mpaka Shinyanga na mwisho itamaliza nchi yetu yote. Mradi wa maji unatoka Ziwa Viktoria, upishane na gesi kwenda kule. Nchi yetu ni kubwa, ni soko tosha la miradi yetu ya kimkakati kwa hiyo tuitumie vizuri kwa kuhakikisha gesi hii inafika Singida kama ambavyo ulikuwa umesema kwenye hotuba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sipendi sana kugongewa kelele. Naomba nishukuru na kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri uje na majibu kuhusu jambo hili la gesi. Ahsante sana na suala la umeme kule Mwangi na vijiji vilivyobaki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mtinga. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga yupo? Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kweli nilikuwa nimejiandaa kuchangia kesho lakini tuendelee. Ni heshima kubwa umenipa, ninashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo nilitaka kuzungumza tumesema kwamba tunataka kuleta umeme wa vyanzo tofauti tofauti. Nilikwenda kumuona Waziri wakati fulani. Namshukuru, alinipokea. Kuna watu walikuwa wanataka kuweka mradi wa umeme kwenye Jimbo langu, mradi wa *solar*. Nilivyoongea na Waziri alinipokea vizuri lakini nikiangalia utekelezaji wake kwa watendaji wake naona kama iko polepole sana kwa sababu nimekuwa nikifuatilia sioni kama napata majibu vizuri.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema ni nini? Kama mradi huu wa *solar* utaweza kujengwa kwenye Jimbo langu la Kalenga kwanza utausaidia Taifa kupata umeme kwa sababu hawa watu wanataka kuleta *Megawatt 50* ambazo wataziingiza kwenye *grid* ya Taifa. Lakini pia kwenye Jimbo

langu watu watapa ajira, pamoja na kuongeza uchumi katika maisha yao, hii ni muhimu. Nataka nikuambie Waziri hili jambo nitaendelea kulifuatilia na wewe unisaidie kuhakikisha kwamba huu mradi wa *solar* kwenye Jimbo la Kalenga unatekelezwa na huyu mtu ambaye ameonesha nia ya kutaka kuweka huu mradi apate hiyo fursa kwa sababu itatusaidia kufikia malengo ya Kitaifa ya kuhakikisha kwamba tunaongeza *megawatt* na kuwa na vyanzo tofauti tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuishauri Wizara na *TANESCO* kwa ujumla, tunavyopeleka huu umeme wa *REA III* sasa kwenye vijiji tuhakikishe kwamba tunaangalia Taasisi. *Of course*, maagizo wewe Waziri umeshatoa lakini nataka kwa watendaji wako wafahamu hili ni suala muhimu sana taasisi kama shule, kama zahanati, hizo ni muhimu sana zipewe kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninapokea malalamiko hapa watu wananiambia umeme wa *REA* umepita lakini kwenye shule tumeambiwa kwamba tununue nguzo. Nafikiri hilo hapana. Kwamba ni muhimu sana kuona kwamba tunapeleka umeme huko watoto wetu wasome lakini pia na kwenye zahanati watu waweze kupata huduma. Ninavyo vijiji kadhaa hapa ambavyo havina umeme na ninaomba kwamba katika mradi huu wa *REA* tunaokwenda nao sasa tuhakikishe kwamba vijiji ambavyo havijapata umeme tukiangalia kwenye Kata ya Wasa na vijiji kama Ulata lakini tukija kwenye Kata yangu ya Luhota kuna vijiji kama Wangama, Ikuvila ambavyo tayari kwa miaka mitatu watu wameshasuka umeme, wameshalipia lakini umeme haujawashwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru Waziri kwa sababu Wizara yako kweli imefanya kazi hatuwezi kulalamika lakini ni muhimu kwa sababu kwamba kwa kadri tunavyoendelea kuongeza huduma na matamano ya watu ndiyo yanakuwa makubwa. Kikubwa kingine ni kwamba kuna maeneo mengine tuna umeme mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kijiji nilichozaliwa mimi Kijiji cha Nyamihu kwamba tuna *transformer* iko mbali sana na wananchi wangu wamekuwa wakilalamika kwamba tunataka *transformer* isogee hapa kijijini ili sisi tuweze kuwa na umeme wenye *phase* tatu. Tuweke mashine za kukoboa, za kusaga. Kwa kufanya hivyo, tunavyoongezea hii huduma maana yake tunazalisha ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Gambo, siku moja alisema hapa kwamba anashangaa inakuwa kuwaje Serikali imesema itaajiri watu milioni nane. Hapana, Serikali inavyosogea huduma karibu na wananchi kama umeme maana yake kama tunaweka mashine za kusagia maana yake tumezalisha ajira. Tunavyoweka viwanda vidogo vidogo maana yake ndivyo tunavyozalisha ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana kwamba taasisi tuzizingatie. Kwa mfano katika Kata yangu ya Kiwele nimekuwa nikilalamikiwa hapa kuna kitongoji kimoja cha Kipengele, yaani umeme umeruka lakini eneo hilo ndiyo lenye shule na eneo hilo ndilo lenye makanisa. Ndiyo maana tukasema kwamba *focus* iwe kwenye huduma za jamii zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tuangalie vile vitongoji vilivyoko pembezoni, vile vilivyoko pembezoni tukianza navyo hivyo ni rahisi wakati mwingine kurudi katikati. Kwa hiyo, nikuombe sana kwa hayo machache tuone namna gani tunaweza tukapeleka umeme hasa kwenye jimbo langu. Lakini jambo ambalo pia nataka kusisitiza nikukumbushe tu Mheshimiwa Waziri Jimbo la Kalenga ndilo jimbo ambalo Spika wake hapa ndiyo amekaa muda mrefu kuliko mtu mwingine yeyote. Lakini ukiangalia pia Chifu wetu Mkwawa ndiye Chifu ambaye alitetea nchi hii kuona kwamba isitawaliwe na Wajerumani na wengine waliokuja. Kwa hiyo, ni Jimbo moja muhimu sana. Kwa hiyo mnavyofikiri akupeleka huduma lazima hizi *facts* zote mziangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Rais wakati anafanya uteuzi wa Wakuu wa Mikoa amewakumbuka

waasisi wetu. Amechagua mtoto wa Nyerere, akachagua mtoto wa Sokoine. Maana yake amekumbuka michango ya hawa waasisi walichofanya. Lakini na Jimbo la Kalenga katika nchi hii lina mchango mkubwa sana. Kwa hiyo, wewe pamoja na Waziri mwingine wanavyofikiria kupeleka huduma, Jimbo la Kalenga lipewe kipaumbele kwa sababu ya mchango wake mkubwa sana kwenye Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa hayo machache. Naamini mambo mengine tutaendelea kuzungumza. Ahsante sana Spika kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Nilichanganya mambo, unajua humu ndani kuna Jackson Kiswaga wa Kalenga na kuna Boniventura Kiswaga wa Magu. Sasa nimeshika neno Kiswaga kwa hiyo nikakukurupusha bwana. Lakini ilikuwa awe Boniventura Kiswaga, mtani wangu wa Magu. Na wewe umezidi kuroga sasa ndiyo tatizo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Bonivenura utaongea jioni na wengine wote ambao tunao. Tutaanza na Mheshimiwa Fredy Atupele, Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa, Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Venant Protas, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mheshimiwa Selemani Zedi na wengine wote mtapata nafasi ya kuongea jioni. Walio wachache kama kuna mtu angependa kuongea jioni pia nawaalika.

Basi tutaendelea na michango yetu na kwa hatua hii basi naomba nisitishie shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

*(Saa 06.55 Bunge Mchana lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jion Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu!



**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati  
kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, bila kupoteza muda namuita mchangiaji wa kwanza, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete na atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. *(Makofi)*

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati jioni hii ya leo. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametukusanyisha tena mahali hapa jioni hii tukichangia Wizara hii muhimu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa namna ya kipekee kwa kazi nzuri anayowafanyia Watanzania, lakini pia kwa mikataba ambayo tayari tumeshaingia na wenzetu wa Uganda katika bomba hili la mafuta kutoka Uganda mpaka Mkoa wa Tanga. Kipekee pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya nishati pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wa Wizara hii, wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba, Mheshimiwa Waziri wewe tangu umekuwa Naibu Waziri umeitendea haki Wizara hii, kipekee nitambue mchango wako mkubwa, natambua uipokuwa Naibu Waziri Wizara hii ilikuwa ina mapato ya bilioni 9 kwa wiki, leo hii Wizara inakuwa na kati ya bilioni 42 mpaka bilioni 47 ni hatua kubwa sana, lakini pia shirika lilikuwa katika hali ambayo si sawa kifedha, lakini hivi leo shirika linajiendesha lenyewe na baadhi ya miradi

linaweza kusimamia lenyewe kwa fedha za ndani ni hatua kubwa sana hii Mheshimiwa Waziri, lakini jambo lingine pia nikupongeze pamoja na watendaji wako kwa kuchukua hatua; hivi karibuni umechukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wote ambao hawafuati maelekezo ya Wizara. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nataka nikupongeze kwa kusimamia vizuri miradi yote ya kimkakati ukiwemo mradi mkubwa wa Mwalimu Nyerere ambao utazalisha *Megawatt* zaidi ya 2,115 pamoja na miradi mingine mbalimbali ambayo Wizara inaanza kusimamia na kwa hakika mnastahiki pongezi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite zaidi katika umeme huu wa *REA*. Umeme wa *REA* umekuwa mkombozi mkubwa sana katika maeneo yetu katika nchi yetu ya Tanzania. Lazima tukiri Serikali imefanya kazi kubwa na kwa msingi huo Jimbo langu la Busokelo lina vijiji 56 na katika vijiji vyote 56 vimepata umeme vijiji 55, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Na kwa msingi huo bado Kijiji kimoja tu cha Kilugu ambacho kipo Kata ya Itete, nikuombe katika awamu hii na mzunguko unaofuata nacho kipate umeme katika awamu hii inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, licha ya kwamba, vijiji 55 vyote vimepata umeme, lakini kuna changamoto katika kupeleka kwenye vitongoji. Katika kata ambayo ina vijiji vitano na katika kijiji kimojawapo inaweza ikawa na vitongoji sita na katika vitongoji sita vinaweza vikapata vitongoji viwili; tunahesabu kweli kwamba, kijiji kimepata umeme, lakini vitongoji vinne vyote vinakuwa havina umeme. Naamini katika mipango ijayo basi tuwekeze zaidi katika vitongoji, ili vitongoji vyote sasa vya Tanzania tuone kwamba, tuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mmoja anafahamu kwamba, umeme ndio uchumi, umeme ni viwanda. Umeme ni nuru, umeme ni kila kitu katika maisha ya Mtanzania. Kwa maana hiyo, niipongeze pia Wizara kwa kuendelea katika kuratibu

na kuzalisha umeme kwa kutumia njia jadidifu, hususan, *renewable energies*. Na nimeshuhudia miradi hii, *geothermal*, ikiwemo ambayo inaendelea kuchorongwa kule kwangu Jimbo la Busokelo tumechoronga vishimo vitatu na dalili zote za kuonesha kwamba, *geothermal* ipo kwa hiyo, lazima niipongeze sana Serikali kupitia Kampuni tanzu ya *TANESCO, Tanzania Geothermal Development Company*, ambayo inafanya kazi hiyo ya uchorongaji ni hatua kubwa sana hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote nataka pia nizungumzie Shirika letu la *Petro/Nchini, TPDC*. Tumeona gesi inavyozalishwa, lakini pili tumeona kutoridhishwa katika usambazaji wa gesi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lililopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya *PIC*. Tulitembelea maeneo mengi ambapo *TPDC* imepeleka gesi, tunawapongeza sana, lakini kasi yake ya kupeleka kwa wananchi bado hairidhishi. Kupitia hotuba hii Mheshimiwa Waziri, naomba sasa watu wa *TPDC* wajipange namna ya kupeleka *cubic* nyingi zaidi kwa wananchi. Kwa sasa hivi wamepeleka zaidi ya 733,521 futi za ujazo wakati wananchi zaidi ya milioni 50 tupo Watanzania kwa hiyo, waongeze kasi zaidi katika kupeleka umeme maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri utakapokuja tunataka ueleze kinagaubaga Wizara imetoa miongozo kwamba, umeme ni kweli 27,000/= lakini kuna baadhi ya maeneo umeme hawatozwi 27,000/=. Hii imekuwa ni changamoto na Wizara kadiri mnavyotoa maelekezo mara nyingi watendaji wenu wa chini hawawaelewi. Nafikiri kuna namna ambavyo mnaweza mkafanya ili waweze kuelewa kwa sababu, kama Serikali inapeleka umeme kwa 27,000/= lakini watendaji hawafuati hayo basi kutakuwa kuna namna ambavyo inatatakiwa mchukue hatua zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka nizungumzie ni suala la *EWURA*. *EWURA* mwaka 2018 niliweza kuchangia namna ambavyo wanaweza kusambaza ama wakatoa

miongozo na kanuni, niwapongeze kwamba, sasa hivi wametoa miongozo na kanuni namna ambavyo hata vituo au magari ya kuuzia petroli ama dizeli yanaweza kufanya kazi, lakini baadhi ya maeneo ambamo hakuna petroli ama dizeli imekuwa ni changamoto kubwa sana na ukiwafuatilia watu wa *EWURA* wanakwambia kanuni zimekamilika, lakini utekelezaji ndio umekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba suala hili waharrakishe watu wa *EWURA*. Maeneo yote ambayo hayana mafuta, hususan *peripherals*, sehemu ambazo hakuna *petrol stations*, basi watumie njia mbadala ya magari maalum ambayo yana mita na yanaweza yakafanya biashara hii na Serikali ikakusanya kodi yake na pia tukapunguza gharama za wale watumiaji ambao wanatumia mafuta ya kwenye vidumu na wanaua magari yetu, hususan *pump* huwa mara nyingi sana zinakufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nizungumzie suala la umeme kukatikakatika sana. Katika Jimbo langu la Busokelo kwa siku unaweza ukakatika umeme zaidi ya mara 24 na sababu kubwa sana ya kukatika umeme kule ni kwa sababu upepo, mvua pamoja na miti mingi sana, lakini mwaka 2018/19 Serikali ilichukua hatua za kuweza kufyeka miti yote kwenye *line*. Hadi magimbi ya chini walifyeka, lakini tatizo hili mpaka leo bado lipo.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu kwa Serikali, ikiwapendeza kwa sababu, maeneo yale ni mvua nyingi sana kwa mwaka mzima. Basi mjitahidi mje na *solution* ya kuwa na nguzo za zege, lakini pia ikiwezekana nyaya badala ya kupita angani zichimbieni chini ardhini kama wanavyofanya wenzetu wa nchi nyingine zilizoendelea; lakini zaidi Waziri mkija na wazo la kuwa na nguzo za chuma katika maeneo yote ambayo kuna changamoto ya kukatika-katika umeme kwa sababu za kijiografia ya hali ya hewa, basi hii itasaidia na kupunguza hii hali kwa sababu, umeme unapokatika Busokelo, Tukuyu, Rungwe, Ileje, Kyela, lazima hiyo *line* iwe *affected* kwa kukatika kwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala hili la *back-ups* ama *systems* ama mifumo ya teknolojia kwa TANESCO. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulichukua hatua kubwa mara baada ya mifumo kusimama ama ku-*stop* kwa sababu tu *back-ups* hazikuwepo.

Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama mdau wa *ICT* inasikitisha sana kuona kwamba, *systems* zinakuwa *developed*, lakini wanakuwa hawana *back-ups*. Na *back-ups* hizi kuanzia sasa, kitaalamu ama kitaaluma, inatakiwa isiwe katika jingo hilo hilo la mifumo ilipo inawezekana wakaziweka hata Mwanza, hata Mbeya, lakini zikafanya *synchronization* ili ikitokea pengine *any catastrophe* ama janga lolote basi zile *back-ups* ziweze ku-*take off* halafu mifumo iendelee kufanya kazi kuliko kama ilivyotokea hivi karibu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka nizungumzie jambo moja, ni muumini wa *energy mix* na Serikali yetu inafanya kazi hii ya *energy mix*. Ninachotaka kusema kwamba, tunaweza tukafikiri zaidi ya hapa, kuna mifumo mingi ya umeme duniani kwa hivi sasa; ukienda Japan kuna mfumo unaitwa *co-diffusion new hydrogen energy*, mfumo huu ni *off grid*. Inawezekana kwetu sasa tunaweza tukaanza kuufikiria hata kama hatujaanza kuutekeleza, lakini ni mfumo wa kutoa umeme kwa bei nafuu sana pasipo kutumia gharama ya kusafirisha nyaya kama tunavyofanya sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naamini kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri unaweza ukafanya tafiti kupitia wataalamu wako kwamba, umeme utoakanao na *hydrogen energy* ukoje kwa maana ya *off grid* kwa sababu, una faida nyingi. Kwanza hakuna nyaya kama tunavyofanya sasa, kwa mfano kama hivi Dodoma tungekuwa na umeme wa kwetu, Iringa wa kwao, hivyo hivyo kwa hiyo, ingepunguza hizi *distances* za kusafirisha umeme umbali mrefu, lakini kukatikakatika, lakini zaidi mfumo huu unarahisisha kupunguza mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na mwisho kabisa nishukuru sana Serikali kwa kutuletea umeme wa Lumakali ambao utazalisha *Megawatt* 222 katika Mkoa wa Njombe, Jimbo la Makete pamoja na Busokelo. Nina hakika utakuwa na fursa nzuri kwa Watanzania kwa ajili ya kuwekeza, lakini pia kwa ajili ya kuongeza katika uzalishaji wa umeme na viwandani hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa fursa, nikutakie kila la heri Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza bajeti hii na mimi naiunga mkono asilimia 100 ili mkafanye zaidi ya hapa mlipofanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete kwa mchango wako mzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge ninaye mgeni kwenye *gallery* ya Spika kule, mgeni maarufu ambaye ningependa kumtambulisha na ningependa basi ikiwezekana apigiwe makofi ya kutosha, huyo mgeni wangu. Mgeni huyo sio mwingine bali ni Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika. *(Kicheko/Makofi)*

Ahsante sana, nilitaka na yeye mwenyewe aangalie kwenye *gallery* anatafuta mgeni, kumbe mgeni ni yeye. *(Kicheko)*

Mzee wetu huyu ni mmoja wa wazee wetu wa Bunge hili. Kwa uzoefu wa muda mrefu kama Mbunge, kama Waziri, kama mtumishi wa Serikali na tulimkosa kwa kitambo kirefu. Sasa kwa kuwa ndio nimemuona tu sasa hivi nafikiri mtanikubalia tumpe dakika tano atusalimie halafu tuweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, karibu. Karibu utusalimie. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI MAALUM:**  
Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wabunge wenzangu, kama alivyonitambulisha Mheshimiwa

Spika, naitwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Jimbo la Newala Mjini. Nikimaliza *term* hii nitakuwa nimepiga 20 miaka humu ndani; naomba Mungu iwe hivyo nisiugue tena kama juzi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sikuwa na wenzangu Wabunge kwa muda wa miezi karibu mitatu. Nilikwenda matibabu nje ya nchi, lakini nataka nikwambieni kwamba, tatizo lililonipeleka nje limekwisha kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ugonjwa mtu kuugua pingili sio kama UKIMWI, wataalamu wanapiga *operation*, wanazipanga upya, lakini yenyewe iliwa kabisa miguu yangu. Wale mliosoma sayansi wanasema mishipa ya fahamu iko mgongoni, kwa Kiswahili chao kule waliniambia mishipa ya fahamu nayo ilikuwa *disturbed* ndio maana nilienda mlemavu, lakini Mungu bariki wamenitibu wale natembea kwa ukakamavu kama zamani.

Kwa kusema kweli, lazima niishukuru Serikali yangu kwa sababu, iliniruhusu kwenda matibabu na mke wangu, tukahudumiwa vizuri mpaka niko hivi mnavyoniona sina fimbo wala gongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tupeane pole kwa misiba iliyotokea ilinikuta niko India; Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Majaliwa, *Chief Secretary* na wengine.

**SPIKA:** Magufuli. (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI MAALUM:**  
Mheshimiwa Spika, nilisema nani?

**MBUNGE FULANI:** Magufuli, ulisema Majaliwa.  
(*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI MAALUM:**  
Mheshimiwa Spika, unajua ndio taabu ya majina yanayoanza Ma, Ma, Ma. Samahani, naomba radhi. Wazungu wanasema *slip of the tongue*, ulimi uliteleza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tupeane pole kwa msiba wa Rais wetu. Napenda pia kumshukuru Rais, marehemu, aliidhinisha mimi kwenda kutibiwa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaondoka alinipigia simu akaniambia nimeona ruhusa yako unaenda kutibiwa India, nenda katibiwe urudi uchape kazi. Sikujua kwamba, ndio mazungumzo yangu ya mwisho na Rais wangu Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Spika, lakini tupongezane nchi yetu kwamba, tuna Katiba nzuri, nchi nyingine Rais akifa ni vurugu *match*, unaona *West Africa* kule, mara wengine wanasema arithi mtoto wake, mara wanajeshi nao wanataka, nadhani sisi Katiba yetu iko safi, ikitokezea bahati mbaya Rais akafariki Makamu wa Rais ata-*take over*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shwari, tumemaliza msiba, tumetengeneza Serikali yetu. Nataka nimshukuru Rais Samia nikiwa India kitandani watoto wangu wakanipigia simu kwamba, umeteuliwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais. Leo nimeapa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Ikulu, Kazi Maalum, kazi? (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Maalum.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI MAALUM:**

Mheshimiwa Spika, usiniulize kwa sababu, ndio nakwenda kupewa, ile wanajeshi tunasema *Stand Orders* za kufanyia kazi. Gari langu ukiliona limeandikwa tu Waziri wa Nchi, OR - Ofisi ya Rais, basi tumemaliza.

Mheshimiwa Spika, na wewe nakushukuru kabisa, nilifikiri kesho asubuhi utafanya mambo haya, lakini bahati nzuri ukasema hapana, zege halilali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuongea na Wabunge wenzangu kuwaambia kama nimerudi, kuwaambia Watanzania wenzangu kwamba, nimerudi, nimepewa majukumu; nitayatekeleza kwa juhudi na maarifa.



Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru. Aah! Niwapongeze Ndugu zangu wa Simba wanaongoza ligi, ila Kombe la Mapinduzi kule Zanzibar walipata matatizo kidogo wakaondoka usiku uleule, wenzao wakabaki siku mbili. Sasa hatujui ya huko mbele, nimeambiwa tutapangiwa tena tucheze. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda ulionipa umeisha, nakushukuru kunipa nafasi ya kusalimiana na Wabunge wenzangu, ahsanteni sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Karibu sana Mheshimiwa Waziri, karibu sana Mbunge mwenzetu kwakweli tumefarijika sana kuwa nawe sana sana sana tuliku-*miss* haswa, ile miezi hii mitatu ulipokuwa haupo timu yako ya Yanga imekuwa hoi bin taaban lakini kwa vile kuna mechi tarehe mwezi ujao labda mzee umerudi hatuwezi kurudi inawezekana umekuja na mikoba ya kihindi *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa karibu sana Mheshimiwa Mkuchika ahsante sana kaka yangu. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere nimeshakutaja atafuta Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii ya Wizara ya Nishati, binafsi nimefurahi kumuona Senator wetu Mheshimiwa George Mkuchika kwa kweli tuwe wakweli mwanadamu ni roho tu kama roho zetu zipo salama tunatakiana mema humu ndani, tunatakiana mema kwenye roho, roho tu ndio Mungu anaitaka iendeleo kuwepo hiki kiwiliwili ni cha hapa hapa duniani lakini roho ni ya Mungu ikiendelea kuwepo tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara ya Nishati wanafanya kazi nzuri sana sana. Wizara hii sisi ambao tulikuwa wabunge wa CCM tulikuwa tunatekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi kusema kweli sehemu kubwa ya vijijini ya utekelezaji wa Ilani hii Wizara ndio imetekeleza, kura nyingi tulizozipata katika CCM kwa utekelezaji wa Ilani ni pamoja

na hii Wizara ya Nishati, na hasa mradi wa *REA* vijijini kwa hiyo mradi wa *REA* vijijini ni muhimu sana Wizara imefanya kazi lakini Waziri wake na watumishi wengine wote na Naibu, ila tunamfahamu Waziri zaidi kwa sababu tumekaa naye muda mrefu kidogo nidhamu yake haina mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haina kabisa katika watu wanaotaka kupewa nidhamu baadhi ya Mawaziri wanaotaka kupewa nidhamu kwa utendaji na kwa kumpigia simu na kupokea na kunyenyekea na kufanya kazi huyu bwana anafanya kazi kweli sio utani. Anafanya kazi nzuri sana. Sasa niombe, kwamba huko tunakokwenda huko mbele mimi naona kama Wizara imekuwa na shughuli nyingi mno na hili unaweza kulisimamia hii Wizara inapokwenda nimesikia juzi tunatafuta mafuta, kutafuta mafuta ya kuchimba baharini ashughulike Mheshimiwa Dkt. Kalemani Bomba la kutoka Uganda lije Tanzania Mafuta ashughuliye huyo huyo, gesi inayotoka *NLG* aende yeye *sun NLG* wanaita aende yeye wewe msukuma acha, bwawa la Mwalimu Nyerere aende yeye ashughulike sijui na vinasaba na mafuta kutoka Bandarini yeye. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naona tufanye kama wenzetu tuwe na Wizara mbili Wizara ya maendeleo ya Nishati na Wizara ya Maendeleo ya *Petro*/kwani kuna shida gani kama hizi Wizara zina fedha za kutosha mambo ya mafuta ni mabilioni ya fedha, mambo ya umeme yajitegemee hivi leo umeme unakatika kila mahali, umeme wa *REA* hauendi Kalemani ataendaje Bunda, ataendaje Kongwa ataendaje huko wakati wamembana kwenye mikataba ya kwenda Uganda, kusaini Mikataba, tukubaliane Mheshimiwa Rais alione hili tutenganishe hii miradi ya kimkakati iwe na mtu mwingine na hii mradi ya umeme ibaki na watu ambao tunashughulika nao kila siku.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanataka kuona umeme habari ya kuchimba mafuta, habari sijui ya gesi inatoka kwenye mabomba ipewe mtu mwingine kuna shida gani, tuliangalie hilo naona sasa tukiliona hilo vizuri nchi yetu itaenda kwenye jambo la namna hiyo. Nimshukuru

Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri jana nimemuona kule Sokoni anahangaika na matatizo ya wananchi, amesimamia vizuri bomba la mafuta la kutoka Uganda ule ni mradi wa kimkakati wa muda mrefu lakini wenye faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamezungumza Wabunge wengi hapa ushauri wangu kwenye huu mradi Wabunge tuelimishe kuhusu huu mradi, huu mradi una mikataba mitatu mimi leo nikiambiwa mradi ule unafanyaje nitasema utapata ajira nyingi, utafanya nini lakini sijaelewa mikataba ya miradi hiyo ikoje. Kwa hiyo, Wabunge tuelimishe juu ya mikataba mitatu ya huu mradi ukoje, unafanyaje tupate Semina ya kutosha ili na sisi tueleze faida ya mradi huu itaendaje kwenye shughuli za kila siku huko mbele tunapokwenda.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la vinasaba sasa ninashindwa kuelewa wakati fulani ukisoma hadithi au ile *tips* za wakubwa wale watu waliokuwa wanatafuta uhuru akina Stephen Biko, anakwambia akili ya mwanadamu, akili ya mtu anayedhulumiwa yaani mtu anayedhulumiwa ili ajielewe anafanya kazi gani ya kudhulumiwa umpe akili wala usimpe silaha. Sasa ninashindwa kuelewa vinasaba ni nini, vinasaba ni vitu ambavyo mtu ameleta ili kutibu tatizo na nchi hii inaweza kuendeshwa bila vinasaba lakini leo kuna watu wamejipanga vinasaba vinasaba vinasaba.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema jambo moja vile vinasaba sasa hivi vinatozwa shilingi 14,000 mafuta yanayoingia nchini, mafuta tunayotumia sisi ni mafuta yanayotumika hapa nchini ni bilioni 14 ukizidisha na 14 ni bilioni 56 matumizi yake yakitoka *super profit* ni bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, kwanini watu wasiseme kwanini wati *doubt* bilioni 40 unaipeleka wapi? Kwa hiyo niseme kwamba *TBS* inauwezo wa kupima ubora wa mafuta lakini haina uwezo wa kuweka vinasaba mambo ya ajabu duniani hapa ubora wa mafuta *TBS* inauwezo wa kupima lakini kupima kuweka vinasaba haiwezekani vitu vya ajabu sana hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajiuliza madawa yanayotumika hapa nchini, madawa ya wanadamu sisi tunatengeneza hapa si tunaagiza yaani kuagiza madawa ya kutibu wanadamu hapa nchini ni jambo dogo kuliko kuagiza vinasaba, mambo ya ajabu hapa duniani hapa, mambo ya ajabu sana hapa tunaagiza mbolea tunaagiza madawa tunaagiza kila kitu tunafanya operation za binadamu vinasaba ni kitu gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe nishauri niombe vinasaba visimamiwe na *TBS* na *TBS* wachukue shilingi saba kwa sababu vile vinasaba ni shilingi nne unaweza ku-*handle*, shilingi saba nyingine ije *TARURA* tunahangaika hapa na mambo ya *TARURA* mambo ya Barabara na mambo ya nini tuna hela zipo hapa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere nilichokielewa *so far* kwa sababu niko nawasiliza wote wanasema hawa waliochangia kuhusu kinasaba mpaka sasa wanasema kuipa *TBS* sio tatizo ila tunajukumu sisi Wabunge wa kuirekebisha sheria ya *TBS* kwa kuwaongezea hilo jukumu ndani ya sheria, ili wafanye kisheria jambo ambalo nafikiri tumuhimiza Waziri endapo linakubalika ili sasa lifanyike hilo ili *TBS* wafanye ndicho nilichoelewa endelea tu lakini kuchangia. (*Makofi*)

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nadhani hii suala la sheria hivi ngoja nikuulize sisi wote ni Wabunge hapa na wewe ni Mbunge hapa hivi tulipoamua kununua ndege tulileta sheria gani? Si tulileta ndege zikawepo,

Mheshimiwa Spika, mimi ninachokisema umezungumza vizuri sheria ziletwe wakati huo *TBS* iendelee ku-*handle* kwa sababu wale watu hawana mkataba *TBS* iendelee kuwa nalo hilo eneo wakati sheria zinafanya nini, zinaletwa shida iko wapi? Tusiwe watu wa kunyonywa mimi mambo ya kunyonywa ndio siyapenda humu ndani, tuhangaike kwamba hili neno linaendaje ili liweze kuleta mahusiano yetu kwenye mambo kama haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani umeshauri vizuri sheria iletwe haraka, lakini wakati huo huo *TBS* iendelee kufanya hiyo kazi kwa sababu jamaa wale hawana Mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninazungumza kukatika kwa umeme wa REA sasa mimi nashindwa kuelewa ni umeme wa REA ndio unakatika au Umeme mwingine ya mjini haukatiki, kwasababu vijijini umeme wa REA unakatika mara 10 kwa siku shida ni nini kama sisi tunaumeme wa kutosha wa *megawatt* za kutosha katika nchi hii leo shida ni nini umeme unakatika mara kumi kuna watu hawafanyi kazi shinda inatokea wapi kwenye jambo kama hili. Kwa hiyo, ndio maana nimesema hii Wizara tuiangalie upya tuweze kuigawanya ili iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine nililotaka kuzungumza ni suala la mradi wa mikakati tuna bwawa la Mwalimu Nyerere tuna mradi *SGR* suala zuri duniani ambalo Marehemu Dkt. Magufuli tutamkumbuka miaka nenda rudi ni kwamba bwawa la Nyerere mradi ule unaendeshwa kwa Mkopo ambao hautulazimishi kuchukua bwawa wenzetu wa nchi jirani miaka ya karibuni hivi inayokuja miradi mingi ya mikakati itakuwa ya watu Zambia tayari na maeneo mengine tayari, lakini bwawa letu la Nyerere na niombe kwa *style* mliyotumia ya kukopa kwa fedha ya hiyari tusingie tena watu waje kuleta uhifadhi yaani kufadhili ile Rambo lile bwawa la Nyerere halafu liwe la watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ndio jambo, marehemu amefanya jambo kubwa sana kwamba mradi ule sasa hata ukiisha madai yake sisi hatudaiwi kwa nguvu, tutadaiwa kwa hiyari, na hivyo hivyo kwenye reli wenzetu wanaojua miradi ya namna hiyo ya mikakati huko mbele sio yao itakuwa ya watu kwa hiyo ninafikiri kwamba tuendelee kufanya na mimi naona Mama amejitahidi sana kuwa karibu na Miradi ya Mikakati tumuombee Mungu aendelee kuilinda miradi ya mikakati ili nchi yetu iende salama, ahsante. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Boniphace Mwita Getere nilishakutaja Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa na utafuatiwa na Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi pia niweze kuchangia mchango wangu katika hotuba ya Wizara yetu ya Nishati, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo amelitoa na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitoe shukrani kwa Wizara hawa kwa Waziri na Naibu Waziri nakumbuka mwezi Desemba na mwingine mwezi Januari mlifanya ziara Biharamulo mkatutembelea sehemu kubwa mkilenga katika kituo chetu cha kupoozea umeme cha Nyakanazi ambacho kinajengwa kwa hiyo niwashukuru sana kwa *visit* ile ambayo mmeifanya na sehemu zote ambazo tulitembelea na ahadi nzuri ambazo zilitolewa *base done contract* ambayo ilikuwepo pale ambayo tunategemea itamalizika tarehe 30 mwezi wa tatu kama ulivyosema wakati tumetembelea Nyakanazi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa *contract* ile haijamalizia na wale wakandarasi bado wapo site. Labda niseme jambo moja tu tumekuwa na tatizo kubwa sala la kukatika umeme sehemu za Biharamula na Ngara na halikadhalika na Chato, lakini Chato nadhani kuna unafuu ila kwangu kwa sehemu ya Biharamulo tatizo kubwa tupo kwenye *low voltage* umeme unaotoka geita kuja Chato *substation* unakuja kwenye 34 Kv lakini kutoka pale nadhani kuja Biharamulo unakuja uko chini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa umeme ule hauwezi kufanya kazi na sasa hivi tuna shinda kubwa watu hata *fridge* kwenye *supermarket* pale *ice-cream* zinayeyuka napigiwa simu Mbunge, maji sasa hivi tunamgao wa maji Biharamulo maji yenyewe hatuna lakini hata yale machache tuliyonayo Biharamulo tupo kwenye mgao tupo kwenye mgao kwasababu umeme uliopo ni mdogo kwa hiyo pampu zetu

pale Kagango haziwezi kupampu yale maji hatimaye tukaweza kupata maji vizuri pale mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kufuatilia yote haya maana nimejaribu kufanya *follow up* ya *issue* ya Nyakanazi, Nyakanazi imeahidiwa kwenye Ilani ya CCM na pia tulishaenda pale tukatembea kwamba tulikuwa inabidi tupate umeme wa Msongo wa Kilo Volt 220 kutoka Geita uje pale. Nimepita pale juzi ujenzi unaendelea vizuri, lakini lipo tatizo ambalo labda sasa kwasababu na Waziri Mkuu yupo hapa ningependa kujua tuna transfoma mbili ambazo inabidi zije kufungwa pale Nyakanazi. Tangu tarehe 20 Desemba transfoma zile zipo Bandarini hapa, tarehe 20 Desemba *as we are talking* sasa inaenda sasa ni miezi sita. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini shida iliyopo pale ni kwamba TANROADS na TANESCO wanashindwa kuelewana jinsi gani watalipana kwenye *surchage amount* ili waweze ku- *release* zile transformata zile pale Nyakanazi. Lakini kipindi yote haya yanafanyika sisi pale kwetu bado ni shida ndugu zangu, maeneo ya Nyakanazi pale hata kuchaji simu wananchi wananipigia simu hawawezi kuchaji simu umeme upo chini lakini kuna watu wa Serikali hii hii ambayo inatekeleza Ilani ya CCM watu wa Serikali hii hii ambao wameapa kumsaidia Rais wanashindwa kukaa chini na kuelewana kwa vitu vidogo hivi wananchi wanatesema. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba tunapo *windup* nipate kauli ya Serikali hizo transfoma zinatoka lini Serikali ni hii hii moja, maana hata mkizizuia pale mwisho wa siku zitatoka tu hata zikikaa mwaka mzima zitatoa tu sasa kinachoshindikana ni nini hizo transfoma zikatoka leo zikafungwa pale, mambo yenu ya kulipana mnatoa mfuko wa kushoto mnaingiza mfuko wa kulia mtayafanya baadaye kipindi hicho wananchi wanyonge walioko huko vijijini wanapata umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba TANESCO tuwasaidie maana sasa TANESCO nia yetu nyie ni nzuri mlishakuja pale mkasema, lakini 2.3 bilion *per one* transformata hiyo fedha

mnaitoa wapi? Ukiongeza 4.6 *billion* umlipe *TANROADS* hiyo fedha si ingeenda kufanya miradi mingine ya umeme pale! Kwa hiyo, ninadhani kuna vitu vingine nadhani mkae wenyewe humo ndani muelewane lakini sisi tunachohitaji tuone zile transfoma zimefungwa pale wananchi wa Biharamulo waondokane na tatizo la kukatika katika umeme hata wenye viwanda vidogo vidogo pale Nyakanazi waweze kufanya kazi maana leo tuna viwanda lakini hakuna anayeweza kufanya kazi kwasababu umeme una *run under low voltage*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hilo jambo naomba niliweke wazi kama hatutapata majibu ndugu yangu Mheshimiwa Kalemani najua tuna-*share* ma-*generator* ya pale Biharamulo *otherwise* sasa itabidi unipe *permission* Biharamulo tuanze kuwasha *Generator* kwa kutumia mafuta ya *Diesel* kipindi wewe unapata ya kutoka Geita nipate ya Biharamulo kwa kutumia mafuta ya diesel mpaka pale mtakapopata zile transformata tuweze ku-balance tukae pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kulisema hilo lipo jambo jingine moja ambalo nilipenda pia niliongelee Biharamulo tunao mgodi wa *STAMIGOLD* last week nadhani kama wiki mbili nimetembelea mgodini pale. Imeletwa line ya umeme kutoka Geita *Special line* mpaka Mgonini *STAMIGOLD* lakini cha ajabu ile line ipo pale umeme bado haujaingizwa ndani na wale watu wa mgodi wa *STAMIGOLD* mgodi wetu wa Serikali ambao hata *CSR* tu wanashindwa kunisaidia vitu vidogo pale mtaani wale watu wanalipwa 1.2 *billion* kila mwezi kwa ajili ya mafuta ya *diesel* ule mgodi ni wa Serikali ungeniambia ni *GGM* wanalipa hata Bilioni ngapi *I don't care* kwa sababu ni fedha yao labda mna *process* nyingine ya kuwarudishia lakini ile ni fedha ya Serikali ule mgodi ni wetu sisi na *TANESCO* nyie mkishawaingizia umeme kule *your assured* kupata *more than seven hundred million per month* nyie ndio mtakuwa the *large users* wa umeme ukiondoa Kagera sugar kwa Mkoa mzima wa Kagera .

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe hilo jambo mliangalie ili tatizo limalizika na hata wakati wa ku-*wind up*



pia nipate majibu maana sisi tuna mgodi lakini mgodi unaoshindwa hata kunisaidi barabara pale Kaniha huo mgodi ni wa nini? Mgodi unaoshindwa kunisaidia hata kujenga zahanati pale ule mgodi ni wa nini. Lakini kwa sababu wana *run under high cost* kama hizi za kununua mafuta maana wakikulipa wewe Milioni 700 *TANESCO* wanabaki na Milioni 500 itaweza hata kutusaidia na sisi tukiomba *CSR* watusaidie kusaidia jamii iliyozunguka mgodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuja jambo jingine Mheshimiwa Waziri ulipotembelea Biharamulo wakati ule kuna kata kama tano ambazo bado hazijapata umeme kata ya Kalenge lakini najua Kalenge watapata umeme kutoka kwenye hii *substation* ya Nyakanazi pindi unaenda Kigoma kati ya vile vijiji thelathini na ngapi ambavyo vimetajwa, lakini kuna Kata ya Kaniha na pia kuna Kata ya Nyantakara kuna Kata ya Nyanza. Lakini hii Kata ya Kaniha na Nyantakara ulipokuja kuna mkandarasi pale ana umeme wake anawauzia wananchi *Power Janne*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ulitoa maelekezo *specific* kwamba umeme ni shilingi 100 per unit huyu mtu tukakaa kwenye Baraza la Madiwani tunakuelekeza Meneja wa *TANESCO* na Mkuu wa Wilaya wakati ule tulikuwa pamoja leo karudi tena anawaambia watu anawachaji shilingi 2,000 *TANESCO* mmemruhusu, sasa nashindwa kuelewa, yaani Waziri unatoa *order* kuna mtu mwingine nyuma yako naye anatoa barua ingine, mwenye madaraka ni nani hapo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba pia hili jambo la *power Janne* tupate majibu humu ndani maana Diwani wa Kalenga anashinda mjini pale anahangaika kila siku, wale watu wamegoma kuwasha umeme na wamesema wanataka shilingi 2000 na wewe ulishaagiza ni shilingi mia moja, nimemuuliza Naibu Waziri, nimekuuliza wewe mwenyewe umeniambia shilingi mia moja. Kwa hiyo nilikuwa nipate majibu ya Serikali wananchi wa Kalenga wasikie, walioko Mavota wasikie na sehemu nyingine kwamba ni shilingi mia moja ile ile iliyoagizwa na Waziri ndiyo hiyo inayofanyika pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho nilitaka niongee kwasababu ya muda kuhusu *issue* ya bomba la mafuta hili la kutoka Uganda. Niishukuru sana Serikali na hasa nimpungeze Rais kwa kusaini *contract* hii na hatimaye sasa neema hii kubwa inakuja kwenye nchi yetu. Lakini nilikuwa nawaza katika *angle* ya tofauti kidogo, sehemu kubwa ya lile bomba itakuwa ni *project* ile ya mabomba yenyewe yanayolazwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nikawa naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali, kama mnaweza mkaongea na *contractor* najua kutengeneza bomba huko watakapozitengeneza akazisafirisha zile bomba kilomita 1000 azifikishe *transportation cost* tu ile anatosha kuja ku-*setup* kiwanda hapa, *I am sure* tukiangalia *cost* ya ku-*transport* bomba za kilomita 1000 yule mtu akabeba mashine Europe akaja hapa mkampa eneo na watu wake nilicho na uhakika nacho kutakuwa na *transfer of technology* lazima yule mtu baada ya kuondoka hapa watu wetu watakuwa wamejifunza kwa sababu tuna vijana ma-*engineer* tuna watu ambao wamesoma wataajiriwa kwenye kile kiwanda, kwake ni rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukishampa *site* akaweka hapa ni rahisi kwasababu anafanya *servicing* kwa sababu bomba atazizalishia hapa na *the good thing* ni kwamba badala ya kuleta meli nzima imejaa mabomba, ukakodi *truck* zaidi ya 600 zaidi ya 800 zikaanza kusafirisha mabomba kuelekea Uganda unampa *site* hapa, kila siku *truck* kumi anatoa zinaenda *site* zinashusha mabomba, *truck* ngapi anatoa kwake *logistically* itakuwa imekaa vizuri. Kama mtaturuhusu tunaolewa hivi vitu tunaweza tukawasaidia hata kama atakuja hapa ili sasa tushawishi yule mtu kwamba hatukuelekezi boma uje uzalishie hapa leta *material*, fanya kila kitu leta watu wako, leta mashine tumekupa *site* hii hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina hakika baada ya *project* ile yule mtu zile mashine hatazing'oa hapa na sisi tunafanya *research* ya mafuta kesho na kutwa kama vijana wetu wamejifunza watumika wao, *we are sure* leo tumejenga *flying over* pale niliwahi kusema, vijana ma-*engineer* wa

Kitanzania waliohusika na *flying over* ya Ubungo leo wanahusika na kwingine baada ya muda hatutahitaji wageni vijana hawa hawa wa Kitanzania watajenga vile vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe hilo wazo ni zuri kibiashara ni wazo zuri kwa manufaa ya nchi kama mtaweza mshawishini huyu mtu anaweza aka-*set up* hata sehemu mbili au tatu za kuja kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nashukuru sana na naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana *Engineer* Ezra John Chiwelesa. Waheshimiwa Wabunge sauti zenu zinakuwa ziko juu sana mtu anapokuwa anachangia si vema sana kila wakati niwe nakumbusha wewe mwenyewe masikio yako yatakwambia tu nipunguze nipunguze, sasa ni Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila na atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Protas.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo katika Wizara hii muhimu katika ustawi wa Taifa letu. Awali kabisa kwanza ningependa kutoa pongezi kwa Wilaya ya Kigamboni kwa shughuli waliyoifanya ya kuweza kumbaini mwizi wa mafuta kwa kweli nilipoisikiliza ile *clip* nilijisia vibaya sana nikaona kwamba kumbe wafanyabiashara wetu wanahujumiwa kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Sara Msafiri Pamoja na uongozi wake wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na kwa miaka hii miwili niseme kwamba bado wamechelewa wanatakiwa wajidhatiti kuhakikisha maeneo yale ya Kigamboni yanakuwa salama kwa ajili ya kuhakikisha mafuta hayaibiwi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuipongeza Wizara hii kwa sababu Waziri wa Wizara hii na viongozi wake wamekuwa ni watu wanaotusikiliza vyema na pia wamekuwa wakitoa ushirikiano kwetu mkubwa tunapokuwa na

changamoto katika maeneo yetu tunawashukuru sana viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitapenda kujielekeza moja kwa moja kwenye changamoto za wananchi bajeti kweli ni nzuri inatia matumaini lakini kama ilivyo ada hatuwezi tukaacha kuongelea changamoto za wananchi wetu ambazo wanakuwa wanatupasia ili ziweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto ambazo tunakabili nazo ni Pamoja na usambazaji wa umeme ambao unaenda kwa kulega lega na tunapokuwa taunafuatilia tunaambiwa kwamba bajeti inayotoka katika Wizara kwenda katika maeneo yetu kwa ajili ya usambazaji wa umeme inakuwa ni ndogo sana kiasi kwamba mwisho wa siku mameneja wetu katika mikoa na wilaya zetu wanapata changamoto ya kuonekana kama hawafanyikazi kumbe bajeti wanayopewa kwa ajili ya kuhakikisha umeme unawafikia wananchi inakuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, nilitamani kuiomba Wizara itengeneze mkakati mzuri ambao utahakikisha umeme unasambazwa kwa ukubwa kwa maana ya kwamba wanapokuwa wanaweka bajeti ndogo ile tija ya usambazaji wa umeme inakuwa haionekaniki na wananchi watakuwa wanaendelea kuona kwamba watu wa *TANESCO* ni watu wanaokula rushwa sana kitu ambacho wakati mwingine unakuta hata wale mameneja hizo rushwa hawali ila tu ni mazingira ya usambazaji umeme yanakuwa yako duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilipenda kuongelea suala la umeme wa *REA* kwa maeneo ya mjini. Siyo miji yote kwamba ina mitaa katika miji mingine mfano mimi kwangu kule Tunduma tuna maeneo mengine ambayo ni vijiji ndani ya mji mfano Chiwezi, Mpande ni maeneo ambayo kwa kweli ni magumu kwa usambazaji wa bajeti hii inayopelekwa kuweza kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano nikitolea eneo la Chiwezi bajeti tu ya kupeleka umeme kule ili iweze kufika ni takriban bilioni mbili wakati huo huo meneja wetu wa wilaya anapewa bajeti ya milioni 260. Kwa hiyo, unakuta mazingira kama hayo maeneo kama ya Chiwezi yanaweza yakawa hayapati umeme kwa wakati na mwisho wa siku nilitamani sana kuiomba Wizara ichukue hii kama *special mission* ya kuweza kuhakikisha maeneo haya yanapata umeme kwa bajeti ambayo ni nje ya ile wanayokuwa wametoa kwenye wilaya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kumekuwepo na changamoto ya umeme kukosa nguvu na kitendo cha umeme kukosa nguvu mara nyingi huwa kinatokea pale ambapo *transformer* inakuwa imezidiwa uwezo wa kufanyakazi na tukiangalia *transformer* nyingi zinazokuwa zimewekwa vijijini yaani ni zile zenye uwezo mdogo unakuta ndani ya muda mfupi zile *transformer* zinakuwa zinazidiwa kiasi kwamba umeme unakuwa hauna nguvu. Nilitamani sasa kama Wizara waje na mpango mbadala badala ya kupeleka hizo *transformer* zenye uwezo mdogo maeneo yote wajaribu maeneo mengine kwa *assessment* zao wapeleke zile *transformer* ambazo zitakuwa ni kubwa zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umeme unapokuwa unakosa nguvu ina maana kwamba kazi nyingi zinashindwa kufanyika vizuri na hata kama watu wamejajiri kupitia umeme unakuta wanashindwa kufanya kazi zao ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuongelea suala la bei za umeme tunapoongelea Wizara hii ya Nishati kwenye kipengele cha umeme hii ndiyo sehemu watanzania wengi wanaweza kujajiri. Kaatika kujajiri huku gharama za umeme zinapokuwa ziko juu ina maana uendeshaji wa hizo *projects* zao unakuwa uko juu na ndiyo tunarudi palepale kwamba ushindani wa soko wazalishaji wa bidhaa watashindwa kuendana na gharama za soko kwa maana ya kwamba ushindani utakuwa ni mkubwa Zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najaribu ku-*imagine* mfano watu maeneo kama ya *institution* kama shule, labda hospitali,

hoteli hawa watu wanapata wakati mgumu wa ku-run haya maeneo kulingana na kwamba gharama zinakuwa zinapanda na kile kipengele cha kusema sijui kuna *tariff one, tariff two* kwa matumizi ambayo ni ya kawaida tulitamani Wizara iweze kuliangazia na kuliondoa kwa sababu haiwezekaniki mtu anayetumia umeme eti kisa anatomia umeme mwingi ndiyo apewe gharama kubwa wakati yule anayetumia umeme kidogo anapewa gharama kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika *principle* ya soko maeneo yote anayetumia kikubwa ndiye anayeongezewa. Kwa hiyo, nilitamani Wizara katika hili waweze kujitafakari na kuangalia namna gani wanatusaidia watanzania tuwe wateja wao wazuri ili tuweze kufanya mambo ambayo yataleta maendeleo kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kupitia hotuba ya Waziri nimefurahi sana kuona mradi wa kusafirisha umeme kutoka Iringa, Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga kwangu nimeona ni faraja kwa sababu hali ya umeme kwenye eneo letu la Mkoa wa Songwe limekuwa ni jambo ambalo wananchi wanalalamika sana. Umeme haupo, umeme unakatika katika mara kwa mara na inapofika Jumamosi wananchi wameshajiandaa...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge na hasa kuna wengine wananigeuzia na viti kabisa nitafikia mahali nitaanza kutaja makundi ya wazozaji humu ndani itakuwa ni aibu maana yake nawaona nina kioo hapa ambacho kinanionyesha na kutaka kuangalia.

Sasa nikiputaja ni aibu kwa wapiga kura wako lakini pia kanuni hairuhusu kugeuza kiti ukampa mgongo Spika. Kwa hiyo, angalieni huku huku tumuangalie anayechangia. Mheshimiwa Neema Mwandabila endelea. (Makofi)

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nadhani utanilindia muda wangu huo mchache.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kuona huu mradi wa usafirishaji wa umeme unaotoka Iringa kuelekea Sumbawanga ambapo kwa upande wa Tunduma kutakuwa na kituo cha kupozea umeme. Kwangu naiona faraja kwa sababu wananchi ni kitu wanachokisubiria kwa hamu umeme umekuwa ni wa shida sana, na kumekuwa na changamoto ya umeme kukatika kila inapofika Jumamosi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama umeme utakuwa unapozewa Tunduma naamini kabisa zile changamoto zingine zinazokuwa zinatokea zinapelekea umeme kukatika katika zitaweza kupungua, na gharama ya mradi huu ni trilioni 1.4 na nikiangalia kuanzia pesa iliyotengwa hii bilioni moja kwa namna fulani inatupunguza matumaini kwamba utaenda kwa kasi hii japo naamini kabisa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii Pamoja na Katibu Mkuu wako vizuri kuweza kutusaidia, kwa hiyo, nilitamani bajeti iwe angalau inasoma vizuri ili kuweza kututia matumaini kwamba mradi huu utaenda kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sitajitendea haki kama nitashindwa kuongelea suala la joto ardhi sisi kwetu kule Songwe tumebahatika kuwa na eneo ambalo linakiashiria cha joto ardhi eneo la Nanyala Mbozi. Mheshimiwa Waziri aliweza kutembelea eneo lile akaangalia lakini kwenye hii hotuba sijaona akizungumza neno katika eneo hili nilitamani kwa niaba ya wananchi wa Songwe tungependa kusikia kwamba baada ya yeye kutembea pale amekuja na mkakati gani wa kutusaidia kama wana Songwe ile fursa ya kuweza kupata umeme iweze kuwa *revealed* kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia sisi Songwe pia tuna utajiri wa makaa ya mawe sijaona katika hotuba wakiongelea kitu hiki hata kidogo na tunajua makaa ya mawe ni nishati sasa nashindwa kuelewa kwamba haya makaa ya mawe yanachukuliwa kwa namna gani. Kwa hiyo nilitamani kuona kwamba Wizara kama Wizara imejipangaje kutumia haya makaa ya mawe yaliyopo kwetu kule Ileje katika namna

ambayo itakuwa na tija katika uzalishaji wa umeme na nishati zingine.

**SPIKA:** Ahsante Neema Gerald Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante niseme tu naunga mkono hoja na niwatakie viongozi utekelezaji mwema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa liko tangazo moja muhimu kwenu kwamba kwenye *tablets* zenu kwenye sanduku la taarifa za kiofisi tumeweka nyaraka inayoitwa *name and contact details for contractors and taking REA III round II project* ambayo imeandaliwa na kuwasilishwa Bungeni na Waziri wa Nishati kwa ajili ya kuwawezesheni Waheshimiwa Wabunge kuwajua wazabuni wanaotengeneza mradi wa *REA III* katika mikoa yenu mbalimbali Pamoja na mawasiliano yao mtayapata pale. *(Makofi)*

Lakini pia nina wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Maryprisca Mahundi wageni tisa baadhi yao wakitoka Chuo cha Jordan *University* Morogoro na TIA Mbeya pale mlipo naomba msimame karibuni sana vijana wetu karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Venant Protas atafuatiwa na Mheshimiwa Bonaventure Kiswaga.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi niwe miongoni mwa watu ambao watachangia Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza anianze kwa kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri yeye na Naibu wake, Katibu Mkuu kwa kweli wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha wananchi wetu wanapata mwanga ingawa kuna changamoto. Lakini pia niwapongeze viongozi wa *REA, DG* wa *REA* naye anafanya kazi nzuri kuhakikisha anasambaza umeme na sisi



tunajivunia kuwa na *DG* huyu kwa sababu umeme kweli umefika katika vijiji mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo bado tuna changamoto nilipochaguliwa na wananchi wa Jimbo la Igalula nilikuja hapa kujua hatma ya vijiji vyangu ambavyo bado havijafikiwa na nishati ya umeme na uzuri Mheshimiwa Waziri alinijibu Bungeni na bado tukafanya naye safari ya kwenda kwa wananchi wangu kuwaambia lini umeme utawafikia wananchi wangu. Hilo nilikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, tulifika katika Kijiji cha Izumba, Kata ya Miyenze na ulikuta watu wengi, walikupokea kwa furaha kwa sababu walijua wewe ulikuja na umeme. Lakini matarajio yao hayakuwa kama tulivyokuwa tumetarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka na naomba nikunukuu na siku ile tulikuwa wote wewe Waziri na Naibu wako na Mkurugenzi wa *REA* naye alikuwepo na Bodi yako yote ya *REA* ilikuwepo. Uliwaambia wananchi ilikuwa tarehe 16 Machi ukawahakikishia kufikia mwisho wa mwezi wa nne umeme Izumba utakuwa umewaka na ukawahakikishia ukasema leo umekuja na wakandarasi utawaacha pale pale ili waanze kuwasambazia wananchi umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo ni mwezi Juni tarehe 2, 2021; wananchi wa Izumba hawajaona nguzo, yule mkandarasi tulivyoondoka na yeye akaondoka, sasa hivi amebaki anakwenda anaondoka. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tunamaliza Bunge tarehe 30 ya mwezi Juni, 2021 ninakwenda ziara kule sasa kama nikizomewa ujue umenisababishia wewe ule mzomeo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri kwa hizi siku chache naomba uniwashie umeme, nikiunganishi kati ya wananchi na Serikali, ninapokwenda kule tena kuwaambia nitaenda kuiambia Serikali wakati Serikali ndiyo niliipeleka kweli Mheshimiwa Waziri utanipa wakati mgumu mwisho wake na mimi nitakuwa upande wa Serikali nikabaki nashangaa kauli ya Serikali haijatimizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kata za Miyenze, Tura, Miswaki na Lutende wote wanahitaji na wanamatumaini makubwa ya kupatiwa umeme, naomba uwasaidie kwa sababu ulitoa kauli hiyo kwa bashishi kubwa na wao wakakupigia makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kutupelekea umeme, mkandarasi amekwenda kwenye baadhi ya vijiji ameenda kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji wakisema jiandaeni umeme unakuja. Lakini mkandarasi anasema mimi nitaleta umeme, nitasambaza kilometa moja tu kwenye kijiji.

Mheshimiwa Spika, mimi niombe Serikali pamoja na nia njema ya kupeleka umeme, msitupelekee mgogoro mwingine ambao utazalika ndani ya mgogoro mwingine kwa sababu unapopeleka kilometa moja na mkaweka idadi ya watu labda 20 wataunganishiwa wakati watu ambao wapo tayari kuunganishiwa umeme zaidi ya 20.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kama yule mkandarasi mnampa mkataba wa kilometa moja muwe mna fedha za ziada anapomaliza kilometa moja *TANESCO* anaanza kazi ya kuunganishia wateja wengine ambao waliobaki. Leo unaponiambia mji kama wa Kata ya Tura unapeleka nyumba 20 nani umpelekee nani usimpelekee, Mji katika Kata ya Miyenze unapeleka nyumba 20 nani umpelekee na nani usimpelekee; wale wote ni wapiga kura. Niiombe Serikali itusaidie hii *scope* iongezwe kidogo kutoka kwenye kilometa moja basi angalau kwenye kijiji ifike hata kilometa tatu au nne itakuwa imetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna changamoto moja ambayo Serikali maana kwamba Wizara na *TANESCO* wanacheza ngoma mbili tofauti. Leo Serikali inatumbia mwananchi akilipa shilingi 27,000 anaunganishiwa nishati ya umeme. Lakini ukienda kwenye uhalisia sivyo mwananchi analipa shilingi 27,000 unakuta nishati ya umeme iko zaidi ya

kilometa moja huyo akilipa shilingi 27,000 kweli kiuhalisia atapata umeme?

Mheshimiwa Spika, ukienda *TANESCO* anakwambia sina bajeti, siwezi kupeleka umeme kwa sababu inahitaji nguzo zaidi ya kumi, sasa *TANESCO* hujampa fedha na amepokea fedha ya mteja, unapotoa kauli kama Waziri kusema shilingi 27,000 wananchi wanataka kweli kulipa shilingi 27,000 wapate umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali hebu kuweni na dawati maalum la kutoa elimu. Ie shilingi 27,000 ukomo wake uko wapi, je, kama kuna ziada muda gani wa kusubiri ili ninyi mjipange muweze kufanya hiyo kazi ya kumuunganisha umeme, kuliko sasa hivi imekuwa vurugu *match*. Leo hii Kata ya Goweko kuna umeme jazilizi ambao umepeleka kule mradi ambao nilikuomba Mheshimiwa Waziri. Lakini wamepeleka kwa idadi ya nguzo 35 zimekamiliwa, lakini wananchi bado na wameshalipa shilingi 27,000 wanasema sasa sisi tunafanyaje, wameenda *TANESCO* wanaambiwa sisi hatuna bajeti. Nikuombe Goweko pale tuongezee nguzo zingine kwa sababu ulisema hii kauli na wenyewe wanaisimamia hata kama ipo nje ya ule mkataba mimi nikuombe sana nisaidie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nirudi sasa kwenye sekta ya mafuta; kwanza niipongeze Serikali kwa jitihada zake za kuchukua jukumu la kuweka vinasaba, niipongeze sana, mlipoipeleka *TBS* kule mmefanya uamuzi mzuri na sisi kama Wabunge tulitoa hilo kwa sababu kuiona kampuni inanufaika kushinda Serikali na ndiyo maana tukasema hivi vinasaba tuviweke wenyewe. Nikiri tu ni mdau mzuri wa mafuta katika sekta hii naomba nishauri jambo moja. *EWURA* wanafanyakazi nzuri sana, lakini wao nao wana changamoto, leo *EWURA* amekuwa akienda tu sehemu kama kuna makosa, haulizi hata kosa limetokana na nini yeye kazi yake ni kufungia tu kituo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa sijui ndiyo wamesoma *professional* ya kufunga tu, lakini wao hawajikagui kama

wana upungufu, wenyewe wanaona wafanyabiashara ndiyo wana mapungufu. Mimi nitoe ushahidi kidogo juu ya *EWURA* wanavyofanya leo tunasema vinasaba viwekwe kwenye mafuta, lakini mafuta yaliyowekewa vinasaba na ambavyo havijawekewa vinasaba kwa mteja wa kawaida hajui kitu chochote, hata mwenyewe sijui mafuta yapi yamewekewa vinasaba na yapi hayajawekewa vinasaba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo akija yeye na *machine* yake ndiyo anaiamini kama Msahafu au Biblia akiweka pale ikikataa anasema hii ina vinasaba kidogo haijafikia kile kiwango. Sasa hicho kidogo nani aliweka? Na ikiweka inaoneshaje kama imewekwa kidogo? Nikuombe Mheshimiwa Waziri na hili naomba ulichukulie *u-serious* hawa jamaa wanasumbua sana wafanyabiashara yaani wamekuwa wao ndiyo miungu watu wakifika pale funga kiri hapa kuwa nimekuta kuna kosa na kama nataka nifanye biashara na kiri haraka haraka nikulipe faini yako tuachane kisalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini unakuta muda fulani wameonea ukichukua yale yale mafuta ukaenda kupima *machine* nyingine inaleta kipimo tofauti ya kwao ya kwanza, wamepima na wamekufungia na wamekudhalilisha imesema inamakosa, umeenda kwingine ipo sawa ukirudi huku wanasema aisee kanuni ya fidia hamna wewe endelea kufanya biashara. Badilisheni hizi kanuni la sivyo wajianganalie na wao na siye tutakuja siku moja wakaja wakakutana na magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hapa watu wamesema vituo vya vijijini vipunguziwe masharti ni kweli, leo mnaruhusu watu kulala na *petrol* mnashindwa kumruhusu mtu haraka haraka aweke mafuta pale nje *pump* moja mnaweka mavibali mengi, yaani kibali kukamilisha kupata *shell* ya mafuta yaani uwe na siyo chini ya shilingi milioni 30. Sasa kwa mwananchi wa kijijini ukimwambia milioni 30 anaipata wapi? Kuna teknolojia zimekuja nyingi kuna kontena linatembea yaani ukiweka kontena...

**SPIKA:** Ahante sana.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, huku ndiyo kulikuwa panoge, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mbunge wa Wanyamwezi huyo, Mheshimiwa Venant Protas katika Wabunge vijana, Waheshimiwa Boniventura Kiswaga, sasa zamu yako, utafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ambayo nilipaswa kuchangia asubuhi lakini nikaamini kwamba umeniweka akiba.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Naibu wake, Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa *REA* Vijijini bwana Maganga kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwenye nchi hii katika kuhakikisha kwamba umeme unapatikana wa uhakika pamoja na matatizo madogo madogo, lakini angalau wananchi wanaendelea kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miradi hii ya *REA* imesaidia sana kufungua maendeleo kwenye vijiji vyetu kila mahali ambapo umeme umewekwa wa *REA* kuna viwanda vidogo vidogo vimefunguliwa na wananchi kwa hiyo, vimeongeza ajira kubwa sana katika maeneo yetu, lakini pia na kuchangamsha *center* na ujenzi mpya kabisa wa nyumba za kisasa vijijini sasa unaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewahi kutembelea Kamati yetu *PAC* kule Iringa pamoja na Manyara na Singida tumekuta kule vijijini wananchi wako *happy* kabisa kwa sababu ya kuona umeme vijijini umekwenda na ninawapongeza na Waziri kwa kweli Mungu amempa kipaji cha kukariri vijiji vyote vilivyoko hapa Tanzania. Kwa hiyo, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli umeme walipofanya *evaluation* uliongeza tija kwa sababu *scope* zilizokuwa zimeandaliwa mwanzo zilikuwa chache sana na hii imeifanya CCM kupata kura nyingi baada ya umeme huu wa *REA* kufika vijijini. Kwa hiyo, kwa sina kipingamizi cha kupitisha bajeti ili wakatekeleze hasa kwenye vijiji vyangu 42 ambavyo vimebaki kule jimbo la Magu, Kalemani anavijua na Maganga anavijuwa kwa sababu wamekwenda kule karibu mara nne kwenye maeneo yetu, vijiji vya Isolo, Shishani, Ingombe, vyote wanavifahamu, vijiji vya Chandulu, Mwabulenga, Kisamba vyote wanavifahamu, kwa hiyo, nahitaji hivi vijiji 40 viweze kufikiwa umeme wa uhakika ili wananchi waweze kuwekeza viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la *KVA* wamiliki wa viwanda wanalamika wanamatatizo, kwamba unapofanya kazi kwenye viwanda, ni mdau wa kiwanda naomba ni *declare interest* unapochambua pamba miezi miliwi, ukikata umeme unachajiwa *KVA* miezi mitatu bure unalipa hewa. Kwa hiyo, kama mazao yapo umekusanya kidogo ukachambua kwa muda mfupi unaingia hasara tena za kuilipa *TANESCO* bure, miezi mitatu hii inakatisha tamaa wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano kama mwezi wa kwanza ulilipa *bill* ya milioni 60 na mwezi wa pili ukalipa *bill* ya milioni 60 maana yake miezi mitatu utalipa milioni 60 mara tatu milioni 180, ndiyo maana wawekezaji wanashindwa hata kule kwako Kongwa, mwekezaji mkubwa wa kiwanda cha *O//Mea/Kahama*, alikula kwa miezi michache tu mbegu zikaisha. Kwa hiyo, akashindwa kwa sababu faida yote aliyopata akalipa *KVA*, pamoja na hasara zingine kwa hili linaleta shida na sheria hii ilitungwa wakati tunatumia umeme wa mafuta *IPTL*. Kwa hiyo, sasa tunatumia umeme wa kwetu tuondoe hii sheria ili tuweze kuwasaidia wafanyabiashara wa viwanda waweze kuchakata hatuwezi kuvutia wawekezaji kama tunafanya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na hili waziri haliitaji wadau kwa sababu tunataka kuongeza wazalishaji na wasindikaji wa mazao yetu ili alizeti Kongwa Singida, Dodoma Mwanza ilimwe watu wakitegemea viwanda vyao vitafanya kazi kwa murefu bila kulipa *KVA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilizungumze kidogo hili la vinasaba na niweke vizuri kumbukumbu kwamba SIPA ndiye aliyekuwa mwenye Kampuni ya kuuza vinasaba na kuweka vinasaba kwenye nchi mbalimbali, lakini Msumbiji walimfukuza, Uganda walimfukuza, Kenya walimfukuza, Brazil walimfukuza, akaja hapa kwa namna fulani fulani akaanzisha kampuni ya *GFI*, *GFI* ndiyo inayonunua vinasaba kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, uwamuzi wa Serikali hii sikivu wa kuipa TBS wa kushughulika na hili jambo ni uhamuzi sahihi kabisa. Kama kuna watu labda wametumwa kuja kumpigania mnyonyaji washindwe na walege. Kwa sababu, tunajua kwamba *TBS* ndiyo tumeipa kazi sasa na yenyewe *TBS* inanunua hivi vinasaba kwa SIPA. Kwa hiyo, tunaamini kwamba *TBS* itakavyo endelea itatengeneza teknolojia ya kwakwe kuhakikisha kwamba vinasaba hivi hivi vinapatikana hapa hapa au duniani sehemu nyingine. Lakini fedha zile ambazo *TBS* italipwa hizi shilingi 14 zitabaki kwa Serikali yetu hata kama kuna shida ya reli, kuna shida ya umeme hizi fedha zitasaidia kuliko kuipa kampuni nyonyaji hatuwezi kurudi huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge ni mdau wa mafuta pia, siwezi kutetea kampuni nyonyaji, lazima tuitete nchi na nchi ifanye kazi *TBS* inauwezo mkubwa wa kuweza kusimamia hili jambo bila matatizo yoyote. Kwa hiyo, niseme tu kwamba nchi imeamua sahihi na tuhakikishe kwamba tunapokuwa wazalendo, lazima tuangalie vitu vyenye tija siyo vitu ambavyo vinaipunguzia Serikali fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi fedha halipi mfanyabiashara, hizi fedha *EWURA* wanapotengeneza mkokoto wa mafuta,

kwamba Mwanza *petrol* itauzwa 2,400/= kama ilivyo leo maana yake kwamba anayelipa ni mtumiaji wa mwisho. Kwa hiyo, tunaamini kwamba baada ya *TBS* kukaa vizuri wanaweza kuwa wanataja hata shilingi saba kama ambavyo mwezangu Boniface hapa amesema maana yake shilingi saba inaweza kupelekwa kwenye *TARURA*, inaweza kupelekwa kwenye maji tukaongeza mifuko hii ya kutekeleza miradi yetu tukaweza kuwasaidia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niunge mkono kwa sababu Wizara hii Waziri mwenyewe na Naibu wake anaiweza, unajua hapa duniani kuna watu ambao wanauwezo wa kubeba mizigo mizito na hatuna sababu ya kuwapunguzi hiyo mizigo kwa sababu Nishati, Waziri wanatosha, Wakurugenzi wake, wa *REA TANESCO TPDC* nao wanatosha wafanye kazi karibu ili kumsaidia Waziri tusipunguze hapo na hayo maneno, tunaweza tukampa mtu akashindwa sasa sisi tuombe sana kwamba tusigawanye wizara huyu anauwezo wa kuibeba Wizara, ameibeba muda wote. Kwa hiyo, niombe sana mpeni kazi aweze kufanya ahsante sana. (*Makofi/Vigelele*)

**SPIKA:** Huyu anaitwa Mheshimiwa Boniventure Kiswaga, kutoka kule Magu, kwa kigogo Magu maana yake sijui, ukisikia Magu maana yake sifahamu, ahsante sana. Lakini neno moja kasema kweli kwamba mwekezaji mkubwa kule Wilaya ya Kongwa ni Msukuma kutoka Kahama ameweka kiwanda kikubwa cha kukamua alizeti. Sasa hii tutaenda tukaandamane yaani msukuma ndiyo mwekezaji namba moja kwetu (*Kicheko/ Makofi/Vigelele*)

Hii inaonyesha kwamba jamani wekezaji wa ndani nao unawezekana maana tukizungumza neno mwekezaji yaani watu wanafikiria wenzetu weupe, ukizungumza habari ya mwekezaji watu wanafikiria wenzetu wa kutoka bara lile lingine, lakini kumbe hata sisi kwa sisi tunaweza kabisa suala nzima la uwekezaji mradi tuweke mazingira mazuri tu. (*Makofi*)



Mheshimiwa Jumanne Selemani Zedi, nilishakutaja, atafuata na Mheshimiwa Dorothy Kilave Kilave na atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii muhimu sana ya wizara muhimu sana ya Nishati. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuiongoza Wizara ya Nishati na mwezi wa tatu uliopita, Mheshimiwa Waziri alikuja jimboni kwangu kuzindua mpango wa *REA* Awamu ya tatu na alifanya kazi kubwa sana hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na niseme tu kwa kipindi ambacho nimekaa Bungeni, Mheshimiwa Waziri wa Nishati ndugu yangu Kalemani ni Waziri ambaye ni msikivu na niwaziri ambaye anafikika ni *approachable* ni waziri ambaye unamfikia kirahisi na anasikiliza Wabunge kwa kina, hongera sana Mheshimiwa Kalemani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia bomba la mafuta na nina *interest* la bomba la mafuta kwa sababu pale kwenye jimbo langu, Jimbo la Bukene, Kijiji cha Sojo ndipo ambapo itajengwa karakana kubwa ambayo mabomba yote ya kilometa 1,400, kutoka Hoima mpaka Tanga yote kabla ya kufukiwa chini pale ndipo yataandaliwa kwa hiyo, karakana ambayo Mheshimiwa Eng. Ezra itajengwa kwenye Kijiji cha Sojo ambacho kipo ndani ya jimbo la Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pale imechukuwa hekta 400 na sasa hivi wananchi wanasubiri tu fidia ili kazi ya ujenzi wa hiyo inaitwa *courtyard* ianze pale. Sasa *angle* yangu itakuwa ni namna gani Watanzania watanufaika na huu mradi wa bomba la mafuta. Pamoja na faida nyingine ambazo tunazijua za bomba la mafuta ambazo sina haya ya kuzungumzia, lakini kuna faida kubwa sana ambayo Watanzania wanaweza kuipata kama wizara itajipanga vizuri na kuweza kuainisha shughuli zote zitakazofanyika kwenye

ujenzi wa bomba la mafuta na kuwaandaa watanzani ili Watanzania washiriki kikamilifu kwenye hizo shughuli na kuweza kupata manufaa yatakayo patikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi huu unakuja na fedha nyingi sana pale tu kwenye Jimbo la Bukene kwenye *courtyard*, bajeti yake Serikali iko kampuni inayojenga pale itaingiza bilioni 600 ambazo zitakuja kwa ajili ya mfumo wa *activities* mbalimbali. Sasa *as we speak now* sasa hivi Serikali haijaweka wazi ni kazi gani zitakazofanyika pale kwenye bomba hilo la mafuta na kazi hizo zinahitaji ujuzi gani? Zinahitaji *technical capacity* ipi? Kwa sababu, Watanzania hatuwezi kunufaika kama hatujajiandaa mapema kwa sababu hatuwezi kusubiri wakati wa *implementation* ukifika tu alafu na sisi ndiyo tujitokeze *obvious* tutashindwa *ku- compete* na makampuni mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwenye hilo ni kwamba wizara iandae *desk* maalum ambalo litaainisha *activities* zote zitakazofanyika zinahitaji *technical capacity* gani? Zinahitaji *administration capacity* gani? Ili kampuni za kitanzania zianze kujipanga, yanahitajika maandalizi Watanzania wanahitajika kuunda hizi kampuni nyingine inabidi ziundwe ziajiri *technical*/fulani, ziwe na uwezo fulani ili kuweza *ku- compete* kupata hizo kazi, haya mabilioni ya shilingi yatakayoletwa na maradi huo kama hatujajipanga tutayaangalia tu na yatachukuliwa na makampuni nyingine za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea pale pale kwenye bomba la mafuta ni kwamba kama tulivyokubaliana mwanzoni mwaka jana Mheshimiwa Kalemuni na Waziri wa Ardhi walikuja pale kwenye Kijiji cha Sodo kukagua eneo lile ambalo *courtyard* itajengwa ninaomba hapa msisitizo kabla, shughuli hazijaanza basi wananchi wale wote walipwe fidia, zile heka 400 ambazo Serikali imechukua zimeshafanywa uthamini kamishna wa ardhi ameshaizinisha, wananchi wanasubiri fidia na kabla shughuli yoyote haijaanza, ushauri wangu ni kwamba wananchi wale walipwe fidia ili kuondoa migongano inayoweza kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pale ambako *courtyard* inajengwa *as we speak now* hakuna umeme, hakuna maji, lakini tulifanya mazungumzo ya mwanzoni mwaka jana, kwamba kampuni ya *EACOP* ndiyo italetwa umeme pale na ndiyo itale maji pale, kwa hiyo *it right time now* kwa wizara kuisimamia na kuifuatilia kampuni ya *EACOP* ili umeme ulietwe pale na maji yaletwe pale. Na angalizi hapa ni kwamba umeme utakapoletwa siyo uletwe kwenye *point* two ambako *coating yard* itajengwa, lakini vijiji vyote ambavyo vinazunguka pale kwenye Kambi ya Sojo viweze kunifaika na umeme huu na maji ambayo yatafika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninzungumzie kidogo mradi wa *REA* awamu ya tatu, mimi tatizo ninaliona kwa mradi wa *REA* scope hiyo inayoitwa wigo. Sasa hivi kwenye vijiji vyetu utakuta kijiji fulani kinatajwa kwamba kimepata umeme, lakini ukienda kiundani kuangalia unakuta kijiji kinavitongoji sita, kitongoji kilichopata umeme ni kimoja vitano havina umeme, lakini kijiji chote kinatajwa kwamba kimepata umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kuna haya ya kuangalia *scope* ule wigo wa umeme kufika kijijini la sivyo tutakuwa tunahesabu vijiji lakini kumbe ni kakitongoji kamoja tu kwenye kijiji ndiko kana umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wilaya yetu imepata mkandarasi ambaye ni Sillo *Power* ni matumaini yangu kwamba yale makosa yaliyokuwa yamefanywa na mkandarasi wa mwanzo hayatarudiwa tena, kuna vijiji vilikuwa vimerukwa lakini kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa na ninaimani kwamba Mheshimiwa Kalemani anauwezo mkubwa wa kusimamia eneo hilo na ataweza kusukuma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi Mbunge wa Bukene nilikutaja Mheshimiwa Dorothy George Kilave na atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Temeke pia niweze kuishukuru sana Serikali yangu kwa jinsi ambavyo inafanya kazi ni miaka mingi ambayo tukiwa tukilia kuhusiana na umeme lakini sasa nikiri kwamba wizara inafanya kazi vizuri sana. Lakini sio nyuma sana kuwapongeza katika hotuba yako Waziri hotuba nzuri ambayo imeleta matumaini kwetu sisi watanania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizidi kuwapongeza jinsi gani mnafanya miradi ambayo miradi ya kimkakati hasa mradi ule wa bwawa la Julius Nyerere ambalo tuna matumaini nalo litakapoisha hakika hatutakuwa tena na kelele za umeme katika nchi yetu na hata tutakwenda kuuza Jirani. Niwapongeze bado kwa jinsi ambavyo wameweza kujenga sasa ujenzi wa njia ya kuendesha treni ya umeme ambayo tunaamini watanania wote tuna matumaini ya kwenda kuiona na hata sisi wenyewe kuipanda kabla hata ya mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naendelea kuipongeza Wizara ya Nishati kwa jinsi ambavyo mmeweza kuendelea kuipatia kipato *TANESCO* kwa jinsi ambavyo sasa naona hata mambo mengine yatakuwa yanakwenda kwa sababu mmekuwa mmechangamka na kipato sasa ni kikubwa, na tunaweza kuona kwamba miundombinu inaimarika. Lakini siyo tu niweze kuwapongeza pia kwa kuweza kuangalia madeni sugu na niwatie moyo tuendeleo kutafuta madeni yale ili tuweze kuona kwamba sasa nishati inakwenda mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba napenda sana kuwapongeza kwa sababu kazi inaendelea na inaonekana niseme tu kwanza sasa kazi iendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi sana ya kusema lakini nimesimama kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Temeke TMK wenyewe tunajiita, ni jimbo lenye viwanda vingi sana naamini mnafahamu hilo. Lakini si viwanda peke yake lakini wananchi tulioko Temeke ni wananchi wengi sana

ambao tunatumia nishati hii ya umeme. Lakini imekuwa ni tatizo sasa kwetu pamoja na hongera zote pongezi zote nilizowapa niseme tu kwamba wananchi wangu wa Temeke jimbo letu la Temeke hakika hata hapa niliposimama sasa hivi hakuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kila siku simu ni hizo imekuwa ni salamu za sisi kusalimiana umeme hakuna hiyo ndio inanishangaza lakini baada ya kufuatilia kwa muda mrefu na ninawashukuru sana mmekuwa mkinisaidia sana hasa naiibu wako mara nyingi amekuwa akinisaidia mara kwa mara niseme nakushukuru sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kufuatilia hayo yote nimeona ya kwamba sisi tuna vituo viwili ambacho kimoja kinaitwa kingine TOL na kingine kule Tandika hivyo vyote vinatoa *megawatt* jumla 30 tu. Ambayo Tall wanatoa *megawatt* 15 na kule Tandika inatoa megawatts 12 ambazo ni 30. Lakini ukiangalia Jimbo la Temeke sisi wenyewe tunahitaji *megawatt* 117 ili umeme uwake kwa siku zote. Sasa lakini umeme huu hauwaki sijui ndio sababu ambayo hatupati umeme sina uhakika majibu mtaweza kutupa sisi leo wana Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunapata umeme kidogo sana hiyo iliyobaki *megawatts* 87 tunaambiwa tunapata kutoka Ilala Mkoa wa Ilala wa umeme sina uhakika sana lakini sisi wananchi karibu 125 tunaolipa deni tunaotumia *LUKU* na hatuna madeni kwa sababu sisi sote mmetufungia *LUKU*. Sasa niwaombe mtuangelie kwa jicho la kipekee kabisa Temeke, ni jimbo ambao lina watu wengi tunalipa kwa sababu wote mmetufungia *LUKU* hakuna deni sugu kama nilivyosema kwamba jamani endeleeeni kutafuta madeni sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sisi Temeke tunakiri kwamba hatuna madeni sugu hata kule viwandani mkumbuke kwamba ni jimbo ambalo lina viwanda vingi na sisi wenyewe kama jimbo kama halmashauri tunategemea sana kupata fedha kutoka katika yale makampuni au viwanda. Sasa

wakikosa umeme siku moja siku mbili kila siku hata sisi makusanyo yetu yanapungua. Kwa hiyo, niombe sana mtuangelie kwa jicho la kipekee kabisa ili tuone kwamba tunaendelea kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia miundombinu ni chakavu sana mimi ninaamini Temeke ni ya siku nyingi sana na miundo mbinu yetu kule ni chakavu kwa sababu kila siku kama nilivyosema umeme unakatika. Yaani imekuwa ni salamu zetu ikifika tu asubuhi saa nne utapigiwa simu hata hapa naweza nikawaonyesha kwamba mama umeme huku hukuna. Ukiangalia jimbo zima tunakata kumi na 13 Kata ya Keko umeme hakuna sasa hivi Mibulani hakuna umeme Kurasini, hakuna umeme Azimio, Mtoni Makangalawe Sandari Buza Yombo Vituka, Kilakala Temeke 14, Chang'ombe na Tandika kote hakuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana ndugu zangu Temeke ni jimbo ambolo linaangaliwa watu wengi wanakuambia tunaenda TMK ndio kwenye uwanja wa michezo na hata juzi nimeomba kwamba hata ile Arena ije ijengwe Temeke sasa tukikosa umeme namna hii tutafanya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana wizara mliangalie hili sio tu lakini vilevile miundombinu yetu ambayo iliwekwa zamani waya zile kupita juu sasa hivi malori mengi yanaingia na kutoka kwenye viwanda vile. Aidha yanachukuwa mizigo au yanapeleka vifaa vingine kwa ajili ya matengenezo sasa yale malori yanakuwa yanagonga zile nguzo au marefu sana yanakata zile waya hilo nalo ni jambo lingine ambalo linaonekana kabisa kwamba linatufanya tuwe tunakosa umeme mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ushauri wangu tuunde mkakati wa makusudi wakuona kwamba sasa ile miundombinu iliyochakaa ifanyiwe kazi ninatamani sana kama fedha ipo na ninaamini fedha ipo kwamba miundombinu hii sasa ifanyiwe kazi na tuweze kuipitisha chini

badala ya zile waya zinazopita juu kwa sababu nguzo ni za zamani sana ikiguswa kidogo tu imeanguka umeme hakuna.

Mheshimiwa Spika, na mpaka waje watengeneze inachukuwa muda kwa hiyo niombe sana mkakati huu tuujenge pamoja tuko tayari wana Temeke kusubiri kutoka kwenu na nyinyi muweze kutusaidia ili tuendeleo kupata umeme. Kwa hiyo, niombe sana kwa ushauri mwingine wakati tunajipanga kupata miundombinu hii salama niombe sana kitengo cha *emergence* wasingoje wakaambiwa kuna tatizo la umeme mahali fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini kwa sababu ni waajiriwa wa *TANESCO* wana uwezo kabisa wa kufika ofisini bila kuambiwa kwamba kuna tatizo au kuna katizo la umeme wao wenyewe wapite kuhakiki, kutambua na kuinisha sehemu gani ina kasoro kwa kipindi kile kwa sababu wanazijua kila wakati kasoro zinatokea wapi. Kwa hiyo, niombe kabisa kitengo cha *emergence* sasa tufanye kazi kwa pamoja ili Temeke yetu sasa iwake na sio tena kusema kwamba umeme hakuna maana hizo ndio salamu zetu niwaombe sana ndugu zangu badala ya kusubiri simu za itilafu *emergence* sana ifanye kazi ya kila wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa kufanya hivyo ninaamini hiyo salamu yetu ya umeme hakuna Temeke itaisha. Kwa hiyo, niombe sana ndugu zangu na bado niwape hongera na ninaunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge huyo ni Dorothy George Kilave Mbunge wa Temeke - TMK alivyokuwa anataja ile mitaa ya kule Temeke nikajua kweli ni mwanatemeke kwelikweli hongera sana Mheshimiwa Kilave nilikutaja Mheshimiwa Tabasamu utafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Gyson Magesa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa niaba ya jina la Jimbo la Sengerema naomba kuchangia mchango wangu katika bajeti hii ya nishati.

Mheshimiwa Spika, kazi ya uspika ni kazi ya ngumu sana, nilikuwa sijui wakati huo sijawa Mbunge lakini nimeona kwamba una kazi ngumu kiasi gani cha kwanza ni kwamba kuhakikisha Wabunge wako wote wana uwezo wa kufanya kazi katika maeneo gani katika hizi kamati. Mimi tu Mwenyezi Mungu alikuonesha maono kwamba mpeleke Mheshimiwa Tabasamu katika Kamati ya Nishati na Madini hongera sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nikusifie wewe mwenyewe binafsi kuona Mheshimiwa Tabasamu ninafiti pale lakini ninachotaka kukuambia kitu kingine cha msingi sana kilichopo ni Mwenyekiti wa Kamati hii ni mzalendo wa kwelikweli. Yaani haya yote unayoona Waziri anafanikiwa ni kutokana na kamati hii ikiwa na mwenyekiti na msaidizi wake Naibu Mwenyekiti na sisi wajumbe kuwa wazalendo katika kamati hii. Tumezunguka katika kamati kuangalia hii miradi yote ya kimkakati miradi ya umeme mikubwa iliyopo na bado ndo tukaja na maono kuja kukusaidia kwamba tuangalie katika vina saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ya mafuta na gesi ya mwaka 2015 nyinyi mmepitisha Bungeni hapa mnajua inazungumzia nini kuhusiana na suala la usalama wa mafuta kama ni usalama wa nchi, usalama wa Taifa. Lilikuwa ni kosa sana kuachiwa mtu binafsi aendeshe muhimili mkubwa kama huu kwa kuweka vina saba hili lilikuwa ni kosa tusilirudie tena katika nchi hii naomba *Hansard* iweke hiyo na ukiona mtu anakuja kuzungumza hapa kwamba *GFI* basi ujuwe kabisa halitakii mema Taifa hili tunahitaji uzalendo wa kweli kutoka moyoni katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni ya wajanja wawili watatu wanaondoka na milioni 168 kwa siku kwa miaka 6 poleni sana watanzia katika jambo hili inaumiza sana raia yoyote wa Tanzania ambaye ana machungu kwa ajili ya uzalendo wa nchi hii mkaja hapa mnakuja kuzungumza *GFI* kwanza hatujui amelika kodi kiasi gani kwa sababu ameanza kufanya kazi hii mwaka 2015 anachukuwa bilioni tano kila mwezi kwa



mwaka ni bilioni 60 bajeti karibu ya wizara tatu kosa kubwa sana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, huyu mtu kachukuwa bilioni 60 mpaka 72 kwa miaka 6 karibu bilioni 450 hatakiwa kumzungumza mtu huyu kweli tunakuja Wabunge tunakuja kuzungumzia habari ya *GFI* sasa hivi badala ya kuja kujipa pole kwa kazi hii vina saba ni nini? Vina saba ni mafuta hayahaya petroli hii, diseli hii, mafuta ya taa kinachowekwa ni *chemical* tu kidogo wajanja fulani bei ya dola moja anauza huyu *SWISCAP* wamekuja wawili kama *partner* mmoja *SWISCAP* anauza vina saba *GFI* anaweka vina saba halafu *EWURA* anakuja kukugua hivi vina saba kwa miaka sita.

Mheshimiwa Spika, leo tunaleta mawazo ya kizalendo kwamba *TBS* anatosha kuja kufanya kazi hii tuweze kupata pesa kuokoa hizi pesa ambazo walikuwa wanachukuwa wajanja wawili watatu kuna watu wanataka kuja kusema *GFI* aendelee kuweka haya mafuta jamani tunaitakia mema nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukuambia hapa kinachobakia ni uzalendo wa Waziri husika uzalendo wa kwako wewe kama Spika uzalendo wa sisi kama kamati tukushauri vizuri juu ya jambo hili huyu mtu sijui katika hii bilioni 60 alilipa kodi alilipa *payee* hatujui ulipaji wake wa kodi tunamuomba Waziri wa Fedha kwanza afuatilie watu waende wakaangalie *GFI* alilipa kodi kiasi gani na hili jambo lije lielezwe bunge haiwezekani huyu mtu tena aje arudi hapa mkataba wake umeisha mwezi wa tisa akaongezea kwa *cotetion* kazi ya bilioni 60 inaweza ikaongezwa kwa *cotetion* akaongezewa miezi *mitatu*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwezi wa Kumi na Mbili, mkataba umeisha wa miezi mitatu akaongozewa miezi mitatu, tarehe 28 mwezi wa pili kaongezewa miezi mitatu inaumiza sana katika roho leo tunasema aweke *TBS* watu wanakuja kusema hapa sheria kwamba *TBS* hana sheria maana yake ni nini kuitwa *TBS* tunaomba tafsiri ya neno *TBS* ni nini?

Mheshimiwa Spika, hili shirika la viwango la Taifa viwango vya aina yoyote iwe gesi iwe mafuta kila kitu iwe dawa ndio kazi ya *TBS*. Sheria gani ije iundwe tena kwa ajili ya *TBS* na *TBS* huyu naomba kwa manufaa ya nchi niongezewe dakika kidogo naomba nakwenda kwa sababu nakwenda mbele huko kuna jambo kubwa nakuomba sana maana yake nasikia kengele inalia hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza huyu *TBS* sasa hivi akiwezesha, akiwezesha wafanyakazi, miundombinu, akanunua hizi machine zinauzwa Finland zinauzwa Uturuki, machine zinauzwa China na hivi vinasaba ni vitu vinatengenezwa maabara tukatengeneza wataalam wetu wakaja wakafanya hii kazi kwa ajili ya uzalendo hili ni suala la usalama wa nchi hatakiwi kuachiwa mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza hatujui huyu *GFI* hii vina saba alivyokuwa anaviweka yeye katika hizi kampuni za mafuta katika nchi hii depo 22 amewauzia kiasi gani, ya kuwapa kwa sababu hana haki mali ni ya kwake...

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Taarifa

**SPIKA:** Taarifa unapewa na Mheshimiwa Shabiby

## T A A R I F A

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika nataka nimpe taarifa Mheshimiwa mzugumzaji kwamba hata kama *TBS* itafanya kwa bei kubwa bado ile pesa itaingia kwenye taasisi ya Serikali. Kuliko kufanya mtu binafsi nataka nimpe taarifa kwa sababu pesa itaingia kwake.

**SPIKA:** Unaipokea taarifa hiyo Mheshimiwa Tabasamu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika kwa mikono sabini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni kwamba hivi vina saba *SWISSCAM* alikuwa anamuuzia *GFI* kwa dola saba kwa *cubic*

5 lakini sasa hivi baada ya kuonekana *GFI* kakosa kazi *SWISSCAM* anamuuzia vina saba *TBS* kwa dola 3.5 na mimi kwa ajili ya uzalendo nimekwenda kumfuata Mkurugenzi wa *TBS DG* nikamwambia hata hiyo bei bado umewapa kubwa agiza wewe mwenyewe Finland Uturuki utapata kwa 0.8. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya maneno ya wizi ukome katika nchi hii ninachotaka kuwaambieni kama Mheshimiwa Tabasamu nimetishiwa kuuwawa kwa ajili ya hawa watu wa *GFI*, kuleta habari hizi tu hapa Bungeni nikatishiwa kuuwawa nimemwambia Mheshimiwa Spika na kesi hii iko hapo kwa *RPC* Dodoma, na hatujapata majibu walionipigia simu na namba zao ziko pale kwa ajili ya kunitisha kazi hiyo umefanyiwa wapi.

Mheshimiwa Spika, naomba na hili unisaidie kunilinda kwa ajili ya uzalendo nimeleta jambo hili kwa sababu tunatafuta pesa za barabara za *TARURA*, hivi ninavyozungumza na wewe ukiondoa kodi iliyopo hapa kwenye mafuta kwa mfano kwa mwezi huu mambo haya ni madogo sana kwa mwezi huu tu peke yake kodi ya *petrol* ilikuwa ni shilingi 792, kodi ya *diese* ilikuwa ni shilingi 600 kama sikosei hapa kwa lita 666, kodi ya mafuta taa ilikuwa ni shilingi 615 lakini tozo zilizoko hapa nitakuprintia karatasi kesho nikulettee vikampuni vidogo vidogo ambavyo viko kwenye idara zetu mpaka zimefika pamoja na huyu *GFI* alivyokuwepo tumefikisha shilingi 92 tozo peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukichukuwa kodi ya shilingi 790 Mheshimiwa Waziri wa Fedha nisikilize upo hapa hii ndio inayoingia hazina na katika hiyo shilingi 790 kuna shilingi 100 kwa ajili ya *petrol fee* hii ni kwa ajili ya utafiti wa *petrol* na mambo mengine. Pesa inayobakia 690 ndio kodi. Hii shilingi 92 hii inaenda tena kama tozo kwa sababu tunakuja kwenye bajeti kuu ntakuja kukukaba huko hawa kwa nini wanaleta tozo kodi nyingine hii tozo ikatwe kule iende *TARURA* habari ya kutuambia kwamba *TARURA* imepewa bilioni 150 kwamba kila halmashauri imepewa milioni 500 ni kuja kutufunga

mdomo hili tuisema hili jambo haiwezekani Wabunge katika jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili hii shilingi 92 chukueni *calculator* zenu shilingi 92 hizi ambazo zinapotea hapa wanachukuwa huko zinakwenda kwenye tozo kutumika vibaya hizi zikipigiwa hesabu kwa siku tunauza *petrol* peke yake. Lita 5,600,000. Diesel tunauza lita 6,200,000, mafuta ya taa kama lita 100,000 kwa siku ukichukua hapa hizi shilingi mabilioni ya shilingi kwa kila siku hizi zinatoshwa kwenda *TARURA*, jamani inakuwaje haya maneno leo mimi nakuja kutishiwa kuuwawa kwa sababu nimeleta jambo hili heri nife kwa ajili ya Tanzania Spika utanilinda. (Makofi)

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Taarifa

**SPIKA:** Mwenye taarifa endelea.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Niko huku Mheshimiwa

**SPIKA:** Endelea tu.

## T A A R I F A

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwa mzungumzaji Mheshimiwa Tabasamu kwamba kwa ukubwa wa hoja ambayo anaizungumza inayohusu uzalendo wa nchi nimemwomba Mheshimiwa Tabasam nimpe taarifa kwamba ni vizuri Waziri wa Nishati atakapokuja ku-*wind up* atoe *commitment* ya kumpa ulinzi kwa ajili ya usalama wake pia.

**SPIKA:** Bahati mbaya hahusiki sana na masuala ya usalama; endelea kuchangia Mheshimiwa Tabasam, Serikali imesikia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naendelea kukushukuru. Ninachotaka kukwambia ni kwamba hapa tuna mambo mengi sana kuhusiana na hili suala la vinasaba. Hivi vinasaba inaweza ikaandaliwa bajeti

tu ya kununua vinasaba vya mwaka mzima ambavyo haviwezi kuzidi bilioni 10 au 15, huyu *TBS* akaendelea kuweka na ile hela ambayo ilikuwa inakwenda *TBS* au *GFI* yote iletwe *TARURA*. Haya maneno gani haya? Kwa sababu lile ni shirika la Umma linawajibika kufanya kazi ya Umma. Hizi pesa tuziokoe ziende huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza na wewe naomba tu nitoe ushauri wangu mdogo sana kuhusiana na hili suala la umeme. Hili suala la umeme kwa mfano sasa hivi tunapata shida sisi ya kusambaza umeme vijijini, nguzo zipo. Haya, utengenezaji wa nguzo *TANESCO* sasa ifikie mahali inunue mashine yake ya kokoto, inunue mashine ya kutengeneza nguzo, iwe na mashine yake itengeneze nguzo migogoro hii iishe.

Mheshimiwa Spika, lakini suala hili la kufanya kazi hizi kwa kutumia wakandarasi, tunashukuru Mungu tunakwenda kwa kasi, vifaa vingine vinatakiwa viwe vyetu. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa uzalendo wako, endelea kuwa mzalendo hivyo hivyo; Naibu Waziri, endelea kuwa mzalendo; Katibu Mkuu, endelea kuwa mzalendo. Simamieni hii hali ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuomba utuuonge mkono katika hili suala sisi Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri tuliyoifanya kuishauri Serikali kuwaondoa *GFI*. Tupigiwe makofi ndani ya hili Bunge. Lakini habari hii hapana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja; ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam, ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Na ndiyo maana mpaka sasa kwa kweli tuko pamoja, tunawapongeza sana Kamati na wote ambao mmechangia.

Tulichokuwa tunasema – kwa yale ambayo tunayasikia sisi sasa na kuwaelewa wenzetu – wanasema njia ya kwenda jehanamu imejaa nia njema, au kinyume chake, basi iwe itakavyokuwa lakini ni kwamba kuna ile kwa nini umefanya hivi, mtu anajibu aah, shetani tu bwana, na kadhalika. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, yaani kwa maana ya kwamba leo hii tunaisifi Kamati, tunamsifu Mheshimiwa Dkt. Kalemani, kwamba amepeleka *TBS*. Mwakani Kalemani huyu anaweza akaja kivingine, au mwakani, mwaka kesho kutwa yeye siyo Waziri, akaja Waziri mwingine akatumia mamlaka hayahaya akahamisha hapo akapeleka mahali penginge.

Ndiyo maana tunasema kwa vile sisi ni Wabunge, kwa kuwa tunakubaliana jambo hili ni zuri ije sheria, tuseme *TBS*, maana wengine hawaelewi, ukishaweka sheria, awe Kalemani, awe Ndugai, awe nani, palepale. Nafikiri tunaielewana kwa nini tunazungumza jambo hili. (*Makofi*)

*As long as* Serikali sasa inajiridhisha kwamba jambo hili ni zuri, tuwabane waleta sheria, tena haraka ikiwezekana. Maana Bunge halina shida, na limeshatoa *commitment* yake. Sasa shida huwa ni ile *bureaucracy* ya kawaida Serikalini, mpaka nani mpaka nani, zile *bureaucracy* za kawaida, au *GFI* na wenzao wenye mahela mengi wanaweza wakaichelewesha Serikali kwa kukabakaba mtu mmojammoja huko. (*Makofi*)

Sasa hoja yetu ni kwamba sheria ije haraka, leo tarehe ngapi? Tarehe mbili, tuko mpaka tarehe 30. Hivi kwa nini tuondoke tarehe 30 sheria hiyo haijaja? Na yenyewe si *miscellaneous amendment* tu? Ili tukomeshe haya maneno yaishe; ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa – eh, leo wote wanaoongea ni Wasukuma? (*Kicheko*)

Atafuata Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi; Mheshimiwa Magessa. (*Kicheko*)

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia. Lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ambayo nimeipata ya kuzungumza ndani ya Bunge hili siku ya leo katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana kwamba vinasaba hivi vimezungumziwa sana, lakini nafikiri umekwenda kwenye *conclusion* kwamba sheria ije sasa ili twende kwenye maamuzi *TBS* wapate kihalali kutokana na sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, naomba nisijielekeze sana huko, nijielekeze kwenye umeme hapa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwamba katika bajeti hii, nimeona bajeti za mwaka jana na mwaka huu, wao kila wanapotenga fedha za maendeleo zinakuwa karibia asilimia 98, ikionesha kabisa kwamba kuna kazi inakwenda kufanyika. Kwa hiyo, vitabu vyao vyote vinaonesha asilimia 98 huwa inakwenda kwenye maendeleo. Na haya tunayaona kwenye miaka mitano, sasa tuna vijiji zaidi ya 9,000 vilivyoongezeka kuanzia mwaka 2015 ambavyo vimepata umeme.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu inaonekana bajeti imeongezeka kwa asilimia nane, kwa hiyo ninaamini kazi inayokwenda kufanyika itakuwa ni kubwa kuliko hata iliyofanyika mwanzo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, umeme wetu huu ambao ninauona umewekwa kwenye vijiji vyetu, pamoja na miradi mingi ambayo imefunguliwa hapa katikati, bado tuna kazi kubwa ya kupeleka kwenye vitongoji vyetu, huko kwenye senta tu za vijiji na wananchi wamefurahi sasa kupata umeme, kila mmoja ambaye hana umeme sasa anajuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwaombe sana Wizara wajitahidi na wakandarasi ambao wametupatia simu hawa tunaendelea kuwasiliana nao umeme uwezo kuwafikia wnanachi kwa ajili ya kuchachua maendeleo ambayo

yalikuwa yamesimama kwa sababu ya kukosekana kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, tuna vijiji 1,956 havijapata umeme, jimboni kwangu katika vijiji 83 nina vijiji 26 tu ambavyo vina umeme, vijiji 57 havijapata umeme. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, mkandarasi ambaye nimeongea naye jana – nilipata namba yake – ameniambia bado anashughulikia *performance bond CRDB*, kwa hiyo, bado hajaweza kwenda kwenye eneo la tukio kwa ajili ya kutupatia umeme.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana; katika miaka miwili ambayo tumeambiwa Desemba, 2022 kutakuwa na umeme nchi nzima, tuhakikishe kwamba umeme huu unaosemwa uweze kufika kwenye vitongoji ili wananchi waweze kuona maendeleo ambayo tunayasema.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja, nimeona wanasema kuna *densification*. Hii *densification* kuna mahali ambapo watu wameshafanya *wiring* muda mrefu tu, lakini walivyokuwa wanafanyiwa *survey* maelezo yanasema kunatakiwa nguzo mbili, hawezi kuwekewa umeme ule, anatakiwa tena aingie kwenye hii *densification* kwa sababu anaonekana yeye hapo alipo siyo kijiji, ni sehemu tu ya mtaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yako maeneo mengi ambayo yanakaribiana na miji midogo hii yana tatizo hili; watu wengi wamefanya *wiring* na hawana umeme, na malalamiko yao ni makubwa. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, hawa wakandarasi wanaokwenda, pamoja na miradi hii ambayo tumeisema, uweze kuwasaidia wananchi hawa waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye umeme hapo; pamoja na kujenga miundombinu ambayo tunaisema, kuna tatizo kila ninapokwenda ninalikuta mahali kwenye miji yetu. Umeme unapowekwa kati ya nguzo na nguzo kuna kitu wanaita *clearance*, *clearance* ni mahali ambapo nikisimama natakiwa nione *wire* ukiwa juu yangu. Lakini bahati mbaya



kwenye miji yetu hii unaweza ukasimama ukaona *wire* umepita tu karibu nusu mita kutoka kwako ulipo.

Mheshimiwa Spika, sasa huu ujenzi wa miundombinu ya aina hiyo udhibitiwe sana kwa sababu wanaita mawimbi (*magnetic feed*), yale mawimbi yanapopita karibu na mwanadamu yana athari, na hizo athari inawezekana zisitokee kesho au keshokutwa, zikaja baada ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapojenga laini zetu hizi tuhakikishe kwamba ile *clearance* ya mwanadamu kwenda kwenye *wire* iwe ni ile iliyokuwa-*recommended*, iliyosemwa. Ukienda kwenye miji mbalimbali unapita unakuta *wire* unapita tu jirani, maana yake ni kwamba ujenzi uliofanyika ulikuwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niishauri Serikali kwamba ujenzi wa laini zinazojengwa wahakikishe kwamba hicho kinachojengwa kama *clearance* kwenye ile *sag* kati ya nguzo na nguzo kiwe ni kile ambacho kiko *recommended* kwa ajili ya mwanadamu ili mawimbi yale, *magnetic feed*, isimletee madhara kwa namna yoyote ile. Kuna mahali inaoneshwa hata kwenye mitandao mtu anapita karibu anagusa *wire*. Ni hatari sana kwa maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, nihame kwenye umeme niende kwenye *EACOP* (Bomba la Mafuta). Hili bomba la mafuta limesemwa muda mrefu na wananchi wetu wamekuwa wanajiandaa wanajua watauza mchicha, mayai na kuku. Lakini hivi vitu kama alivyosema jirani yangu hapa, Mheshimiwa Zedi, havijana *defined*. Havijajulikana ni vitu gani vitafanyika kwenye biashara ya bomba la mafuta, sasa vingesemwa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kupitia Taasisi ya Uwezeshaji, kwamba ingewezekana wananchi ambao tunao wako wengi wanaotaka kufanya biashara kwenye bomba la mafuta lakini uwezo wao ni mdogo. Hii Taasisi ya Uwezeshaji ambayo ninaamini ipo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, waangalie uwezekano wa kuwa na fedha ambayo itapitishwa kwenye

benki yoyote ili iweze kuwasaidia hawa wafanyabiashara wadogo na wakiweza kukopeshwa kwa utaratibu wa benki wataweza kufanya biashara hizo. Ili isifike biashara hii ikavamiwa na wageni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo wako watu wamejiandaa kufanya biashara na bomba la mafuta, wataonekana kama ni Watanzania lakini itakuwa ni hela kutoka kwa watu wengine wenye uwezo mkubwa na siyo wale Watanzania wenyewe. Kwa hiyo, hii Taasisi ya Uwezeshaji iangalie inaweza kupita mahali gani kwenye benki zetu ikawawezesha hawa waweze kufanya kazi katika miaka hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mtu atahitaji labda kuku 1,000, tukiuliza kuku 1,000 nani anao ili aweze ku-*supply*, utaona mwananchi anaanza kuhangaika, anakusanya huku na huku. Lakini kama wamewezeshwa watakuwa wameandaliwa kwa ajili ya kuvuna hiki ambacho tunakisema ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikumbushe suala la mwisho kwa Mheshimiwa Waziri; kuna mradi kutoka Geita, Mpomvu kwenda Nyakanazi, ambao ndugu yangu, Mheshimiwa Ezra, aliu sema pale. Huu mradi umesemwa muda mrefu sana lakini haukamiliki. Kwa hiyo, ni ombi langu Mheshimiwa Waziri, hawa wakandarasi wanaokuja sasa wahakikishe kwamba mradi huu unakamilika, vijiji vingi sana vinapitiwa na mradi ule na kama haukamiliki maana yake wale wananchi hawawezi kupata umeme kwa sababu ndiyo laini pekee kwenye *backborn* inayoweza kuwapelekea umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kusema maneno machache kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara. Wamefanya kazi kubwa sana kwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, na kwa mfano mdogo ukiangalia usambazaji wa umeme kimsingi kumekuwa na ufanisi kwa sababu kwa kipindi cha miaka takribani mitano, vijiji zaidi ya 8,000 vimepewa umeme kama nyongeza kwenye vijiji vya awali vilivyokuwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili nitoe ushauri tu; pamoja na kwamba tumepeleka umeme kwenye vijiji zaidi ya 10,000 lakini ukiangalia wigo wa maeneo yaliyopelekewa umeme kwenye kijiji chenye vitongoji saba, umeme umepelekwa makao makuu ya kijiji na katika makao makuu ya kijiji umeme unapelekwa kwenye kaya zisizozidi 20. Bado wigo ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakuta vitongoji zaidi ya vitano, vitongoji sita kwa mfano kwa Ukerewe, vijiji vyenye vitongoji saba, kitongoji kimoja kwa kaya 20 pekee ndizo zimepata umeme, sehemu kubwa ya wanakijiji wanakuwa hawajapata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado tunahitaji kuwekeza pesa nyingi kwa *TANESCO* ili mradi unapofikisha umeme kwenye makao makuu ya kijiji basi *TANESCO* wabaki na jukumu la kusambaza umeme kwenye eneo la vitongoji ili mwisho wa siku basi wananchi wapate umeme na lile lengo tunalolitarajia la wananchi kunufaika na nishati hii, kujiletea maendeleo, tuweze kulfikia.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ninataka kuliongelea – nitaendelea kuongelea suala la umeme – ni juu ya kukatikakatika kwa umeme; Ukerewe tumekuwa na shida kubwa ya kukatikakatika kwa umeme kwa takribani

miaka miwili sasa. Na chanzo cha kukatikatika kwa umeme ni tatizo la *submarine cable* inayotuunganisha kati ya Kisiwa cha Ukerewe na Bunda.

Mheshimiwa Spika, ile *cable* imechoka na kwa maana hiyo imekuwa mara kwa mara maji yakigusa inakatika. Sasa imesababisha adha kubwa sana kwa wananchi wa Ukerewe, wawekezaji wanakimbia, wenye dhamira ya kuwekeza wanashindwa kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, inaathiri kwa ujumla uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Na wakati mwingine wananchi wenye uwekezaji wao kwenye Visiwa vya Ukerewe wanapata hasara kwa sababu vifaa vyao vingi vinaharibika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na timu yako niwapongeze; mmekuwa na jitihada kadhaa ambazo mmekuwa mnazifanya. Na hivi tunavyoongea ninashukuru angalau sehemu fulani ya kipande cha *cable* ile mmeweza kuipata. Lakini niombe; ile sehemu ya kipande kingine cha *cable* iweze kupatikana haraka, tuweze kupata suluhisho la kudumu la umeme kwenye Visiwa vya Ukerewe na hasa Kisiwa kikubwa cha Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kusoma hotuba hapa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako ukurasa wa 51 umeongelea umeme wa maeneo ambayo yapo nje ya Gridi ya Taifa, pia maeneo ya visiwa. Ukerewe tuna visiwa 38, katika hivyo, kisiwa kikubwa kile, sawa tuna umeme wa Gridi ya Taifa; visiwa 37 vinavyobaki vyote tunategemea umeme wa jua na umeme mwingine kama ambavyo mtautoa kwenye maeneo yaliyo nje ya Gridi ta Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, unajua katika visiwa 37 vya Ukerewe, ni visiwa vitatu pekee vidogo vyenye umeme; Kisiwa cha Ukara ambacho kinakuwa-*supplied* na watu wa Jumeme; Kisiwa cha Ilugwa ambacho kiko *supplied* na watu wa Jumeme na Kisiwa cha Liegoba ambacho kinakuwa *supplied* na watu wa *Power Gen*.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wa Liegoba kwa umeme wanaopewa wanatozwa shilingi 1,000 kwa siku, wananunua umeme kwa *bundle*, *bundle* lile inanunuliwa shilingi 1,000, haijalishi yule mteja ametumia umeme ule au hajatumia mwisho wa siku lile *bundle* inakuwa haifanyi kazi tena na matokeo yake kesho yake yule mteja anatakiwa kununua tena *bundle* lingine la shilingi 1,000, kitu ambacho ni gharama sana kwa mwananchi wa kawaida. Mheshimiwa Dkt. Kalemani, nimekuwa ninakueleza jambo hili. Hii si sawa kwa mwananchi wetu wa kawaida, mwananchi wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la Ilugwa na Kisiwa cha Ukara ambapo wako *supplied* na watu wa Jumeme, ni kweli walikuwa wanatiozwa shilingi 3,500 kwa *unit*. Ulisema hapa Bungeni ukatoa maelekezo wakapunguziwa mpaka shilingi 100, lakini baada ya kupunguziwa na kuanza kulipa shilingi 100 wananchi hawa wakawa wanapata umeme kuanzia saa nne asubuhi mpaka saa 12.00, baada ya saa 12.00 usiku mzima wananchi hawana umeme.

Mheshimiwa Spika, nimeendelea kupiga kelele na hatimaye mwezi Machi wananchi wakaingia makubaliano mapya na watu wa Jumeme kwamba wako tayari kulipa shilingi 2,000 kwa *unit* ili tu waweze kupata umeme kwa saa zote 24. Hivi ninavyoongea pamoja na wananchi hawa kuendelea kulipa shilingi 2,000 lakini hawapati umeme kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Serikali ilianganalie jambo hili, nimekuwa ninalisema mara kwa mara hapa lakini ifike mwisho sasa tuone kwamba huu mradi wa kusambaza umeme kwenye maeneo yaliyo *off-grid* angalau basi Visiwa vya Ukerewe viweze kunufaika na mradi huu. Vile ambavyo havijapata umeme moja kwa moja viweze kupelekewa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye Visiwa kwa mfano vya Ghana, Bulubi n.k. mkandarasi alipeleka nguzo tokea mwaka 2016 akaziacha pale. Mpaka leo hakuna chochote

kilichofanyika. Niombe watu wa Ukerewe wanahitaji huduma hii ya umeme, wanahitaji kuchochea maendeleo na maisha yao kwa ujumla wake, basi wapate nishati hii ya umeme. Hasa watu wa visiwa vidogo vile; watu wa Jumeme ule mgogoro wa bei uliopo uweze kutatuliwa na mwisho wa siku waweze kupata huduma hii ya umeme na waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi kama tunavyowatarajia.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo, endelea na taarifa hiyo.

### T A A R I F A

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nataka tu kumueleza mzungumzaji kwamba tatizo la watu wa kwenye visiwa kutozwa gharama kubwa ya umeme halipo kwenye visiwa vyake peke yake. Natoka kwenye Visiwa vya Maisome pamoja Zilagula ambako kwa hivi sasa tunavyoongea wananunua *unit* moja ya umeme kwa shilingi 2,400; nilitaka kuzungumzia jambo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa hiyo kwa mikono yote miwili. Na unaweza kuona namna gani wananchi wetu wanavyotaabika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwananchi wa kawaida wa kijijini kununua *unit* moja kwa shilingi 2,000 au kama wanavyotoza kwenye Kisiwa cha Liegoba, ananunua *unit* kwa shilingi 1,000, *bundle* ile, halafu mwisho wa siku ile *bundle* iki-*expire* kesho yake anatakiwa kununua tena haijalishi ametumia au hajatumia, ni lazima Serikali i-*intervene* katika jambo hili. Ifike mahali wananchi hawa tuwape fursa ya kujiletea maendeleo kupitia nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilitaka kusema kwenye hayo maeneo matatu tu juu ya umeme. Lakini niombe sana Mheshimiwa Waziri; suala la *cab*

inayotuunganisha kati ya Lugezi na Kisorya pale kupeleka umeme kwenye Kisiwa kikubwa cha Ukerewe, tupate ufumbuzi wa kudumu. Lakini suala la visiwa vidogo hasa kwenye eneo la bei vilevile tupate *solution* ili mwisho wa siku wananchi wa Ukerewe waweze ku-*enjoy* maisha na maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa fursa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkundi Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, atafuatiwa na Mheshimiwa Assa Nelson Makanika.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya katika wizara hii pia na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia naomba nimshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya. Tunao ushahidi mkubwa kwamba nchi yetu ilikuwa na giza, lakini sasa mwanga unaonekana, pamoja na kwamba zipo changamoto. Lakini nipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanywa ya kuhakikisha kwamba tunapata *megawatt* 2115 katika bwawa lile la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli huo utakuwa ni ufumbuzi wa kudumu kuondokana na giza tuliokuwa nalo katika nchi yetu, lakini pia ni kwamba kutokana na umeme ni mwingi ambao utakwenda kuuzwa katika nchi jirani maana yake bwawa lile litakwenda kuongeza pato la Taifa pale ambapo tutakwenda kuuza umeme katika nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo la kupongeza sana Awamu ya Tano ambayo iliingia mkataba na ilifanya maamuzi magumu kwa kuhakikisha kwamba bwawa lile

linajengwa pamoja na kwamba mipango ile ilikuwepo kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niipongeze Serikali kwa kuingia mkataba wa kuona namna ya kujenga ile eneo la Malagarasi pale Igamba ambayo kwa kweli ni katika Jimbo langu la Kigoma Kusini huu mradi unakwenda kutekelezwa kulingana na hotuba ya Waziri wa Nishati naomba Mheshimiwa Waziri mradi huu unaonekana utaanza Septemba mwaka huu na utakwenda kuisha Septemba tena 2024, maana yake ni miaka minne.

Mheshimiwa Spika, naomba Mkoa wa Kigoma umekuwa ukitumia mafuta, umeme wa mafuta kwa muda mrefu sana na ndiyo maana unaweza kuona kwamba kimkoa hatuna viwanda, isingewezekana kupata kiwanda au viwanda katika eneo ambalo tunatumia umeme wa mafuta. Ambao umeme wa mafuta una gharama kubwa sana katika uendeshaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayo imani, kwamba mradi huu ambao una megawatt 49.5 utakwenda kuwa ufumbuzi na wa Mkoa wa Kigoma kwa ujumla, lakini ninayo imani kutokana na bajeti yako na ulivyoonyesha, umeonyesha kabisa kwamba umeme wa *grid* ya Taifa utawahi kuingia Kigoma kabla ya mradi huu ambao utajengwa pale, pale Igamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona ulitakiwa kufanya ziara kwenye Mkoa wa Kigoma pale Nguruka ambapo tayari kumeshaandaliwa na palishajengwa kwa ajili ya kupokelea umeme ambao ndiyo utakuwa unapoozewa pale. Lakini ninayofuraha kuona kwamba mpango wako Mheshimiwa Waziri kuingiza umeme wa *grid* ya Taifa Kigoma maana yake upande mmoja wa Tabora unaingilia Nguruka ambapo ni kwenye Jimbo langu pale katika Kijiji cha Mgaza pameshajengwa tayari, *compound* imeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia umeme mwingine wa *grid* ya Taifa unaingilia Kankoko kutokea Nyakanazi hii



mipango miwili ikikamilika Mheshimiwa Waziri kwa kweli na sisi Kigoma tutakuwa tumepata ukombozi kutoka kwenye giza. Na ninayo imani sasa wawekezaji watakuja kwa ajili ya kuwekeza viwanda katika mkoa wetu ili na sisi mkoa wetu uweze kuinuka kiuchumi na wananchi wetu wa Kigoma waweze kupata ajira, kwa sababu bila viwanda ni vigumu sana kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo hili la Ujenzi wa Igamba nimefurahi kuona kwamba tayari fedha zimekwisha patikana kwa ajili ya fidia, wananchi katika eneo hili walitwaliwa maeneo yao kwa muda mrefu na walizuliwa wasiendeleo kwa hiyo walikuwa hawawezi kufanya chochote kwa sababu ya mradi huo, lakini naona kabisa kwamba sasa fedha ya fidia nayo pia imepatikana. Naomba Mheshimiwa Waziri jambo hili uende kulifanyia kazi ili wananchi wale waweze kupata fidia katika maeneo ambayo waliyaachia kwa ajili ya mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kuna vijiji 61 ni kweli vipo vijiji 17 tayari vimekwishapata umeme na maana yake kuna vijiji 14 bado havijapata umeme kabisa, lakini kwamba hata hivi vijiji 17 ambavyo vimekwishapata umeme ni katika maeneo tu kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanavyoongea. Na hii imetuletea malalamiko makubwa sana sisi Wabunge, tunalalamikiwa sana kwamba kwanini umeme unakuja hapa na baadaye kwenye vitongoji vingine umeme haufiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapata wakati mgumu katika kujibu maswali tunaomba Mheshimiwa Waziri hili jambo lifanyie kazi. Nafurahi kuona kwamba unao mpango mzuri kwamba tayari makandarasi wameshapatikana na nimekuwa nikikusumbua sana, lakini mpango wa Serikali ni kwamba umeme utapatikana 2022 kwa maana ya nchi nzima, kwa maana ya vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba wakandarasi hawa ambao sasa wameteuliwa waweze kwenda kuondoa hizi kero pamoja na kwamba tunatakiwa tuendeleo kumaliza vile

vijiji 14, lakini pia huku kwenye vijiji 17 ambavyo tayari vina umeme lakini kuna maeneo mbalimbali hayana umeme katika vijiji hivi kwenye vitongoji na hiyo kazi pia iendelee kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kigoma Kusini zipo Kata nne, Sigunga, Mgambo, Kalya na Igalula, kata hizi zinatimia umeme wa jua, wananchi hawa wamekuwa wakilalamika sana kila siku napigiwa simu kwamba kwanini mkandarasi huyu ambaye ni Jumeme kwanini anawauzia umeme *unit* moja shilingi 4000. Shilingi 4000 tunakuwa na bei mbili kwenye nchi moja hivi hawa wananchi tunawaonaje, tunawasaidiaje Mheshimiwa Waziri, nimekwisha kuja kwako mara nyingi sana, lakini ulionyesha kutatua tatizo hili na leo pia umetoa tamko, lakini pia bado nakuomba ziara yako ya kwenda Kigoma kutokea Tabora iendelee kuwepo na nitaomba nishirikiane na wewe unipe taarifa lini utakwenda nione uende kutoa tamko ili kusudi hawa watu wakome, wakome kabisa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Ahsante Mheshimiwa Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naoamba basi niweze kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nashon Willson Bidyanguze, Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi niweze kuchangia wizara hii muhimu sana ambayo hakika ni injini ya uchumi ambao tunatarajia kuuendea kama Taifa, Uchumi wa Viwanda yaani *Industry Economy*.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naanza kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuchangia katika wizara hii. Lakini jambo la pili naishukuru Serikali kwa jinsi inavyofanya kazi kwa mambo makuu mawili katika mkoa

wetu wa Kigoma. Kigoma ilikuwa ipo gizani lakini mpaka dakika ya sasa Serikali imeweza kuchukua juhudi kubwa sana tunaunganishwa na umeme wa *grid* ya Taifa na hatua zinaendelea vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili kabisa ambalo ninaishukuru Serikali inayoongozwa na Jemedari Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kusaini mkataba wa kufua umeme katika chanzo cha Mto Malagarasi. Sisi Kigoma na *location* tuliyonayo tunaitegemea hii wizara sana kuliko kitu kingine, kwa sababu ukiangalia katika eneo lile tullionalo la Kigoma na majirani tulionao bila hii wizara kututazama hatuwezi tukatoka mahala tulipo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tupo tumepakana na nchi jirani zile nchi zote ku-*survive* zinaitegemea Kigoma na haziwezi zika-*survive* bila Kigoma bila kuja kula Kigoma, lakini Kigoma haiwezi ikawalisha wale watu bila hii Wizara muhimu sana wizara ya Nishati. Nakumbuka nimejaribu kupitia sana hapo nyuma Mzee wangu Mwijage aliweza kuwa na wawekezaji kipindi yupo ni Waziri wa Viwanda alipata wawekezaji ambao walipaswa waje kuwekeza katika mkoa wetu wa Kigoma kwa ajili ya kuzalisha sukari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini wale wawekezaji hawakufanikiwa kuzalisha sukari katika mkoa wetu wa Kigoma ukifuatilia vitu ambavyo vilivyo wakwamisha cha kwanza ilikuwa ni ukiritimba wa sheria za uwekezaji. Lakini jambo la pili ilikuwa ni kukosekana kwa nishati ya kuweza kusimika kiwanda cha kuzalisha sukari pale Kigoma, walishindwa lakini mpaka sasa kuna watu wanakuja kuchukua sukari Rwanda wanapeleka mpaka Zambia na wakati ilihali tungezalisha pale Kigoma, lakini hiyo yote ilishindikana ni kwa sababu hatukuwa na nishati ya kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo naomba nielezee hali halisi ya nishati katika mkoa wetu wa Kigoma. Katika mkoa wetu wa Kigoma tunatumia umeme unaotokana na ma-*generator* tuna vituo vitatu katika mkoa

wetu wa Kigoma, kituo cha kwanza ni Kigoma Mji na kituo cha pili ni Kasulu na kituo cha tatu ni Kibondo. Vituo hivi vyote vitatu vinauwezo wa kuzalisha *megawatt* 11.25, lakini na sisi mahitaji yetu kama mkoa tunahitaji kuwa na *megawatt* 10.57, pamoja na hayo yote bado watumiaji wameongezeka kwa kasi sana kutokana na kwamba Serikali imeleta kuwaunganisha wananchi wengi na watumiaji wengi wameongezeka kupitia mfumo huu wa *REA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na baada ya kutokana na hiyo ukija ukaangalia hiki kituo cha Kigoma Mji kinahudumia maeneo ya Kigoma Ujiji, kinahudumia na maeneo ya Wilaya ya Uvinza kinakwenda na sehemu ya maeneo ya Wilaya ya Buhigwe, lakini hiki kituo kina uwezo wa kuzalisha *megawatt* 6.25 tu, ili kiweze kuhudumia hizi wilaya tatu. Pamoja na hayo yote bado kinazidiwa, kinazidiwa kwa sababu hizi wilaya tatu zinazidi hizo *megawatt* zinazozalishwa na kituo hiki cha Kigoma Mji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kituo cha Kasulu kina mashine mbili nacho kinalisha Kasulu na kinalisha na sehemu ya Buhigwe, lakini ile mashine moja mpaka sasa haifanyi kazi iseme imekufa. Kwa hiyo, imebidi sasa *TANESCO* wachukue sehemu ya Buhigwe wairudishe Kigoma Mji mpaka dakika ya sasa wananchi wa Kigoma wananusishwa umeme. Jana umeme umekatika saa kumi na mbili wanarudishiwa asubuhi na imekuwa ni *trend* ambayo inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hali hii iliyopo kuna minong'ono mingi sana huko kwanini umeme uanze kukatika sasa na kwanini haukuwa una katika hapo nyuma najua mlengo wa Serikali ni kwamba hakuna mgao wa umeme, lakini lazima tuzungumzie uhalisia kabisa ya kwamba upo umeme una katika na wananchi kila siku lazima umeme ukatike na shughuli zinamama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ningepomba wizara iweze kulichukulia umaanani wake, ukija Kibondo kadhalika hivyo hivyo ina uwezo wa kuzalisha *megawatt* 2.5 hiki kituo cha Kibondo kinalisha Kankoko, kinalisha na Kibondo, lakini

kinahitaji zaidi ya *megawatt* 3.2 ili kiweze kulisha hizi wilaya mbili nacho kinauwezo wa kulisha hii 2.5.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Serikali najua kuna namna ambavyo inataka kufanya kwa ajili ya kutoa mashine kutoka Loliondo kuja kuisimika pale kituo cha Kasulu, hilo ni zuri kabisa na ningeomba sana wizara iweze kuharakisha kwa sababu sisi Kigoma tumekuwa kwenye hii hali wakati ilihali wenzetu wananufaika na umeme *grid* sasa ningeomba hii bajeti iweze kuangalia *a quick solution* ya kuitoa Kigoma mahala ilipo mpaka sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuoneshe tu jambo dogo ambalo mpaka sasa ukija ukaangalia Serikali inatumia pesa za watu masikini kutumia kwa ajili ya kutumia haya *generator* na kama ikiweza kuharakisha kwa mfano; *grid* ya Taifa wamesema kufika Kigoma itakuwa imefika mwaka 2023 jambo ambalo ikifika mpaka huo mwaka tutakuwa tumesha hangaika vya kutosha. Ningeomba Serikali ina uwezo kulingana na hii hatua tuliyonayo iweze ku-*speedup* huu mradi wa umeme wa *grid* ya Taifa angalau hata tufike 2022 uwe umeweza kufika ili kuweza kuwa na *permanent solution* katika Mkoa wetu wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpaka dakika ya sasa katika Mkoa wa Kigoma *unit* moja ya umeme inazalishwa kwa shilingi za kitanzania 645, lakini *unit* moja hiyo hiyo ya umeme ukienda Singida inazalishwa kwa shilingi za kitanzania 36 mpaka 50 na Serikali hii hii inaweza kutumia bilioni 1.6 kwa mwezi kwa ajili ya kuzalisha umeme katika Mkoa wetu wa Kigoma hizi ni pesa nyingi sana, kwa nini tusiharakishe sana ili umeme wa *grid* uweze kufika tuweze kuokoa pesa hizi na hatimaye mwananchi aweze kuona ya kwamba ana unafuu wa kuweza ku-*utilize* umeme katika mkoa wetu wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri mambo machache sana katika wizara hii ili iweze kuyachukulia kwa uharaka sana ambayo moja itakuwa ni *permanent Solution*, lakini nyingine itakuwa *a quick solution* kwa ajili ya kuokoa hii

hali inayotokana, inayojitokeza kila muda katika mkoa wetu wa Kigoma. Moja kabisa, ni kama nilivyosema ni kuharakisha huu mradi wa umeme wa *grid* ya Taifa ili uweze kufika kwa haraka sana hiyo ndiyo *permanent Solution* sisi watu wa Kigoma tutakayoiona ya kwamba mmetutoa kwenye giza, lakini jambo la pili ni kuweza kuharakisha hiyo mashine kutoka Loliondo iweze kufungwa pale katika kituo cha Kasulu ili tuweze kuepukana na hii hali ya umeme kukatika kila iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, na jambo la tatu kabisa na la mwisho, nimuombe Waziri pale kwetu Kigoma kuna muwekezaji ambaye anaitwa *the next Solar Wazi Limited* amewekeza pale Kigoma anauwezo wa kuzalisha *megawatt* 4 mpaka 5, lakini anazalisha chini ya *megawatt* hizo ambapo vilevile tumejaribu kumuona hapo miezi ya nyuma anasema ndio anaweza, lakini Serikali iweze kumpa ushirikiano ili aweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niombe Waziri uweze kuongea na muwekezaji ili aweze kuzalisha zaidi ya hicho kiwango ili tuweze kuepukana na hali ya mgao huu wa umeme katika mkoa wetu wa Kigoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa!

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa machache hayo naona muda umekimbia, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza awali ya yote niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu

Hassan kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya na hasa kuwaunganisha wataanzania wote wa mjini na vijijini kwenye mtandao wa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa sababu imetambua kwamba umeme ni suala la msingi na wala si la *luxury* na kwa msingi huo inaendeleza ujenzi wa mradi wa umeme ambao unajulikana kwa jina la Mwalimu Nyerere ambao utazalisha *megawatts* nyingi na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema mradi huo utatusaidia kwa kiasi kikubwa kuondokana na giza.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali pia inaendeleza mradi wa *REA* kwa sasa ni mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili ambapo na hiyo inafanyika kwa nia njema ya kuwaunganisha wananchi vijijini wao waweze pia kupata umeme. Natambua juhudi zinazofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, lakini naomba tu nichangie kwa uchache sana katika Mkoa wa Mtwara ambapo ninawawakilisha wanawake wa Mkoa wa Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwamba katika Mkoa wa Mtwara bado tunavyo vijiji 281 ambavyo havina umeme, lakini natambua pia kwamba ipo jitihada Mheshimiwa Waziri anaifanya ya kuwapelekea vijiji hivi 281 umeme wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa pili, lakini ningepomba tu kwamba kwakuwa vijiji hivi ni vingi pengine wakandarasi wawili wasingetosha na ili pia mradi utekelezeke kwa haraka. Pengine wakandarasi wangeongezeka wangukuwa watatu kama ambavyo tuliahidiwa huko nyuma pengine vijiji hivi 281 vingefikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali, huko nyuma kabla ya mwezi wa 3 Mkoa wa Mtwara ulikuwa na tatizo kubwa la kukatikakatika kwa umeme kwenye wilaya zote sita. Lakini Serikali ilituletea mashine mbili za kuchakata umeme, kila mojawapo ilikuwa na uwezo wa kuchakata megawati 4.3. Ninaishukuru sana Serikali kwa sababu, sasa kwenye wilaya nne umeme umekaa vizuri hauna tatizo kubwa la kukatikakatika. Changamoto imebaki katika Wilaya

za Masasi na Nanyumbu, huku kuna tatizo kubwa la kukatika kwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwa Serikali na kwa kuwa natambua ni Serikali sikivu. Kwa upande wa Masasi, ambako kumekuwa na tatizo kubwa la kukatika kwa umeme kwa sababu tu, umeme wake unaunganishwa kutoka Mkoa wa Ruvuma kule Madaba. Unatoka Madaba unapita Songea, unapita Namtumbo, unapita Tunduru, unakuja Mangaka ndio unakuja Masasi. Lakini pia, kuna njia nyingine inayotoka Mahumbika ambayo iko Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, hizo zote mbili haziwapatii wananchi wa Masasi umeme wa uhakika na hivyo wameendelea kuukosa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri, ili kuondoa tatizo hili kwa suluhisho la muda mfupi, Serikali ijenge *line* mpya kutoka Mahumbika kwenda Masasi na hii itaondoa tatizo la umeme ule wa Masasi kutumika njiani kabla haujafika Masasi. Lakini halikadhalika watu wa Nanyumbu waunganishwe pia kwenye gridi hiyo, ikiwezekana sasa hivi waunganishwe watu wa Nanyumbu kwenye gridi ya Mtwara, ambayo imeimarika itasaidia kuondokana na hilo tatizo. Lakini, pale Masasi tunacho kifaa ambacho wataalam wanajua tunakiita *AVR Automatic Voltage Regulator* tunacho pale Masasi. Lakini wakati mwingine pengine hakitusaidii kwa sababu, tayari ule umeme unapofika unakuwa umeshapungua nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kifaa hiki *AVR*, kiwekwe Tunduru na kiwe kifaa kikubwa kisaidie sasa ule umeme wa Tunduru, lakini pamoja na Nanyumbu na Masasi kwa sasa ambao ndio tunatumia uwe ni umeme wa uhakika. Lakini kwa suluhisho la muda mrefu nilikuwa napendeleza pia, kwa sababu Mtwara tunatambua kuna gesi ambayo tayari imeshaanza kutumika. Kwa suluhisho la muda mrefu kwa Wilaya za Masasi na Nanyumbu ni vyema pia, kungejengwa bomba la gesi kutoka Mahumbika kuja Masasi, ambapo pia wanufaika watakuwa Wilaya za Masasi na Wilaya za Nanyumbu na kuendelea kwa sababu bado tutakuwa tunauhitaji huu umeme kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, napendekeza hayo kwasababu, tunatambua kwamba kwa sasa, Serikali inafanya jitihada pia ya kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuweka viwanda mbalimbali katika Mkoa wa Mtwara na hasa Masasi pia, kwa ajili ya kuchakata korosho, mabibo na yale mabibo yaliyokauka ambayo tumependekeza kutengenezwe *spirit* na viwanda vya mafuta ambapo kuna uhaba wa mafuta ya kula. Tunao ufuta na karanga kule, lakini wawekezaji hawa watakama kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kutokana na kukosa umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu umeme ukiimarika kwa Serikali kuweka hayo masuluhisho ambayo nimeyapendekeza, hiyo changamoto itakuwa imeondoka. Na hivyo wawekezaji watakutika kuja kuwekeza katika Mkoa wa Mtwara katika wilaya zote kwa sababu ya uhakika na hivyo kutakuwa na shughuli za uzalishaji mali na wananchi wataondokana pia na umasikini ambao kwa namna moja au nyingine, wanashindwa kujikwamua kutokana na mazingira ambayo kimsingi Serikali yetu sikivu inaweza kuyatibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa tatizo la kukatika kwa umeme lililopo, inapelekea wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kuunguza vitu vyao na tunajua sote kwamba, hakuna utaratibu mwananchi mmoja mmoja anapofanya shughuli zake kama labda ana mashine, labda saluni, ama mashine ya kusaga, ama *fridge* wapo wakinamama wanaotengeneza *ice cream*, waweze kuuza na shughuli zingine zozote zinazohusisha umeme. Vifaa hivyo vimekuwa vikiungua kwa sababu, umeme unakuja na nguvu kubwa pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wanaathirika kwa hiyo, wanapata hasara kubwa, lakini hata wale wafanyabiashara wanaouza hivyo vifaa vya umeme. Kwa sababu, kama wanapewa *warrant* ina maana kila siku wakiuza wanatakiwa warudishe ama wafidie, wakiuza wafidie. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa hiyo imekuwa ni

changamoto kubwa kwa wajasiriamali, lakini na kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mtwara, ambapo ninaamini kabisa, Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, inaweza ikalitibu hili tatizo kwa njia hiyo ya muda mfupi lakini pia kwa njia hiyo ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa umeme huu utakapokuwa umeimarika hata zile changamoto za Kituo cha Afya kama Nagaga na vingine kule Newala vitakuwa pia ambapo hawapati umeme wa kutosha, Newala, Nanyamba, Mtwara Vijijini, Jimbo la Ndanda, Lulindi ambako kumekuwa na tatizo la umeme usiokuwa wa uhakika basi hiyo changamoto itaondoka. Katika Wilaya ya Masasi pale mjini tunavyo vijiji 19 lakini pia, tuna mitaa kadhaa ambayo haijaunganishwa kabisa haina umeme. Ni imani... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa...

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi ya kuchangia lakini pia, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ananipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na wasaidizi wake, lakini kipekee nimtaje Mkurugenzi wa *REA*, huyu mtu amekuwa ni mtu wa pekee, ukimtafuta wakati wowote anapatikana na ni mtu ambaye kwa kweli ni msikivu, nimpongeze sana na aendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme ni ajira, umeme ni viwanda, umeme ni uchumi, umeme ni maendeleo. Niongelee umeme kwa upande wa Mkoa wa Kagera, kwa kweli pamoja na juhudi za Serikali, Mkoa wa Kagera

tumekuwa tukipata taabu sana tuna umeme ambao hauna uhakika. Kwa siku moja unaweza ukakatika zaidi hata ya mara 20, lakini pia umeme huu umekuwa ni umeme ambao nguvu yake ni kidogo. Kwa hiyo, niombe sana Serikali Mheshimiwa Waziri unafanya kazi nzuri mpambane iwezekanavyo, ili Mkoa wa Kagera uweze kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Kwa sababu, umeme tunaoutumia sasa hivi, ni umeme ambao unatoka katika nchi Jirani na hatuna uhakika nao kwa sababu, sio wa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri hili upambane nalo, ili Mkoa wa Kagera na sisi tuwe na umeme wa uhakika na ninaamini, hiki kinaweza kikawa kinachangia kwa Mkoa wa Kagera kuwa miongoni mwa mikoa ambayo ni masikini. Na ukija kuangalia mikoa yote kama Kigoma, Kagera na mikoa mingine ambayo iko kwenye orodha ya mikoa masikini, ni mikoa ambayo haina umeme wa uhakika. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili ulifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwa upande wa Kyerwa Mheshimiwa Waziri, nikushukuru tumekaa mara nyingi, ninakuomba sana kwa ajili ya vijiji vyangu ambavyo havijafikiwa. Nina vijiji 99, vijiji 29 bado havijapatiwa umeme. Lakini tumekaa tumezungumza muda mrefu umenipatia vijiji 19 bado vijiji 10 havijapatiwa umeme na nikuombe sana kwenye kata hizi ambazo zilikuwa hazijapatiwa umeme, yaani umeme haujawahi kugusa kabisa. Kwa mfano, ukienda kwenye Kata ya Bugala kuna Kijiji cha Bugala, Mugaba kwenye Kata ya Businde kuna Businde, Nyakashenyi, kwenye Kata ya Kibale kuna Kibale, Kijumbura, Kigorogoro, kwenye Kata ya Rukuraijo kuna Kijiji cha Mkombozi pamoja na Mgorogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, Kata ya Bugomora kuna Kijiji cha Nyakatera, vijiji hivi havijawekwa kwenye orodha ya kupatiwa umeme. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hili ulipe kipaumbele, hawa watu wanahitaji umeme muda mrefu na nilitegemea mkandarasi anapoenda anapeleka umeme maeneo yote. Kwa hiyo, niombe sana

Mheshimiwa Waziri vijiji hivi ambavyo nimevitaja, viweze kupatiwa umeme, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri. Lakini jambo lingine mimi nina vitongoji 670, vitongoji 503 bado havijapata umeme, kwa hiyo, unaposema mmepeleka umeme kwenye vijiji bado vitongoji vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa Kyerwa naweza nikasema umeme haujafika hata asilimia 30 kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili uliangalie. Mnasema mmepeleka umeme kwenye vijiji vingi, lakini vitongoji vingi havijafikiwa. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hivi vitongoji 503 kati ya vitongoji 607, niombe sana vipelekewe umeme. Na umeme wa kwanza ulipokuja ile *REA* ya kwanza walipitisha nguzo juu, lakini vitongoji vyote ambavyo viko chini pale havikuweza kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine Mheshimiwa Waziri, ulitoa maelekezo ukasema *TANESCO* wapeleke umeme kwenye taasisi za dini, kwenye mashule, kwenye vituo vya afya, maeneo mengi hayajafikiwa kwa upande wa Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili na lenyewe uliangalie. Jambo lingine ni suala la wananchi kuuziwa nguzo. Hili bado lipo Mheshimiwa Waziri na ikiwezekana niombe utoe maelekezo kwa maandishi, kila Mbunge awe na hii barua tuipeleke kwa wananchi. Kwa sababu, wanapopima wanakuambia mwananchi uko nje ya ramani ambayo tumepewa. Kwa hiyo, wewe unatakiwa ulipie nguzo tatu au nne. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri hili uliangalie.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, pale Kyerwa kwenye Kata ya Mulongo mpakani na Uganda, kuna mradi wa Kikagati, ule mradi Mheshimiwa Waziri sisi kama wana Kyerwa au wana Kagera, hatuelewi nini kinaendelea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, unaona upande wa pili ndio wanashughulika, lakini sisi hata ukienda pale kupata

taarifa, haupewi taarifa inayohusiana na ule mradi. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri tujue sisi kama Kagera kwasababu, ule mradi ni wa Uganda pamoja na Tanzania. Tujue sisi kama Kagera tunapata nini? Lakini mradi huu unakamilika lini Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Spika, ninaamini mradi huu utakapokamilika ndio unaweza kuwa mkombozi, wakati Mkoa wa Kagera bado hatujaunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Mradi huu unaweza ukasaidia angalau kutupunguzia yale makali tunayoyapata kwenye kukatika umeme kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimpongeze Waziri na niseme mradi wa Julius Mwalimu Nyerere. Mradi huu ni mradi ambao kwa kweli Mheshimiwa Waziri, Serikali yetu itapata heshima kubwa, lakini pia wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri, ninaamini mradi huu umeanzisha wewe na mradi huu utakupa heshima kubwa na jina lako litakumbukwa milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mchungaji Innocent Seba Bilakwate. Sasa mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo, ni Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Vedaustus Mathayo Manyinyi.

Mheshimiwa Manyinyi hayupo? Basi imekuwa siku njema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale wote ambao walikuwa hawakupata nafasi ya kuzungumza siku ya leo, kwa kweli wamepata nafasi ya kufanya hivyo na Wizara hii tunaendelea nayo kesho. Kwa hiyo, wale ambao hawakupata nafasi basi kesho tutapata nafasi ya kufanya hivyo na kesho hiyo hiyo tutahitimisha hoja hii ya Wizara ya Nishati.

Tuna wageni 100 wa Mheshimiwa Humphrey Polepole, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *UDOM*, naomba wana *UDOM* msimame. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, ahsanteni sana kwa kufika vijana wetu tunafurahi sana tunapojiunga nanyi mnapotutembelea hapa Bungeni. Lakini pia Waheshimiwa Wabunge mnaona *contribution* ya *UDOM* kwa wasomi wa nchi yetu. Kila Jimbo hapa lina wanafunzi wengi tu ambao wanasoma *UDOM*. Tunawatakia kila la kheri vijana wetu, tunaomba mjitahidi sana katika masomo yenu mjelimisha kadri mnavyoweza. Tunakutegemeeni, tunakuaminieni, kwa hiyo msituangushe. *(Makofi)*

Basi baada ya maneno hayo kwa vile tunaendelea na shughuli hizi kesho naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho Saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi  
Tarehe 3 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*